Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Saba – Tarehe 13 Mei, 2014

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI KUJENGA TAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2014/2015.

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 41

Vyuo vya Serikali Kutoza Ada Kubwa

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Serikali husisitiza umuhimu wa Watanzania wote kupata elimu bora na kwa usawa:-

(a) Je, kwa nini Vyuo vya Serikali hutoza ada kubwa ambayo Watanzania wa kawaida hushindwa kuimudu. Kwa mfano Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, hutoza kiasi cha shilingi 1,500,000/= kwa mwaka bila chakula?

(b) Je, kwa nini wanafunzi hawa wasilipe ada kama zile wanazolipa wenzao wanaosoma vyuo vya *VETA* na Ualimu ambao ada yao ina uwiano na kipato cha Mtanzania?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vyuo vya Serikali hutoza ada kwa kuzingatia gharama za uendeshaji na utoaji huduma bora kwa wanafunzi wanaodahiliwa na vyuo husika. Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo hutoza ada inayojumuisha malazi *(hostel)*, ada ya usajili, mitihani, kitambulisho, uanachama wa umoja wa wanafunzi, ushiriki wa michezo, matibabu, mafunzo ya awali na gharama za mafunzo kwa vitendo. Mwaka 2013/2014 ada kwa Astashahada (Cheti) ni shilingi 1,120,000/= na Stashahada *(Diploma)* mwaka wa kwanza shilingi 1,220,000/= na mwaka wa pili shilingi 1.190,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, sifa na gharama na mahitaji ya mafunzo Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ni tofauti na vyuo vya kawaida vya VETA au Vyuo vya Ualimu. Sifa na mahitaji ya wanafunzi wanaodahiliwa na chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kwa kozi ya Diploma na Cheti ziko chini ya udhibiti wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* tofauti na wale wanaodahiliwa katika vyuo vingine vya Ufundi Stadi vilivyo chini ya *VETA*.

Aidha, vyuo vya VETA hupata ruzuku moja kwa moja kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Skills Development Levy ambayo inasaidia sana kuchangia gharama za mafunzo.

MHE. ALIKO N. KIBONA: mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wapo wanafunzi wengi waliomaliza katika Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo na baada ya kumaliza masomo yao, wako vijijini wamekosa ajira, wakati huo huo

Serikali zetu za Mitaa kwa maana ya Halmashauri hawana Watendaji katika Kata zao na vijiji vyao.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuwaagiza Wakurugenzi wote au kuandaa utaratibu maalum ili wale vijana waliomaliza pale Hombolo kwa gharama kubwa za wazazi wao na hawa kazi wapate ajira? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, anachosema kuhusu hii ada anayoizungumzia ni kweli watu wengi tunaowapeleka pale sasa hivi. Watendaji wetu wa Vijiji na Kata wanakwenda pale kutegemeana na Halmashauri yenyewe inavyotaka. Wako wanafunzi wengi ambao wanaondoka pale wanakwenda mitaani na hawana kazi.

Lakini suala zima la uratibu wa ajira za watumishi katika nchi hautuondoi sisi kuwa chini ya Ofisi ya Rais (UTUMISHI). Kwa hiyo, mambo ya Bajeti na utaratibu wake na watu wake watakaopatikana wote, ni kweli hao anaowasema wako humo lakini bado itakwenda pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi utakumbuka kwamba hapa tumepitisha sheria na Kanuni zimepita hapa ambazo zinaruhusu sasa Halmashauri kada hii ya chini hii iweze kuajiriwa moja kwa moja kule katika Halmashauri bila kuhitaji tena kwenda kule Utumishi.

Lakini bado idadi ya wale watumishi watakaoajiriwa pale awe ni mpishi, awe ni korokoroni, awe ni nani, wote hawa bado lazima ipitie Utumishi.

Kwa hiyo, nataka kusema tunaiona hoja hiyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Utumishi ili kuhakikisha kuwa hilo analosema Mheshimiwa Kibona linatekelezwa.

SPIKA: Sikumwona mtu mwingine kwa hiyo tunaendelea. Mnatakiwa msimame kabla, siyo baadaye mkisikia majibu msimame, haiwezekani. Mheshimkiwa Said Arfi, swali linalofuata. *(Makofi)*

Na. 42

Tatizo la Maji Kakese na Mwamkulu

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika vijiji vya Mwamkulu na Kakese na vitongoji vyake ambalo linatishia ustawi na maendeleo yao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kakese ina jumla ya wakazi wapatao 21,360 kati yake ni wakazi 1,750 sawa na asilimia 8 tu ndiyo wanapata huduma ya maji safi na salama toka kwenye miradi ya visima virefu sita na kisima kifupi kimoja.

Mheshiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ya Mji wa Mpanda imetenga jumla ya shilingi 47,689,000/= kutoka kwenye vyanzo

vyake vya ndani na pia imepeleka ombi maalum Wizara ya Fedha la jumla ya shilingi 67,500,000/= kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji hivyo. Hata hivyo mpaka sasa hakuna fedha zilizopokelewa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2014/20125 Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imetenga jumla ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuchimba visima vitano kwa maeneo ya Kakese Mbugani (1), Mwamkulu (1), Kamakuka (1), Kawanzige (1) na Kakese Mkwajuni (1).

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kutatua tatizo hilo, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Kata ya Kakese na maeneo mengine nchini kwa kadiri rasilimali fedha inavyopatikana.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kabla sijauliza swali la nyongeza, kwa namna ya kipekee nilikuwa napenda nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, aliyekuwa Waziri wa Maji, kwa namna alivyoweza kutusaidia kuingiza mpango wa maji wa Ikolongo ambapo watu wanakwenda Mpanda wanaropoka kwamba Mbunge hafahamu, Mbunge analifahamu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na majibu haya ya kujirudiadia kwa sababu swali hili Mheshimiwa Waziri umelijibu sasa ni mara ya tatu, lakini kwa takwimu tu na hakuna utekelezaji wowote. Bajeti ya 2012/2013 tuliomba maombi maalum kwa ajili ya eneo hili, hakuna fedha iliyopelekwa. Mwaka 2013/2014 kama jibu linavyojionyesha kwamba hakuna fedha iliyopelekwa ni tarakimu tu hapa na 2014/2015 mnatupa matumaini wakati huku 2013/2014 hakuna fedha mliyopeleka.

Je, Mheshimiwa Waziri, kama unavyoona kwamba ni asilimia 8 tu ya watu wanaopata maji eneo hilo lenye wakazi zaidi ya 21,000, nini ahadi ya Serikali kwa sasa katika muda huu uliobakia wa kuchimba hivyo visima viwili?

Swali la pili, kwa kuwa mradi wa maji wa Ikolongo ambao kama nilivyotangulia kumshukuru Profesa Mark Mwandosya, unaendelezwa sasa chini ya Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe na fedha nimeahidiwa pia mwaka huu 2013/2014 tutapelekewa. Lakini Kata ya Misunkumilo ambayo inanufaika na mradi wa Ikolongo, vijiji vyake vina tatizo kubwa la maji. Tumeomba fedha, nini ahadi ya Serikali ya kumaliza tatizo la maji katika Kata ya Misunkumilo na Kata ya Kakese?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 na 2014/2014 Serikali itaendelea na ujenzi wa mradi wa maji ambao unaupatia maji Mji Mkuu wa Mkoa wa Katavi na katika ujenzi huu Serikali itaendelea kupanua upatikanaji wa maji katika eneo hilo la Mji Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupanua upatikanaji wa maji katika Mji huo wa Mkoa na Kata hizo ambazo Mheshimiwa Arfi amezitaja.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Tatizo la maji ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu na naamini hata katika Jimbo lako la Njombe.

Miongoni mwa matatizo na wenye uhitaji mkubwa wa maji ni Wilaya ya Bunda. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mradi mkubwa ambao unasuasua na moja ya tatizo

inasemekana mkandarasi hafanyi kazi vizuri na kwamba fedha zinazoingizwa katika kutekeleza ule mradi yeye haziingizi kwenye mradi na najua Mheshimiwa Profesa Maghembe analifahamu hili. Lini wakazi wa Bunda watapata maji safi na salama?

SPIKA: Unawahisha mambo hapa, maana naona tunamwuliza Prof. Maghembe badala ya Waziri Mkuu. Sijui nani au jibu Profesa, mradi mkubwa Bunda na ni swali jipya lakini.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni kweli kwamba unajengwa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika mji wa Bunda. Ujenzi wa mradi huo umekuwa unakwendwa pole pole kwa sababu ya matatizo yanayomhusu mkandarasi pamoja na upatikanaji wa fedha.

Mheshimikwa Spika, katika mwezi Aprili mwaka huu 2014 Wziara ilimwita mkandarasi pale Wizarani pamoja na msimamizi wa mradi ambaye ni Mamlaka ya Maji ya Musoma na kujadiliana naye na kuhakikisha kwamba anafanya kazi hiyo sasa na kuikamilisha katika mwaka huu wa fedha.

Kitu kilichokuwa kinangojwa ni pamoja na mabomba, mabomba yote yamenunuliwa na mitaro sasa inachimbwa na tunategemea kwamba mradi huo utakamilika katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji hapa Tanzania ni kubwa sana na ni tatizo la dunia vile vile. Lengo la saba la *millennia* la *sustainability and environmental protection* lina kipengele cha uvunaji, uhifadhi, kutumia na kuyatawala maji na Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zimesaini haya malengo ya *millennia*.

Ni kwa kiasi gani elimu iliyo rasmi na isiyo rasmi imetolewa kwa jamii nzima ya Watanzania ili tuweze tukayavuna maji haya ambayo Mwenyezi Mungu anatupatia kila mwaka ili kwa kiasi kikubwa iweze kuondoa tatizo la maji katika nchi ya Tanzania?

SPIKA: Bado ni Waziri wa Maji! Mmetangulia leo, mmewahisha ajenda.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna tatizo kubwa la maji hapa nchini na tatizo hili la maji liko pia katika ukanda wetu wa Afrika na katika dunia kwa ujumla.

Kwanza kuna mabadiliko ya tabianchi ambayo wakati mwingine kunakuwa na mvua nyingi na mafuriko makubwa, lakini muda mrefu pia kunakuwa hamna mvua na ukame. Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo mbaya na ongezeko kubwa la watu pamoja na shughuli za binadamu za kilimo lakini pia na viwanda, kwamba kuna ushindani mkubwa katika kuyatumia maji.

Sisi kama Tanzania tumetia saini maendeleo ya *millennia* na moja ya hayo ni upatikanaji wa maji. Tumelenga kwamba mwaka kesho tutatimiza malengo ya *millennia* kwa upatikanaji wa maji katika nyumba zetu, katika maeneo ya vijijini na mijini ili mradi Bunge hili Tukufu litatupatia fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, miradi yote tumeishaipanga iko tunangoja

fedha ili tu wakandarasi waliosimama waanze kazi na kuitekeleza na tutafikia malengo ya *millennia* kwa Tanzania.

Ninawaomba pia Watanzania watunze vyanzo vya maji na kutunza mifumo ya mito na maziwa ili kulinda rasilimali ya maji iliyoko kwetu.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Silvester Francis Koka.

Na. 43

Uwezo wa Hospitali ya Rufaa Tumbi

MHE. SILVESTER F. KOKA aliuliza:-

Serikali ilikuwa na nia njema kujenga Hospitali ya Rufaa Tumbi - Kibaha, lakini ujenzi huo umesimama kwa muda mrefu sana. Wakati huo huo wagonjwa wanasongamana kwenye hospitali hiyo wakikosa huduma zenye hadhi ya Hospitali ya Rufaa:-

Je, Serikali inalitatuaje tatizo hili kubwa kwa vigezo vya muda mfupi na mrefu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silverster Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuifanya hospitali ya Tumbi kuwa ya rufaa Serikali ilipanga kujenga jengo kuu la kutolea huduma za tiba, wodi ya wanaume na wanawake, jengo la wodi maalum, jengo la maabara na dawa na jengo la ofisi ya utawala. Utekelezaji wa mpango huu ulianza mwaka wa fedha 2008/2009.

Gharama za upanuzi kulingana na *BoQs* ya mwaka huo ilikuwa imekwishatoa shilingi bilioni 5,137,542,587/= kwa ajili ya upanuzi wa hospitali hii na zimetumika kukamilisha awamu ya kwanza ya jengo kuu.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha awamu ya pili shilingi bilioni nane. Kiasi cha bilioni 8,000,000,000/= kinahitajika. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Shirika lilishaidhinishiwa shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ikiwa ni pamoja na chumba cha kuhifadhi maiti. Vyumba vya Madaktari pamoja na chumba cha upasuaji. Hii ikiwa ni moja ya Mkakati wa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Mkoa wa Pwani umetenga shilingi 1,000,000,000/= katika mpango wake wa Maendeleo na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetenga shilingi millioni 150,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza ukarabati wa Hospitali hii. Aidha Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imewasilisha maombi maalum Ofisi ya Rais Tume ya Mipango, kwa ajili ya kupatiwa shilingi 6,000,000,000/= ili kukamilisha awamu ya pili.

SPIKI: Ahsante sana, swali la nyongeza Mheshimiwa Koka.

MHE. SILVESTER F. KOKA: Mheshimiwa Spika, asante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jengo jipya katika upanuzi wa hospitali hii ya Tumbi limechukua muda mrefu na awamu ya kwanza ya hili jengo kwa maana ya ujenzi wa jengo lenyewe umekamilika. Lakini ni takriban sasa miaka miwili vifaa tiba vya kufunga katika jengo hili angalau liweze kuanza kutumika havijapatikana na matokeo yake jengo hili sasa wanaishi popo na wanyama wengine.

Lakini juu ya hilo, awamu ya pili ambayo miundombinu iko sambamba na hii awamu ya kwanza, kwa zaidi ya miaka miwili nondo zimesimama pale na zinaendelea kuoza, hakuna hatua za haraka ambazo zimeishachukuliwa, na nikikumbuka wazi mwezi Oktoba Mheshimiwa Rais alipotutembelea aliahidi vile vile kutusaidia kupata utatuzi wa tatizo hili kwa haraka.

Je, Serikali haioni inapata hasara kubwa sana katika kuacha mradi huu unakaa miaka mingi na lile jengo lililoanza kujengwa linaendelea kuharibika?

Swali la pili,…
SPIKA: Naomba uulize kwa kifupi, hizo hotuba hapana.

MHE. SILVESTER F. KOKA: Swali la pili. Kwa kuwa sasa ile hospitali ya Tumbi imekwishatajwa ni ya rufaa na Kituo cha Afya cha pale Mkoani. Kituo kina changamoto kubwa mbali na Halmashauri kujitahidi kujenga *ward* ya akina mama kwa kutenga shilingi milioni 250, bado kituo kile hakina chumba cha upasuaji. Lakini vile vile hakina *Ward* ya kawaida ya kulaza wagonjwa wanaougua ambao wanastahili kupata huduma pale badala ya kupelekwa hospitali ya Tumbi.

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia kituo hiki ili kiweze kupata hadhi ya Hospitali ya Wilaya kuondokana na kero kwa wagonjwa wanaokwenda pale?

SPIKA: Hotuba ilikuwa ndefu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza hili la Tumbi. Tumbi Mheshimkiwa wala hatuna haja ya kueleza sana hapa, ni *concern* ya kila mtu hapa. Nakuomba hata usiwaruhusu wengine waulize kwa sababu wote sisi tunajua kwamba Tumbi ndiyo *fallback position yetu*, wanaotoka Arusha, wanaotoka Tanga, wanaotoka Iringa, wanaotoka mahali popote ikianguka hapo, ukasikia Sumry imeanguka pale, ujue kwamba wote watapelekwa hapo panapozungumzwa.

Anachosema hapa, hii sehemu ya chini ya jengo linalozungumzwa hapa imekamilika, na Mbunge ana-*pose* hapa kwamba kama imekamilika kwa nini tusianze kazi hiyo! Na ndiyo maana tumetaja milioni 500, tumetaja hata na milioni 150 kwa ajili ya vifaa ili kuhakikisha kwamba hiki anachosema Mheshimiwa Mbunge kinatekelezwa. Kwa hiyo sisi tutakwenda pale, tutakwenda kushughulikia, kusimamia na kuhakikisha.

Lakini tuelewane pia kwamba pale unahitaji bilioni 6 ndiyo maana tumesema tunakwenda Ofisi ya Rais – Mipango kuomba hizo fedha tunazozungumzia hapa. Lakini hii sehemu ya chini hata katika Kamati ya Mheshimiwa Kigwangala tumezungumzia jambo hili na tumeelewana kuhusu hilo eneo.

Mwisho, anazungumza kuhusu hiki Kituo cha Afya, ambacho kinaonekana kwamba kina matatizo. Anasema kwamba hakuna chumba cha kupasulia.

Mheshimiwa Spika, tutakwenda kuangalia. Tutakwenda kuangalia kwamba kiko katika *stage* gani. Vituo vya Afya vyote hivi tumeviweka chini ya Halmashauri na tukiona kwamba pale pana matatizo haya madogo madogo anayoyasema na kwamba ni suala la kuanza tu, *issue* hapa anayoizungumza ambayo ni ngumu kidogo na mimi lazima nikiri mbele yako, anazungumza kuhusu pendekezo la kukifanya kituo hiki kiwe hospitali ya Wilaya. Hiyo habari huwezi kuifanya wewe mwenyewe TAMISEMI, lazima uende *in collaboration*na *with* Wizara ya Afya. Twende tukazungumze na Mheshimiwa Dkt. Seif, tukubaliane naye, tuangalie kama wamefuata huo utaratibu. Huo utaratibu ukimalizika, sisi tutafanya kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutoa fedha za kutosha ili kukamilisha Ujenzi wa Wodi ya Wazazi na Chumba cha Upasuaji katika Hospiali ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi)? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu, nilikuwa na wasiwasi huo huo, kwamba Tumbi ni moja tu. Sasa inakuwaje. Sijui nifanyeje na hili linaulizwa kila siku. Hebu jibu kwa kifupi sana. Kwa sababu ni upendeleo tu lakini siyo swali lenyewe.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaogopa, nilifikiri utazuia lisijibiwe, kwa sababu na mimi ni mdau. Hiyo Hospitali anayoizungumzia Mheshimiwa Grace Kiwelu, ni hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, swali hili limekuwa linaulizwa mara kwa mara. Kila wakati tumekuwa tunalifuatilia. Kwenye hii *Current Budget,* kuna shilinrgi milioni 700,000,000/=. Lakini pia ile ambayo inakuja, ndiyo ninajua anatikisa kichwa kwa sababu hazijaenda kule. Halafu na shilingi bilioni 1,000,000,000/= ambazo zimetengwa kwa ajili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ile *Maternity Ward* pamoja na lile jengo linalosemwa palle ni karibu shilingi bilioni 16,000,000,000/=, ndiyo maana tuliwahi kusema hapa. Tukasema tukifuata mfumo huu wa kibajeti. Baajeti ni mpango wa Serikali unaonyesha jinsi hela zitakavyopatikana na jinsi zitakavyotumika.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 16,000,000,000/= hata Mkoa wa Kilimanjaro huwa hawapati. Lakini Mheshimiwa Grace Kiwelu amekuwa anafuatilia jambo hili kwa karibu. Tumewahi kuondoka naye tukaenda naye mpaka kwenye hiyo Hospitali. Mimi ninataka nitoe *credit* pale ambapo ina-*deserve*. Tutaendelea kufuatilia hizi hela. Mimi mwenyewe ni *beneficiary* wa kwangu kule Siha wakikwama wanapelekwa Mawenzi pale, ndicho anachozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa tunachofanya sasa hivi ni kusukuma hizi hela. Hata Mheshimiwa Hawa Ghasia, anafahamu, maana yake tumekuwa tunalifuatilia hili jambo karibu. Ili hela hizo zipatikane kwa ajili ya kwenda kumalizi ile *Maternity Ward* na kile chumba cha upasuaji.

SPIKA: Sasa, mkiwa mnajibu maswali. Msiwe mnawaangalia wale waliowauliza. Muwe mnamwangalia Spika. Ndiyo maana unaona wanatikisa vichwa. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, uko sahihi. Ni Dkt. Kebwe. Samahani kukurudisha nyuma kidogo kuhusu Hospitali ya Tumbi.

Mheshimiwa Spika, ninashukurusana kwa majibu ya Naibu Waziri (TAMISEMI – Mheshimiwa Mwanri). Pale Tumbi, kwa ushauri ambao tuliutoa. Ni kweli sehemu ile ya ngazi ya chini imekwishakamilika kwa kiwango kikubwa, ukiacha suala la vifaa.

Huduma ya tiba ile ambayo hahitaji vifaa, au *operation* kubwa au vipimo kwenye *diagnostic* kama ambavyo walikuwa wamepanga kuweka *MRI, CITSCAN, X-RAY,* na vitu vingine vya *Ndeospopies.*Tunashauri sehemu ile itumike jengo lile lisikae halafu likaanza kuharibika. Kuna huduma ya tiba ambayo inaweza ikafanyika, kwa mfano magonjwa haya ya jumla ya tiba. Huduma ya watoto.

Mhedshimiwa Spika, sehemu ile itumike katika kuondoa *congestion* ya wagonjwa ambayo ipokwenye kituo kwa sasa. Lakini sehemu ya pili, ya kuhusu Kituo cha Afya kuwa Hospitali ya Wilaya.

Suala hilo ni zuri, kuna *process* ambayo tunaiita ni *Step Wise, Certification for Acriditation.* Yaani kwenda kwa hatua, katika hatua ya Hisbati. Tunashauri tutashirikiana na TAMISEMI, twende tufanye Ukaguzi na baada ya hapo tuweze kutoa ushauri wa kitaalam. *(Makofi)*

SPIKA: Weheshimiwa Wabunge, ninaomba tuendele, muda umekwisha. Tumetumia dakika 12, ambapo tulitakiwa tutumie dakika tano (5).

Na. 44

Pori la Akiba la Kigosi Kutengwa na Kuboreshwa

MHE. AUGUSTINE MANYANDA MASELE aliuliza:-

Pori la Akiba la Kigosi linakabiliwa na upungufu mkubwa wa wanyama kutokana na vitendo vya kijangili na uvamizi wa makundi ya ng'ombe kutoka ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Pori la Akiba la Kigosi linatengwa na kuwa na utawala wake?

(b) Je, Serikali itaweka lini miundombinu ya barabara na *Game Ranger Posts* ndani ya Pori hilo ili kuboresha utalii?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agustine Manyanda Maselle, Mbunge wa Mbongwe, lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kigosi lilitangazwa na Serikali kuwa Pori la Akiba mwaka 1983 na linaungana na Pori la Akiba la Moyowosi lilioanzishwa mwaka 1981 ambapo kwa pamoja mapori haya yana ukubwa wa kilometa za mraba 13,000 (Kigosi 7,000 na Moyowosi 6,000).

Idara ya Wanyamapori kwa sasa Idara ina Wahifadhi 1091 ambao husimamia kilometa za mraba zaidi ya 200,000. Hii inafanya uwiano wa Mhifadhi mmoja kusimamia zaidi ya kilometa za mraba 250 ikilinganishwa na kiwango cha Kimataifa cha Mhifadhimmoja kwa kilometa za mraba 25 (1:25 km). Hivyo kuwana upungufu wa watumishi hususani katikakada ya wahifadhi wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kigosi peke yake kwa sasa lina watumishi 20 wakati wa mahitaji yake halisi nizaidi ya watumishi 300, hivyo kufanya Mapori ya Kigosi na Moyowosi kuwa chini ya utawala wa Meneja mmoja. Hii inatokana na upungufu wa watumishi. Sambamba na upungufu wa watumishi, Wizara inakabiliwa na ufinyu wa Bajeti pamoja na uhaba wa viendeaa kazi. Changomoti hizi zinafanya Wizara ishindwe kuyatengeneza Mapori haya.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kubadilisha Idara ya wanyamapori kuwa Mamlaka na mchakato wake unatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Wizara yangu itahakikisha kuwa Pori la Akiba la Kigosi linatengwa na kuwa na utawala wake ili kuimarisha ulinzi na kupunguza kama siyo kumaliza au kukomesha kabisa vitendo vya ujangili na uvamizi wa mifugo kutoka ndani na nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kigosi lina barabara zenye urefu wa kilometa 247 ambazo zinapitika kwa muda wa kiangazi za kilometa 30 ambazo zinapitika kipindi chote. Katika Mwaka ujao wa fedha 2014/2015, Wizara yangu inatarajia kutengeneza barabara za ndani zenye urefu wa kilometa 50 ili kuwezesha na kuboresha miundombinu na hivyo kufanya watumishi waweze kuendesha doria bila matatizo yoyote. Sambamba na mpango hiyo Wizara yangu imekamilisha matengnezo ya *Grader* ambalo litatumika katika matengenezo ya barabara hizo.

Pori la Akiba la Kigosi lina *Game Rangers Posts (3)* tatu kwa sasa ambazo ni Rwahika iliyo na watumishi watatu (3), Iponya ina mtumishi mmoja (1) na Uliwa ambayo haina mtumishi baada ya mtumishi wake aliyekuwa hapo kufariki dunia.

MHE. AUGUSTINE MANYANDA MASELE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru, ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Waziri amesema kwamba mwaka huu wametutengea kilometa 50 za barabara sasa hizi kilometa nyingine 197 Serikali ina mpango gani wa kuweza kutupatia fedha. Ili kusudi baraba yote yenye urefu wa kilometa 247 inaweza kukamilika?

Swali la pili, nchi yetu imejaliwa kuwa na mapori mengi ya Akiba, ambayo yanakabiliwa na matatizo yanayofanana. Serikali ina mpango gani wa kuyatangaza mapori haya, kwa wadau mbalimbali Ulimwenguni ili yawe vituo vya Wataali ambao wanaweza kusaidia katika

kuboresha uhifadhi wa mapori haya ikiwa ni pamoja na kuongeza uchumi wa Taifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana kwa kuuliza maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe jibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI MALIASILINA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nichkue fursa hii kumpongeza sana Ndugu yangu Mheshimiwa Masele. Ameitembelea kwenye ofisi yetu mara nyingi sana kuzungumzia tatizo la pori, lililopo katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Watalaam wangu. Tuliamua kutembelea kwenye pori hilo na tuligundua lina matatizo mengi, ikiwepo uhaba wa watumishi. Ikiwepo vitendea kazina miundo mbinu katika eneo hilo.

Tulichojipanga kama Wizara, ni kuhakikisha Miundo mbinu inapitika mwaka mzima. Mara ya kwanza ilikuwa kilometa 30. Lakini kwa sasa hivi tumejipanfga kuhakikisha kilometa 50 zinapitika. Na tumetenga fedha kwa ajili ya kuteneneza *Grader,* lililopo pale kwenye Bajeti ya mwaka huu wa fedha. Ninanata nikuhakikishie kwamba kama *Grader* litafanya vizuri badala ya klometa 50 ambazo tumekusudia kuzitengeneza kilomea nyingi zaidi zitatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, analolizungumza Mheshimiwa Masele, ni kweli kuna haja ya sisi kama Serikali kuliangalia lile Pori. Lakini kulikuwa kuna tatizo la msingi. Ambapo palikuwepo kuna matatizo ya majangili. Kulikuwa kuna matatizo ya uhaba wa watumishi, na palikuwa na matatizo ya vitendea kazi.

Lakini sisi kama Wizara tumejipanga, safari hii tunategemea kuajiri wafanyakazi 950, Watumishi kwa ajili ya kusaidia kulinda mbuga zile kwa hiyo Wawekezaji watakuwa hawana hofu. Kwa hiyo Wawekezaji wengi walikuwa na hofu ya kuwekeza katika pori lile kwa sababu kuliku wa halina uhakika wa ulinzi uliokuwepo pale. Lakini la pili. Miundombinu ikiimarika ikikaa vizuri Wawekezaji watakuwa hawana shaka katika kuwekeza katika maeneo haya. *(Makofi)*

MHE. DKT. TEREZYA P. L. HUVISA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la Pori la Msitu wa Kigosi, linalingana na tatizo la Msitu wa Kazimzumbwe ambao umevamiliwa na wananchi wengi sana pale na kuendelea kukata misitu.

Je, ni lini Serikali itaamua kuwatoa wananchi hao kwa sababu tatizo hili lilikuwa limeishafikia mwisho. Ninaiomba Serikali, itoe kauli sasa hivi. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala hili. Juzi nilikutana na Mkuu wa mkoa wa Dares Salaam, na Mkuu wa Mkoa wa Pwani. Tukalizungumza kwa kina na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alishaunda Tume kwa ajili ya kushughulikia suala hili. Tmejipanga na muda si mrefu tutawatoa. Serikali imeamua kuwatoa ninataka niwahakikishie tutawatoa katika lile eneo. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Waziri amenukuliwa akisema kwamba, Majangili wanaouwa Wanyama wetu wanafahamika kwamba ni baadhi ya Wafanyabiashara wakubwa wakishirikiana na baadhi ya viongozi. Sasa je, ni lini Serikali itawataja na kuwakamata? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiswa Spika, suala la kupambana na Majangili siyo la Serilali peke yake. Lina wadau takriban wanne (4). Kwanza Serikali, Sekta Binafsi, Jamii inayozunguka mbuga zetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sisi wote kwa pamoja tunatakiwa tushirikiane ili kuhakikisha tunawafahamu hawa Majangili. Hawa majangili tunaishi nao na tunakaa nao.

MBUNGE FULANI: Hakusikika.

SPIKA: Amelielewa na amejibu. Tunaendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 45

Uharibifu wa Mazao Unaotokana na Wanyama Kwenye Hifadhi ya Ngorongoro

MHE. MCH. ISRAEL YOHNA NATSE aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na uharibifu wa mazao ya wakulima katika vijiji vinavyopakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngongoro pamoja na watu kuuwawa na wanyama wakali kama tembo na nyati:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kurekebisha hali hiyo?

(b) Je, Wananchi wangapi ambao wameuwawa kwa miaka mitano (5) iliyopita na ni wangapi wameshalipwa fidia au kifuta machozi?

(c) Je, Serikali ipo tayari kulipa fidia ya Mazao ya wananchi yaliyoharibiwa na kusababisha hatari ya njaa?

NAIBU WAZIRI WA MALISILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua uwepo wa tatizo la wanyamapori wakatili na waharibifu ambao wamekuwa wakitoka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na kuvamia Makazi na Mashamba ya wananchi vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo. Kufokana na tatizo hilo Wizara ya Maliasili na Utalii imejipanga kuimarisha ushirikiano wake na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na Karatu, katikakudhibiti Wanyama Pori wakali na waharibifu. Wanaohatarisha maisha ya watu na mali. Aidha, doria za msako wa mara kwa mara za kudhibiti Wanyamapori wakali na waharibifu hufanywa na Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kaskazini.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2009 mpaka mwaka 2014. Wizara yangu imepokea Taarifa kutoka kwa wananchi sita, waliowawa na Wanyama pori wakali katika Wilaya ya Ngorongoro. Jumla ya Shilingi Milioni tatu zimelipwa na Idara ya Wanyama Pori kama kifuta machozi kwa familia ya marehemu hao sita (6).

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina utaratibu wa kulipa fidia kwa watu wanaouwawa, kujeruhiwa na mazao yao kuharibiwa na wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo kwa kuwa Serikali ya CCM ni sikivu, Wizara yangu imeendelea na utaratibu wa kutoa kifuta jasho/machozi kwa wananchi walioharibiwa mashamba yao, kujeruhiwa au kuuawa na wanyamapori kwa kuzingatia sheria Na.5 ya mwaka 2009 ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Kanuni za Kifuta Jasho/Macholzi cha Mwaka 2011.

(d) Mheshimiwa Spika, Kwa mfano kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wizara yangu ililipa jumla ya Shilingi 20,471,000/= kama kifuta jasho kwa familia 187 za vijiji vya Lositati, Mang'ola juu, kambi ya Simba, Bashai, Kiteto na Shahmo katika Wilaya ya Karatu. *(Makofi)*

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimwia Spika, niliuliza Wilaya ya Karatu, kabla ya kuuliza swali, ninaomba kama ni kosa la uchapaji au ndivyo alivyojibu?

(c) Kwamba ni watu sita Wilaya Ngorongoro na siyo Karatu. Anisaidie, kama ni Ngorongoro basi swali langu halikupata majibu. Ndipo niulize maswali mengine mawili ya nyongeza.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri umesema Ngorongoro. Ndivyo lilivyo jibu lako?

Mheshimiwa Mbunge anataka kuwa-*clarified* kwamba ni Ngorongoro au kule kwake Karatu?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni Ngorongoro. *(Makofi)*

SPIKA: Ni ngorongoro kama ulivyoandika. Kwa hiyo, maana yake Mheshimiwa unanisikia? Jibu lako unasema hivi katika kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2014 Wizara yangu imepokea taarifa ya wananchi sita (6) waliouawa na wananyamapori wakali katika Wilaya ya Ngorongoro. Sasa huyu huyu anauliza ni Ngorongoro au ni Karatu?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ambayo inazunguka Ngorongoro.

SPIKA: Kwa nini imeandikwa Ngorongoro? Nenda kaangalie tena. Kwa hiyo, na wewe unaahirisha maswali yako?

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Nitaendelea nitaomba Hansard kama anafanya marekebisho ni Wilaya ya Karatu na siyo Ngorongoro kama ni Ngorongoro hakujibu swali langu pamoja na hivyo ninaomba kujibu maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali haina utaratibu wa kulipa fidia kwa watu wanaouawa na wale waoaharibiwa mazao yao kwa kisingizio cha Sheria No. 5 ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 2011. ninaomba kuuliza swali dogo Je, Serikali haioni kwamba Sheria hii ni kandamizi kwa wananchi wake na inatoa kauli gani?

Swali la pili Doria na msako zinazodaiwa kufanywa katika ukanda wa Hifadhi ya Ngorongoro ni dhaifu sana kwa kisingizio kwamba hakuna magari, hakuna askari kama gari lipo hakuna mafuta na kama mafuta yakiwepo hakuna risasi.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa usalama wa wananchi na mazao yao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Sheria zinatungwa ndani ya Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuilaumu Serikali kama inaoenekana Sheria ina mapungufu sisi Wabunge tuna haki ya kuzileta hapa Bungeni na zinaweza kufanyiwa marekebisho. Hata sisi Wizara tumeyaona haya mapungufu tunategemea kuunda Mamlaka ya Wanyamapori.

Kwa hiyo, tutapitia mapungufu yote tuliyoyaona kwa sababu hakuna sehemu yoyote Duniani ambapo unaweza kulipa uhai wa mtu, haipo lakini ninataka kumwambia kuwa tumejipanga na tutakapokuwa tumeanzisha Mamlaka tutaangalia baadhi ya zile Sheria ndogondogo na tutafanya marekebisho.

Lakini ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kama kuna jambo haliko sawa sisi tuna haki ya kutunga Sheria na Sheria zote zinatungwa hapa tunaomba Sheria ziletwe Sheria tuzipitie kwa pamoja na kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mchungaji, suala la kujilinda na wanyama ni la sisi sote, sisi kama Serikali kwa nafasi yetu na maeneo yetu na wananchi wana maeneo yao. Kwa hiyo, kuna mambo ya msingi tunatakiwa tuyaangalie. Watu wengi sasa hivi kwenye vijiji wamejenga karibu na Hifadhi zetu na hili ni tatizo na hawakuacha maeneo *Buffer Zone*. Kwa hiyo, tunawaomba sisi na wananchi tushirikiane kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri unatakiwa ku- *clarify* ile ni Ngorongoro au Karatu kufuatana na utafiti wa ofisini kwako. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni Vijana na Michezo Mheshimiwa Agripina Buyogera, atauliza swali hilo kwa niaba yake ni Mheshimiwa Felix Mkosamali.

Na. 46

Kulinda Haki za Wasanii Kisheria

MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA) aliuliza:-

Kwa muda mrefu Wasanii wa Filamu na Muziki wamekuwa wakidhulumiwa haki zao bila ya kupata msaada wowote licha ya kuwa usanii ni ajira inayolipa kama ilivyo nchini Marekani.

(a) Je, ni lini Serikali itawatambua Wasanii wetu Kisheria ili kulinda kazi zao sambamba na kutoza kodi stahiki kwa maslahi ya Wasanii na Taifa kwa ujumla?

(b) Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ili kutunga Sheria nzuri kwa lengo la kulinda Haki za Wasanii hasa ikizingatiwa kuwa hiki ni kilio cha Wasanii cha muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inawatambua Wasanii wa Filamu na Muziki na pia inazitambua tasnia hizo na fani nyinginezo za sekta ya Utamaduni na imeziwekea mfumo wa Kisheria tangu mwaka 1930. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya kwanza ya kusimamia picha za sinema Sura ya 230 ya Mwaka 1930.

Sheria inayotumika mpaka sasa ya Filamu za Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976 na Kanuni zake. Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi Na.7 ya Mwaka 1999, Sheria ya BASATA Na. 23 ya Mwaka 1984 na Kanuni za *Stamp* kwa bidhaa za Filamu na Muziki za Mwaka 2013 zilizotungwa chini ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa. Serikali kwa kutambua umuhimu tasnia ya Filamu na Muziki umuhimu wa wasanii na haki zao ilichukua hatua ya kuzirasimisha tasnia hizo. Urasimishaji huo ulianza rasmi Januari 2013 kupitia urasimishaji huo, kazi zote za Filamu na Muziki zinawekewa *Stamp* ambazo zinatumika kuzilinda kazi hizo jambo ambalo halikuwa likifanyika hapo awali. Aidha, kazi ya usanii huchangia pia Uchumi wa Taifa.

(b) Tasnia ya Filamu inasimamiwa na Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976 kuna hatua mbalimbali ambazo zilichukuliwa zinazohusu tasnia wasanii na haki zao, kwanza marekebisho ya Sera ya Utamaduni yameshafanyika na ukamilishaji upo katika hatua za mwisho. Vile vile rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Filamu ipo katika hatua nzuri inasubiri ukamilishaji wa Sera ya Utamaduni.

Aidha, Sheria ya haki miliki na Haki Shirikishi ipo katika hatua za maamuzi Serikalini. Marekebisho ya Sera ya Utamaduni ipo katika hatua za maamuzi Serikalini Marekebishio ya Sera na Utamaduni na Sheria hizi mbili tumeweka mkazo mkubwa katika suala la kulinda haki bunifu, haki miliki, haki za wasanii na maendeleo ya tasnia za Filamu na Muziki na fani nyingine za sekta ya Utamaduni. *(Makofi)*

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru, na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba Serikali imeanzisha Utamaduni wa kuweka *stamp* ambao ni mzuri tu. Lakini changamoto kubwa iliyopo ni kwamba udhibiti wa kazi za wasanii ambazo hazina *stamp* bado zinauzwa na kuzagaa mitaani. Sasa tunataka majibu ya Serikali, Serikali itaanza lini sasa kudhibiti hizi kazi ambazo hazina *stamp* ili wasanii waweze kupata haki zao?

Swali la pili, ni kwamba nchi ya Uganda hapa jirani wana kitengo maalum ambacho kinasimamia usambazaji wa kazi za Filamu. Hapa Tanzania kuna kampuni inaitewa *Steps* ambayo imekuwa ikiwanyonya na kuwakandamiza Wasanii. Kwa nini Serikali isiige nchi ya Uganda ikawa na kitengo ambacho kitakuwa kinasimamia usambazaji wa kazi za wasanii, kuliko kuendelea na utaratibu kama huu uliopo ambao unawanyonya na kuwakandamiza wasanii?

NAIBU WAZIRI WA HABARI. VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo taarifa kuwa kazi za Wasanii nyingi zimezagaa mitaani. Serikali tumechukua hatua lakini suala hili halikosi changamoto kazi yoyote ni lazima iwe na changamoto, ukiwa na chanagamoto ndiyo unajifunza ni namna gani udhibiti wa hizo chanagamoto. Sisi kwa upande

wa Serikali tunajaribu kulifanyia kazi kwa kushirikiana na wadau ili kuondoa changamoto hizi za kazi za Wasanii zinazozagaa mitaani.

Ni kweli baadhi ya Wasanii wamekuwa wakinyonywa kupitia Kampuni uliyoisema sisi tutachukua hatua. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Alex Msama kwa ushirikiano anaofanya na Serikali katika kuhakikisha kuwa haki za Wasanii zinapatikana.

Kuhusu suala la pili kwamba wenzetu Uganda wana kitengo maalum kinachosimamia suala hili la haki za Wasanii wa Uganda, Uganda siyo mbali, tutakwenda kujifunza tuone kama kweli kinafanya kazi vizuri na sisi tunaweza kuanzisha kitu kama hicho. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru ninaomba nimwambie Waziri na kumwuliza swali. Stika anazozizungumzia za *TRA* ambazo na mimi nimeziweka hapa, ni stika ambazo zinakusanya ushuru peke yake, hazilindi kazi za Wasanii.

Sheria ya Mwaka 2006 ambayo ilipelekea kutunga Kanuni za kuwa na stika za Kosota za Haki Gramu ambazo zingekuwa na *categories* mbali mbali kwa sababu kazi hizi zina matabaka mbali mbali ndizo, zingeweza kusaidia kazi za wasanii. Ninamwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini utashirikiana na *TRA* wakawa ni ma-*agent* tu siyo kwa ajili ya kukusanya ushuru kutoka kwa wasanii ili uweze kulinda kazi za Wasanii. Ahsante sana.

SPIKA: Ninaona Waziri wa Fedha pale atajibu.

MHE. MWIGULU L. N. NCHEMBA (NAIBU WAZIRI WA FEDHA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri alivyojibu niseme tu kwamba sisi kama *TRA* ni kweli tunashughulika na kukusanya ushuru.

Lakini ni jambo la msingi kwanza kulinda kazi za Wasanii kabla hatujakusanya ushuru kutoka kwenye kazi zao. Sasa niwaagize KOSOTA ndani ya siku tano za kazi wakutane na *TRA* wakubaliane kwa namna nzuri ambayo tuta *harmonise* stika ambazo zinatumika kukusnaya ushuru na zile za kulinda kazi za wasanii ili tuweze kwanza kulinda kazi na kuweza kupata mapato kutokana na kazi zao.

Lakini jambo la pili niagize vyombo vinavyohusika, baada ya kuwa tumetengeneza utaratibu wa kutambua kazi halali basi zile kazi zingine ambazo zitakuwa zimetengenezwa kwa kukopi kazi halali ziweze kuchukuliwa hatua kama bidhaa zingine feki ambazo zuinachukuliwa hatua. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Obama, atauliza swali hilo kwa niaba yake Mheshimiwa Mkeketa.

Na. 47

Hospitali ya Misheni ya Heri Kuwa ya DDH

MHE. ABDUL R. MKEKETA (K.n.y. MHE. ARBERT OBAMA NTABALIBA): Mheshimiwa Spika, ninashukurukwa kunipa nafasi hii kwanza ninataka kutoa pole kwa wana Kilombero kwa mafuriko makubwa na pili ninashukuru Serikali kwa kupeleka maboti haraka sana kama tulivyoomba, ninapenda kuwakilisha swali namba 47 la Bwana Manyovu ninaomba Mheshimiwa Spika lijibiwe.

Hospitali ya Misheni ya Heri Jimboni Manyovu inatibu wagonjwa wengi sana kutoka kwenye vijiji visivyopungua 15.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haifanyi Hospitali hii kuwa ya *DDH* ili kutekeleza Sera ya Huduma za Afya bure kwa akina mama na watoto?

(b) Je, ni vigezo gani vitimizwe ili hospitali hiyo iwe ya *DDH?*

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuiatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Heri inamilikiwa na kanisa la Sabato iko katika Wilaya mpya ya Muhambwe Mkoani Kigoma na ina ukubwa wa vitanda 97 ili iwe hospitali ya Heri iwe Teule ya Wilaya ya (DDH) Halmashauri husika ya (Muhambwe) inapaswa kuwasilisha ombi kwa mmiliki wa hospitali katika kuitumia kama hospitali Teule ya Wilaya. Kanisa likaridhia kupitia kikao cha uongozi cha hospitali litaijibu Halmashauri na kuipatia muhtasari kikao kilicho kilichoidhinishwa.

Halmashauri itaitisha kikao cha Baraza la Madiwani kujadili uamuzi uliofikiwa na kanisa. Muhtasari wa kikao cha Baraza la Madiwani na ule wa kikao cha uongozi wa hospitali itaambatanishwa na barua kwenda Wizarani. Ombi litajadiliwa na Wizara, Hospitali itafanyiwa ukaguzi na kuwasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Ikiwa ataridhia Halmashauri huarifiwa ili makubaliano na kanisa kwa njia ya mkataba yafanyike. Taratibu zingine za kuomba fedha za kuendesha hospitali zitafanywa kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

(b) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyohitajika ili hospitali iwe hospitali Teule ya Wilaya *(DDH)* ni pamoja na uwezo wa kutoa huduma sawa na zile zinazotolewa na Hospitali za Wilaya za Serikali. Vigezo vinajumuisha kuwepo kwa:-

(i) Miundombinu ya majengo ya kutolea huduma za wagonjwa wa nje *(OPD),* wagonjwa wanaolazwa *(IPD),* upasuaji mdogo na mkubwa, Afya ya kinywa, macho, Maabara, mionzi, dawa na vitendanishi, huduma ya afya ya Mama na Mtoto na ushauri Nasaha kwa wenye VVU, pamoja na Elimu ya Afya.

(ii) Watumishi wa kada mbalimbali za Afya ambazo ni madaktari, wauguzi, na wataalamu wengine kulingana huduma zinazotolewa.

SPIKA: Mheshimiwa Mkeketa swali la nyongeza

MHE. ABDUL R. MKEKETA: Kwa kuwa, hospitali ya *Saint Francis* ya Ifakara inatumia huduma hii ya *DDH* na Serikali inawekeza sana katika hospitali ya Ifakara lakini gharama zinakuwa kubwa sana.

Je, Serikali itachukua hatua gani za kupunguza gharama hizi kwa wananchi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maana ya hizo mnazozichukua mnapunguzaje gharama zao?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hospitali hizi kwa mujibu wa uendeshaji kuna Bodi zile za hospitali na Bodi zile za hospitali za Halmashauri kwa lugha ya zamani hospitali ambazo zime- sign mkataba wa kushirikiana na Halmashauri inapaswa kuitwa ni Kamati ya Hospitali kwa sababu huwezi kuwa na Bodi ambayo inawajibika katika Bodi kimuundo. Kuna Bodi ya Afya ya Wilaya, kwa hiyo katika ngazi ya hospitali hizi Teule za Wilaya inaitwa ni Kamati ya hospitali.

Kwa hiyo, tunashauri kupitia Kamati hiyo ya hospitali na Bodi ya Afya ya Wilaya iweze kuridhia viwango ambavyo vimependekezwa kulingana na mwongozo ambao ulitolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwaka 1994. Kwa hiyo, mimi ninashauri viwango vile vipitiwe na Halmashauri husika ili iweze kuidhinisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Kutokana na matatizo ya muda, tunaendelea na Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir.

Na. 48

Gharama za Matibabu kwa Watu Wenye Ulemavu

MHE. AL- SHAYMAA J. KWEGYIR aliuliza

Familia nyingi zenye watoto wenye ulemavu ni zile zilizokuwa na hali duni kifedha hivyo kuwawia vigumu kumudu kulipia mahitaji muhimu kwa ukamilifu hususan elimu, matibabu na kadhalika.

Je, serikali ina mikakati gani ya kuwasamehe kulipia gharama za matibabu watu wenye ulemavu pale inapobidi?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Al- Shymaa John Kwegyir, Viti Maalumu, kama ifuatavyo ninaomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ulemavu ni hali inayotokana na dosari mwilini au akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika kutekeleza majukumu yake katika jamii.

Kizuizi katika utendaji unatokana na mfumo wa mtizamo wa jamii dhidi ya mtu mwenye ulemavu. Katika jamii yetu na kwingineko Duniani hali ya mtu kuwa na ulemavu inaambatana na unyanyapaa unaotokana na mila zilizopitwa na wakati. Kutokana na hali hii watu wenye ulemavu wanaonekana kuwa ni tegemezi wasiojiweza na wanaostahili kusaidiwa na watu wasio na ulemavu katika kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya utangulizi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Al – Shaymaa Kwegyir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha wanayoipata watu wasiokuwa na uwezo katika kulipia gharama za matibabu, kwa kutambua hilo Wizara yangu imefanya juhudi za makusudi kwa kutoa mwongozo wa utoaji wa msamaha wa matibabu kwa watu wasiokuwa na uwezo Wizara ilikwisha ziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilisha takwimu za watu wenye ulemavu na wazee wasiojiweza wanaopatiwa msamaha wa huduma za matibabu kupitia zahananti na hospitali.

Kwa kutambua mahitaji ya watu wenye ulemavu katika mwaka huu wa fedha Serikali inakusudia kuanzisha Mfuko wa Taifa wa kushughulikia mahitaji ya kiuchumi, kielimu, afya na mafunzo ya ufundi ili kukabiliana na chanagamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Kwa kuundwa mfuko huu ni mwanzo mzuri utakaofungua milango kwa wadau wengine kuchangia. Aidha mfuko huo utaanza kutengewa fidia na fedha katika Bajeti ya Serikali ili kuwezesha watu wenye ulemavu kupata fedha kwa ajili ya ujasiriamali, kama ilivyo kwa mfuko wa wanawake na vijana. *(Makofi)*

MHE. AL- SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika ahsante jina langu linakupa taabu ni Kwegyir. Ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna Mfuko na Mfuko huu alisema unaanzishwa toka mwaka jana tunaambiwa kuna mfuko utaanzishwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu kiuchumi, kielimu, kiafya na mafunzo ya ufundi. Sasa swali langu ni kwamba Mfuko huu Mheshimiwa Naibu atuambie umefikia wapi?

Swali la pili Mheshimiwa Waziri ninamwomba na pia ni swali juu yake. Kuna Mfuko wa *Natinal Health Insurance Fund (NHIF)*. Huu Mfuko wa Bima ya Afya ni mzuri mno Mheshimiwa Waziri anaonaje masuala ya Afya yatolewe kwenye huu mfuko yapelekwe kwenye hii *NHIF* kwa ajili ya watu wenye ulemavu wapatiwe matibabu. Kule kuna vipimo, dawa kila kitu kinapatika bila ya matataizo na ni bure. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie

Je, haiwezekani kwa watu wenye ulemavu kuingizwa kwenye Mfuko huu? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI AFYA, USTAWI NA JAMII: Sehemu ya Mfuko umefikia wapi. Katika jibu la msingi la awali utaratibu uliopo na kwa ajili ya kujenga uelewa mzuri kwa Watanzania wote, itaingizwa katika hotuba ya Wizara ambayo itawasilishwa hapa Bungeni tarehe 3 Juni, 2014 ili kujenga uelewa wa kina katika utaratibu mzima wa maandalizi ya kuwasaidia hawa wenye mahitaji maalum. Ni suala la msingi na nimshukuru sana Mheshimiwa Shymaa kufuatilia suala hili la uwakilishi la wale wenye ulemavu kwa umahiri mkubwa sana. Unajua Watanzania takribani asilimia 10 hadi 13 wapo katika kundi hili la uhitaji maalum. Kwa hiyo, suala hilo Wizara inalifanyia kazi kwa ukaribu sana.

Sehemu ya pili, kwamba kulingana na huduma bora ya kuridhisha inayotolewa chini ya bima ya taifa *NHIF* ni kwanini kundi hili lisiingie katika huduma hii? Kwa sababu muundo wa Sheria ya utoaji na Mafao yanayopatikana katika bima ya Afya ya taifa ni wazo zuri, tumelipokea na tutaangalia Sheria ile inasimamia nini, lakini kwa ujumla wake kisera, nchi yetu

wale wote wenye ulemavu ambao takribani asilimia 13 wanapaswa kupata huduma ya bure katika maeneo husika.

Kwa hiyo, atawasilisha jibu kwa kina, tutakaa naye na tutaangalia Sheria inasema nini ili kusudi aweze kuwa na kumbukumbu sahihi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ukae. Mheshimiwa Naibu Waziri swali namba 47 mtajibu tena maana Wataalamu wako hawakuelewa wanajibu nini. Hakuna Halmashauri ya Muhambwe.

Swali linalofuata Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Rukia Ahmed.

Na. 49

Waathirika Kutokana na Vita ya Uganda

MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-

Wanajeshi waliokwenda kupigana Vita vya Uganda walipewa zawadi ya ahsante na Mwalimu Julius Nyerere na Tanzania ilipewa fidia na Serikali ya Uganda kwa ajili ya vita hivyo.

Je, Serikali iliwapa nini wale wote waliothirika na vita hivi ambao sasa hivi ni walemavu na wengine wajane na yatima waliopoteza wanaume na wazee wao kwenye vita hiyo.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Walemavu wote waliopata ulemavu wakiwa katika Vita vya Uganda wanalipwa Pensheni ya ulemavu *(Disability Pension)* kulingana na viwango vya ulemavu waliopata. Pensheni hii hulipwa hadi mhusika atakapofariki.

Kwa upande wa waliofariki vitani, familia zao (Wajane na yatima) wanalipwa pensheni ya kifo *(Death Pension)*. Mjane hulipwa moja ya sita ya mshahara wa mumewe wakati anafariki kama pensheni kwa mwezi na kila mtoto hulipwa moja ya nane ya mjane kwa mwezi. Malipo haya kwa mjane huendelea hadi naye atakapofariki isipokuwa endapo ataolewa tena, malipo haya hukoma. Kwa watoto wataendelea kulipwa hadi watakapofikisha umri wa miaka 21. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Rukia swali la nyongeza.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini bado nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Wanajeshi hawa waliokwenda kupigana vita vya Uganda ni watu ambao ni majasiri wali-*risk* maisha yao kwa kuitetea nchi hii na sasa wanaishi katika mazingira magumu sana.

Je, Serikali kwa nini haifikirii kuwalipa fidia ili iwe ni changamoto kwa Wanajeshi wengine?

Swali la pili, k wakuwa kikawaida pesheni za Wanajeshi wetu ni ndogo sana, Wanajeshi wengi wanapostaafu kazi wanaishi katika mazingira magumu, wengi wao wanakuwa ni walinzi katika nyumba za matajiri na maofisi.

Je, Serikali inasemaje juu ya kuwaongezea pensheni Wanajeshi wote wanapostaafu ili kujengea heshima jeshi letu?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba utaratibu wa Kisheria uliopo ni kuwalipa pensheni waliopata ulemavu na waliopoteza maisha basi wajane au watoto wao wanalipwa pesheni. Hii ndio Sheria ilivyo sasa kwa hiyo, hakuna utaratibu wa fidia bali kilichopo ni pensheni.

Kwa swali la pili kwamba pensheni ni ndogo sana, tunakiri kwamba pensheni ni ndogo haikidhi mahitaji na imepitwa na wakati. Kwa hivyo, lengo ni kufanya utaratibu wa marekebisho ya Sheria ili iandane na viwango vya mshahara vya sasa ndipo tutakapoweza kupata pensheni ambayo ilikuwa angalau inaweza ikakidhi mahitaji kwa wahusika. Kwa hiyo, tunachoweza kusema tutarekebisha Sheria zilizopo ili hatimaye na uwezo wa Serikali ukiruhusu viwango vya pensheni viweze kuongezwa ili kuweza kukidhi mahitaji. Kwa kweli tunakiri kwamba kwa sasa ni vidogo sana.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea kwa sababu Wizara yenyewe inaingia baada ya hapa tu. Kwa hiyo, Wizara ya Maji tunaendelea Mheshimiwa Rage!

Na. 50

Mradi Wa Maji Toka Ziwa Victoria- Tabora

MHE. ISMAIL A. RAGE aliuliza:-

Kuhusu Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Tabora, ni lini Upembuzi yakinifu umefanyika ni Kampuni gani iliyopewa na gharama zake ni kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, Wizara ya Maji na kampuni ya Serikali ya India *WAPCOS,* zilisaini Mkataba wa Makubaliano *(MoU)* kuhusu upembuzi yakinifu wa Mradi wa maji (Kahama/Shinyanga – Nzega- Igunga- Tabora). Kazi hiyo ilikamilika mwaka 2013 na kuandaa makisio ya awali ya gharama za Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kupitia kazi iliyofanywa na *WAPCOS,* Serikali inatafuta fedha ili kujenga Mradi huo. Aidha, tarehe 30 Aprili, 2014 Serikali imesaini mkataba na Mhandisi Mshauri (*Metaferia Engineers* kutoka Ethiopia akishirikiana na *G-PES na Don Consult* wa Tanzania).

Mtaalam Mshauri huyo ataendeleza kazi hiyo kwa kupitia upembuzi yakinifu uliofanywa awali pamoja na kufanya usanifu wa kina, kuandaa vitabu vya zabuni na kutathmini athari za kimazingira na kijamii. Gharama ya kazi hiyo ni Dola za kimarekani 838,525 na kazi hii itachukua

miezi kumi na mbili (12) hadi kukamilika. Ujenzi wa Mradi huo utahusisha vijiji vyote ambavyo vitakuwa umbali usiozidi kilomita 12 kila upande kutoka kwenye bomba kuu.

SPIKA: Mheshimiwa Rage Swali ya nyongeza.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina Maswali mawili ya nyongeza tarehe 8 Machi, 2010 tarehe 22 Septemba 2010, tarehe 6 Januari 2013, Rais wa Jamhuri ya Muungano aliwakikishia wananchi wa Tabora watapata maji kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ibara ya 17(a-e)

Je, Mheshimiwa Waziri ujenzi wa mabomba hayo kutoka Shinyanga mpaka Tabora kwa kupitia Nzega na Igunga utaanza lini?

Swali la pili, Kwa kuwa matatizo ya Maji katika Manispaa ya Tabora na Mkoa wa Tabora imekuwa ni tatizo sugu, uko tayari kwenda na mimi Tabora ukawaeleze wananchi wa Tabora mipango yako?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi, kuwapatia wananchi wake Maji kutokana na ilani kama ambavyo alisema Mheshimiwa Rais na sisi tumhakikishie tu kwamba tutaitekeleza na tumeanza kwa pale Tabora mjini kwa maana ya kwamba kuna kazi mbili zinafanyika za kuboresha miundombinu kwa pale mjini. Lakini pia kuboresha chanzo kule katika Bwawa la Igombe.

Niseme pia kwamba kwa Mradi wa Maji kutoka Kahama, Nzega, Igunga, Tabora kama mlivyosema ni kwamba tayari tumeshatiana saini kwa hiyo, unafanyika usanifu ambao utafanyika kwa miezi kumi na mbili lakini naamini kabisa baada ya kazi hiyo sasa atatafutwa Mkandarasi na hii ni kuanzia mwaka 2015.

Lakini kuhusu suala la kwenda kuwaambia wananchi hao tumpongeze Mheshiwa Rage kwa kulifuatia suala hili mara kwa mara na kuuliza maswali mengi lakini nimekuhakikishia toka jana niko tayari tarehe 18 tutakuwa na mkutano wa hadhara pale Tabora Mjini ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa wajibu wa kuangalia muda ni wa kwangu pamoja na nyie. Nyie mnasimama tutaendelea mpaka lini?Maswali yameisha naomba nitambue Wageni waliopo.

Tunao wageni katika viti vya Mheshimiwa Spika, tunao wageni kumi na moja wa Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao wapo chini ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Pamoja na hao wapo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Job Msima, naomba aimame! Halafu yupo Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwitango Rose Shelukindo, Mkuu wa Majeshi Generali Davis Mwamunyange. *(Makofi)*

Wanashangilia kwa sababu ya vyombo vya ile tarehe 26 Aprili, 2014. Yupo Mnadhimu Mkuu wa Majeshi Luteni Generali Samweli Ndomba, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Meja Jeneral Raphael Mhonga, wale askari wa humu ndani hata hawashangilii wameshasahau.*(Makofi/Kicheko)*

Yupo Kamishna wa Sera na Mipango Ndugu Elbirati Dauku, Mkuu wa Shirika la Mizenga Meneja Generali Charles Nzanila, Mkuu wa *Land Force* Meja Generali Salum Kijuu. Mkuu wa Komandi ya Anga ya Meja Generali Joseph Furaha Kapani, Mkuu wa Kamandi ya Wanamaji, Brigedia Generali Logasiani Shabani Luwasai, Mkuu wa Shirika la Nyumbu Kanali John Nchimbi na wako wengine wengi sipendi kuwasimamisha mnawaona kwa nguo zao. *(Makofi)*

Halafu kuna Wageni saba wa Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mbunge wa Kilombero, akiongozwa na Ndugu Hassan Kidamba, Diwani wa Kata ya Chita na wenzako, naomba msimame. Halafu tunao wageni ambao wamefika kwa ajili ya Mafunzo. Wapo wanafunzi 35 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* naomba msimame, karibuni na mkazane kusoma. Wapo wanafunzi 100 kutoka Lukundo Sekondari - Dodoma na wenyewe wasimame walipo wote kwa pamoja. Haya msome kwa bidii wanafunzi na uwezo wenu upo katika kusoma vizuri. *(Makofi)*

Sasa matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba tarehe 13 Mei, 2014 saa saba mchana katika Ukumbi Namba 227. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa saa saba mchana, watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 229. Halafu Mwenyekiti wa Kamati za Bunge Masuala ya Ukimwi, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na Mkutano katika Ukumbi wa Msekwa, hawa wa ukimwi.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie Wabunge Wanamichezo wa Mpira wa miguu na Mpira wa Pete na mazoezi ya viungo kuwa mazoezi ya kujiandaa na michezo ya kirafiki yanaendelea katika uwanja wa Jamhuri kuanzia saa kumi na mbili asubuhi. Wote wanaombwa kuhudhuria. Kwa hiyo, ni vizuri mkahudhuria kule. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

SPIKA: Ngoja nitafakari unachosema sio unisomee tu. Mheshimiwa mtoa hoja!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHE. Dkt. HUSSEIN ALI MWINYI: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hoja yangu, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia kuwa na uzima na afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Aidha, namshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa majeshi shupavu ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mara ya pili.

Ahadi yangu kwake Mheshimiwa Rais, kwenu Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania wenzangu, hususan wenye mapenzi mema na nchi yetu, yenye amani, utulivu, upendo na mshikamano ni kwamba, nitatumia uwezo na nguvu zangu zote kutekeleza

majukumu mazito na nyeti mliyonikabidhi kwa umakini mkubwa, uaminifu na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda, (Mb) kwa miongozo, ushauri na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Vile vile, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Kamati yako Tukufu ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah (Mb), kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kutoa ushauri, maelekezo na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati yako ya Ulinzi na Usalama kwa kutenga muda wao adhimu kwenda kuwatembelea wanajeshi wetu wanaotekeleza jukumu zito la kimataifa la Ulinzi wa Amani huko Darfur nchini Sudan.

Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa ziara yao hiyo ilileta hamasa na kuongeza ari kubwa kwa wapiganaji wetu katika utendaji wao wa kazi. Ni matumaini yangu kuwa Kamati itaendelea kufanya ziara kama hiyo katika vikosi vyetu vingine vilivyopo nje ya nchi ikiwemo *Force Intervention Brigade (FIB)* iliyopo huko Mashariki mwa Kongo.

Aidha, namshukuru mtangulizi wangu, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha (Mb), kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi chake cha uongozi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wabunge wenzetu waliaga dunia. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Said Ramadhan Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze. Napenda kuungana na wenzangu walionitangulia kutoa pole za dhati kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ndugu, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa hao. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuwa ile ile ya kuwa Taasisi iliyotukuka ya kudumisha amani na usalama wa Taifa. Vivyo hivyo, Dhima ya Wizara hii bado ni kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi na kuhakikisha kuwa mamlaka ya nchi *(National Sovereignty)* na maslahi ya Taifa letu *(national interests)* yako salama.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia Dhima yake, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina malengo yafuatayo:-

(i) Kuwa na Jeshi dogo la Ulinzi wa nchi lenye taaluma, zana na vifaa vya kisasa.

(ii) Kujenga na kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na makazi.

(iii) Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia ya kijeshi katika mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(iv) Kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema na utaifa kwa vijana wa kitanzania.

(v) Kuimarisha jeshi la akiba.

(vi) Kuimarisha mawasiliano salama jeshini.

(vii) Kuimarisha umiliki wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya jeshi.

(viii) Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa, Wizara imekusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandikisha wanajeshi wa kutosha wenye sifa zinazohitajika kwa ajili ya ulinzi wa Taifa na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kinadharia na kivitendo.

(ii) Kuwapatia wanajeshi makazi, zana, vifaa na vitendea kazi bora na vya kisasa.

(iii) Kusimamia matunzo na matumizi mazuri ya zana, vifaa na vitendea kazi.

(iv) Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi na kuendesha mafunzo ya ulinzi wa mgambo.

(v) Kuendeleza mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria na ya kujitolea ili kuwaandaa kwa ukamilifu vijana wa Kitanzania na kuwajengea moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa katika kutekeleza shughuli za kujitegemea.

(vi) Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi na kuzalisha mali kupitia mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(vii) Kuliwezesha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) liweze kuzalisha kwa tija na faida itakayochangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa.

(viii) Kushirikiana na Mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga ili kuwapatia wahanga misaada ya kibinadamu.

(ix) Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na

(x) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika masuala ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2013/2014 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kadhaa kwa Wizara hii yaliyolenga kuboresha utendaji wa majukumu yake. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi. Aidha, hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa katika mpango na Bajeti ya mwaka 2014/2015 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa mipaka ya nchi yetu (nchi kavu, maji na anga) kwa mwaka 2013/2014 ilikuwa shwari kwa ujumla. Licha ya kuwepo kwa matishio na mashambulizi ya kigaidi katika eneo la Afrika Mashariki, hakukujitokeza tukio lolote la uharamia kwa upande wa bahari yetu. Hata hivyo, vitendo vya usafirishaji wa madawa ya kulevya na biashara haramu ya usafirishaji binadamu vilijitokeza. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya Usalama vimeendelea kushirikiana katika kukabiliana na hali hiyo.

Kwa upande wa mipaka, matukio ya uharibifu wa alama za mipaka na ujenzi holela unaofanywa na wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani hususan maeneo ya Namanga, Jasini, Tunduma na Mtukula yameendelea kujitokeza.

Hata hivyo, vikao vya wataalamu kutoka Serikali za Tanzania na nchi jirani za Kenya, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* na Zambia vyenye lengo la kutatua matatizo hayo vimeanza. Kufuatia vikao hivyo, alama nane za mpaka (umbali wa km 14.8) zilizokuwa zimeharibiwa katika Wilaya za Tarime (Tanzania) na Kurya (Kenya) zimeimarishwa, ambapo alama saba zimejengwa upya na moja imekarabatiwa. Aidha, alama mpya sabini zimejengwa katikati ya *beacons* za zamani ili kufanya mpaka huo uonekane kwa urahisi. Mazungumzo kuhusiana na utata wa mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa yanaendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Pamoja na hali hiyo, hakuna uhasama wowote wa kijeshi uliojitokeza baina ya nchi zetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 68,206,000/= kutoka kwenye mafungu yake matatu ya 38 - Ngome, 39 – JKT, na 57 - Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 mafungu hayo yalikusanya mapato ya jumla ya Sh. 43,317,624/= sawa na asilimia 63.5 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya Sh. 1,102,999,529,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba mtulie, tunasikiliza. Waziri naomba uendelee.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo Sh. 857,417,502,000/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 245,882,027,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia machi 2014, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Sh. 768,496,687,343/= sawa na asilimia 69.7 ya bajeti yake. Kati ya fedha hizo Sh. 719,118,556,008/= zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 83.8 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi hayo.

Kwa upande wa matumizi ya Maendeleo fedha zilizopokelewa ni Sh. 49,378,131,335/= sawa na asilimia 20.1 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yote matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi Machi, 2014 umeoneshwa katika kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya fedha zilizopokelewa inaonesha kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi hicho kiujumla ulikuwa ni wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Hata hivyo, fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo hadi kufikia Machi, 2014 zilikuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji. Hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali ili kufikia malengo niliyoyaeleza hapo awali. Shughuli hizo ni pamoja na kulipa stahili mbalimbali za Wanajeshi, Watumishi wa Umma na Vijana waliopo katika mafunzo ya JKT, kusafirisha wastaafu na kutoa huduma muhimu za chakula, tiba na sare.

Wizara pia ilipanga kulipa huduma za umeme, maji, simu na mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya ulinzi zikiwemo za mafunzo ya Kijeshi, mafunzo ya Ulinzi wa mgambo na kutengeneza vifaa na zana za Kijeshi.

Mheshimiwa Spika, uimara wa Jeshi lolote duniani unategemea mafunzo pamoja na mazoezi ya mara kwa mara, katika mwaka 2013/2014 Jeshi letu lilipata fursa ya kushiriki mazoezi mbalimbali ya pamoja na nchi marafiki. Miongoni mwa mazoezi hayo ni zoezi la Kituo cha Uamrishaji, *Command Post Exercise (CPX)*. Zoezi hilo la Uamrishaji lilikuwa ni sehemu ya Maandalizi la zoezi la Medani litakalohusisha majeshi ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zoezi hilo lijulikano kwa jina la Ushirikiano Imara 2014, Field Tactical Exercise litafanyika katika Jimbo la Mwaro nchini Burundi tarehe 13 hadi 26 Oktoba, 2014.

Aidha, kupitia Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* Jeshi letu limeshiriki katika mazoezi ya *EX WILWETCHIA* lililofanyika Mwezi Septemba mwaka 2013 nchini Namibia, *EX blue* Zambezi lililofanyika nchini Angola mwezi Oktoba, 2013; na *EX CUTLASS EPRESS'* lililofanyika Mwezi Novemba, 2013 nchini Seychelles.

Mheshimiwa Spika, Jeshi linategemea pia kushiriki katika zoezi linaloandaliwa na Umoja wa Afrika zoezi hilo lijulikanalo kwa jina la Amani Afrika II litakalofanyika nchini Lesotho mwezi Oktoba/Novemba, 2014. Mazoezi ya namna hii siyo tu yameimarisha Jeshi letu kimedani, bali pia yamekuwa chachu kubwa ya kuboresha mahusiano na majeshi mengine.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuweka umuhimu wa mafunzo ya mgambo. Katika kipindi hiki, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama limeendesha mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa wananchi 13,484 (Wanaume 12,337 na wanawake 1,147) ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.8 ikilinganishwa na mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Viongozi wa Wilaya na Mikoa kuongeza kasi ya usimamizi na ushiriki wa mafunzo hayo na kutoa huduma stahiki za usafiri kwa wakufunzi wetu, hifadhi ya silaha na maeneo ya mafunzo. Matarajio ya baadaye ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ni kuanzisha rasmi Kamandi ya Jeshi la Akiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya kiulinzi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za tiba kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, familia za Wanajeshi na wananchi kwa ujumla. Huduma hizo zimezidi kuimarika baada ya kuboresha hospitali za JWTZ zilizoko Mwanza, Mbeya, Bububu (Unguja), Tabora, Nyumbu (Pwani) na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (Arusha).

Lengo letu ni kuboresha huduma hiyo pia katika ngazi ya vituo vya afya vikosini. Ningependa Bunge lako Tukufu litambue kwamba asilimia 80 ya wagonjwa wanaohudumiwa na hospitali na vituo vyetu ni wananchi wanaoishi maeneo jirani.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi ni suala muhimu katika mustakabali wa ulinzi na usalama duniani. Hivyo basi, nchi yetu inaendelea kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi na nchi mbalimbali zikiwemo: - China, Ujerumani, Marekani, Afrika ya Kusini, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uingereza, Canada na Urusi. Kupitia ushirikiano huo, Jeshi letu, pamoja na mambo mengine limenufaika katika maeneo yakiwemo ya nyanja za mafunzo ya kijeshi na kitaaluma, zana na vifaa, mazoezi na michezo. Kwa ujumla, ushirikiano huu umekuwa ni wa manufaa makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea kudumisha ushirikiano katika Jumuiya za kikanda *(Regional Cooperation)* hususan za Afrika Mashariki *(EAC)* na Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Ushirikiano huo ulijikita katika nyanja za mafunzo, mazoezi na michezo baina ya majeshi ya nchi zetu. Kama nitakavyoeleza hapo baadaye, Tanzania, tukiwa wanachama wa nchi za SADC tumepeleka nchini *DRC* kikosi cha ulinzi wa amani kuungana na majeshi ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Vyuo vyetu, Jeshi letu limeendelea kutoa nafasi za mafunzo ya kijeshi kwa Majeshi ya nchi za Botswana, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Namibia, Seychelles, Swaziland na Zimbabwe, kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (National Defence College- NDC); Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (Command and Staff College-CSC); na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (Tanzania Military Academy-TMA). Vivyo hivyo, Maafisa wetu nao walipata mafunzo katika baadhi ya nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali. Hadi sasa, ushiriki wa wanajeshi wetu katika Operesheni hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kikosi kimoja kipo Darfur nchini Sudan(TANZBATT – 8);

(ii) Kikosi kimoja kipo Mashariki mwa DRC ikiwa ni sehemu ya *MONUSCO Force Intervention Brigade(TANZBATT – 1);*

(iii) Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon; na

(iv) Waangalizi wa amani *(Military Observers)* na Maafisa Wanadhimu (Staff Officers) wapo katika baadhi ya nchi ikiwemo Sudani Kusini.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kutoa mafunzo kwa vijana wa kujitolea na wa Mujibu wa Sheria. Malengo ya mafunzo hayo ni pamoja na kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa na kuwapa stadi za maisha vijana wa Kitanzania. Katika mwaka 2013/2014 JKT linaendesha operesheni moja ya mafunzo ya vijana wa kujitolea ijulikanayo kama Operesheni Miaka 50 ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika operesheni hii idadi ya vijana 8,439 (kati yao wavulana 6,610 na wasichana 1,829) wanaendelea na mafunzo yaliyoanza mwezi Machi 2014. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeanza kutekeleza utaratibu wa kuajiri vijana waliopitia mafunzo ya JKT. Idadi ya vijana 7,062 walichukuliwa na vyombo hivyo kwa mwaka huu. Aidha, vijana 155 walichukuliwa na Taasisi na makampuni binafsi (Benki Kuu ya Tanzania-BOT, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA, Barrick Gold Mine na Geita Gold Mines).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafunzo ya mujibu wa sheria, na kama ilivyoelezwa mwaka jana, 2013 mafunzo hayo yalirejeshwa kwa wahitimu wa Kidato cha Sita kuanzia mwezi Machi 2013. Mafunzo haya yaliendelea kutolewa ambapo jumla ya vijana 10,505 wameweza kuhitimu mafunzo hayo kipindi hiki. Kati yao, vijana 9,510 walihitimu mafunzo awamu ya pili iliyomalizika mwezi Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, ingawa mategemeo yalikuwa kuchukua idadi ya vijana 15,000 wajiunge na mafunzo awamu ya tatu, ni vijana 1,002 waliweza kujiunga na mafunzo hayo yaliyoanza mwezi Oktoba, 2013 hadi Januari, 2014, ambapo vijana 995 ndio waliohitimu. Kupatikana kwa idadi ndogo ya vijana wa awamu ya tatu na kutopatikana kabisa kwa vijana

wa awamu ya nne, kulitokana na vijana wengi kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu ambapo muhula wa masomo huanza mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za maendeleo hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ujumla haukuwa mzuri. Mafungu yote matatu yalipokea wastani wa asilimia 20.1 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa mapokezi hayo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeweza kutekeleza miradi ifuatayo:-

Mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 za makazi ya Wanajeshi, kulipia madeni ya kimkataba, kukarabati majengo pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi katika makambi na viteule vya JKT, ulipiaji fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi, kuboresha mawasiliano jeshini, ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi Kihangaiko, kulipia ujenzi wa viporo vya miradi ya maji Msangani na Ngerengere na ukarabati wa viteule vya Kasanga, Kalando na Hospitali ya Jeshi Lugalo, kuboresha miundombinu ya Shirika la Nyumbu na ununuzi wa malighafi kwa Shirika la Mzinga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara yangu iliiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, maandalizi ya ujenzi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya makazi ya askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania yamekamilika, ambapo ujenzi wa nyumba 6,064 za awamu ya kwanza ungeanza. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa nyumba hizo unaotekelezwa na Kampuni ya *Shanghai Construction (Group) General Company* ulianza rasmi tarehe 17 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi huo utakaofanyika katika vikosi 37 vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa utakuwa katika mikoa tisa kwa mgawanyo ufuatao:-

Arusha (792), Dar es Salaam (2,288), Dodoma (592), Kagera (144), Morogoro (616), Pemba (320), Pwani (840), Kigoma (160) na Tanga (312). Ujenzi huu utachukua muda wa miezi 50. Hadi sasa, ujenzi tayari umeanza kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambapo hatua ya ujenzi huo imefikia asilimia 80. Maandalizi ya ujenzi katika Mikoa ya Arusha, Morogoro, Pemba na Tanga unaotarajiwa kuanza mwezi Juni 2014 yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na azma yake ya kuimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa. Katika mwaka 2013/2014 Jeshi lilipokea zana na vifaa vya kisasa ambavyo vimeendelea kutumika katika shughuli za ulinzi na mafunzo.

Nisingependa kuwachosha Waheshimiwa Wabunge katika eneo hili kwani mwenye macho alijionea mwenyewe yaliyojiri siku ya kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano tarehe 26 Aprili, 2014. Kwa yule ambaye hakubahatika kuyaona, ni imani yangu kuwa alisimuliwa. Mpango wa ununuzi wa zana za kisasa na bora ni endelevu, hivyo natarajia Bunge lako Tukufu litaendelea kuidhinisha fedha za kutekeleza mpango huo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (SUMA JKT) linaendelea kutekeleza majukumu yake kupitia Idara zake za uhandisi na ujenzi, viwanda na kilimo, biashara na utalii. Utekelezaji wa shughuli hizi unalenga katika kuhakikisha kuwa SUMA JKT inafanikisha malengo iliyojiwekea kwa tija na ufanisi mkubwa. Katika kutekeleza azma ya kujitosheleza kwa chakula, mwaka 2013/2014 SUMA JKT lilifanikiwa kulima ekari 4,390 za mazao mbalimbali ya chakula na ekari 1,913 za mbegu bora. Tatizo linaloendelea kulikabili SUMA JKT katika eneo hili ni kutokulipwa madeni. Hadi sasa jumla ya Sh. 495,792,000/= hazijalipwa na

makampuni yaliyouziwa mbegu hizo. Makampuni hayo ni Agricultural Seed Agency, Tropical Seed Co. Ltd na Southern Highland Seed Growers Ltd.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT kupitia National Service Construction Department inatekeleza miradi ya ujenzi wa majengo na barabara. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Jeshi la Kujenga Taifa limefanya mageuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha ujuzi wa wataalam, kuongeza matumizi ya zana na mitambo pamoja na kuimarisha uwezo wa Idara zake ili kujikita kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa majengo na barabara. Miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni ya ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali, Kihangaiko, ujenzi wa barabara kiwango cha lami Wilayani Chato, ujenzi wa barabara za ndani katika mgodi wa Tulawaka na ukarabati wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ulinzi wa mali za wananchi, SUMA JKT imejizatiti katika shughuli za ulinzi kupitia kampuni tanzu ya *SUMA JKT Guard Ltd*. Vijana wanaotoa huduma hii ni wale waliohitimu mafunzo ya JKT ambao sasa wanafikia idadi ya 1,668. Hadi sasa *SUMA JKT Guard Ltd* wameweza kupata zabuni ya kutoa huduma hiyo ya ulinzi kwa taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na binafsi, viwanda na migodi. Katika mwaka 2014/2015 Kampuni hii inatarajia kuajiri vijana 2,000 kuongeza idadi ya nguvukazi iliyopo na hivyo kupanua utoaji huduma hiyo katika Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya mwaka 2013/2014 kuhusiana na mradi wa matrekta, matrekta 1,558 na zana za kilimo zenye thamani ya Sh. 53,675,837,001/= ziliuzwa kwa mkopo kwa wadau mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Wilaya, vikundi vya uzalishaji mali, *SACCOS* na watu binafsi wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Marejesho ya mikopo hii hadi kufikia Machi, 2014 ni kiasi cha Sh. 26,162,374,328.96.

Baada ya mauzo ya awamu ya kwanza kukamilika, SUMA JKT bado limeendelea kutekeleza mradi wa uingizaji wa matrekta mengine pamoja na zana za kilimo. Hivi sasa yapo matrekta 197 aina ya New Holland na Farmtrac kwenye Kituo cha Mwenge. Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri za Wilaya, vikundi vya uzalishaji mali, *SACCOS* na watu binafsi wenye mkopo mnakumbushwa kurejesha mikopo yenu na mnahamasishwa kuja kununua matrekta mapya.

Mheshimiwa Spika, shughuli za msingi za Shirika la Mzinga na kampuni yake tanzu ya Mzinga Holdings zimeendelea kwa mafanikio. Uzalishaji wa mazao ya risasi na milipuko umeongezeka ikiwa ni pamoja na kupata masoko mapya ya mazao hayo nje ya nchi. Aidha, katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki, Shirika la Mzinga limeteuliwa kuwa *Centre of Excellence*. Kwa upande wa Mzinga Holdings shughuli zake zimejikita katika ujenzi na ukarabati wa majengo na uendeshaji wa maduka ya kuuza bidhaa zisizolipiwa kodi (Duty Free Shops) kwenye vikosi na makambi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafiti katika Shirika la Nyumbu hazikuwa na mafanikio makubwa kutokana na kutopatikana kwa fedha za maendeleo. Hivyo tafiti zinazohusiana na mitambo ya kuchuna mkonge, engine na gear box za matrekta madogo na uzalishaji wa vipuri vya mashine (prototype) na pampu ya umwagiliaji hazikukamilika. Hata hivyo, shughuli za uzalishaji vipuri mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa vipuri vya Shirika la Reli hususan brake blocks zimeendelea.

Aidha, Shirika limeendelea kutoa huduma ya kutengeneza pampu za maji za *DAWASCO* na pia kuhusika katika ufungaji na ukarabati wa vifaa vinavyotumiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa ajili ya Ulinzi wa Amani huko Darfur - Sudan, Lebanon na Mashariki

mwa *DRC*. Miongoni mwa vifaa vilivyofanyiwa ukarabati na Nyumbu ni magari ya kubebea mizigo, maji, mafuta na askari.

Mheshimiwa Spika, Aidha, uzalishaji na upatikanaji wa Powered Brick making machine, mashine za kusaga na kukoboa nafaka unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ukarabati na uboreshaji wa mawasiliano Jeshini imeendelea kutekelezwa. Awamu ya kwanza ya mradi wa uboreshaji wa mawasiliano ndani ya vikosi imekamilika katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kazi ya uboreshaji wa mawasilianao ndani ya vikosi vilivyo nje ya Mkoa wa Dar es Salaam haijafanyika kutokana na kutokupatikana kwa fedha za maendeleo. Hivyo utekelezaji wa kazi hiyo pamoja na awamu ya pili ya kuunganisha mfumo wa Satellite utategemeana na upatikanaji wa fedha. Zoezi la kusimika minara ya mawasiliano huru na salama nchi nzima linaendelea.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uvamizi wa maeneo ya Jeshi bado linaendelea kujitokeza. Katika kipindi hiki maeneo yaliyoathirika na tatizo hilo ni pamoja na Tondoroni – Pwani, Tanganyika Packers na Monduli –Arusha, Kimbiji – Dar es Salaam, Chita – Morogoro, Itaka na Uyole – Mbeya, Uwanja wa Ndege na Ilemela – Mwanza na Kisakasaka - Unguja. Pamoja na hatua zinazochukuliwa zikiwemo za kisheria, nawasihi wananchi wasivamie maeneo ya Jeshi wala kuendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia, katika mwaka 2013/2014 Wizara imekamilisha kulipa fidia katika maeneo yafuatayo:-

Mwakidila (Tanga), Cheyo (Tabora), Mwantini (Shinyanga) na Mataya Kiromo (Pwani). Mipango yetu ya kulipa fidia katika maeneo mengine yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi inaendelea. Aidha, maeneo tunayoyalenga kulipa fidia katika mwaka 2014/2015 ni ya Makambako (Njombe), Ilemela na Kigongo Ferry (Mwanza). Zoezi la kupima na kuweka alama za mipaka, mabango na buffer zones linaendelea.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni ya Wizara kuidhinishiwa kiwango kidogo cha bajeti ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2013/2014 wakati mahitaji halisi kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara yalikuwa ni Sh. 1,741,888,249,500/=, bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh. 1,102,999,529,000/= sawa na asilimia 63.3 ya mahitaji. Hali hiyo imepelekea utekelezaji wa shughuli za Wizara hususan shughuli za maendeleo kutofikia malengo yaliyokusudiwa. Baadhi ya shughuli zilizoathirika ni za uboreshaji wa viwanda, utafiti na uzalishaji wa bidhaa za kijeshi, kulipia huduma na mahitaji muhimu kama vile mafuta, maji na umeme. Hali hiyo imesababisha Wizara kulimbikiza madeni makubwa ya kimkataba. Kwa upande wa matumizi ya kawaida, changamoto hii imesababisha ongezeko kubwa la madeni yakiwemo ya Wazabuni na ya Taasisi zinazotoa huduma muhimu za maji, umeme na simu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayoikabili Wizara ni mtiririko wa fedha kutoka Hazina kutozingatia mpango kazi wa Wizara, ambapo fedha zinapoidhinishwa, hutolewa zikiwa pungufu na bila kuzingatia ratiba ya mikataba. Hali hii imesababisha shughuli za Wizara hususan za maendeleo kutotekelezwa kama ilivyopangwa. Matokeo yake ni kuwa, Wizara imeshindwa kukamilisha ujenzi wa majengo na miundombinu katika makambi, kushindwa kulipa mikopo mbalimbali ukiwemo wa NSSF wa kushindwa kulipa malipo ya kimkataba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2014/2015 umekusudia kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika kutekeleza majukumu ya Ulinzi wa Taifa kulingana na dira, dhima na malengo ya Wizara. Vilevile, mpango umelenga kuimarisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Mujibu wa Sheria na wale wa kujitolea. Aidha, Wizara inakusudia kukamilisha miradi inayoendelea na kulipa madeni ya kimkataba. Hivyo, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kununua vifaa na zana za kijeshi ikiwemo vifaa vya uhandisi wa medani na ndege vita;

(ii) Kuanza ujenzi wa gati katika Kamandi ya Jeshi la Wanamaji;'

(iii) Kuboresha mifumo ya mawasiliano ya ndani na nje ya vikosi na Makambi ya Jeshi;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa nyumba 6,064 kwa ajili ya makazi ya wanajeshi;

(v) Kukamilisha ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi– Kihangaiko Pwani na Chuo cha Ukamanda na Unadhimu – Tengeru Arusha'

(vi) Kuboresha viwanda vya Mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

(vii) Kulipa mkopo wa NSSF wa ujenzi wa nyumba za makazi ya wanajeshi;

(viii) Upimaji na ulipaji wa fidia ya ardhi katika maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi;

(ix) Kuanza ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi huko Mataya - Kiromo Pwani;

(x) Ujenzi na umaliziaji wa viporo vya nyumba, bwalo na bweni huko Pemba;

(xi) Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha na zana pamoja na kuboresha mawasiliano;

(xii) Kulipia gharama za matumizi ya mahitaji muhimu ya umeme, maji, simu na huduma za uendeshaji wa majukumu ya kimsingi;

(xiii) Kulipia stahili mbalimbali za wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa Umma;

(xiv) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na ulinzi;

(xv) Kulipa madeni ya kimkataba;

(xvi) Kuongeza uwezo wa makambi ya JKT kuweza kuchukua idadi kubwa ya vijana kwa wakati mmoja; na

(xvii) Kupanua wigo wa makundi ya vijana wa kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee na kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kuwasilisha salamu za pongezi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa wanajeshi wote kwa kufanikisha miaka 50 ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kazi walioifanya ni kubwa na waliifanikisha kwa uweledi, utii, uhodari, ujasiri na kwa kishindo cha hali ya juu. Ushiriki wao huo umeudhihirishia Umma wa Watanzania na ulimwengu kwa ujumla kuwa Jeshi letu ni imara, shupavu na lipo tayari kulinda, kutetea na kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia na kwa niaba ya wanajeshi wote, namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, hiba yake ya Uongozi ushupavu, uvumilivu na maridhiriano, itakumbukwa na kuenziwa na vizazi kwa vizazi hususan kwetu sisi wenye dhamana ya ulinzi wa nchi yetu. Ahadi yetu kwake ni kuwa tutaendelea kusimama imara, kupokea na kutii amri na maelekezo yake bila hila yoyote na kutoyumbishwa na kauli potovu za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka 2014/2015, vyanzo vya mapato ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake bado ni vidogo. Chanzo kikuu cha mapato kwa Wizara ya Ulinzi na JKT na Taasisi zake kimeendelea kutegemea uuzaji wa nyaraka za zabuni. Hivyo, makadirio ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kukusanya mapato yenye jumla ya Sh. 60,506,000/= kwa mchanganuo ufuatao:-

Fungu 38 – NGOME	= Sh.	2,001,000.00
Fungu 39 – JKT	= Sh.	48,503,000.00
Fungu 57 – Wizara	= Sh.	10,002,000.00
Jumla	= Sh.	60,506,000.00

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2014/2015 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 1,269,076,056,000/= ambazo kati yake Sh. 1,020,076,056,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 249,000,000,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa kuzingatia mafungu ya Wizara ni ifuatao:-

FUNGU 38 – NGOME

Matumizi ya Kawaida	Sh.	803,542,549,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh.	12,000,000,000.00
Jumla ya Makadirio kwa Fungu 38	Sh.	815,542,549,000.00

FUNGU 39 JKT

Matumizi ya Kawaida	Sh.	6,822,661,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh.	7,000,000,000.00
Jumla ya Makadirio kwa Fungu 39	Sh.	203,822,661,000.00

FUNGU 57 WIZARA YA ULINZI

Matumizi ya Kawaida	Sh.	19,710,846,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh.	230,000,000,000.00
Jumla ya Makadirio kwa Fungu 57	Sh.	249,710,846,000.00

hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo imeonyeshwa hapo na ninaomba Hansard iingine yale yote ambayo katika kitabu changu cha hotuba kwa sababu mengi niliyapunguza ili kukidhi muda. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani. Sasa nitamwita Mwenyekiti aliyeshughulikia Wizara hii, au Makamu wake, mwakilishi wake Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 99(9) na Kifungu cha 117(11), Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa linajumuisha mafungu matatu yafuatayo: Wizara ya Ulinzi – Fungu 57, Ngome - Fungu 38 na Jeshi la Kujenga Taifa – Fungu 39.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 3 Mei, 2014 Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Alli Mwinyi. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ushauri iliyoutoa kwa Wizara wakati wa kupitisha makadirio na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014; Kamati yangu ilitoa ushauri na maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wa Wizara hii ili kuhakikisha inatimiza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.
Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilionesha kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ulizingatiwa na kwamba mambo yaliyotolewa ushauri baadhi yametekelezwa na mengine utekelezaji wake bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati.Moja, Kamati ilitoa ushauri kwamba Serikali itenge fedha kuwezesha Wanajeshi wote wanaotarajia kustaafu kupata stahili zao na kuwarejesha makwao mara wanapostaafu.Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2013/2014 kiasi cha Shilingi bilioni 4.6 kiliidhinishwa kwa ajili hii. Hata hivyo, baada ya Kamati hii kutoa ushauri, fedha ziliongezwa hadi kufikia Sh. 6,133,000,000/= ambazo Kamati imejulishwa kuwa zimepatikana zote na wanajeshi wote waliostaafu wamehudumiwa ipasavyo. Ushauri wa pili wa Kamati ulikuwa Serikali itumie samani zilizotengenezwa na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeshaagiza samani zote katika Ofisi za Serikali zinunuliwe ndani ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ulinzi inanunua samani zake kutoka mashirika ya Mzinga na JKT.Tatu, ushauri wa tatu ulikuwa ongezeko la Shilingi milioni 22.8 lipelekwe kwenye Kasma 227500 inayohusu upimaji ardhi na ulipaji wa fidia wa ardhi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Hazina walikubali mapendekezo hayo na fedha zilihamishwa kama ilivyoelekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa nne ulikuwa kwamba Serikali iongeze muda wa mafunzo ya JKT kwa vijana wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria kutoka miezi mitatu ya sasa hadi miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeeleza kwamba pendekezo hili limeanza kufanyiwa kazi lakini hadi sasa utekelezaji umekuwa mgumu kwa vile Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imebadili muhula wa masomo kwa wanafunzi wa Kidato cha VI, ambao sasa watamaliza masomo mwezi Mei ya kila mwaka na kujiunga na Vyuo Vikuu mwezi Oktoba. Kwa hiyo, kwa utaratibu huu muda wa mafunzo ya JKT hautazidi miezi minne.

Tano, Kupata mafunzo ya JKT na JKU iwe ni moja ya vigezo muhimu kwa vijana watakaoajiriwa katika vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama (JWTZ, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Usalama wa Taifa). (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara imeeleza kwamba ushauri huu wa Kamati uliwekewa uzito na agizo la Amiri Jeshi Mkuu kwamba vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama viajiri vijana waliomaliza mafunzo ya JKT. Tayari JWTZ, Polisi, Magereza, Zimamoto na Usalama wa Taifa wameanza kutekeleza agizo hili kwa viwango tofauti.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa sita, Kamati iliishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iratibu na kuzielekeza Wizara husika na uwekaji wa alama za mipaka ya nchi kuweka mikakati ya pamoja ya kurudisha alama za mipaka zilizoharibiwa au kung'olewa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara imeeleza kwamba zoezi la kurudisha alama za mipakani limeanza kufanyika kwenye mpaka wetu na Kenya maeneo ya Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, uhauri wa sita, ulihusu miradi wa nyumba za Wanajeshi. Kamati ilisisitiza kwamba mpango wa ujenzi wa nyumba 10,000, na hasa zile 6,064 za awamu ya kwanza mgao wake kwa vikosi vyote Kimkoa uwe wazi. Aidha, mpango wa ujenzi wa nyumba 3,936 za awamu ya pili maandalizi yaanze mapema.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara ilieleza kwamba ujenzi wa nyumba 6,064 za awamu ya kwanza, umeanza na zimesambazwa katika Vikosi 37 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Morogoro, Pemba, Pwani, Kigoma na Tanga.Ujenzi umeanzia Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambayo kazi imefikia 80%. Mwezi Juni, 2014 ujenzi utaanza katika Mikoa ya Tanga, Pemba, Arusha, Dodoma na Morogoro. Mapema mwakani ujenzi utaanza Mkoa wa Kigoma na Kagera. Kuhusu ujenzi wa nyumba 3,936 za awamu ya pili, maandalizi yameanza kwa kuanzisha mchakato wa kutafuta fedha za kugharamia kazi hii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa nane ulikuwa Serikali iongeze juhudi katika kuondoa na kuzuia mambo yanayotishia usalama wa nchi yetu hasa uhamiaji haramu ambao ni moja ya vyanzo vya kuzagaa kwa silaha nchini. Kamati iliitaka Serikali ichukue hatua za haraka kudhibiti wahamiaji haramu wanaojipenyeza mipakani ili kudumisha amani na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Serikali inaeleza kuwa, kwa jumla hali ya ulinzi na usalama mipakani ni shwari, na kwamba operesheni mbalimbali zimefanyika ikiwemo operesheni Kimbunga kwa lengo la kuwabaini na kuwaondoa nchini wahamiaji haramu. Vilevile vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinashirikiana kudhibiti hali ya ulinzi mipakani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tisa ulikuwa Shirika la *SUMA JKT GUARD Ltd* litumike kufanya kazi ya ulinzi wa mabenki na baadhi ya makazi ya Viongozi ili kutoa nafasi kwa Jeshi la Polisi kushughulikia majukumu mengine ya kulinda maisha na mali za raia.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji imeeleza kwamba *SUMAJKT Guard Ltd* ilipata zabuni za ulinzi Taasisi mbalimbali zikiwemo: *TANESCO, CRDB, Bank of Africa, UDOM, Ferry Kigamboni, TPDC, Mpiga* Chapa Mkuu wa Serikali, Wizara za:-

Fedha, Maliasili na Mambo ya Nje, pia Bomba la Gesi, Mamlaka ya Hali ya Hewa na ujenzi wa barabara ya Namtumbo Songea.Juhudi za kuliimarisha Shirika hili kutanua huduma zake zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika utekelezaji wa kazi mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

Moja, ni ufinyu wa Bajeti. Hali ya ufinyu wa bajeti imeendelea kuwa tatizo kwa Wizara hii. Tatizo hili linafanya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kuwa ngumu na kutofanikisha malengo. Aidha, fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitoki zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni madeni ya wazabuni. Tatizo la madeni la wazabuni limekuwa sugu miongoni mwa Majeshi yetu hapa nchini. Kumekuwa na madeni ya muda mrefu. Mfano Kamati ilifahamishwa ya kuwa Wizara inadaiwa fedha kwa ajili ya umeme na maji. Pamoja na ahadi ya Hazina kulipa madeni hayo, lakini utekelezaji bado unasuasua.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu ni kusahaulika kwa barabara za mipakani. Barabara za mipakani zimesahaulika kufanyiwa matengenezo na baadhi zimeanza kupotea. Hali hii inasababisha kazi ya ulinzi mipakani kuwa ngumu kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vyenye dhamana ya ulinzi mipakani. Suala la barabara za mpakani ni muhimu sana kiulinzi na kiuchumi. Katika Taarifa ya Kamati hii katika Bunge hili la Desemba, 2013, Kamati ilishauri Serikali kwamba fedha za kukarabati barabara za ulinzi mipakani wapewe JWTZ kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara hizi. Lakini hadi sasa ushauri huo haujafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nne ni uvamizi wa Maeneo ya Jeshi. Maeneo ya Vikosi vya Jeshi sehemu mbalimbali hapa nchini yamekuwa yanavamiwa na watu mbalimbali katika kukabili tatizo hili. Mwaka 2013/2014 Bunge liliidhinisha Shilingi bilioni 22.8/= kwa ajili ya upimaji ardhi ya Jeshi na ulipaji wa fidia. Kamati inazidi kusisitiza kwamba Serikali itenge kila mwaka fedha kwa ajili ya upimaji ardhi ya Jeshi na kuwalipa fidia wananchi wanaolazimika kuhama katika maeneo yao ili kupisha shughuli za Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na uhaba wa makazi kwa ajili ya Wanajeshi katika vikosi vingi vya JWTZ na JKT katika Mikoa mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali

kwa kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 awamu ya kwanza kwa ajili ya Wanajeshi. Kamati iliridhika na ubora wa nyumba zilizoanza kujengwa Lugalo.

Mheshimiwa Spika, naomba hapa Hansard iondoe "na Kijitonyama." Ni Lugalo. Katika Kambi ya Lugalo.Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya JKT na JKU kuwa kigezo cha kujiunga na Vyombo vya Ulinzi na Usalama:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba utekelezaji wa kuajiri vijana waliohitimu JKT katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama umeshaanza, lakini utekelezaji wake bado hauridhishi kwani idadi ya vijana wanaochukuliwa na Jeshi la Polisi, Magereza na Zimamoto ni wachache. Kamati inazidi kushauri kwamba vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vinapoajiri vijana asilimia kubwa watoke JKT. Vile vile kwa miaka inayokuja, kigezo cha mafunzo ya JKT na JKU kije kutumika wakati wa kuajiri watumishi wa Serikali kwani watakuwa wamepata mafunzo ya ukakamavu, nidhamu, uzalendo na ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa makadiriao ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imetengewa jumla ya Sh. 1,269,076,056,000/=. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:- Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa: Jumla ya fedha zinazoombwa ni Sh .249,710,846,000/=. Kati yake Sh.19,710,846,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida, Sh. 230,000,000,000/= zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fungu - 38 Ngome: Jumla ya fedha zinazoombwa ni Sh. 815,542,549,000/= kati yake Sh. 803,542,549,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shs.12,000,000,000/= zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. - Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa: Jumla ya fedha zinazoombwa ni Sh. 203,822,661,000/= kati yake Sh.196,822,661,000/= ni kwa matumizi ya kawaida, na Sh. 7,000,000,000/= zinaombwa kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya kamati ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara hii na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa nchi yetu, na hivyo kudumisha amani, utulivu na umoja wetu. Aidha, Kamati inapongeza Majeshi yetu yote kwa kufanikisha Sherehe za Muungano. Sherehe hizo zilifana na kuwahakikishia Watanzania kuwa nchi yetu ipo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 3 Mei, pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama yalivyoainishwa kwa kila kifungu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya Wizara hii na hasa kwa kuzingatia wao ndio walinzi wa mipaka yetu; Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote na kwa wakati, zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakumbushwa kuwa Jeshi linahitaji kuendelea kufanya mazoezi ya kijeshi wakati wa amani, kwani upo msemo wa Kijeshi usemao: "Toa jasho wakati wa amani ili kupunguza damu wakati wa vita". Vile vile Jeshi linahitaji kutoa mafunzo kwa Wanajeshi wapya, pamoja na wa zamani hivyo fedha zinahitajika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati inashauri na kusisitiza kwamba Serikali kila mwaka itenge fedha za kutosha kuliwezesha Jeshi na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kusimamia amani na utulivu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa HAZINA imeahidi kuwa mwaka wa fedha 2014/2015 italipa madeni yote ya vyombo vya Ulinzi na Usalama, na kwamba havitaanza na bajeti yenye madeni, Kamati inasisitiza kwamba azma hiyo itekelezwe kwa ukamilifu. Aidha, madeni yote ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo yamekwishahakikiwa yalipwe ili Wizara ianze bajeti mpya bila kuwa na madeni ya miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa hivi sasa hakuna Taasisi maalum ya kukarabati barabara za ulinzi mipakani, Kamati inazidi kuikumbusha Serikali kwamba jukumu hilo wakabidhiwe JWTZ kwani wana zana na utaalam, wanachohitaji ni fedha. Kwa hiyo, Kamati inashauri fedha za matengenezo ya barabara za mipakani zipewe Wizara hii ili iweze kuzifanyia matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Jeshi linahitaji maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali mfano maeneo ya mazoezi, Kamati inashauri Wizara ianzishe Kitengo maalum cha kusimamia ardhi ya Jeshi. Kitengo hiki kitakuwa na shughuli maalum ya kuhakikisha kuwa maeneo ya Jeshi yanapimwa na yanapata hati miliki na pia hayavamiwi hovyo na wananchi na maeneo hayo ya Jeshi yanaendelezwa kwa manufaa ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi unaotekelezwa wa awamu ya kwanza, ujenzi wa nyumba 10,000, bado Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya askari. Aidha, ujenzi wa mahanga kwa ajili ya Askari kapera katika makambi mbalimbali nao uanze.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wahitimu wa JKT kutoajiriwa kwa wingi kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama, Kamati inashauri kwamba agizo la Amiri Jeshi Mkuu kwamba vyombo vya Ulinzi na Usalama viajiri vijana kutoka JKT litekelezwe kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kupokea taarifa ya Serikali kwamba mafunzo kwa vijana kwa mujibu wa Sheria yatolewe kwa muda wa angalau miezi sita, kushindikana kutekelezwa kutokana na mabadiliko ya mihula ya Kidato cha Sita; bado Kamati inazidi kuisisitiza Serikali iwezeshe mafunzo kwa vijana wote wanaohitimu Kidato cha Sita wajiunge na JKT; na kwamba vijana ambao hawataripoti kwa mafunzo bila ya sababu za msingi, Serikali iwachukulie hatua kwa vile wanavunja sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa Chuo cha Unadhimu *(Staff Command College)* kule Duluti unasua sua kawa miaka mingi na hivyo kusababisha Chuo hicho kukosa majengo, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kila mwaka ili kuharakisha kukamilika kwa majengo ya Chuo hiki muhimu kwa Ulinzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi na wasaidizi wake kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki katika ziara za Kamati Mikoani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa mara ambao umekuwa ukiisaidia Wizara hii kufanya maboresho ya utendaji kazi wake. Aidha, Kamati hii inapenda kutambua uteuzi na inatoa pongezi kwa Mjumbe kutoka Kamati yetu Mheshimiwa Masoud

Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kwa kuteuliwa kuwa Waziri kivuli wa Wizara hii. Kamati hii inapenda kutoa pongezi nyingi kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Na sisi tunampongeza kwa kupanda cheo. *(Makofi/Kicheko)*

Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyowasilishwa Mezani

1.0 Utangulizi:Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu 99(9) na 117(11), Toleo la April 2013, naomba kuwasilisha katika Bunge lako tukufu Taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa linajumuisha mafungu matatu yafuatayo:- Wizara ya Ulinzi Fungu 57,Ngome Fungu 38 na Jeshi la Kujenga Taifa Fungu 39.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 3 Mei, 2014 Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi. Aidha Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ushauri iliyoutoa kwa Wizara wakati wa kupitisha makadirio na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014:

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilitoa ushauri na maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji wa Wizara hii ili kuhakikisha inatimiza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mhe. Waziri ilionesha kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ulizingatiwa na kwamba mambo yaliyotolewa ushauri baadhi yametekelezwa na mengine utekelezaji wake bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati.

2.1 Serikali itenge fedha kuwawezesha Wanajeshi wote wanaotarajia kustaafu kupata stahili zao na kuwarejesha makwao mara wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2013/2014 kiasi cha shilingi billion 4.6 kiliidhinishwa kwa ajili hii, hata hivyo baada ya Kamati hii kutoa ushauri, fedha ziliongezwa hadi kufikia sh. 6,133,000,000 ambazo Kamati imejulishwa kuwa zimepatikana zote na Wanajeshi wote waliostaafu wamehudumiwa ipasavyo.

2.2 Serikali itumie samani zilizotengenezwa na Jeshi la Kujenga Taifa:

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeshaagiza samani zote katika ofisi za Serikali zinunuliwe ndani ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ulinzi inanunua samani zake kutoka mashirika ya Mzinga na JKT.**2.3 Ongezeko la shilingi milioni 22.8 lipelekwe kwenye Kasma 227500 inayohusu upimaji ardhi na ulipaji wa fidia wa ardhi ya Jeshi. Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Hazina walikubali mapendekezo hayo na fedha zilihamishwa kama ilivyoelekezwa na Kamati.
2.4 Kwamba Serikali iongeze muda wa mafunzo ya JKT kwa vijana wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria kutoka miezi mitatu ya sasa hadi miezi sita.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeeleza kwamba pendekezo hili limeanza kufanyiwa kazi lakini hadi sasa utekelezaji umekuwa mgumu kwa vile Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imebadili muhula wa masomo kwa wanafunzi wa Kidato cha 6, ambao sasa watamaliza masomo mwezi Mei ya kila mwaka na kujiunga na Vyuo vikuu mwezi Oktoba, kwa hiyo kwa utaratibu huu muda wa mafunzo ya JKT hautazidi miezi 4.

2.5 Kupata mafunzo ya JKT na JKU iwe ni moja ya vigezo muhimu kwa vijana watakaoajiriwa katika vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama (JWTZ, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Usalama wa Taifa).

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara imeeleza kwamba ushauri huu wa Kamati uliwekewa uzito na agizo la Amiri Jeshi Mkuu kwamba vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama viajiri vijana waliomaliza mafunzo ya JKT. Tayari JWTZ, Polisi, Magereza, Zimamoto na Usalama wa Taifa wameanza kutekeleza agizo hili kwa viwango tofauti.

2.6 Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iratibu na kuzielekeza Wizara husika na uwekaji wa alama za mipaka ya nchi kuweka mikakati ya pamoja ya kurudisha alama za mipaka zilizoharibiwa au kung'olewa.Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara imeeleza kwamba zoezi la kurudishia alama za mipakani limeanza kufanyika kwenye mpaka wetu na Kenya maeneo ya Mkoa wa Mara.

2.7 Kuhusu Mradi wa nyumba za Wanajeshi, Kamati ilisisitiza kwamba mpango wa ujenzi wa nyumba 10,000, na hasa zile 6,064 za awamu ya kwanza mgao wake kwa vikosi vyote Kimkoa uwe wazi. Aidha mpango wa ujenzi wa nyumba 3,936 za awamu ya pili maandalizi yaanze mapema.
Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara ilieleza kwamba ujenzi wa nyumba 6,064 za awamu ya kwanza, umeanza na zimesambazwa katika vikosi 37 katika Mikoa ya Arusha **(792),** Dar es Salaam **(2,288),** Dodoma **(592),** Kagera **(144),** Morogoro (**616),** Pemba (**320),** Pwani **(840),** Kigoma **(160)** na Tanga **(312).**Ujenzi umeanzia Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambayo kazi imefikia 80%, Mwezi Juni 2014 ujenzi utaanza katika Mikoa ya Tanga, Pemba, Arusha, Dodoma na Morogoro. Mapema mwakani ujenzi utaanza Mkoa wa Kigoma na Kagera.Kuhusu ujenzi wa nyumba 3,936 za awamu ya pili, maandalizi yameanza kwa kuanzisha mchakato wa kutafuta fedha za kugharamia kazi hii.

2.8 Serikali iongeze juhudi katika kuondoa na kuzuia mambo yanayotishia usalama wa nchi yetu hasa uhamiaji haramu ambao ni moja ya vyanzo vya kuzagaa kwa silaha nchini. Kamati inaitaka Serikali ichukue hatua za haraka kudhibiti wahamiaji haramu wanaojipenyeza mipakani ili kudumisha amani na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Serikali inaeleza kuwa, kwa jumla hali ya ulinzi na usalama mipakani ni shwari, na kwamba operesheni mbalimbali zimefanyika ikiwemo operesheni Kimbunga kwa lengo la kuwabaini na kuwaondoa nchini wahamiaji haramu. Vilevile vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinashirikiana kudhibiti hali ya ulinzi mipakani.

2.9 Shirika la SUMA JKT GUARD Ltd litumike kufanya kazi ya ulinzi wa mabenki na baadhi ya Makazi ya Viongozi ili kutoa nafasi kwa Jeshi la Polisi kushughulikia majukumu mengine ya kulinda maisha na mali za raia.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji imeeleza kwamba SUMAJKT Guard Ltd ilipata zabuni za ulinzi Taasisi mbalimbali zikiwemo: TANESCO, CRDB, Bank of Africa, UDOM, Ferry Kigamboni, TPDC, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Wizara za:- Fedha, Maliasili na Mambo ya Nje, pia Bomba la Gesi, Mamlaka ya Hali ya Hewa na ujenzi wa barabara ya Namtumbo Songea.Juhudi za kuliimarisha Shirika hili kutanua huduma zake zinaendelea.

3.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KATIKA UTEKELEZAJI WA KAZI 2013/2014:

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake, baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

3.1 Ufinyu wa Bajeti:

Mheshimiwa Spika, Hali ya ufinyu wa bajeti imeendelea kuwa tatizo kwa Wizara hii. Tatizo hili linafanya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kuwa ngumu na kutofanikisha malengo. Aidha fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitoki zote na kwa wakati.

3.2 Madeni ya Wazabuni:

Mheshimiwa Spika, tatizo la madeni ya wazabuni limekuwa sugu miongoni mwa Majeshi yetu hapa nchini. Kumekuwa na madeni ya muda mrefu mfano Kamati ilifahamishwa ya kuwa Wizara inadaiwa fedha kwa ajili ya umeme na maji. Pamoja na ahadi ya HAZINA kulipa madeni hayo lakini utekelezaji unasuasua.

3.3 Kusahaulika kwa Barabara za Mipakani:

Mheshimiwa Spika, barabara za mipakani zimesahaulika kufanyiwa matengenezo na baadhi zimeanza kupotea hali hii inafanya kazi ya kufanya kazi za ulinzi mipakani kuwa ngumu kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vyenye dhamana ya ulinzi mipakani. Suala la barabara za mpakani ni muhimu sana kiulinzi na kiuchumi. Katika Taarifa ya Kamati hii katika Bunge hili ya Desemba 2013, Kamati ilishauri Serikali kwamba fedha za kukarabati barabara za ulinzi mipakani wapewe JWTZ kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara hizi, lakini hadi sasa ushauri huo haujafanyiwa kazi.

3.4 Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi:

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Vikosi vya Jeshi sehemu mbalimbali hapa nchini yamekuwa yanavamiwa na watu mbali mbali. Katika kukabili tatizo hili Mwaka 2013/2014 Bunge liliidhinisha shilingi bn. 22.8/= kwa ajili ya upimaji ardhi ya Jeshi na ulipaji wa fidia. Kamati inazidi kusisitiza

kwamba Serikali itenge kila mwaka fedha kwa ajili ya upimaji ardhi ya Jeshi na kuwalipa fidia wananchi wanaolazimika kuhama katika maeneo yao ili kupisha shughuli za Jeshi.

3.5 Uhaba wa Makazi :Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na uhaba wa makazi kwa ajili ya Wanajeshi katika vikosi vingi vya JWTZ na JKT katika Mikoa mbalimbali. Hata hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 awamu ya kwanza kwa ajili ya Wanajeshi. Kamati iliridhika na ubora wa nyumba zilizoanza kujengwa Lugalo na Kijitonyama.

3.6 Mafunzo ya JKT na JKU kuwa kigezo cha kujiunga na Vyombo vya Ulinzi na Usalama:

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba utekelezaji wa kuajiri vijana waliohitimu JKT katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama umeshaanza, lakini utekelezaji wake bado hauridhishi kwani idadi ya vijana wanaochukuliwa na Polisi, Magereza na Zimamoto ni wachache. Kamati inazidi kushauri kwamba vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vinapoajiri vijana asilimia kubwa watoke JKT. Vilevile kwa miaka inayokuja kigezo cha mafunzo ya JKT na JKU kije kutumika wakati wa kuajiri watumishi wa Serikali kwani watakuwa wamepata mafunzo ya ukakamavu, nidhamu, uzalendo na ulinzi wa Taifa.

4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIAO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015:

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imetengewa jumla ya **Shs.1,269,076,056,000/=.** Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:- **Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa :**Jumla ya fedha zinazoombwa ni **Shs.249,710,846,000/=.** Kati yake **Shs.19,710,846,000/=** zinaombwa kwa matumizi ya kawaida, **sh.230,000,000,000/=** zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. **Fungu - 38 Ngome:** Jumla ya fedha zinazoombwa ni Shs. **815,542,549,000/=** kati yake **Shs.803,542,549,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shs.12,000,000,000/=** zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. **Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa:** Jumla ya fedha zinazoombwa ni **Shs. 203,822,661,000/=** kati yake **Shs.196,822,661,000** ni kwa matumizi ya kawaida, na **Shs.7,000,000,000** zinaombwa kwa miradi ya maendeleo.

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI:

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara hii na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa nchi yetu, na hivyo kudumisha amani, utulivu na umoja wetu. Aidha Kamati inapongeza Majeshi yetu yote kwa kufanikisha Sherehe za Muungano. Sherehe hizo zilifana na kuwahakikishia Watanzania kuwa nchi yetu ipo salama.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 3 Mei, pamoja na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama yalivyoainishwa kwa kila fungu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

5.1 Kuhusu Ufinyu wa Bajeti:

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya Wizara hii na hasa kwa kuzingatia wao ndio walinzi wa mipaka yetu; Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote na kwa wakati, zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka.
Mheshimiwa Spika, Serikali inakumbushwa kuwa Jeshi linahitaji kuendelea kufanya mazoezi ya kijeshi wakati wa amani kwani upo msemo wa Kijeshi usemao "Toa jasho wakati wa amani ili

kupunguza damu wakati wa vita". Vile vile Jeshi linahitaji kutoa mafunzo kwa Wanajeshi wapya, pamoja na wa zamani hivyo fedha zinahitajika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake. Hivyo Kamati inashauri na kusisitiza kwamba Serikali kila mwaka itenge fedha za kutosha kuliwezesha Jeshi na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kusimamia amani na utulivu nchini.

5.2 Madeni:

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa HAZINA imeahidi kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 italipa madeni yote ya vyombo vya Ulinzi na Usalama, na kwamba havitaanza na bajeti yenye madeni, Kamati inasisitiza kwamba azma hiyo itekelezwe kwa ukamilifu. Aidha madeni yote ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo yamekwisha hakikiwa yalipwe ili Wizara waanze bajeti mpya bila kuwa na madeni ya miaka ya nyuma.

5.3 Matengenezo ya Barabara za Ulinzi wa Mipakani:

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa hivi sasa hakuna taasisi maalum ya kukarabati barabara za ulinzi mipakani Kamati inazidi kuikumbusha Serikali kwamba jukumu hilo wakabidhiwe JWTZ kwani wana zana na utaalam wanachohitaji ni fedha. Kwa hiyo Kamati inashauri fedha za matengenezo ya barabara za mipakani zipewe Wizara hii ili iweze kuzifanyia matengenezo.

5.4 Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi:

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Jeshi linahitaji maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali mfano maeneo ya mazoezi. Kamati inashauri Wizara ianzishe kitengo maalum cha kusimamia ardhi ya Jeshi. Kitengo hiki kitakuwa na shughuli maalum ya kuhakikisha kuwa maeneo ya Jeshi yanapimwa na yanapata hati miliki na pia hayavamiwi hovyo na wananchi na maeneo hayo ya Jeshi yanaendelezwa kwa manufaa ya Jeshi.

5.5 Uhaba wa Makazi:

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi unaotekelezwa wa awamu ya kwanza ujenzi wa nyumba 10,000, bado Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya askari. Aidha ujenzi wa mahanga kwa ajili ya Askari kapera katika kambi mbalimbali uanze.

5.6 Wahitimu wa JKT kutoajiriwa kwa wingi kwenye vyombo vya Ulinzi na Usalama:

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba agizo la Amiri Jeshi Mkuu kwamba vyombo vya Ulinzi na Usalama viajiri vijana kutoka JKT litekelezwe kwa ukamilifu.

5.7 Mafunzo ya JKT yatolewe Kwa Miezi Sita:

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kupokea taarifa ya Serikali kwamba mafunzo kwa vijana wa mujibu wa Sheria yatolewe kwa muda wa angalau miezi 6, kushindikana kutekelezwa kutokana na mabadiliko ya mihula ya kidato cha sita; bado Kamati inazidi kuisisitiza Serikali iwezeshe mafunzo kwa vijana wote wanaohitimu kidato cha 6 wajiunge na JKT; na kwamba

vijana ambao hawataripoti kwa mafunzo bila ya sababu za msingi, Serikali iwachukulie hatua kwa vile wanavunja sheria.

5.8 Kukamilisha Ujenzi wa Chuo cha Maafisa Wanadhimu – Duluti: Kwa kuwa ujenzi wa Chuo cha Unadhimu (Staff Command College) kule Duluti unasua sua kawa miaka mingi na hivyo kusababisha Chuo hicho kukosa majengo, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kila mwaka ili kuharakisha kukamilika kwa majengo ya Chuo hiki muhimu kwa Ulinzi wa Taifa letu.

6.0 HITIMISHO:

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na wasaidizi wake kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki katika ziara za Kamati Mikoani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa mara ambao umekuwa ukiisaidia Wizara hii kufanya maboresho ya utendaji kazi wake. Aidha Kamati hii inapenda kutambua uteuzi na inatoa pongezi kwa Mjumbe kutoka Kamati yetu Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb kwa kuteuliwa kuwa Waziri kivuli wa Wizara hii. Kamati hii inapenda kutoa pongezi kwake. Naomba niwatambue Wajumbe kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Anna Margreth Abdallah, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Muhamed Seif Khatib, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Brig. Gen (Rtd) Hassan Ngwilizi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Capt. (Rtd) John Zefania Chiligati, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mariam Mfaki, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mhe. Dr. Agustino Lyatonga Mrema, Mb- Mjumbe
7. Mhe. Cynthia Hilda Ngoye, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dkt. David Mciwa Mallole, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Eng. Stella Manyanya, Mb- Mjumbe
10. Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Musa H. Musa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Rahel Mashishanga Robert, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Hamad Ali Hamadi, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Vincent Nyerere, Mb-Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Charles Mloka, Ndugu Theonest Ruhilabake na ndugu Nesta Kawamala kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi taarifa hii ilipoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako tukufu, likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Anna M. Abdallah, (Mb)

MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA
14 Mei, 2014

SPIKA: Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, si ndio Masoud mwenyewe? Hongera sana. (Kicheko/Makofi)

Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na hii inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa ilitungwa tangu mwaka 1966 kwa madhumuni ya kuunda, kuendesha, kusimamia na kuhudumia Majeshi ya Ulinzi kulingana na majukumu yake. Kwa miaka kadhaa sasa Serikali imekuwa ikitoa ahadi nyingi Bungeni tangu mwaka 2008 kuwa ipo katika mchakato wa kuweza kurekebisha Sera na Sheria ulinzi wa Taifa ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Serikali kutoleta Bungeni kwa muda wa miaka saba sasa tangu Serikali ilipoahidi kuleta sera na mapitio ya Sheria hiyo kama ilivyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa suala la ulinzi na usalama ni suala la Muungano. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji na kutaka majibu ya Serikali juu ya namna Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kama nchi mshirika wa Muungano, ilivyoshirikishwa juu ya jambo hili katika kutoa maoni na mapendekezo kama ilivyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu ya taarifa za utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni ukurasa 377 hadi 379 ya Januari 2007 Serikali ilieleza jinsi gani imeweka mkakati wa upimaji wa maeneo ya jeshi na JKT na kuyapatia hati miliki zake na taratibu za kutoa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi na JKT.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kigugumizi cha Serikali kwa muda wa miaka kadhaa sasa kulidanganya Bunge na kuwadanganya wananchi kwa kutowapatia haki zao tangu mwaka 2007 yakibakia maandishi yasiyo na utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji mkakati wa Serikali wa kutoa fidia maeneo ya raia yaliyochukuliwa na jeshi kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Arusha ni Oldonyo Sambu na Tanganyika Packers 977KJ. Serikali hamjawailipa wananchi, walalamika. Je, ni lini wananchi hao watalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam - Kunduchi Transit Camp na Kunduchi Rifle Range, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi, Ubungo Kibangu, Mwenge TPDF flats, Keko TPDF flats na Magogoni. Katika maeneo haya Serikali hadi leo

hamjatoa fidia na ahadi zimekuwa ni nyingi na hivyo kupelekea malalamiko makubwa ya wananchi. Je ni lini fidia hizi zitatolewa?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma ni Makutupora JKT na Kombania ya Radar. Katika maeneo haya wananchi wamechoka kupewa ahadi hewa zisizo na majibu kwa miaka mingi sasa. Je ni lini fedha hizi mtawalipa?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera, ni Biharamuro na Mkoa wa Kigoma, ni Bulombora JKT; nako manung'uniko yamekuwa ni makubwa na Serikali imeahidi utekelezaji bila majibu hadi sasa. Je, kuna mpango wowote wa kuwalipa?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi ni Singino Radar; Mkoa Mara ni Rwamkoma JKT na Kiabakari, Buhemba JKT ambapo napo masikitiko yamezidi kiwango na wanahoji kuwa je, haya ndiyo malipo ya Serikali yao waliyoichagua kuthubutu kuwadhulumu?

Mheshimiwa Spika, Mkoa Morogoro ni Chita JKT na Ngerengere, wananchi wanauliza na kuhoji kuwa ni lini haki zao watazipata? Au mpaka watoto wa Marehemu nao wafariki dunia wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa Mtwara ni Umoja Camp, katika eneo hili pia ni kilio kisichoisha kwa wananchi kudai haki zao, wamekata tama. Je Serikali inaeleza nini juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma ni Mlale JKT na Tunduru TPDF; Mkoa wa Rukwa ni Kasanga TPDF; Mkoa wa Tanga ni Maramba JKT, Mgambo JKT na Songa.

Mheshimiwa Spika, kwa maumivu waliyonayo wananchi imepelekea kuuliza Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia fedha zao?

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua hatma ya maeneo yaliyofanyiwa tathmini na kusubiri fedha za fidia kama ifuatavyo: Duluthi Estate Tengeru, Singino Kilwa na Mapinga Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na inahuzunishwa na Serikali kulidanganya Bunge na kuwadanganya wananchi kutowapatia haki zao hizo kwa miaka saba sasa. Kambi Rasmi inaitaka Serikali kutoa mkakati wa haraka wa kuwafidia wananchi wa maeneo haya na hasa ikizingatiwa na kudhihirika kuwa baadhi ya maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi ambapo wananchi waliokuwa wanayamiliki wameshafariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa JKT inachukua vijana waliomaliza Kidato cha Sita kwa mujibu wa Sheria; na kwa kuwa vijana wanaotarajia kumaliza Kidato cha Sita kwa mwaka huu ni 454,000; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua ni sababu zipi za msingi zilizopelekea fedha za maendeleo za JKT kwa mwaka 2013/2014 ambazo zilikuwa kiasi cha Shilingi bilioni sita lakini hadi sasa zimetolewa Shilingi milioni 525 tu huku ikia imebakia miezi miwili kumalizika kwa bajeti. Je, hii siyo aibu kwa Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizo za maendeleo za JKT ambazo zimekwishatolewa ni asilimia 8.8, huku Serikali ikijisifu kuwa inahitaji kuendeleza JKT: Je, huo siyo uongo wa Serikali kulidanganya Bunge na wananchi kwa ujumla wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji aibu na fedheha hii ya kutoipatia fedha za maendeleo JKT ni lini itakoma? Je, fedha hizi za maendeleo, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuzitoa kabla ya tarehe 30 Juni mwaka huu ili kukamilisha miradi ya maendeleo ya JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya JKT Kanembwa Kigoma imetelekezwa kwa muda mrefu na hasa askari wa JKT Kanembwa ambao hawajalipwa fedha zao za mizigo na hawajalipwa fedha za likizo kwa muda mrefu sasa tangu mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, pamoja na mkakati wa Serikali wa kudhibiti UKIMWI Jeshini bado Serikali imewatenganisha askari hao na familia zao kwa muda mrefu sasa, jambo ambalo hupelekea migogoro kati ya familia za vijiji jirani na Kambi hiyo ya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo sahihi juu ya malipo ya madeni ya fedha za likizo na mizigo katika Kambi ya JKT Kanembwa na maeneo yote ya Jeshi la Wananchi na JKT.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMA JKT) liliagiza matrekta kutoka nchini India kwa mkopo wa bei nafuu katika mpango wa Kilimo Kwanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa kiasi gani hadi sasa tumeanza kurejesha fedha hizo za madeni ya matrekta hayo na Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuagiza tena matrekta mengine ili kuweza kuboresha mpango wa Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuelewa kiwanda cha kushona nguo cha kijeshi CAMISUMA kimepata faida kiasi gani kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Sambasamba na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuelewa juu ya ubia wa kiwanda cha kutengeneza madawa ya kibinadamu baina ya Tanzania na China *(TANZANSINO)* kwa kushirikiana na ubia wa Kampuni ya Halley Group?

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Wananchi la Ulinzi wa Amani katika Umoja wa bado linaendelea kushiriki katika operesheni za Ulinzi wa amani katika Umoja wa Mataifa. Pamoja na jeshi letu kushiriki katika ulinzi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji na kuitaka Serikali kueleza na kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuhusu hali za wanajeshi wetu huko nchini Sudan, DRC, Sudan Kusini, Lebanon na Ivory Coast.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na inataka kujua idadi ya wanajeshi mpaka sasa waliouawa katika kulinda amani katika Mataifa haya.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa wanajeshi ambao wanauawa katika operesheni wameacha familia na wajane huko nyumbani. Katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kuitaka Serikali kueleza Bunge lako Tukufu juu ya namna ambavyo inasaidia familia za waliofiwa ikiwemo wajane na watoto ambao ni tegemezi kwa wanajeshi hao waliouawa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mkakati wa ziada kwa familia za wafiwa wa Marehemu waliouawa kwenye kulinda amani na elimu kwa familia za wanajeshi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuanza kurejesha alama za mipaka (beacons), Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua alama za mipaka zilizong'olewa baina ya Tarime Tanzania na Migori Kenya katika Vijiji vya Kirongwe, Ikoma, Panyakoo, Ruche, Kagoja na Nyamhunda. Ni lini alama hizo zitarejeshwa kwa kuwa suala hili ni mtambuka kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujanga Taifa, Wizara ya Ardhi, Mambo ya Nje pamoja na TAMISEMI. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi wa ziada ni nchi gani jirani tulizopakana nazo wanaokwamisha zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mkoa wa Kagera alama za mipaka zilizong'olewa katika Vijiji vya Kakunyo, Bugango, Rubale, Mtukula, Minziro na Kashanze ni lini zitarejeshwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alama hizo zilizong'olewa zinahatarisha ulinzi na usalama mipakani lakini pia zinaweza kuleta mgogoro unaoweza kulikumbuka Taifa letu na nchi jirani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kwa nini tatizo hilo limeshindwa kutatuliwa kwa muda mrefu na lini litapatiwa ufumbuzi ili kuepusha migogoro inayoweza kutokea?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imegundua kuwa fedha zinazohitajika katika kutatua tatizo hili la alama za mipaka zimekuwa hazitolewi na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa fedha hizi haraka iwezekanavyo ili kuliepusha na migogoro na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, maisha ya wanajeshi wetu wastaahafu yanasikitisha licha ya kulitumikia Taifa hili kwa muda mrefu, kwa uadilifu na uzalendo mkubwa. Hata hivyo, hali zao za maisha zimekuwa duni, mbaya na kubakia ombaomba ambayo hailingani na utumishi wao walioufanya kwa uadilifu na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imewatelekeza wanajeshi wastaahafu na kuwaacha mitaani bila kujua nini kitu cha kufanya, tayari wameanzisha umoja wao unaojulikana kama Muungano wa Wanajeshi Wastaahafu Tanzania (MUWAWATA). Wanajeshi hawa wastaahafu ni jeshi la akiba (Reserved Army).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kuitaka Serikali kutoa mkakati wa Serikali wa kuweza kuboresha maisha ya wanajeshi wastaahafu na hasa kwenye viwango vya pensheni kwa Maofisa na Askari wa kawaida toka private hadi Brigedia General. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi ya India imeweka mazingira mazuri ya kuwasaidia wanajeshi wastaahafu kuajiriwa uraiani au kuwezesha kujiajiri wenyewe. Hili ni jambo jema na lenye mfano wa kuigwa. Je, Tanzania ina mpango gani juu ya kurekebisha kasoro hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kila askari wa leo ni mstaahafu mtarajiwa. Hata hivyo, askari wastaafu wanaendelea kudharauliwa, kupuuzwa na kutotendewa haki kwa madai ya msingi juu ya hatma ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji sababu zilizopekelea kuwafanya wanajeshi wetu wastaafu kuwa ombaomba, kwani hata haki zao wanazostahili kupewa yaani pensheni za kila baada ya miezi mitatu hazitolewi kwa wakati. Huu ni mtindo wa kuwadhulumu na kuwanyonya askari wetu wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mara moja tabia ya kuwadhulumu na kuwanyonya askari wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakuaje leo mstaafu wa cheo cha Staff Sergent aliyeitumikia nchi hii kwa muda wa miaka 32 kwenye mazingira magumu leo mnawalipa pensheni ya Sh. 350,000/= kwa muda wa miezi mitatu ambayo ni sawa na Sh.117,000/= kwa mwezi, ambayo pia ni wastani wa Sh. 4,000/= kwa siku, fedha ambazo hata chai ya asubuhi kwa familia hazitoshi? Je, haya ndiyo malipo waliyostahili kuwalipa kwa ngazi ngumu waliyoifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashindwa kuelewa juu ya mkakati wa Serikali wa kuweza kuboresha pensheni za askari wastaafu huku gharama za maisha zikipanda kila kukicha. Je, kwa mwaka huu wa fedha askari wastaafu wa Jeshi la Wananchi wataongezewa kiasi gani cha fedha? Tunaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiadhimisha Siku ya Mashujaa kwa kila mwaka kwa ajili ya kuwakumbuka mashujaa wetu walioshiriki katika vita vya Msumbiji pamoja na vita ya Kagera. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua namna familia za Marehemu za mashujaa hao zinapata matunzo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa wajane wa marehemu wa mashujaa hao hali zao za kimaisha ni mbaya na wanatesekea na njaa huku watoto wa mashujaa hao wamekosa hata kupata elimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua mkakati wa ziada wa Serikali wa kuweza kuboresha maisha ya wajane wa mashujaa hao pamoja na familia zao kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa sana na kutumika kwa mamilioni ya fedha kuchimba mifupa ya mashujaa hao nchini Msumbiji kwa gharama za mamilioni ya fedha na kuizika Naliendele Mtwara huku Serikali ikizitelekeza familia za Marehemu hao na kuwaacha ombaomba na kuendelea kulalamika. Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa jambo hili kulipatia ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Spika, mashujaa waliopata ulemavu kwenye Vita vya Kagera na Msumbiji nao wametelekezwa na Serikali na wamekuwa wakijiuliza maswali mengi bila majibu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha ni njia moja muhimu sana katika kulinda maisha ya wanajeshi na raia. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014 ambayo inakaribia kukamilika fedha zilizokuwa zimetengwa ni kiasi cha Shilingi bilioni tano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imegundua kuwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa maghala 2013/2014 hadi leo fedha hizo hazijatolewa. Kambi rasmi ya Upinzani inataka kujua ni sababu zipi za msingi zilizopelekea fedha za ujenzi wa maghala kutotolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa maghala ya silaha yameshaleta madhara mara kadhaa katika Mkoa wa Dar es Salaam maeneo ya Mbagala na Gongolamboto. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na Serikali kutojifunza kwa madhara ambayo yameshatokea kuhusu masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa kiasi gani serikali imelipa fidia ya waathirika wa milipuko katika Kambi ya Gongolamboto na kama wapo wananchi ambao hawajalipwa ni sababu zipi zilizopelekea hadi kutopatiwa fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na madeni ya muda mrefu ya Wanajeshi na Wazabuni waliolihudumia jeshi letu. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imegundua kuwa baadhi ya wazabuni wametishia kusitisha huduma zao hadi hapo watakapolipwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua tatizo hili kubwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na inataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kulipa madeni hayo ili kuondokana na aibu inayoweza kulikumba Jeshi letu. Kwa kuwa fedha za maendeleo kwa fungu 38 - Ngome kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ziliidhinishiwa Shilingi bilioni 10 na hadi Machi, 2014 fedha zilizotolewa zilikuwa Shilingi bilioni 1.6 sawa asilimia 16. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kuwanyima na kuwadhulumu kwa kutowapatia wanajeshi fedha zilizoidhinishwa na Bunge Tukufu, ni kwa nini fedha hizi hazitolewi na ni lini mtindo huu mchafu utakoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kuwa Serikali iliyopelekea kutotoa fedha za maendeleo kwa JKT na Jeshi la Wananchi ni mfumo wa serikali mbili tulionao na wala siyo mfumo wa Serikali tatu unaozungumzwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaweka msimamo wake hadharani baada ya kugundua kuwa kuna mchezo mchafu wa Serikali kupitia Hazina kwa pamoja kunyima fedha za maendeleo Fungu 38 - JKT na Fungu 38 - Ngome na kuazimia ifikapo tarehe 29/06/2014 fedha Shilingi bilioni 5.4 za JKT hazijatolewa na Shilingi bilioni 8.4 za Ngome hazijatolewa. Tutafanya maandamano makubwa nchi nzima kuilazimisha Serikali kutoa fedha hizo za maendeleo na tunaomba Watanzania watuunge mkono kwani suala la Ulinzi halina mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina Hospitali moja tu ya Rufaa iliyopo Lugalo Jijini Dar es Salaam na nyingine za Kanda kama vile Nyumbu Kibaha, Mbeya, Arusha, Mwanza na Zanzibar na kimsingi asilimia 80 ya huduma ya hospitali hizi hutolewa kwa raia. Pamoja na umuhimu wa hospitali hizi, Serikali kwa mwaka uliopita ilitoa fedha kidogo sana ambazo hazifiki asilimia 10 za mahitaji. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa Serikali inaleta mchezo na afya za Wanajeshi wetu. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni kwa nini Serikali isiongeze fedha kutoka Shilingi bilioni 2.4 hadi Shilingi bilioni 10 kwa kuwa hospitali hizi uhudumia pia raia kama tulivyokwishasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vituo teule yaani De touch. Vituo teule sambamba na barabara za mipakani ni jambo muhimu sana katika ulinzi wa nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mkakati wa ziada wa Serikali wa kuzikarabati barabara zote zinazokwenda kwenye vituo teule kuweza kutumika wakati wote. Ikumbukwe kuwa katika nchi nyingine duniani, suala la kuzikarabati barabara za mipakani ni jukumu la Wizara ya Ulinzi na siyo jukumu la Halmashauri kama ilivyo Serikali ya Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua ni lini Serikali itazihamisha barabara zote teule kuwa chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi Kujenga Taifa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu juu ya vijana wanaoajiriwa kutoka ngazi za Mikoa na Wilaya wanaojiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwa mfumo huo haupo wazi mbali na mkakati wa vijana hao kuchukuliwa JKT na JKU. Malalamiko haya ya kuwepo kwa uwazi katika uajiri hata Wabunge wenyewe na hasa kutoka Zanzibar hawaelewi ni lini na wakati gani ajira zinapatikana. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua mkakati wa Wizara ya Ulinzi kuwapatia taarifa Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa muda, siku na mazingira ya ajira hizi Jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa hali ya uharamia katika Bahari ya Hindi na hasa katika Pwani ya Afrika Mashariki imedhibitiwa kwa kiasi fulani, Tangu kufanyika kwa marekebisho ya Sheria yetu ya Makosa ya Jinai ili kuruhusu mashtaka dhidi ya maharamia wanaokamatwa Bahari Kuu kushtakiwa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji na kutaka kujua ni maharamia wangapi wamekamatwa kutoka Januari 2013 hadi Machi 2014?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Dar es Salaam ni kituo cha upashanaji habari za majini kwa ukanda wa nchi wanachama wa Mkataba wa Djibout kufuatia ushirikiano wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na nchi za Umoja wa Ulaya ambapo Jeshi letu lilifanikiwa kuwanasa watuhumiwa watano wa uharamia kwenye kisiwa cha Ukuza Wilaya ya Kilwa tangu tarehe 18/04/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua watuhumiwa hao wako wapi na hukumu yao ilitolewa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Ulinzi imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi trilioni 1.269 kwa mgao ufuatao: Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi Shilingi bilioni 19.7 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 230 kwa matumizi ya maendeleo. Kwa ujumla fungu hilo ni Shilingi bilioni 249.7.

Mheshimiwa Spika, Fungu 38 – Ngome, fedha kiasa cha Shilingi bilioni 803.5 zimetengwa kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 12 kwa miradi ya maendeleo. Jumla ni Shilingi bilioni 815.5. Fungu 39 - JKT kiasi cha fedha Shilingi bilioni 196.8 zimetengwa kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni saba kwa miradi ya maendeleo. Jumla ya fedha zote katika fungu hili ni Shilingi bilioni 203.8. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa fedha za maendeleo za JKT zimetolewa asilimia 8.8 tu hadi sasa na fedha za maendeleo za ngome zimetolewa asilimia 16 tu hadi sasa. Fedha hizo ambazo hazijatolewa, zitolewe haraka sana kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha na hizo zilizotengwa kwa mwaka 2014/2015 zitolewe mapema iwezekanavyo ili kuepuka hali ya mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Kama ilivyowasilishwa Mezani

SPIKA: Ahsante sana. Kwa kweli ni lazima mpige makofi, maana ni mara ya kwanza, kwa hiyo sasa nitawaita wachangiaji wafuatao; Mheshimiwa Anna Abdallah atachangia atafuatiwa na Mheshimiwa Yusuph Salim Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa John Chiligati na Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia katika hoja hii. Kwanza, nimpongeze sana Waziri mhusika kwa vile tumeshirikiana naye vizuri sana katika Kamati na kwa kweli Kamati imeridhika sana na yale tuliyoagiza katika bajeti iliyopita jinsi walivyotekeleza. Kwa kweli wametekeleza kwa kiasi kikubwa. Pale ambapo hawakutekeleza ni kwa kuwa fedha hawakuzipata tu, lakini kazi ni nzuri, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni suala ambalo tumekuwa tukilizungumza sana hapa na nashukuru kwamba hata Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameisema kuhusu Sera na Sheria ya ulinzi tumekuwa tukiidai na kila siku tunapata majibu kwamba wanangoja maoni kutoka upande wa pili wa Muungano.

Sheria ile imezeeka, imechakaa na inayo mambo ya kizamani sana ambayo lazima yabadilike na hatuwezi tu tukawa tunabadilisha kila kitu kimoja kimoja. Dawa yake ni kubadilisha kabisa ile Sheria. Kwa hiyo, tungependa Waziri atuambie wamefikia wapi na tatizo ni nini kwa sababu hili ni Bunge la pili tunaeleza jambo hili halifanyiki.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka kusisitiza ni barabara za ulinzi mipakani mwetu. Zamani hasa sisi tunaotoka kwa mfano kusini zamani unaweza ukatoka Mtwara vijijini, ukapita kando kando na Msumbiji mpaka ukafika Tunduru, nafikiri mpaka Songea; na waliweka na madaraja yale ya chuma na nini, ilikuwa ni rahisi sana labda ni kwa ajili ya wakati wa vita lakini wakati wa amani zile barabara zinatakiwa kwa sababu vita siyo lazima vita ya bunduki.

Kuna vita vya uchumi; hii habari ya kusafirisha watu mipakani na hivi, magendo na sasa hivi barabara zote zimekufa na ndiyo maana watu wanang'oa beacons. Hakuna mtu anaweza kwenda, ni maporini tu na hata kama ni nchi jirani kama wanaona nyinyi wenyewe tu wakulima

wamebeba majembe yao begani, kwa kweli wanaona kumbe hapa ni mahali pa kuingia kwa urahisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba na sisi tulipendekeza ingawa halikujitokeza vizuri kwenye Kamati kwamba katika ile Road Fund kuna fedha inabakia Wizara ya Ujenzi, kuna fedha inakwenda kwenye Halmashauri tunajua hata Halmashauri yenyewe inadai fedha zaidi, lakini katika fedha zile zile kungekuwa na percent ya kupeleka Jeshini wa-maintain zile barabara za mpakani za ulinzi, zitasaidia hata Halmashauri kufanya doria zao mbalimbali, zitasaidia hata watu wa immigration kufanya doria mbalimbali. Lakini leo hakuna mtu anazishughulikia na mimi kwa kweli sipendi kusema Halmashauri zifanye, kwa kuwa Halmashauri hizi zina kazi zao nyingi na barabara hiyo kama ya mpakani haina tija kwao, hawaweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana kwamba hebu tungekuwa na category hiyo ya barabara za mpakani, za ulinzi katika barabara za vijijini ili Jeshi liweze kuishughulikia. Kwa sababu Jeshi wana kikosi cha ujenzi, wana vifaa na wameandikishwa wao ni makandarasi. Kwa hiyo, ikiwa ni kazi yao na fedha wanazo kwa kweli wanaweza kuifanya kazi hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulisemea ni kwamba katika mipaka yetu ukienda mpaka wetu na Zambia pale Tunduma kwa kweli utakuta nyumba ya mtu, chumba chake kipo Tanzania, jiko liko upande wa Zambia na vise versa.

Mwingine sitting room yake anakula chakula Zambia jiko analopika chakula chake yuko Tanzania. Hakuna no man's land na Sheria inatutaka kuwe na eneo kati ya mpaka wa nchi na nchi watu wasijenge lakini tumeachia mno, nafikiri habari hii iko karibu mipaka yote. Hata tukisemaje, lazima jamani hili jambo tulitekeleze. Kweli kabisa! Halafu wengine wanachukua zile beacons, tumeambiwa kwamba wanapasua kuchukua kokoto na zile nondo zilizoko mle ndani, lakini ziko porini mno. Kwa kuwa hakuna barabara wala hawaogopi kwa sababu hakuna mtu atapita katika maeneo hayo mpaka pale tu kuna shida ya kwenda kutafuta hizo *beacons.*

Mheshimiwa Spika, naomba jambo moja tu ambalo sijui kama linafanyika siku hizi. Unapomteua Mkuu wa Wilaya mpya ni pamoja na kumwonyesha beacons za Wilaya yake, mipaka yake iko wapi. Sasa hivi tunasikia kuna mipaka, kuna migogoro ya mipaka kwa kweli watu wa wanateuliwa na kwenda kuapishwa tu, haonyeshwi kwamba Wilaya yako mipaka yake hii hapa, inapita hapa, hasa mpakani; na beacons ziko wapi ili katika shughuli zao pia wawe wanakwenda kuzitembelea. Lakini bila barabara hizi za mipakani tutapata shida sana.

Mheshimiwa Spika, niomba suala la ulinzi hili tusilichezee. Unajua amani nayo inatupumbaza! Sisi ugomvi tunaoujua ni wa Vyama tu, tunagombana wenyewe kwa wenyewe. Huyu anasema hiki na wengine wanajibu hiki; huo tunaujua. Ule ni ugomvi ambao kwa watu wastaarabu wa demokrasia ni kiasi cha kuvumiliana tu kwa sababu ni maneno. Lakini kama tungekuwa kama wenzetu wasiokuwa na amani kati ya Wilaya na Wilaya ndiyo tungejua faida ya kuimarisha Jeshi.

Sisi tunachukulia mfano tu wa mambo kama ya kienyeji kienyeji tu. Ni lazima tuliwezeshe Jeshi letu na hapa hatuwezi kusema wanunue kitu gani. Tuna vikosi vingine kazi yake kutengeneza zana, hatuipi fedha, matokeo yake tunanunua zana za kutoka nje, jambo ambalo tungeweza kuzitengeneza humu humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi jana nilikuwa nimekutana na Kamati ya Bajeti, niliwaomba kwamba tutakapofanya vikao vingine vya Kamati niwaalike baadhi ya Wajumbe wa Bajeti watakaokuwa tayari twende kwenye Vikosi hivi vinavyotengeneza zana waende wakavione,

waone na akili inayopotea pale na vifaa vinavyooza tu, vinahitaji matengenezo, yaani watu wana akili, wamesoma kule katika baadhi ya hivi Vikosi kwa mfano Nyumbu pale; kuna watu wana akili, kama wangekwenda katika private sector huko ndio wangekuwa ma-DG wa viwanda hivyo. Lakini wanasema wanaipenda nchi, wamebakia pale hawapewi fedha ya kuendesha, tunawapa mishahara. Kwa kweli kumlipa mtu asiyefanya kazi ni kupoteza fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwamba hivi vitu tuviandae, nami nikubaliane na ule usemi kwamba wakati wa amani ndiyo wakati wa kutoa jasho jingi. Ukitoa jasho jingi wakati huu, basi wakati ikija kutokezea utaona kwamba damu inakuwa kidogo sana. Nami nasema Umoja wa Mataifa unapenda Wanajeshi wetu na kila wanakokwenda wanafanya kazi nzuri sana kwa sababu wale wachache wanaopata nafasi hiyo ndio wanatoka katika vile vikosi ambavyo vinafanya shughuli za mazoezi.

Wakienda kule hawana kazi kubwa sana ya kufanya mazoezi pamoja na kwamba kule wanafanya mazoezi. Lakini nasema tungeeza kufanya vizuri zaidi na kwa sababu nchi dunia inatutegemea sisi katika maeneo haya ya Afrika kwamba Wanajeshi wetu ndiyo wenye weledi wa kutosha, wanaweza…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzunguzaji)

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Ahsante. Ama bado dakika mbili?

SPIKA: Muda umekwisha.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwisha Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiligati.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi asubuhi ya leo kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nianze na masikitiko kwamba hata katika Wizara hii ambayo ni tegemeo la Taifa letu bajeti yao bado miezi miwili haijakamilika.

Ni kitu cha kusikitisha na Mheshimiwa Waziri nadhani itabidi uchukue juhudi za makusudi za kuwachukua hawa kuanzia Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha waende Jeshini na wao waone utamu na uchungu wa kuwa Mwanajeshi ili wasiweze kuzuia fedha za Wanajeshi zifike kwa wakati. Mimi nadhani kama na wao wameenda wakajua, basi wasingeweza kufanya mchezo kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili linalonisikitisha ni kwamba ulimwengu wa sasa suala la ulinzi ni suala la kisayansi zaidi, ni suala la kitaalamu zaidi. Inasikitisha kuona kwamba hata fedha haitoki na suala la mawasiliano linakuwa ni dogo mno, ni kwa asilimia 20 tu. Watawezaje Wanajeshi wetu kutulinda, watawezaje kupambana kama hawana mawasiliano? Suala la mawasiliano ni suala muhimu mno na hapa fedha inahitajika itoke kwa namna yoyote kwa sababu Jeshi ni mawasiliano. Bila mawasiliano hakuna Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia Wanajeshi wetu ambao wako katika mapambano au wapo katika nchi zile kwa mwamvuli wa Umoja wa Mataifa. Tuna Wanajeshi wapo huko katika Chapter Six na Chapter Seven lakini nataka kujua hawa Wanajeshi wetu walioko huko:

Je, wanapata zile stahiki zao kulingana na viwango vile vya UN au wanapata stahiki zao kwa viwango vipi? Kwa sababu pale wako chini ya mwamvuli ule na wanapambana pale siyo nchi yetu, ni mwamvuli wa UN.

Kwa hiyo, pale kuna malipo kulingana na viwango vya kimataifa, je, Wanajeshi wetu wanapata stahiki hizo au hawapati? Je, kabla ya kwenda katika nchi hizo chini ya mwamvuli huo Umoja wa Mataifa wanafahamu stahiki zao? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili ni katika Wizara za Muungano ambazo Wazanzibar au upande wa pili wa Muungano tunapata haki wala hatuwezi kulalamika ni hapa maana Wanajeshi wa Zanzibar wanashiriki kwa wingi sana katika mambo haya nje ya nchi yetu katika vita. Kwa hiyo, hapa mgawo unakwenda sawa kabisa. Katika hili tunashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri unaweza kutuambia ni wangapi ambao wamepoteza maisha katika nchi hizo chini ya mwamvuli huu? Je, familia zao sasa zinatunzwa vipi na zinapata huduma zipi kulingana na haya ambayo yanatendeka huko?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira sasa, imependekezwa hapa na imesisitizwa kwamba vijana wote ambao wataajiriwa katika vyombo vyetu vya ulinzi ni lazima wawe wamepitia JKT, ama JKU. Mheshimiwa Waziri mie katika hili kwa upande wa Zanzibar sasa nakuomba ulifuatilie na uwe makini sana. Tunahofu na kuna tetesi kwamba vijana wanaoajiriwa katika vyombo hivi hawajapita JKU wengi wao na pia kuna ujanjaujanja hapa ambao unatumika katika kuwaingiza katika vyombo hivi. Sasa hizi ajira jamani si ajira za kuchezea, tunahitaji watu ambao ni makini, wenye uwezo ambao wataweza kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na uaminifu mkubwa. Kwa hiyo, mimi napenda katika hili Mheshimiwa Waziri uwe makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linatusikitisha hizi nafasi huwa ni za Tanganyika na za Zanzibar, tuna hofu au kuna tetesi kwamba zile Zanzibar pia zinachukuliwa huku. Wanatoka vijana huku ikifika nyakati zile wanakuja kuchukua nafasi kule. Mheshimiwa Waziri tunaomba hili nalo ulifanyie kazi kwa uzuri kabisa. Nasikitika Waziri aliyepita alihusika na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sababu naona nilishapigiwa kengele, ni wastaafu. Katika watu ambao wanadhalilika katika maisha yao baada ya utumishi wao jeshini ni Wanajeshi wastaafu. Kwa hiyo, hii nchi yetu kuwa pambo la jeneza tu kuwasifu Wanajeshi wetu, mahiri, mahodari, waaminifu, weledi katika kipindi ambacho wako katika kazi tu lakini wakistaafu basi hatuwatunzi tena, hatuwathamini tena, hatuwajali tena ni watu ambao sasa waende wakawe walinzi katika taasisi nyingine, ni kitu ambacho kinasikitisha sana. Jamani hebu tuthamini ile damu na maisha yao wanaojitolea wahanga hawa katika mapambano ambayo yanatokea na tuthamini maisha yao baada ya utumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anamaliza Jeshi anastaafu akiwa Luteni akiwa Meja lakini baada ya mwaka mmoja akiwa huko mitaani unajiuliza huyu alikuwa Mwanajeshi kweli? Jamani katika hili tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hili suala la wastaafu liangaliwe upya, pensheni zao ziangaliwe upya kulingana na maisha ya sasa na stahiki zao ziangaliwe upya kwa sababu hawa watu wanatumia nguvu nyingi sana wakati wa ujana wao wakiwa katika zile kazi. Kwa hiyo, wanapostaafu ni dhahiri kwamba wamechoka, wanastahiki kupumzika, wanastahiki kutunzwa

na Taifa hili. Tusiwasifu wakati wa mapambano tu, tusiwasifu wakati wakiwa katika vita tu lakini ile sifa ije kwa vitendo, ije kwa kuwatunza katika kipindi ambacho wamestaafu na maisha yao ya uzeeni wayamalizie katika hali ambayo na wao watajua kwamba walilitumikia Taifa hili kwa uaminifu. Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri stahiki za Wanajeshi na wastaafu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo. *(Makofi)*

SPIKA: Nimwite Mheshiwa Chiligati halafu Mheshimiwa Christowaja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mawazo yangu kuhusu ajenda iliyo mbele. Kwanza naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kutoa pongezi kwa Jeshi la Wananchi na kwa kweli kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na amani na inakuwa salama. Ni jambo ambalo Watanzania wengi wanalichukua tu hivihivi, wanadhani ulinzi na amani ni kama tu hewa iko hivihivi si kweli. Amani hii tunayoiona, utulivu tunaouona ni kwa sababu kuna baadhi ya Watanzania wenzetu usiku na mchana hawana Jumamosi, hawana Jumapili, hawana sikukuu wanailinda nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri tu Serikali kwamba kulinda amani ni ghali lazima tuwekeze katika kulinda amani na utulivu. Tukisema kwamba tumechoka amani basi tushindwe kuwekeza kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Nalisema hili kwa sababu naona Wizara ya Fedha inapotoa fedha katika Wizara mbalimbali hivi vyombo vya ulinzi na usalama vinachukuliwa kama navyo ni Idara za kawaida tu si sawa! Hata sisi hapa Bungeni, tuko hapa kwa sababu pana utulivu, likitokea la kutokea Spika utatokea mlango wako na sisi mlango wetu na hivyohivyo katika shule, katika kilimo, katika ufugaji na kila mahali. Kwa hiyo, nasema Serikali tunapotoa fedha katika Wizara, hizi Wizara za Ulinzi na Usalama tuwape kipaumbele kwa sababu ndiyo wanaolinda amani na utulivu tunaouhitaji wakati wote kwa ajili ya kuendeleza shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa katika baadhi ya mafungu Wizara hii imepokea asilimia 20 tu tangu Julai mwaka jana mpaka leo. Hii imeonesha kwamba tumechukua jambo hili kama jambo la kawaida kawaida, si sawa! Ningependa katika hili Serikali kwa kweli tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo la pili, nizungumzie habari za Wanajeshi wastaafu na Kanuni zetu zinasema usizungumze jambo ambalo wewe unamaslahi nalo lakini lazima kwanza ku-*declare interest* na mimi ni mstaafu. Tangu mwaka 1992 vilipokuja vyama vingi tukaamua tuchague ama uendelee na Jeshi ama uende uraiani, nikaenda uraiani. Basi kwa sababu sasa nimesha-*declare interest* kwamba mimi nazungumza jambo ambalo nimo sasa nina ruksa kuendelea nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu wa Jeshi bado mambo yao hayajakaa vizuri. Kamati yetu miezi michache iliyopita tulitembelea Bunge la India na tukakutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge la India. Katika Jambo ambalo tulitaka kujifunza kutoka kwao, ni jinsi gani wao wanavyowahudumia Wanajeshi wastaafu.

Mheshimiwa Spika, sasa kule tulichokiona ni kitu gani? Kwanza, pesheni za Wanajeshi wastaafu utaratibu wao ni tofauti na huu mwingine wa uraiani. Sisi tumefananisha tu kana kwamba sisi wote ni sawa. Hawa ni watu ambao katika maisha yao usiku na mchana wamekuwa wanalinda nchi hii kwa hiyo pensheni yao ni tofauti. Wao wakishastaafu, karibu asilimia 80 ya mshahara wake anakwenda nao kama pesheni yake. Kwa hiyo, hawana shida kama hizi za kwetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa sababu Wanajeshi wanasataafu katika umri mbalimbali na wengine wanastaafu wakiwa bado vijana tu, ikitegemea na cheo chako. Kuna watu wanastaafu wana miaka 45, 48, 50, 55 siyo sisi huku ambako uraiani unastaafu katika miaka 60. Jeshini wanastaafu kwa kadri ya cheo chako kilivyo, kwa hiyo wanastaafu bado wadogo. Kwa hiyo, India kule wanachofanya hawa wanaostaafu bado wadogo wanafanya mambo makubwa mawili kuwasaidia. Kwanza, wanawatafutia kazi uraiani maana hawa vijana hawa Jeshini ni wajuzi wa fani mbalimbali ambako na uraiani zipo, kwa hiyo wanakuwa *re-engaged,* wanawekewa utaratibu wa kutafutiwa kazi uraiani. Kama ulikuwa ni fundi, ulikuwa na ujuzi gani kulingana na ujuzi wako unatafutiwa kazi uraiani, kwa sababu wanastaafu wakiwa bado vijana. Sasa sisi huku mtu alikuwa ni *Engineer* lakini ni Koplo kastaafu ana miaka 45 kwaheri.

MBUNGE FULANI: Aaah, sio sawasawa.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Nadhani si sawasawa na sisi tuliwaambia kwamba Wizara ya Ulinzi hebu wakafanye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kama hawezi kuajiriwa uraiani wanamuwezesha ili aweze kujiari mwenyewe. Akishakaribia kustaafu anapelekwa kwenye mafunzo ya ujasiriamali, anapewa mafunzo jinsi gani anaweza akafanya shughuli yeye mwenyewe. Halafu pili, anaunganishwa na vyombo vya fedha ili akopeshwe mtaji wa kufanya hiyo shughuli aliyochagua kuifanya na hayo mambo yote yanaratibiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulivyokutana na Wizara tukasema kwa sababu India ni marafiki zetu wanafanya vizuri kuwatunza hawa Wanajeshi wastaafu, nendeni mfanye utafiti mjifunze ili haya mambo mazuri wanaofanyiwa Wanajeshi wastaafu wa India na hawa wa kwetu tuwafanyie. Haifai tu tunawasifu sasa hivi wamefanya kazi nzuri, wakishastaafu hatuna habari nao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo nilikuwa naomba sana Serikali kupitia Wizara hii hebu watazame mifumo mizuri pengine kuna mfumo mzuri kuliko hata wa India, watazame mifumo yote jinsi gani ya kuwatunza Wanajeshi. Sasa hivi kwa kweli wanahangaika mpaka wameanzisha kama ka-TUCTA kao ka uraiani, huu muungano wa Wanajeshi wastaafu katika kuhangaika jinsi ya kupigania mambo yao. Sasa kule wanachaguana, Wanajeshi wastaafu hawa bado ni Askari wa akiba, kimsingi bado ni Askari ikitokea vita wanaweza wakaitwa. Sasa wameachwa mitaani, wameanzisha umoja wao, wanahangaika, wakishakutana pale wanachaguana Mwenyekiti Koplo, sasa Brigedia ndio anakuwa Katibu, haifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima Wizara kile kitengo kinachotazama Wanajeshi wastaafu kitazame na hili, mfumo wao uendelee kuwa uleule wa kijeshi, haka ka-TUCTA kao kapembeni haka wanakafanya tu kwa sababu hatujawaundia utaratibu mzuri wa kijeshi. Waundiwe utaratibu wa Kijeshi na kile kitengo pale Makao Makuu ya Jeshi kinachowatazama kiwezeshwe ili kiwasimamie vizuri zaidi. Hili la Wanajeshi wastaafu ni kapacha kabaya kabisa katika jamii yetu lazima tukazibe ili tuendelee kuwaenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hotuba ya rafiki yangu Waziri Kivuli imenifurahisha, ilikuwa ni hotuba ambayo ina hoja, ina ushauri, haina matusi, haina kejeli. Mimi nafikiri na Mawaziri Vivuli wengine wangeiga mfano wake, kwa sababu jamani tunajenga nyumba moja haya matusi na kejeli ndani ya Bunge hayasaidii kujenga.

Mheshimiwa Spika, ila tu jambo moja sikubaliani naye aliposema kwamba…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Bahati yako mbaya mtakubaliana naye huko.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Nianze na hotuba ya Waziri, ukurasa wa tisa, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2013/2014 hususan katika kipengele cha mapato. Waziri ametuonesha kwamba mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa bajeti inayoishia mwaka huu ni jumla ya Sh.68,206,000/=. Cha kushangaza pamoja na udogo wa makadirio ya makusanyo hayo yaliyokusanywa mpaka Machi ni Sh.43,317,624/= tu sawa na asilimia 63.5. Kama hiyo haitoshi, ukurasa wa 32, makadirio ya mapato mwaka huu yameshuka mpaka Sh.60,506,000/=.

Mheshimiwa Spika, cha kujiuliza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lina vyanzo vingi sana vya mapato, mfano nitoe tu Shirika moja la SUMA JKT na taasisi zingine au mashirika mengine yaliyo chini ya Wizara hii. Ni kwa nini Jeshi linashindwa kukusanya au Wizara inashindwa kukusanya mapato na badala yake inakuja kulia tena na yenyewe kuomba iongezewe fedha zaidi. Sasa hivi nchi yetu iko kwenye amani, ni wakati sasa wa Jeshi letu la wananchi pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa kuzalisha ili pale ambapo tutaingia katika hali ya sintofahamu tuwe na fedha au tuwe na rasilimali za kutosha kuweza kujiendesha. Naomba sasa Jeshi liongeze au Wizara hii iongeze makadirio ya mapato kwa mwaka huu ambao unaanza haya yaliyoonyeshwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala ambalo limezungumzwa sana hapa hata Waziri amesisitiza na amepongeza sana kuhusu maonesho yaliyofanyika au maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano. Waziri ametuambia analipongeza Jeshi na Jeshi liko tayari kuulinda Muungano kwa hali yoyote ile. Labda tu mimi niseme Jeshi au Muungano wetu haulindwi kwa silaha kali, Muungano wetu haulindwi kwa maonyesho mazito mazito ya silaha, ila Muungano unalindwa kwa uzalendo wa watu wake pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, pamoja na kwamba ni vizuri kabisa na ni haki ya wananchi wa Watanzania kuonyeshwa uwezo wa Jeshi letu, uwezo wa kisilaha, ukakamavu ili tuwe na amani kwamba sasa tuna ulinzi wa kutosha. Kilichofanyika siku ile kilipita mipaka, Waheshimiwa hatuwezi kuonyesha kila kitu mpaka nguo ya ndani. Tumeoneshwa kila kitu, tumewaona makomandoo, tumeona kila kitu, hivi tunamuonyesha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuonyesha kila kitu, adui anayetuangalia atafanya zaidi. Pamoja na kupongeza kwamba mna silaha za kutosha haikuwa sawasawa kutuonyesha zote kiasi kile. Tuna Siku ya Mashujaa tarehe 25 Julai, inakuja tunategemea kuona silaha ambazo

zipo, siyo za namna hiyo, najua mtatoa majibu ya ku-*criticize* lakini haikuwa sawasawa na sasa tusifanye siasa hata kwenye Jeshi, haifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siasa kwenye Jeshi haifai, matokeo yake tulisikia hata Kamati moja ya Katiba na Sheria wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu ikipendekeza sasa Jeshi wakati wa maafa lipunguze masharti ya ulinzi. Jeshi haliwezi kupunguza masharti ya ulinzi, likipunguza masharti ya ulinzi inakuwaje? Tuko salama hapo? Mimi sikupendezewa na nafikiri hata Wanajeshi wenyewe nadhani hawakupendezewa hata wananchi wengi hawakupendezewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja nyingine ambayo nimekuwa nikiizungumza kila siku. Tangu nimeingia Bunge hili mwaka 2010 hoja yangu ni maduka ya Jeshi. Maduka yale ni *duty free,* tunajua wanapunguziwa asilimia 18 ya vifaa wanavyoagiza. Nimekuwa kila siku nikizungumza na nikiikumbusha Serikali kwa nini maduka yale hayawatendei haki Wanajeshi, yanaendelea kuuza vifaa vyao kwa bei ya juu, wanashindana na wafanyabiashara wa Kariakoo? Mheshimiwa Waziri leo naomba uniambie ni lini mtakwenda kuhakiki zile bei zinazoendeshwa na yale maduka?

Mheshimiwa Spika, tena sasa mwaka juzi nilijibiwa hapa kwamba utaratibu unafanyika wa kupitia bei za bidhaa zile na sasa niliuliza ni kwa nini Wahindi wasiojua hata Kiswahili wanaendesha maduka yale badala ya tenda zile kupewa wazawa, mpaka Jeshini Wahindi wameingia. Niliambiwa mchakato unafanywa kupewa wazawa maduka yale. Huo mchakato unafanyika kwa miaka mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani hapa tunawapenda Wanajeshi tunawaambia wakakamavu, tunawasifia sana, haki zao za msingi kwa nini tunawanyima? Zile bei hazifai na wale Wahindi waondoke wazawa waendeshe maduka yale. Mimi siyo mbaguzi lakini kwa kweli ni haki ya wazawa hata kama hatuna mitaji mikubwa lakini kuendesha maduka ya Jeshi tunaweza kuendesha zile *super market* na pia kwa ulinzi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ni kuhusu nyumba za Wanajeshi. Wizara imetueleza miradi mingi ya kujenga nyumba sawa tunashukuru lakini…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa…

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge walikuwa wakiongea)

SPIKA: Kwanza kabisa, naomba nitangaze kwamba Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa John Mnyika anawatangazia Mawaziri wote Kivuli wakutane kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kufanya *cabinet* yao ya Kivuli na asikose mtu nadhani baada ya kuahirisha shughuli hizi mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, pili, utaratibu wetu wa kuchangia ni kwanza ni wale walioomba kuchangia, pili tunafuata ile *formula* ya wingi wa Wabunge humu na tatu kuna watu ambao mimi naweza kuwaita nikitaka, nina nafasi yangu. Kwa Wizara hii kidogo utaratibu huu unakuwa haujakaa vizuri kwa sababu walioomba kuchangia ni tisa na wako tisa kwa hiyo nitawaita. Kwa mfano, leo CUF ilikuwa moja, CHADEMA ilikuwa moja na CCM ilikuwa tano. Kwa

hiyo, mkiniona sasa naita ninavyoita msidhani kwamba nimevuruga utaratibu wote ni kwa Wizara hii *special* tu basi. Kwa hiyo, namuita Mheshimiwa Rajab Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza leo kuchangia kwa bajeti hii nzima, kwanza nichukue nafasi hii kupongeza Viongozi wote wa Upinzani ambao wameamua sasa wapinzani kufanya kazi kwa pamoja kitu ambacho tayari imeonekana ni mwiba ambao unawachoma wengine na baadhi yao kutamaluki na kutubadilisha hata majina kama ambavyo tulisikia jana hapa, mmoja anatuita sisi ni Lusu. Bahati mbaya yeye anafahamu maana ya Lusu lakini wengine hawafahamu lakini ni vyema aelewe kwamba Lusu ni yule aliyekuwa hana mkia sasa …

SPIKA: Mheshimiwa Rajab! Mimi napenda ungeendelea kujadili tu, vitu vya namna hiyo havina tija kwa mtu yeyote ndiyo maana huwa tunadharau, naomba uendelee kujadili hoja yako.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naweka sawa baadhi ya mambo lakini nashukuru kwamba kanielewa, ni vyema ajiangalie vizuri bwana Chomboh kwamba yeye ni *kelbu* tu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la kuchangia kuhusu Jeshi letu. Nianze na suala ambalo Mheshimiwa Waziri amelieleza katika hotuba yake ukurasa wa 27, mpango wa mwaka 2014/2015 linahusiana na ujenzi na umaliziaji wa viporo vya nyumba, bwalo na bweni huko Pemba. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili lakini nataka nimwambie kwamba pale siyo kumaliza viporo. Kinachoonekana katika nyumba zile za Wanajeshi katika kambi ya Ali Hamisi ni kwamba zile nyumba zimejengwa chini ya kiwango. Sasa hivi nyumba zile hazijahamiwa lakini zimejaa nyufa, tayari zinavuja hata wale ambao wako pale wanashindwa kuingia na zile ambazo zimeshahamiwa kwa kweli hali yao ni mbaya sana. Kwa hiyo, nimtake tu Mheshimiwa Waziri hebu aangalie upya mchakato ambao ulitumika katika ujenzi wa nyumba zile na hatua za kinidhamu kama zinahitajika basi ni vyema zichukuliwe ili hali katika majengo yale iwe nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwapongeze Wanajeshi wale wa kambi ya Ali Hamisi kwa namna ambavyo wameamua kuanzisha shule pale. Shule ambayo mbali ya kuwasaidia watoto wa Jeshi lakini vilevile inawasaidia wananchi wa kawaida. Hali hii imeweza kujenga imani na ushirikiano baina ya Jeshi letu na wananchi na kiasi cha kujiona kwamba Wanajeshi na wao ni sehemu ya raia na raia kujiona kwamba na wao ni sehemu ya Jeshi lao, hili nalipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala ambalo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye hotuba yake ni nzuri na naipongeza sana, hali ya uharamia katika Pwani ya Afrika Mashariki. Katika kupambana na hali ya uharamia katika Pwani ya Afrika Mashariki, ikumbukwe kwamba Pemba ni moja ya kisiwa ambacho kiko pembeni au katika mpaka. Katika eneo la Rasi Kigomasha itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Waziri pale palikuwa na Kambi ya Jeshi lakini ni eneo ambalo vilevile katika Pwani ile maharamia wengi wanapatumia hasa wa Kisomali. Sasa tunashangaa ni kwa nini kambi ile katika Rasi Kogomasha sasa hivi imehamishwa. Ni vyema Waziri utueleze ni kwa nini Kambi ile imehamishwa wakati ambapo sasa hivi tuna hali ya uharamia katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, naomba niongelee suala la kupatiwa fedha Wanajeshi. Kwa kweli hili linasikitisha kama mwenzangu Yussuf alivyosema kwamba hii hali ya kutokuwapatia fedha Wanajeshi kwa kweli inasikitisha sana. Kutowapatia Wanajeshi wetu fedha ukiangalia katika

mitandao ya kimataifa, imesababisha uwezo wa Jeshi letu, *rank* ya Jeshi letu la Tanzania kushuka. Sasa hivi Tanzania ni nchi ya 102 katika *military power* kwa *rank* zinazotolewa kimataifa. Katika Afrika Tanzania ni nchi ya 22, yaani tunashindwa na Uganda, tunashindwa na Kenya, tunashindwa na Sudan, tunashindwa hata na Somalia katika nguvu hizi za Kijeshi. Hii iko katika *Global Fire Power Ranking* ambayo wameitoa tarehe 4/3/2014, hivi ni vigezo ambavyo wameweza kuvitoa. Sasa ni vyema Serikali ione namna gani sasa hivi kuna haja ya kulipatia Jeshi letu fedha au Wizara hii fedha ili Jeshi letu liwe imara na liwe na nguvu zaidi kuliko maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, naomba niwapongeze sana Jeshi letu na niwaambie kwamba wasivunjike moyo na maoni na maelezo ambayo yanatolewa na baadhi ya viongozi hasa ukizingatia kazi kubwa ambayo wanaifanya. Matamshi ambayo yanatolewa na badhi ya viongozi ya kwamba iwapo maoni ya wananchi yaliyowasilishwa na Jaji Warioba yatatekelezwa na Rasimu ile ya Serikali tatu itapita, basi huenda Jeshi likachukua Serikali. Hili Mheshimiwa Waziri pamoja na Jeshi lako tunaomba msiyachukue, haya ni maneno ya porojo tu ya viongozi na ni maneno ya wale watu ambao tunawaita wasaka tonge. Kwa hiyo, tunaomba sana Wanajeshi wetu maneno haya msiyachukue na myaache kama yalivyo, kwamba ni maneno ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vyema kabisa Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa kuhitimisha hoja yako, ukatoa tamko rasmi la Serikali juu ya kauli zile kwamba Jeshi litachukua madaraka pale mfumo wa Serikali tatu utakaopokuwepo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Hilo hatajibu kwa sababu ni hoja ya Bunge Maalum, huku hakuna kitu. *(Makofi)*

Kama nilivyosema sasa nitamuita Mheshimiwa Sabreena halafu atafuatiwa na Hamad Rashid Mohammed halafu Ridhiwani. Sabreena ameshaongea, aah Sabreena nitakuita, nimechanganya.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Yahya Kassim na siyo Sabreena. *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa umesemaje?

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, ulisema baada ya Mheshimiwa Rajab nitakuja mimi Yahya Kassim Issa, sasa ndipo nilipokuwa nauliza sijui imekuwaje?

SPIKA: Usipoteze muda wako endelea nitawaita wote hawa!

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mimi natoa pongezi kutokana na sherehe ya miaka 50, kutokana na maonyesho ya Jeshi letu. Tusiwe na wasiwasi wananchi ile ni bashrafu tu hata robo ya shughuli za Kijeshi haikutimia. Ile ni kuwafahamisha wananchi wetu kwamba katika mambo tunayofanya na haya yamo tu basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna swali ambalo mimi kila mara napenda kulizungumza, UKIMWI. Kutokana na Jeshi letu hatuwezi kusema kwamba kupima UKIMWI hiari. Kazi ya Jeshi siyo kazi za aina nyingine yoyote. Mwanajeshi anatakiwa kila mara awe tayari kwa lolote ambalo

litajitokeza. Mwanajeshi tunaona kwamba anakwenda kazini, anapimwa hadi UKIMWI kabla ya kuajiriwa. Ina maana kama amepata ndani ya kazi, Mkuu wake wa Jeshi anawajibika kumjua kwamba Askari wangu fulani ana matatizo fulani lakini ukisema kwa hiari ina maana hatutakuwa na Jeshi imara, kwa sababu linaweza kutokea tatizo tukampeleka mtu hajafika anakotakiwa akafa njiani. Hatuwezi kabisa, suala hili tuondowe, ikiwa yeye mwenyewe Askari anajua au hajui, lakini Jeshi kupima UKIMWI lisiwe jambo la hiari, hilo moja.

Mheshimiwa Spika, la pili katika Bunge hili nilizungumza kutokana na maeneo yanayochukuliwa na Jeshi na moja nikasema sehemu ya Cheju ambayo ndiko kunakofanywa mafunzo. Nilipata barua shughuli ilishamalizika, nimewauliza wananchi wa Cheju hakuna anayenijibu muafaka ina mana tulichukua watu wasio masikio ambao hawasikii, tulichukua watu wasio macho ambao hawaoni. Mheshimiwa Waziri ninakuomba tufanye kikao Cheju, wananchi wa Cheju akiwemo na Mbunge wao na wananchi wa Unguja Ukuu tuelewe suala hili limefikia wapi ili tupate muafaka. Hatuna matatizo kwa sababu Jeshi ni letu, nchi yetu na tunataka Jeshi letu liwe imara kwa kuwa ni sehemu wanapata mafunzo kwa vyovyote hakuna matatizo tutafika mahala muafaka. Hata hivyo na sisi tushirikishwe kama kiongozi wao wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali hivi sasa kuchukua vijana kijiunga na JKT na hivi sasa naishukuru zaidi kwa sababu hata kule Zanzibar wanafika sana kuwachukua hawa vijana. Ninaloomba isijekuwa sababu hii ya kujaizika JKU. Ikifika wakati kwamba vijana labda wanachukuliwa sehemu moja ya Muungano kwa kuwa vijana nao Wazanzibar nao wamo humu kwa hiyo mtachukua hukuhuku bila ya kufika kule Zanzibar kuchukuliwa na wale vijana wa JKU. Hili nasisitiza sana kwa sababu kuna malalamiko chini kwa chini kidogo katika uchukuzi wenyewe. Kwa hiyo, hili nataka ulitilie maanani kabisa liwe jambo la maana ili wananchi wajenge imani kutokana na Jeshi lao na nchi yao matatizo na bughudha ziweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, mwisho. Nakushukuru wewe Waziri mwenyewe kutokana na harakati zaidi na jithada zako unazofanya na Mungu akujaze kheri zaidi uweze kufanikisha shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sabreena atafuatiwa na Mheshimwia Ridhiwani halafu Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabsia nilitaka niwatoe hofu Watanzania na Jeshi letu la Ulinzi kwa ujumla kwamba Wapinzani hawapo hapa kwa sababu ya kuvunja amani ya Tanzania, lakini wako hapa kwa ajili ya kushirikiana na Serikali iliyopo na Jeshi lenyewe. Napenda Jeshi letu tulitambue, kama Wapinzani tutachukuwa nchi 2015 basi hii *ration allowance* ya Sh. 7,500 kwa Mwanajeshi itakuwa ni mwanzo mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tumeangalia maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tumeona vifaru, tumeona makomandoo wenye misuli, wenye nini lakini komandoo yule Sh.7500/- inamtoshaje kwa siku. Wanasiasa wamekaa hapa wanakaula zaidi ya Sh.250,000/- kwa siku. Inakuwaje leo Wanajeshi ambao wanafanya kazi kubwa ambao tunawategemea, ambao tukitaka kuwashughulikiwa Wapinzani tunawafuata wao unawapa Sh.7,500 kwa siku? Mheshimiwa Waziri Mwinyi, naomba kiwango hiki kiongezeke na kisipoongezwa mimi nitakuwa wa kwanza kukamata shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa kusema haya najua uchungu wa JKT, nimepita Bulombola, Askari toka saa kumi na moja alfajiri anavaa buti mpaka saa nne usiku. Wana kazi ngumu sana, wanaishi kwenye mazingira duni, hawana maji, hawana umeme. Kwanza, hivi ninavyoongea Ziwa Tanganyika lipo katika hati hati ya kukumbwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira. Kundi zima la watoto ambao tulikuwa JKT wanaondoka pale kwenda kufanya shughuli zao zote za kutwa nzima kichwani mpaka mguuni katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimwia Spika, miaka hamsini ya Uhuru Majeshi yetu yanaendelea katika hali hii, hapana huu siyo uzalendo. Uzalendo tulifundishwa ni pale ambapo unamuona mwenzako anaanguka unamshika mkono. Haiwezekani kwenye taifa hili kuna watu wanaishi maisha ya juu sana lakini vyombo vya Ulinzi kama hivi tunaviacha Wanajeshi wetu wamekuwa katika *status* ya chini sana. Hili suala halikubaliki, kama sisi ni wazalendo na tunaipenda nchi yetu, basi tuangalie watu ambao wanatulinda wakati wa raha na shida. Vinginevyo utakuwa ni unafiki na kutaka kulitumia Jeshi la nchi hii kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, suala la pili, tuliona vifaa vya maonesho vingi na ningependa Waziri Mwinyi aniambie kwenye randama yake, vifaa hivi vimewekewa bajeti ya vilainisho? Tukiangalia miaka miwili, mitatu iliyopita kuna mabomu yalianza kulipuka yenyewe kwa yenyewe. Mimi siyo mtaalam wala si Mwanasayansi siwezi kusema ni sababu gani lakini inawezekana ukosefu wa hii bajeti ya vilainisho. Sasa Waziri Mwinyi utuambie mwaka huu, vialinisho vya yale magari, matrekta na kadhalika tulioyaona siku ya maadhimisho bajeti hiyo ipo?

Mheshimiwa Spika, suala lingine nilitaka kuiomba Wizara, tumeona vitu vingi, tumeona vifaa ambavyo vinaweza kuchimba visima kwa muda mfupi sana, tumeona madaraja ambayo yanaweza yakasaidia nchi kwa muda mfupi sana. Mimi naomba badala ya vifaa hivi kuendelea kuvifungia katika makambi mbalimbali ya nchi yetu na Watanzania wengi wamekuwa na shida ya maji, Jimbo la Ubungo pale ndugu yangu Mnyika amekuwa akipiga kelele miaka yote kuhusu shida ya maji, vijijini huko, kambi ya Buhombola nimepiga kelele nako maji hakuna, kwa nini vifaa hivi ambavyo vinaweza vikachimba maji kwa muda mfupi kama tulivyoonyeshwa pale msivipeleke huko vikafanya kazi badala ya kuviweka ndani vikisubiri vita na nchi hii vita haitatokea kwa sababu Watanzania tunapenda amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusu *tender* mbalimbali zinazoendelea nchini. Kumekuwa kuna uchakachuaji mkubwa sana wa ujenzi wa barabara na ujenzi mwingine mbalimbali unaoendelea. Barabara inajengwa leo, kesho kutwa imeharibika. Tunawatumiaje Wanajeshi wetu, tunawatumiaje wataalam wetu ambao hata mama yangu mama Anna Abdallah kasema kuna wataalam wa hali ya juu sana katika makambi yetu, kwa nini tunawaacha kule na tusiwape *tender* hizi mbalimbali kama hizi za ujenzi wa madaraja, barabara na sehemu nyingine. Wamejenga daraja zuri Kinyerezi, wamejenga daraja zuri Kawe na maeneo mbalimbali ya nchi, kwa nini tunawaacha watu hawa wanabaki na utaalam wao mpaka wanafariki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilitaka kuliongelea ni suala la pesa za uhamisho. Nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri akielezea katika ukurasa wa 14 mapambano dhidi ya UKIMWI. Hatuwezi kutegemea hata siku moja janga la UKIMWI katika nchi yetu likaisha kama tutahamisha Wanajeshi mbali na familia zao miaka miwili mpaka minne pesa ya uhamisho wa kuleta familia yake haijapatikana. Huyu Mwanajeshi ni binadamu anakula, ana *hormone,* anahitaji huduma nyingine kama Watanzania wengine wanavyozipata, ataishije Mwanajeshi huyu ni lazima ataanza kutoka nje ya ndoa yake, atakutana na maradhi.

Mheshimiwa Spika, sisi tulivyoingia JKT, jambo la kwanza ilikuwa unanyoosha mkono unapima damu na upimwa vipimo vyote majibu yanatoka uko salama, unaingia. Hata hivyo, tunakuja kujiuliza kama Wanajeshi wanaingia wakiwa *clean* wanapatia wapi maradhi haya na kule Jeshini kuna *system* ya kupimwa kila mwaka lakini maradhi haya wanayapata kwa sababu familia zao hamzipeleki na wao ni binadamu wanachepuka wanapambana na maradhi. Kwa hiyo, fedha za uhamisho wa familia za Wanajeshi Mheshimiwa Waziri, naomba iwe ni kipaumbele. Hatuwezi kutegemea watu watulinde kama afya zao zitakuwa *dhooful hali,* watakaa nyuma, wataumwa, kwa hiyo lazima muwape pesa watu hawa waweze kuhamishika na siyo kutegemea tu kwamba kila siku ka sungura kadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kasungura wa nchi siyo mdogo, tumeona hapa ripoti ya CAG inasema asilimia kumi ya bajeti ya nchi hii ni misamaha ya kodi. Tunasamehe misamaha ya kodi Wanajeshi wetu tanawaambia sungura mdogo. Hata ukiangalia bajeti ya maendeleo ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri ni asilimia 20 tu katika mafungu yote matatu ndiyo imepatikana mpaka Machi 30 mwaka huu. Sasa huyu sungura mdogo huku tunasamehe asilimia kumi ya bajeti ya nchi hii haieleweki Mheshimiwa Waziri! Kwa hiyo, ningeomba hilo nalo ulitolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni ajira. Kama unavyokumbuka sasa hivi tuna wanafunzi wengi wanaingia kwa mujibu wa sheria katika makambi yetu. Wanafunzi wale wanavyomaliza, acha wale wa mujibu wa sheria, lakini hata hawa wa mafunzo ya kawaida, kumekuwa kuna ajira chache sana kwa Wanajeshi wetu wanaomaliza mafunzo, huku kundi kubwa likiachwa mtaani.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wanafundishwa utumiaji wa zana mbalimbali, wanafundishwa risasi, wanafundishwa mabomu, wanafundishwa jinsi ya kujihami, wanafundishwa kila kitu. Kundi lile hulipi ajira, unalipeleka mtaani, likakae. Leo hii akipata mtu wa kumshawishi akamwambia sehemu fulani kuna milioni 100 tukachukue, mtu huyu atakataa wakati amepigika ana hali ngumu? Kwa hiyo, ni vyema sasa watu hawa waweze kupatiwa ajira za kutosha ili sasa na wao waweze kujua kabisa kwamba nchi hii, Serikali yao inawajali na siyo propaganda.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ninataka kuzungumzia, ni malipo kwa Askari ambao wanaokwenda *course*. Utaratibu wa zamani ilikuwa Askari wale wakifika kule, chakula wanakuwa wanalipa na kunakuwa kuna fungu la chakula kutoka Serikalini lakini sasa hivi wanajitegemea wenyewe kutoka mifukoni.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ningependa Waziri ashughulikie masuala haya ambayo nimeya-*address*. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa ikigonga kengele maana yake kimya, siyo zaidi ya hapo. Mheshimiwa Ridhiwani, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tutaangalia muda.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kuniona maana nimesimama sana lakini *may be* umbo langu sionekani hata hivyo, nikushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kipekee nirudie tena kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chalinze kwa kunipa nafasi ya kuwawakilisha ndani ya Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti, mimi namuunga mkono na ninaunga mkono hiyo hoja nzima ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niendelee kuwatia moyo wapiganaji wetu, Wanajeshi wetu ambao kwa namna moja ama nyingine wameendelea kutupa heshima, nchi yetu hasa wanapotuwakilisha nje ya mikapa yetu. Pia nawashukuru kwa kutuonyesha kwamba nchi yetu bado iko salaam maana yale mambo ya tarehe 26, ni mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwatoe wasiwasi wenzetu wa upinzani kule, utamaduni wa kuonyesha vifaa mlivyonavyo ni utamaduni wa kawaida kabisa duniani. Si jambo jipya, China wanafanya hivyo, Russia wanafanya hivyo, Korea wanafanya hivyo na Amerika pia wanafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la msingi zaidi lazima waelewe kwamba iliyoonyeshwa pale ni sehemu ndogo ya vitu tulivyo navyo. Lazima mfahamu hilo na ndiyo nchi inapopata heshima yake kwamba mnaonekana mna nguvu ya namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nilikuwa nataka nichangie kidogo katika bajeti hii, juu ya mgogoro wa ardhi uliokuwepo baina ya wanakijiji cha Pongwe Msungura na Kambi ya Jeshi Kihangaiko. Katika kambi ile mgogoro huu ni wa siku nyingi kidogo, mazungumzo yamekuwa yanafanyika lakini kwa mara ya mwisho makundi haya mawili yalikutana miaka mitatu iliyopita. Makubaliano ilikuwa ni kwamba wananchi wa kijiji kile cha Pongwe Msungura waseme wanataka mpaka wao uwe wapi. Walipata nafasi ya kupendekeza na timu yako Mheshimiwa Waziri ilirudi kwenda kuisoma vizuri ile *proposal* ya wananchi ili waje watoe majibu, sasa ni miaka mitatu hatujapata majibu yale. Nimeangalia bajeti ya Wizara, nimeangalia bajeti hata ya Kambi ya Upinzani, pamoja na mambo mazuri wanayosemea juu ya nchi hii lakini hili la Kihangaiko sidhani kama wameliona la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamaliziamalizia kutoa mambo yake, basi angewaeleza wananchi wale wa kijiji cha Pongwe Msungura, Msata kule, wapate kuelewa nini hatima ya ardhi ambayo ninyi wenyewe mlikwenda mkakutana nao na mkakubaliana nini hatima ya ardhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba, wananchi wa jimbo la Chalinze wanaendelea kukupongeza tena hasa kwa kuendelea kuaminiwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia kwa mchango mkubwa ambao Jeshi letu linatoa kwa nchi hii. Kwa kweli mimi binafsi nimalize tu kwa kumpongeza sana *General* Mwamnyange na wenzake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamuita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushuruku na nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake, Mwenyekiti na Kambi ya Upinzani imetoa hutoba nzuri sana, wote nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka ku-*share experience* kidogo tu. Mwaka 2005, tulikwenda Ujerumani tukakutana na Mkuu wa Jeshi. Sasa nilimkuta kwenye Kamati ya Bajeti ya Ujerumani akielezea vifaa vyote na kila kitu walichonacho. Sisi tukamuuliza, mbona unatoa habari zote ulizonazo ndani, akasema, katika siri ya Jeshi ni mambo matatu, kwanza ni *smartness* ya Jeshi lako, muda utakaotumia silaha na silaha utakayoitumia kwa wakati gani, hiyo ndiyo siri yaliyobaki mengine yeye alisema kila mtu anayajua, nilitaka kuendelea kutoa *experience* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza nizungumzie suala la *Ali Khamis Camp*. Napenda nichukue nafasi hii kwanza kulishukuru Jeshi pale lilipo hasa kwa kuanzisha shule, shule ambayo kwa kweli imekuwa ni kivutio kikubwa kwa wananchi wa Pemba, imewasaidia na hivi karibuni nategemea kuwapelekea *computers,* kuanzisha darasa la *computers* pale. Nimshukuru sana Mkuu wa Jeshi naye kwa kutoa msaada, naomba tumalizie yale madarasa matatu yaliyobaki ili sasa wananchi na Wanajeshi walioko pale wapate huduma nzuri. Ni shule nzuri na inafanya kazi vizuri sana, nawapongeza na naomba msaada uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ningeomba vilevile Wanajeshi pale wanapokaa katika mazingira wanayokaa, wajitahidi sana kwenda na mila na desturi za watu wanaokaa pale. Kwa sababu katika maeneo yetu haya tunachanganyika sana na watu na kila kabila, kila watu wana tabia zao. Kwa mfano, pale nyumbani kwetu, ukionekana unakunywa pombe hovyohovyo au kila mahali, wananchi wanaona si ustaarabu waliouzoea. Kwa hiyo, nafikiri kuna mazingira fulani ni lazima wayatazame wanapoishi na watu. Watu wanapenda wawe nao lakini ni vizuri wakaangalia mazingira wanaoishi nayo yaende nayo pamoja, hili naiomba sana litazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni suala la Mzinga na Nyumbu. Hizi taasisi zilianzishwa muda mrefu na madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwao ni kwamba ifike mahali tuweze kujitegemea wenyewe, hayo ndiyo malengo makubwa katika silaha, katika vifaa mbalimbali ambavyo tutazalisha lakini kwa muda mrefu sana *programs* hazikwenda vizuri. Kwa bahati mbaya ukiangalia *development* bajeti kwa ujumla yote, ni asilimia 50 ndiyo *across* Wizara zote. Sasa hapa kuna tatizo la msingi, tatizo la kwanza nililoliona, ukitazama katika vitabu vyote vya bajeti na hii nafikiri ni kwa Kamati zote, utakuta kuna *cut and paste*. Unaweza kuwa na mafungu matano, chukua Ulinzi tu hapa, yote yana *figure* moja mwaka jana na mwaka huu, hiyo haiwezekani. Kwa hiyo, kuna kazi haijafanywa vizuri ya kufanya *budgeting* na hili nalisema wakati wote, mkikaa kwenye Kamati, mkikaa Wizarani tazameni mafungu yote matano, *figure* ni hiyohiyo moja miaka miwili, mitatu, haiwezekani lazima kukutakuwa na mabadiliko, ukizisoma hapa utazikuta namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara yenyewe na hata Kamati zetu, zikae sasa ziangalie haya mafungu ya *budget*, je, ni kweli ni *actual* au watu wamechoka, wanachukua *figure* ya mwaka jana wanaiweka tu pale. Mimi nafikiri hili ni tatizo la msingi na ndiyo tunaona kuna matumizi mengine katika Wizara mbalimbali haziendi sawasawa kwa sababu tu kuna ile *cut and paste* kila mahali. Hili ningeomba kwa ujumla liweze kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine napenda niwapongeze Wanajeshi wetu wote kwa ujumla. Nchi yetu imebaki katika amani na yule ambaye anafikiri kwamba vita ni vizuri, basi akawaulize wale ambao wako kwenye vita, havichagui. Ukiangalia sasa hivi hali ya watu Syria, watoto wanavyobakwa, wanawake wanavyobakwa, maisha yao yalivyo magumu, ni kwa sababu kuna vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, ili kuvisaidia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, viongozi, wananchi, lazima tujitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kabisa tunaweka

matamshi yetu, kauli zetu zile ambazo zinaendana na ulinzi wa nchi yetu. Kwa sababu jambo dogo tu linaweza likachafua hali ya hewa na matatizo yakatokea na watakaoathirika ni wanawake na watoto kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana, vijana wetu wamejitahidi lakini sisi tunatakiwa kutoa mchango mkubwa zaidi kuwasaidia wao wadumishe amani hii.

Mheshimiwa Spika, suala la kujitegemea SUMA JKT. Bahati mbaya hatujapanga *program* nzuri sana na ningeomba sana Wizara isaidie suala hili kwamba hebu tuseme mwaka huu tunataka kulima hekta ngapi, mahitaji yetu ni yapi, halafu tuone kile kilichopatikana basi nacho kinatunzwa vizuri. Utunzaji wa mapato bado haujakuwa mzuri katika taasisi nyingi sana. Mimi nafikiri ndiyo maana hakuna *development*, fedha zinazopatikana haziingii katika kuendeleza kwa sababu hakuna makusanyo mazuri. Sasa mimi nafikiri hili lazima Waziri alisimamie vizuri, yale malengo yatafikiwa tu kama kile unachokipata unakitumia vizuri. Unauza silaha, ujue silaha zimeuzwa na kilichopatikana kimekwenda wapi. Mimi nafikiri kama hakuna *retention scheme*, tungekaa tukaangalia *retention scheme* ifanyike, ili kuhakikisha fedha inayopatikana kuna maendelezo kwa kile ambacho kinataka kufikiwa. Vinginevyo tutakuwa kila siku tunakwenda na utaratibu huu ambao tunangoja ruzuku kutoka Serikalini, jambo ambalo halitasaidia sana. Kwa hiyo, mimi nilifikiri wajipange katika *proper planning* ya kuhakikisha tunazalisha kitu ambacho tunakihitaji na tunakihitaji kwa madhumuni gani.

Mheshimiwa Spika, tuliona ndugu zetu wale makomandoo pale, pamoja na watu kusema wanalipwa pesa ndogo lakini huwezi kuwa komandoo kama hushibi, inaelekea wanashiba vizuri. Mazingira wanayotengeneza wenyewe Askari wahakikishe wanashiba, ndiyo yale tuliyoyaona, huwezi ukawa na njaa ukafanya kazi ile, hii kazi ni ngumu sana na lazima Askari wafanye kazi katika mazingira magumu ili waweze kupambana katika maisha yao ya kazi, kwa sababu wao ni watu wa kupambana kila wakati. Kwa hiyo, usichukulie Askari kuishi maisha magumu ukafikiri ni tatizo lakini ndiyo hali halisi ya utendaji wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimuite Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri *comrade* Mwinyi pale kwa *speech* yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa hali itakavyokuwa katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda. Pia niipongeze sana hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo hata rafiki yangu *Captain* Chiligati ameisema pale, kwa kweli imekuwa hotuba nzuri sana ambayo imetoa mwelekeo wa nini tufanye ili twende mbele badala ya kulumbana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nianze na suala zima la bajeti. Inaonekana kuna tatizo kubwa kwa sababu unapotenga bajeti, halafu huipeleki bajeti, sijui maana yake ni nini? Ukiangalia vitabu kwa mfano labda fedha za maendeleo katika JKT, JKT ambayo hapa nyuma ilikuwa imelala lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama ilikuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Lowassa kwa wakati ule ambapo sisi wengine tulikuwa Wajumbe wake pamoja na msukumo mzuri wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Serikali iliamua kurudisha tena JKT lakini sasa unairudisha kwa maneno au unairudisha kwa kuiwezesha? Ikiwa uliitengea shilingi bilioni sita, unapeleka milioni 525, hiyo ni asilimia 8.8, hivi kweli unakusudia kuifufua JKT, kuiendeleza JKT, au maana yake nini? Mimi nataka niwe mtu wa mwisho kusema kuwa fedha haipo, fedha inapatikana lakini labda vipaumbele vinakuwa ni vidogo. Sasa mimi nahisi tunaweza kuchezea mambo mengine lakini hatuwezi kuchezea vitu vinavyohusiana na ulinzi. Kwa sababu kwenye JKT ndiko ambako

tunachukua vijana wa kuwapeleka kwenye Jeshi na kwenye JKU kwa upande wa Zanzibar tunafanya hivyohivyo. Sasa vyombo viwili hivi lazima uvipe bajeti ya kutosha ili uweze kupata vijana wa kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mwingine wa Ngome, imesemwa hapa, Ngome walitengewa shilingi bilioni 10, wamepewa shilingi bilioni 1.6 mpaka juzi, hii ni asilimia 16 tu ya bajeti! Sasa katika asilimia 100, unapeleka asilimia 16, *are we real serious or what!* Kwa sababu sehemu nyingine tunaona fedha zinatumika sana tu, sana tu, lakini kama unatumia fedha sehemu nyingine basi na kwenye ulinzi upeleke.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye wastaafu, wastaafu wamekuwa wakipigiwa kelele na wakati mwingine wamekuwa wakipiga kelele wenyewe lakini bado inaonekana kuna tatizo na kama tatizo ni sheria basi mimi nafikiri hii sheria sasa tunahitaji kubadilisha. Mheshimiwa Waziri ninaomba uiombe Serikali ilete haraka mabadiliko ya sheria vinginevyo utakuwa unalaumiwa kila siku. Mfano umesema hapa wewe leo ulipokuwa ukijibu swali la Mheshimiwa Rukia, kuwa wale Askari wanaokufa vitani, wajane wao wanalipwa asilimia $^{1}/_{6}$ ya mshahara wao na watoto $^{1}/_{8}$ ya mshahara wao, lakini mshahara wa Askari wa mwaka 1978 unatoa $^{1}/_{6}$ ya mshahara ule, hivi kweli mtu huyo leo atapata fedha gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri wakati umefika wa kuangalia mshahara wa wakati huo halafu ndiyo utoe, vinginevyo utamwangamiza tu. Sisi tunaelewa hapa, viongozi wastaafu wanalipwa kiwango fulani cha mshahara wa kiongozi aliyepo madarakani kwa wakati huo. Huwezi kuchukua mshahara wa Waziri Mkuu wa mwaka 1961, ukasema umlipe asilimia 80 ya mshahara huo leo, utakuwa umempa fedha ngapi? Sasa kama ninyi wakubwa mnatengenezeana na hawa wadogo muwatengenezee pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano hai wa *Staff Sergeant* aliyetumikia taifa hili kwa miaka 32, anastaafu, akistaafu anapelekewa pensheni kwa mkupuo wa miezi mitatu, mitatu, anapewa shilingi laki tatu na elfu hamsini. Hii maana yake ni shilingi laki moja na kumi na saba elfu kwa mwezi, ni shilingi elfu nne kwa siku. Hivi kweli hizi shilingi elfu nne kwa siku, nani katika sisi hapa anatumia shilingi elfu nne kwa siku? Nani anatumia shilingi elfu nne kwa siku hapa ndani? Sasa kama inatukuna sisi hapa kuwa hatupati fedha, tunapiga kelele sana, basi pia itukere na kwa wenzetu walioko mtaani maana yake sisi angalau tuko katika Serikali hapa tuna mambo mengi ya kufanya, lakini wenzetu kule, ndiyo matokeo yake sasa wanakuwa walinzi katika hoteli, tena walazalilishwa sana. Wala mimi sidhani kama hoja sijui ni kuwatafutia mikopo, hoja ni kuwawezesha, wapeni mishahara mikubwa, wapeni pensheni ya kujulikana ili waweze kujitegemea, vinginevyo tutakuwa tunawaonea tu na kuwadhalilisha. Askari aliyetumikia nchi yake ili umtunze na aone kuwa umemsaidia aweze kuishi hata baada ya kuacha kazi, kama ambavyo sisi tunataka. Sasa kama jambo unalitaka wewe basi na mwenzako umtakie lilelile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilipongeze sana Jeshi, inaonekana wazi kuwa *CDF* Mwamnyange anafanya kazi nzuri sana. Hata huku mitaani ile migongano baina ya Wanajeshi na raia sasa imepungua kwa sababu nidhamu inadhibitiwa vizuri sana. Mambo ya Askari kwenda mahali wakalewa, wakatafuta wanawake, wakapiga watu baadaye, hilo halipo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi niseme, hata migogoro ya nchi jirani hizi ambazo vijana wetu wamepelekwa, ukawasikia wamenuna, wanakuwa wakali ni kwa sababu vijana wako makini katika kazi walizopewa. Kama kaambiwa alinde hapo na bwana mkubwa alikuwa kifaidika na hapo panapolindwa, basi alie tu maana vijana ndiyo wamepewa jukumu hilo na

wanaifanya itakiwavyo. Mimi napenda niwapongeze sana kwa kazi nzuri na ili pongezi hii iwe ina maana, basi hizi fedha ambazo zimekusudiwa kupelekwa, zipelekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia na hili ni la kwako, utamaduni wa Bunge lako umebadilika sana. Kauli iliyotolewa jana imenishtua. Kiarabu *Lusu* maana yake ni mbwa, *is that means* yule Mbunge pale anawaita watu mbwa humu ndani halafu watu wengine wanacheka! *This is very serious.* Lazima uwe mkali, usimruhusu mtu humu ndani anatumia Bunge hili kutukana watu. Hakuna *university* ya kujifunza matusi, *universities* zote zinatoa taaluma nzuri tu. Sasa kama wanakuja watu hapa wanajifanya ni wakereketwa wanatukana watu, mtu yeyote anaweza kutukana, lakini siyo ustaarabu, lazima tuwe na nidhamu, lazima tujue kuwa sote humu ndani ni watu wazima, haiwezekani hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chomboh amezoea, ni mtaje kwa jina, kutukana watu hapa, *this is not fair!* Sisi tunamheshimu yeye na jamaa zake, kwa nini anatutukana, kwa nini anatukana watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Matusi mengine, sijui ya Kiarabu, watu wengine hawajui hata kama ni matusi. *(Kicheko)*

Kwa mfano, mimi sikuelewa anasema nini, Rajab ilibidi nim-*stop* kwamba bwana hebu changieni hoja, mimi sikuelewa hata kama ni tusi.

Sasa baada ya kipindi cha maswali kufuatana na *Order Papers* zetu, naomba tusikilizane, kawaida katika *Order Papers* zetu baada ya kipindi cha maswali, huwa inakuwa ni Kauli za Mawaziri. Sasa leo hatukufanya hivyo kwa sababu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake walikuwa safari mpaka jana, wameingia usiku na Kanuni ile ya Kauli za Mawaziri ile *document* inatakiwa iwe imechapishwa na inagawiwa kwa Wabunge wakati inasomwa, haukuwa tayari. Kwa hiyo, kwa kutimia mamlaka yangu sasa hivi nitamuita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii aweze kutoa Kauli kuhusu tatizo lile la ugonjwa ambao upo na ni swali ambalo hatuwezi kusubiri, ni jambo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri!

KAULI ZA MAWAZIRI

Kauli ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu Ugonjwa wa Dengue *(Dengue Fever)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kufuatia maelezo yaliyotolewa jana hapa Bungeni na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, naomba kutoa maelezo ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapenda kutoa taarifa kwa umma juu ya mwenendo wa ugonjwa wa *dengue* yaani *dengue fever* hapa nchini. Ugonjwa huu umethibitika baada ya sampuli zilizochukuliwa kutoka watu waliohisiwa kuwa na ugonjwa huu jijini Dar es Salaam kupelekwa kwenye maabara yetu Dar es Salaam na kuthibitishwa kuwa na virusi vya homa ya *dengue* mnamo mwishoni mwa mwezi Januari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa idadi ya wagonjwa ambao wamethibitishwa kuwa na ugonjwa huu kuanzia Januari 2014 hadi sasa ni 458 na vifo vitatu. Kwa wiki iliyoishia tarehe 9 Mei, 2014, idadi ya wagonjwa waliogundulika Mkoani Dar es Salaam kwa wiki moja ni 60. Wagonjwa arobaini na wawili wakiwa Kinondoni, kumi na wanne Temeke wanne Ilala na idadi ya wagonjwa waliopo wodini mpaka sasa ni sita kutoka Temeke, sita Amana na wanne Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi jirani hadi kufikia tarehe 10 Mei, 2014, takwimu zinaonesha nchi za Msumbiji na Kenya kumegundulika kuwa na wagonjwa katika maeneo Cabo Delgado pale Msumbiji na wagonjwa 30 Mombasa kule Kenya. Kwa hiyo, Msumbiji wanao wagonjwa 100.

Aidha, mlipuko wa ugonjwa huu si mpya hapa nchini kwani uligundulika kwa mara ya kwanza mwezi Juni 2010 Mkoani Dar es Salaam ambapo idadi ya watu 40 walithibitika kuwa na ugonjwa huu. Pia kati ya mwezi Mei na Julai 2013 waliweza kupatikana wagonjwa 172 ambao walithibitishwa.

Mheshimiwa Spika, homa ya *dengue* ni ugonjwa unaosababishwa na kirusi ambacho kinaendezwa na mbu aina ya *aedes*. Dengue ni ugonjwa uliosambaa duniani katika nchi za ukanda wa joto. Takriban asilimia 40 ya watu wote duniani wanaishi katika maeneo yenye ugonjwa huu. Takwimu za Shirika la Afya duniani zinathibitisha kuwa takriban matukio milioni tano ya *dengue* yanatolewa taarifa kila mwaka ambapo ni *dengue* kali. Watu watano hadi laki tano hulazwa hospitali kwa kuathirika na *dengue* kali. Homa ya *dengue* imeshatokea katika nchi zipatazo 34 katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, hapa Afrika *dengue* ni ugonjwa unaojulikana kwa kiwango kidogo sana licha ya kwamba milipuko ya kwanza imetokea tangu mwanzoni mwa karne ya 19. Matukio ya ugonjwa huu yameongezeka Afrika tangu mwaka 1980. Matukio mengi yalitokea nchi za ukanda wa Mashariki mwa Afrika ikiwa ni pamoja na Msumbiji, Somalia, Kenya, Comoro, Djibouti na Tanzania. Ikumbukwe kuwa jina *dengue* linatokana na neno la Kiswahili 'dinga' linalomaanisha ugonjwa unaotokana na pepo yaani kudinga pepo. Mabaharia wa Kispanish waliokuja kwenye pwani ya Afrika Mashariki walirudi kwao na kuiita *dengue*.

Mheshimiwa Spika, dalili za ugonjwa huu ni homa, kuumwa kichwa, maumivu ya viungo na uchovu. Dalili hizi huanza kujitokeza kuanzia kati ya siku tatu na kumi na nne tangu mtu anapoambukizwa kirusi cha homa ya *dengue*. Kwa wakati mwingine dalili za ugonjwa huu zinaweza kufanana sana na dalili za malaria, hivyo basi, wananchi wanaombwa kuwa wakipata homa kuhakikisha wanapima ili kugundua kama wana vimelea vya malaria au la ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna aina tatu tofauti za ugonjwa huu kama ifuatavyo:-

(i) Homa ya *dengue* ya kawaida (*dengue febrile illness)*. Aina hii huambatana na dalili kuu tatu za homa kali ya ghafla, kuumwa kichwa na maumivu ya viungo au uchovu. Aidha, kwa Tanzania hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa waliojitokeza wana dalili hizi.

(ii) *Dengue* ya damu (*dengue haemorrhagic fever)*. Aina hii ya homa ya *dengue* huambatana na dalili za mgonjwa kutokwa damu kwenye fizi au puani. Vilevile kutokwa na damu chini ya ngozi yaani *petechial hemorrage*. Iwapo mgonjwa huyu ataumwa sehemu yoyote ni rahisi kwake kupoteza damu nyingi kupitia kwenye mchubuko.

(iii) *Dengue* ya kupoteza fahamu *(dengue shock syndrome)*. Aina hii ya homa ya *dengue* huambatana na mgonjwa kupoteza fahamu ambayo hupelekea mgonjwa kuishiwa fahamu. Dalili hizi zinaonekana kwa mgonjwa mmoja kati ya wagonjwa mia nne waliokwisha kuthibitishwa kuwa na ugonjwa huo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kirusi cha homa ya *dengue* kinaambukizwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kwa kuumwa na mbu wa aina ya *aedes* na hapa kwetu ni *Aedes Aegypti*. Mbu huyu anaishi katika mazingira ya makazi ya binadamu, huuma wakati wa mchana ndani ya nyumba au kwenye maeneo yenye vivuli hususan majira ya asubuhi na jioni kabla jua halijazama.

Mheshimiwa Spika, mbu huyu anazaliana katika maji yaliyotuama hasa kwenye vyombo vya nyumbani, makinga maji ya paa za nyumba yaani *gutters*, matairi ya magari ambayo bahati mbaya yametupwa hovyo, ndoo, vikopo na kadhalika. Kwa bahati mbaya mbu huyu huweza kuzaliana katika vifaa vidogo ambavyo watu wengi huvidharau. Hivi ni pamoja na makopo ya kuoteshea maua, vikombe, vifuu vya nazi na kadhalika. Majani mapana yanayohifadhi maji ni mazingira mazuri kwa kuzaliana kwa mbu huyu, hivyo maeneo ya bustani si ajabu kuwa mahali pazuri kwa mbu hawa.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu hauambukizwi kwa kumhudumia mgonjwa au kugusa maji yanayotokana na mgonjwa. Homa ya *dengue* inaweza kutibika kama mgonjwa atapelekwa hospitali mapema na kupatiwa matibabu ya haraka. Hakuna dawa maalum ya ugonjwa huu wala chanjo bali mgonjwa anatibiwa kutokana na dalili ambazo zimeambatana na ugonjwa huu kama vile homa, kupungukiwa maji au damu. Endapo mgonjwa atachelewa kupatiwa matibabu anaweza kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa homa ya *dengue* ni kwanza kwa kuangamiza mazalia ya mbu kwa kufukia madimbwi ya maji yaliyotuama au kunyunyizia viuatilifu vya kuua viluwiluwi vya mbu kwenye madimbwi hayo. Pia ondoa vitu vyote vinavyoweza kuweka mazalia ya mbu kama vile vifuu vya nazi, makopo, magurudumu ya magari yanayotupwa hovyo. Fyeka vichaka vilivyo karibu na makazi ya watu. Hakikisha maua yanayopandwa kwenye makopo au ndoo hayaruhusu maji kutuama. Funika mashimo ya majitaka kwa mfuniko imara. Safisha gata za paa la nyumba ili kutoruhusu maji kutuama.

Mheshimiwa Spika, pili ni kujikinga na kuumwa na mbu kwa kutumia viuatilifu vya kufukiza mbu yaani *mosquito repellants*. Vaa nguo ndefu kujikinga na kuumwa na mbu. Tumia vyandarua vilivyosindikwa viuatilifu kwa wale wanaolala majira ya mchana na hasa kwa watoto. Weka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Wizara. Hatua za dharura, moja, ni kwa kufanya uratibu. Timu ya taifa ya maafa inayoshirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na wadau wa maendeleo hukutana kila mara mbili kwa wiki kutathmini mikakati na dharura ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Spika, pili, ni uelimishaji na uhamasishaji wa jamii. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitoa tamko la Serikali kwa nyakati tofauti kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa *dengue*. Tamko la kwanza lilitolewa kwenye vyombo vya habari tarehe 4 Februari, 2014 na Machi, 2014. Kuendelea kutoa taarifa ya tahadhari ya ugonjwa huu kwa kupitia Mganga Mkuu wa Mkoa na Wilaya zote kwa Tanzania Bara. Aidha, taarifa hii pia inajumuisha namna mgonjwa anavyoweza kutambulika yaani ainisho la ugonjwa, tunaita *standard case definition*. Ukweli kuhusu ugonjwa ambao ni *fact sheet* chini ya mwongozo wa *WHO* na mwongozo kwa watumishi wa afya na namna ya kuchukua sampuli, vipeperushi, vinavyoelezea jinsi ya kujikinga na maambukizi ya

ugonjwa huu vimetolewa. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia redio na luninga. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji wameendelea kutumia Maafisa wa Afya ikiwemo kata na uongozi wa mtaa kuwaelimisha wananchi namna ya kudhibiti ugonjwa huu kwa kutumia vipaza sauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mafunzo kwa wataalam wa afya. Kuendelea kutoa elimu ya afya kwa watumishi wa afya ikiwa ni pamoja na Madaktari, Mafundi Sanifu wa maabara juu namna ya kutambua ugonjwa huu. Aidha, watumishi wa hospitali za Muhimbili, Mwananyamala, Amana na Temeke wameshapewa mafunzo haya na bado wanaendelea kupewa kupitia mikutano yao ya asubuhi yaani *clinical meetings*. Mafunzo haya pia yanaendelea kutolewa kwa vituo vya afya nchini kupitia Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nne, kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na mawasiliano. Kuimarisha ufuatiliaji wa ugonjwa huu katika vituo vya kutolea huduma ya afya pamoja na mipakani kupitia mifumo ya *surveillance system* yaani *IDSR* ya Wizara pamoja na mwongozo huu ambao umetolewa. Wizara ya Afya ya Ustawi wa Jamii imetoa maelekezo kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya hapa nchini kutoa taarifa za wagonjwa wa homa ya *dengue* pale inapobainika kupitia taarifa za kila juma zinazohusu magonjwa ya kuambukiza yaani *IDWE (Infectious Diseases Week Ending)*.

Mheshimiwa Spika, kutoa miongozo ya ufuatiliaji wa ugonjwa huu katika maeneo ya mipakani kuhusu kutokuwepo kwa aina yoyote ya vikwazo vinavyowekwa kwa ajili ya wasafiri. Aidha, maelekezo haya yameainishwa kuwa iwapo msafiri anayeondoka au kurudi nchini akiwa na dalili tajwa atoe taarifa kwa watumishi wa afya wa mpakani, yaani kwenye *heath port* ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia kwa karibu ongezeko la wagonjwa wenye homa isiyo ya kawaida kwa Mikoa na Wilaya zote nchini ili kuweza kufanya uchunguzi wa kina kama kuna mgonjwa au la. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeshafanya utafiti Mkoani Kagera, Morogoro, Kigoma na kuthibitisha kuwa haijaathirika na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa vituo maalum vya ufuatiliaji wa ugonjwa huu katika hospitali za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, yaani Mwananyamala, Amana na Temeke. Aidha, kituo cha *International School of Tanganyika (IST)* kilichopo Manispaa ya Kinondoni na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zinaendelea na ufuatiliaji wa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itafungua pia vituo Mkoani Tanga na Mtwara, Mikoa inayopakana na nchi jirani ya Kenya kutokana na taarifa za ugonjwa ambazo zimeshatolewa. Kupeleka taarifa ya mlipuko huu Shirika la Afya Ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, tano, upimaji na tiba. Kuimarisha uwezo wa kutambua ugonjwa huu kwa kina kupitia Maabara ya Taifa (*National Health Laboratory Quality Assurance Training Center* iliyoko NIMR. Vilevile Wizara inapeleka vipimo sawia yaani *dengue rapid test kits* kwa kituo cha Dar es Salaam kuimarisha utambuzi. Vituo hivyo ni pamoja na hospitali ya Muhimbili, Amana, Mwananyamala, Temeke Hospitali na *International School of Tanganyika*. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeagiza bohari kuu ya dawa kuhakikisha vitendanishi vyote vinakuwepo ili kurahisisha upatikanaji wake kwa Halmashauri zote na kupelekwa kwenye vituo vya ngazi za chini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeagiza vipimo sawia yaani *test kits* 750 vya nyongeza ambavyo tunatarajia kuvipata muda wowote kuanzia sasa. Kwa sasa tunavyo vipimo yaani *test kits* 350 ambavyo vitahimili kwa muda wa miezi miwili kama hali ya mtiririko wa wagonjwa itaendelea kuwa kama ilivyo. Wizara imeweka utaratibu wa kuhakikisha vifaa tiba vinapatikana wakati wowote katika vituo vyote kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wanaogundulika na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, sita, udhibiti wa mbu na mazalia. Kudhibiti mbu kupitia kwa kupulizia na kunyunyizia viuatilifu katika baadhi ya maeneo yaliyoathirika katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo wametokea wagonjwa wengi wa dengue. Hii inalenga kuangamiza mbu wapevu na viluwiluwi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa (NIMR) iko katika maandalizi ya kufanya utafiti kuhusu *dengue* kwa kuangalia makubwa mawili kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Muhimbili. Ukubwa wa tatizo katika binadamu, mbu waambukizao ugonjwa huu wa homa ya dengue - kujua jamii husika, tabia ya kuuma watu, wapi wanapopendelea kuuma, wapi waakozaliana kwa wingi na mazingira yao ya kawaida. Tafiti hizi zinaanzia Dar es Salaam na kuhusisha Wilaya zote tatu yaani Ilala, Kinondoni na Temeke. Tafiti zitaendelea katika baadhi ya Mikoa ikiwa ni pamoja na Mikoa minane ambako vituo vyetu vipo. Takwimu zitakazopatikana zitaonesha mbinu za kupambana na ugonjwa huu kwa mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, hatua za kudumu. Wizara Afya na Ustawi wa Jamii imeandaa mpango wa namna ya kukabiliana na ugonjwa wa homa ya *dengue*. Mpango huu umeandaliwa kwa kushirikiana na sekta mbalimbali. Afua mbalimbali za namna ya kudhibiti ugonjwa huu zimeshaainishwa. Hadi sasa Serikali imetumia kiasi cha Sh.132,000,000 kwa ajili ya ugonjwa huu. Aidha, Serikali imetenga na fedha hizi ziko tayari, Sh.540,000,000 kwa ajili ya kuendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huu. Serikali itaendelea kutoa fedha kwa mapambano haya kadiri itakavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Wananchi wanashauriwa kutokuwa na hofu kubwa juu ya ugonjwa huu kwani hauambukizwi kwa kumhumia mgonjwa au kwa kugusana. Hata hivyo, tunawashauri wananchi kwenda kwenye vituo vya afya haraka pindi wanapoona dalili hizo za ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, mlipuko wa *dengue* unadhihirisha kuwa mazingira yetu tunayoishi sisi si salama. Ikumbukwe kuwa kwa sehemu kubwa ugonjwa huu unachochewa na mazingira machafu. Aidha, mvua hizi kubwa zinazoendelea zinachangia kwa kiwango kikubwa sana kuongezeka kwa mazalia ya mbu. Utupaji ovyo na uhifadhi ya taka katika miji yetu hauridhishi kiasi ambacho kinatoa fursa kwa mazalia ya mbu kuongezeka na hata kuwa karibu zaidi ya makazi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa hatuna chanjo wala dawa maalum kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa huu, njia kubwa ya kupambana na ugonjwa huu ni kumzuia binadamu asiumwe na mbu. Hivyo basi, mbinu shirikishi za kutokomeza mbu inabidi zitiliwe mkazo katika mapambano dhidi ya homa ya *dengue*. Njia bora na rahisi ni kuhakikisha mazalia yote ya mbu yanatokomezwa. Hili linaweza kufanywa na kila mtu kwa nafasi yake. Tunashauri watu wavae nguo ambazo zinafunika mikono na miguu na kutumia dawa zinazofukuza mbu yaani *mosquito repellants*. Tunaelewa kuwa si kila mtu atakuwa na uwezo wa kununua dawa hizi na ndiyo maana tunakazania suala la kuangamiza mazalia ya mbu ambalo ni jukumu letu wote. Tunaendelea kuhamasisha watu na hasa watoto walale ndani ya vyandarua vyenye viuatilifu wanapolala wakati wa mchana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha wananchi wa Tanzania kuwa huu ni muda muafaka wa kuzingatia utunzaji bora wa mazingira yetu. Tukitunza mazingira yetu nayo yatatutunza na kutuepusha na maradhi ambayo yanaambatana na mazingira machafu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Ndiyo, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nishukuru kwa Serikali hatimaye kutoa Kauli juu ya ugonjwa huu. Ningeomba mwongozo kwako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 49.

Mheshimiwa Spika, moja, ni wazi wakati Mheshimiwa Waziri anasoma kauli yake Kanuni ya 49(3) haikufuatwa kwa maana ya Wabunge kupewa nakala. Sasa kwa umuhimu wa jambo lenyewe na udharura wa jambo lenyewe siku-*raise* hili jambo lakini sasa kwa sababu ni muhimu kufuatilia utekelezaji wa haya ambayo Waziri ameyasema nitaomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika ili Waziri atakiwe kutoa nakala ya jambo hili mapema.

Mheshimiwa Spika, pili, Kanuni ya 49(2) inasema kwamba Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahsusi, halisi na zisizozua mjadala, nasisitiza haya maneno zisizozua mjadala.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Dar es Salaam, toka asubuhi tumekuwa tukipokea taarifa kuhusu hali ya ugonjwa na nimelinganisha taarifa ambazo Waziri amesema na taarifa ambazo Katibu Mkuu wa Wizara amesema jana, naona kuna mgongano kwenye baadhi ya mambo. Kwa mfano, Katibu Mkuu kwenye taarifa yake kama jambo la dharura amesema kwa mfano vipeperushi vya masuala ya ugonjwa huu havijasambazwa bado vitatolewa. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri katika maelezo yake hapa ameeleza kwamba tayari vipeperushi vimeshatolewa. Sasa maana yake ni kwamba uhalisia wa utekelezaji uko tofauti.

Mheshimiwa Spika, vile vikao vya asubuhi, *clinical meetings* kwenye *level* za Manispaa vinafanyika lakini kwenye ngazi ya chini ajenda hii ya mafunzo kwenye zahanati na kwenye maeneo mengine, kwa maeneo ambayo nimefuatilia asubuhi, maeneo mengi havijafanyika bado. Mpangilio wa vituo hivi vya ufuatiliaji, ukiweka kituo kwa mfano *IST, International School Oysterbay*, kituo kiko *periphery* kidogo kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sitaki kutumia sana muda wako, kuna maeneo mengi sana, hivi vifaa vya *rapid test*, sasa nachoomba…

SPIKA: Nilifikiri unakuwa *brief* kumbe unaendelea?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ndiyo nakuomba sasa utoe mwongozo hii Kauli kwa sababu haiwezi kujadiliwa ipelekwe kwenye Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ili Kamati hiyo kwa niaba ya Bunge ifuatilie utekelezaji wa yote haya kunusuru wananchi wa Dar

es Salaam na kunusuru ugonjwa huu kusambaa maeneo mengine. Ni hilo tu ndilo ambalo naliomba.

SPIKA: Nashukuru. Wakati naanza kuzungumza nilisema Kanuni hiyo ya Kauli za Mawaziri ni lazima wawe na *document* iliyoandikwa na ndiyo maana tumechelewa kuitoa saa nne kwa sababu hiyo na hizo *document* ndiyo zinagawiwa sasa, kwa hiyo hilo halina umuhimu.

La pili, mimi ninayeendesha Kiti hiki, nitafanya inavyofaa.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli mpaka saa kumi jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa Esther Bulaya.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi pia na-*declare interest* kwamba ni *Service Lady*, naona na kijana mwenzangu Mheshimiwa Mdee tulikuwa kambi moja ya Ruvu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwanza kwa kuridhia mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba sisi wahitimu tuliokuwa katika Kambi ya JKT Ruvu, kwenye risala yetu kwa Mheshimiwa Rais ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu, tulipendekeza kwamba katika *intakes* zingine kwa Wabunge vijana watakaoenda kama akina Mheshimiwa Mnyika ambao hawajaenda, wakatumikie kwa kipindi cha miezi miwili au mitatu kwa sababu tumeona uzuri wa mafunzo haya kwa sisi viongozi vijana ambao hatukupitia, lakini pia tumeona kwamba muda ule ulikuwa mchache sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wale akina Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Catherine Magige na wengine watakaoenda basi waende kwa ruhusa ya ofisi yako uwape ruhusa ya miezi mitatu ili wakajifunze zaidi mambo ya msingi ya ulinzi na ushiriki katika ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kutoa ushauri kwamba Wizara iangalie kwa umuhimu wake, tunajua suala la vijana wanaoenda katika mafunzo ya JKT wako wa aina mbili; kuna wale wanaoenda kwa mujibu wa sheria, lakini kuna wale ambao wanaenda kwa kujitolea ambao mwisho wa siku wanafanikiwa kupata ajira katika vyombo vyetu vya ulinzi. Sasa siyo wote ambao wanafanikiwa kupata ajira, nilichokuwa nikiomba wale ambao hawawezi kuajiriwa waweze kupata mafunzo ya kawaida ya ujasiriamali na mambo mengine ya msingi, lakini wasiweze kupata mafunzo ya silaha kwa sababu hakuna binadamu aliyekamilika, inawezekana wakapata yale mafunzo ya matumizi ya silaha baadaye wakarudi mtaani, kutokana na ukosefu wa ajira mwisho wakashawishika kutumia vibaya ule ujuzi walioupata katika mafunzo ya JKT katika vitendo vya uhalifu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kulizingatia hilo.

Lakini pia Mheshimiwa Waziri nilikuwa napenda kutoa ushauri…

SPIKA: Unapaswa kusema Mheshimiwa Spika...

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika,

SPIKA: Eeh!

MHE. ESTHER A. BULAYA: Pia kambi zetu nyingi za jeshi katika ile changamoto ya kuanza haya mafunzo kuna vitu ambavyo kidogo vilikuwa bado havijakaa vizuri hasa katika sekta ya afya ambapo tuliona kulikuwa kuna upungufu wa vifaa vya huduma ya afya kwa wale vijana ambao walikuwa wakienda kule. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba Wizara ijipange vizuri katika suala zima la matibabu vifaa na dawa za kutosha viwepo.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa napenda kuzungumzia malalamiko ya wanajeshi wastaafu. Mheshimiwa Chiligati amelizungumzia sana, na sisi huko tunakotoka kuna wazee wetu ambao wanasema bado wana madai yao sana, bado ile heshima waliyokuwa wakiipata katika utumishi wamekuwa wakiikosa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iliangalie kwa namna ya pekee kwa sababu hawa ni wanajeshi wa akiba, lakini maisha ambayo wanaishi sasa hivi ni tofauti na waliyokuwa wakiishi wakati wa utumishi wao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuangalia hawa wanajeshi wa ngazi za chini ni jinsi gani wanaweza kuboreshewa mishahara na posho zao kutokana na kazi ambayo wanaifanya ya ulinzi wa taifa letu mchana na usiku. Kwa hiyo, ni vyema fedha wanazozipata ziendane na kazi ambayo wanaifanya. Natambua kwamba sasa hivi kumekuwa na mabadiliko makubwa, jeshi lile ambalo lilipambana na Iddi Amini na sasa hivi ni vitu viwili tofauti, lakini ni vema likaendelea kubadilika na mapato wakaendelea kuwa nayo kutokana na nyakati zinavyobadilika na hali ya mazingira ya sasa hivi yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa kuwapongeza kwa ushiriki wao wa asilimia 100 katika miaka 50 ya uhuru. Nipende kusema kwamba si jambo geni kwetu sisi, na kwamba hata sisi tuliopitia huko tunajua yale si mambo yote ambayo yameoneshwa. Lakini ni vyema kuonesha na kujivunia nguvu ya jeshi lako, hata kama kuna maadui walikuwa wananyemelea, nadhani baada ya kuona yale mambo wanajua kabisa Jeshi la Tanzania liko imara na haliwezi likachezewa chezewa kama ambavyo ambao hawalitakii mema jeshi letu wanaweza kufikiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninachoweza kusema ni kwamba, ulinzi ni jambo la msingi, kwa hiyo, ni vyema Wizara hii ikaangaliwa kwa jicho la pekee. Tumeona nchi za wenzetu kwamba uhaba wa bajeti katika Wizara ya Ulinzi ni changamoto ambayo wamekuwa wakiitatua na katika nchi za wenzetu tunaona Wizara hii ya Ulinzi imekuwa ikipewa kipaumbele. Kwa sababu kuna umuhimu sana wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu unazingatiwa hasa katika maeneo ya mipakani ambako ndiko wako wanajeshi ambao wanafanya kazi ya ulinzi usiku na mchana. Kwa hiyo, ni vema tuhakikishe zile changamoto ambazo zinatukabili zinafanyiwa kazi kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ninashukuru kwa kupata nafasi hii. (*Makofi*)

SPIKA: Asante. Mheshimiwa mtoa hoja!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, asante sana. Naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida nianze kwa kuwatambua waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

SPIKA: Hatufanyi hivyo siku hizi!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Aa, samahani!

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nasema hivyo kwa sababu karibu michango yote ilikuwa ni ya kujenga na hakukuwa na michango ya kubomoa. Kwa hiyo, pamoja na tofauti za itikadi zetu, lakini walio wengi karibu wote mmechangia kwa madhumuni ya kuweza kujenga, na hilo tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Kwanza kulikuwa kuna hoja ya ufinyu wa bajeti. Kamati inaeleza kwamba kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya Wizara hii kwa nchi yetu na hasa kwa kuzingatia kwamba wao ndio walinzi wa mipaka yetu, Kamati inashauri kuwa Serikali ijitahidi kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka.

Serikali inakumbushwa kuwa jeshi linahitaji kuendelea kufanya mazoezi ya kijeshi wakati wa amani, kutoa mafunzo kwa wanajeshi wapya pamoja na wa zamani, hivyo linahitaji fedha kwa ajili ya mafuta, *stationery* na zana nyingine za kufundishia. Hivyo, Kamati inasisitiza kuwa Serikali kila mwaka itenge fedha za kutosha kuliwezesha jeshi na vyombo vyote vya ulinzi na usalama ili kusimamia amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana sana na Kamati kwamba ni muhimu sana kupata bajeti ya kutosha ili kazi ziweze kutimizwa ipasavyo. Wizara inaendelea kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha na Kamati ya Bajeti ya Bunge, kuona jinsi ya kuongeza kiwango cha bajeti kwa ajili ya kugharamia mahitaji haya, yakiwemo mazoezi ya kijeshi wakati wa amani, kutoa mafunzo kwa wanajeshi wapya pamoja na wa zamani, na mafuta ya magari, vifaa na zana ili kuliwezesha jeshi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni matarajio yangu kuwa Serikali itazingatia ushauri wa Kamati kulingana na uwezo utakaokuwepo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni madeni: Kwa kuwa Hazina imeahidi kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 italipa madeni yote na haitaanza kwenye bajeti ya madeni, Kamati inasisitiza kuwa madeni ya Wazabuni wanaoidai Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, walipwe ili waweze kuendelea kutoa huduma kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara na mafungu yake kwa kutopata fedha kama zilivyoidhinishwa kumefanya kulimbikiza madeni katika mafungu yake yanayofikia jumla ya Shilingi Bilioni 314.86 ambapo kati yake madeni ya kimkataba ni Shilingi Bilioni 224.4 na Hazina inaendelea kulifanyia kazi jambo hili. Nimepata fursa ya kuzungumza na Waziri wa Fedha, ili tuone ni njia gani bora ya kuhakikisha madeni haya yanalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kwamba Wizara ya Ulinzi iachiwe kazi ya matengenezo ya barabara za ulinzi wa mipakani. Kamati inazidi kusisitiza kuwa, barabara za mipakani ni muhimu kwa majeshi yetu kufanya doria katika mipaka yetu. Kwa kuwa, hivi sasa barabara hizo hazina chombo cha kuzikarabati, basi Kamati inazidi kuishauri Serikali kwamba jukumu hilo wakabidhiwe JKT, hivyo fedha za matengenezo ya barabara za mipakani ipewe Wizara ili iweze kuzifanyia matengenezo.

Aidha, Kamati inashauri Wizara ya Ulinzi ianzishe kitengo maalum cha kusimamia matengenezo ya barabara mipakani *(security roads)* kwa kuwa jeshi lina zana na wataalam wa kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya mawasiliano na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara ya Ujenzi, Hazina na wadau wengine ili kuona kama jambo hili tunaweza tukalitimiza kwa sababu upande wa jeshi tunacho kitengo maalum cha matengenezo, kinachokosekana ni fedha kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, kama tukikubaliana kwamba fedha hizo zitatengwa basi

jeshi litaweza kutimiza kazi hii ya kuhakikisha barabara za mipakani zinapitika kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala la uvamizi wa maeneo ya jeshi. Kwa kuzingatia kwamba jeshi linahitaji maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali, mfano, maeneo ya mazoezi. Kamati inashauri Wizara ianzishe kitengo maalum cha kusimamia ardhi ya jeshi. Kitengo hiki kitakuwa na shughuli maalum ya kuhakikisha kuwa maeneo ya jeshi yanapimwa na yanapata hatimiliki na pia hayavamiwi hovyo na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ardhi ambacho kinaitwa Kitengo cha Usimamizi na Maendeleo ya Miliki, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kazi kubwa ya kitengo hiki ni kuratibu kazi zote za utoaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya jeshi na kuchambua na kushauri hatua za kuchukua katika kutatua migogoro ya ardhi iliyopo kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na raia.

Mheshimiwa Spika, hatua za kutatua migogoro ya ardhi ni kama ifuatavyo:- Kwanza, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imewasiliana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuhusu jeshi kupewa hatimiliki ya ardhi. Serikali inatayarisha marekebisho ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 ili kurekebisha kasoro zilizokuwepo. Pili, Wizara imeendelea na zoezi la kupima maeneo ya JWTZ kwa kuweka *beacons*. Tatu, kuweka mabango kwenye mipaka ya maeneo ya JWTZ ili mipaka ionekane wazi. Nne, Wizara kwa kushirikiana na baadhi ya halmashauri imefanya upimaji mpya kulingana na hali halisi ya uvamizi. Mfano ni eneo la KTC Kunduchi Dar es Salaam na Kisakasaka Zanzibar. Tano, Wizara inahimiza halmashauri za miji kutayarisha mpango kabambe wa matumizi ya ardhi kwa maeneo yote yanayozunguka kambi za jeshi ambapo ardhi yote inayopakana na kambi ipimwe na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria. Hali iliyopo sasa maeneo mengi yanayozunguka makambi ya jeshi kuna ujenzi holela ambao unachochea uvamizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeendelea na zoezi la kulipa fidia ka maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya jeshi. Mfano mwaka 2013/14 Wizara imelipa fidia kiasi cha Shilingi Bilioni 2.28 kwa maeneo ya Cheyo - Tabora, Mwakidila - Tanga, Mwantini - Shinyanga na Mataya Kilomo - Pwani. Mwaka 2014/15 Wizara itaendelea na kulipa fidia kwa maeneo ya Mahongole - Makambako, Ilemela na Kigongo Feri – Mwanza na Ronsoti – Tarime kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni suala la uhaba wa makazi. Pamoja na mradi unaotekelezwa wa ujenzi wa nyumba 10,000 bado Kamati inaishauri kuwa Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya askari pamoja na ujenzi wa mabweni kwa ajili ya Chuo cha Kijeshi cha Monduli na katika makambi ya JKT ili kukabiliana na upungufu wa nyumba za askari pamoja na uchache wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi.

Fedha kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ya nyumba za jeshi zilizobakia mazungumzo yanaendelea ambapo waliotukopesha wameonesha nia ya kuendelea na awamu ya pili ili kuzifanya zitimie 10,000. Hivyo, kipengele cha uchangiaji wa fedha zinazotolewa kwa upande wa Serikali ya Tanzania ni kigezo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa mradi huu iwapo mchango huo utatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hapa napenda niongezee kwamba, kwa kipindi kirefu tatizo la makazi limekuwa kubwa katika makambi yetu, lakini mradi huu ambao umeanza utapunguza tatizo kwa kiasi kikubwa. Lakini hatuutegemei mradi huu tu, bado kuna

fedha kidogo ambazo zinatengwa kwa ajili ukarabati wa nyumba ambazo tayari zipo kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliovyoshauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni wahitimu wa JKT kutoajiriwa kwa wingi kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Hapa ninachoweza kusema ni kwamba, kwa kiwango kikubwa majeshi yetu (vyombo vya ulinzi na usalama) yameanza kuajiri. Jeshi linaajiri kutoka huko peke yake, lakini vyombo vingine vya ulinzi na usalama bado vinachanganya changanya. Tunakubaliana kwamba tukae pamoja tuhakikishe vyombo vyote vinaajiri kwa asilimia mia moja kutoka JKT na hatimaye tuweze kuondoa tatizo la wale wanaopitia JKT kukosa ajira baada ya muda wao kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kutolewa kwa miezi Sita. Kamati imepokea taarifa ya Serikali kwamba ushauri wa mafunzo kwa vijana wa mujibu wa sheria yatolewe kwa muda wa angalau miezi Sita imeshindikana kutekelezwa kutokana na mabadiliko ya mihula ya Kidato cha Sita. Kamati inaishauri Serikali iwakutanishe wadau wote hasa Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Elimu (TAMISEMI) ili suala hili lijadiliwe kwa pamoja kwa lengo la kupata suluhu ya kuoanisha mihula ya kidato cha Sita na mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, Wizara inachukua maoni haya na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hii. *(Makofi)*

Serikali itumia samani kwenye ofisi za Serikali zinazotengenezwa na Jeshi la Kujenga Taifa na Shirika la Mzinga. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tayari imetekeleza agizo hilo. Aidha, baadhi ya Wizara na Taasisi nyingine zimetekeleza agizo hili na ninaomba nizitaje chache tu kwa mfano, Ofisi ya Rais, Utumishi, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomelo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Mkuu wa Wilaya ya Mvomelo na Bodi ya Mishahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna ambao wametengeneza samani zao kupitia SUMA JKT ambao ni Dar es Salaam *City Council*, *Land Forces Command*, RAS – Dar es Salaam, Makao Makuu ya JKT, RAS – Singida, Nyumbu SACCOS, *Public Service College* – Mtwara, Uhamiaji Dodoma na *National Land Use Commission* ya Dar es Salaam. Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa kiwango fulani taasisi zetu hizi zimeweza kuwa zinapeleka samani katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niingie katika hoja za Kambi ya Upinzani. Kwanza, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Serikali kutoleta Bungeni kwa muda wa miaka saba tangu Serikali ilipoahidi kuleta sera na mapitio ya sheria hiyo kama ilivyokusudiwa? Hapa tunazungumzia Sera ya Ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala hili liliwasilishwa tena Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukumbusha walete maoni kuhusiana na rasimu ya sera waliyopewa siku za nyuma. Kwa vile suala hili ni la muda mrefu, tunashauri kwamba Bunge lako tukufu liridhie tuendelee na hatua za kukamilisha sera hii kama Zanzibar wataendelea kutoleta hayo maoni. Lakini hata hivyo nimepata nafasi ya kuzungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambaye amenihakikishia kwamba katika kipindi kifupi kijacho watakuwa wamefikisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali juu ya namna ya Serikali ya Mapinduzi inavyoshirikishwa katika jambo hili, kama tulivyosema kwa kipindi kirefu tumeshindwa kuileta sera hii kwa kusubiri tu maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa maana hiyo Serikali hiyo inashirikishwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kwamba Serikali ieleze jinsi gani imeweka mkakati wa upimaji wa maeneo ya Jeshi na JKT na kuyapatia hatimiliki na taratibu za kutoa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na yametajwa maeneo mengi kabisa Mheshimiwa ameyazunguzamza. Naomba nieleze tu kwa ufupi kwamba ni kweli mwaka 2002 Serikali iliweka mkakati wa upimaji wa maeneo ya Jeshi na JKT na kuyapatia hatimiliki.

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mkakati huo kwa kupima na kulipa fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi kulingana na na uwezo wa kifedha. Kwa kuzingatia sheria za ardhi zilizopo, zaidi ya asilimia 70 ya maeneo ya Jeshi yamepimwa na ramani zake kusajiliwa. Zoezi la kulipa fidia linaendelea kila mwaka wa fedha kuzingatia uwezo wa kibajeti.

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imetayarisha mabadiliko kwenye Sheria ya Ardhi Na.4 na 5 za mwaka 1999 ili kuwezesha Jeshi kumilikishwa ardhi kwa njia ya hatimiliki. Aidha, hatua kadhaa zimechukuliwa kuondoa migogoro iliyokuwepo ikiwepo maeneo ya Oldonyo Sambu Arusha, Kunduchi *Transit Camp* – Dar e salaam, Makao Makuu ya Jeshi Dar es salaam na Kisakasaka Zanzibar.

Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ukurasa wa 35, kazi ya kupima na kulipa fidia kwa maeneo ya Jeshi ni endelevu. Maeneo mengi yaliyotajwa kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa yana mgogoro yalishafanyiwa kazi, na ambayo bado juhudi zinaendelea kuondoa kero zilizopo. Maeneo yaliyolipwa fidia na migogoro kuisha ni pamoja na haya yafuatayo:- Singino - Kilwa, Mapinga - Bagamoyo, Nduruma - Tengeru, Oldonyo - Sambu - Arusha, Mwantini - Shinyanga, Mwakidila - Tanga, Cheyo - Tabora na Mataya Kiromo - Pwani.

Mheshimiwa Spika, hali halisi kuhusu migogoro ya ardhi katika vikosi vingine ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika vikosi wa vya Jeshi la Kujenga Taifa vya Makutopora, Bulombola, Mlalo, Malamba na Mgambo hakuna maeneo ya raia yaliyochukuliwa kwa ajili ya shughuli za kijeshi. Katika Kikosi cha Rwamkoma eneo la Kiteule cha Tarime lilitwaliwa na Serikali na kukabidhiwa kwa JKT ili kuepusha mapigano yaliyokuwa yakijitokeza mara kwa mara na kusababisha vifo vya raia, mifugo na uharibifu wa mali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii naomba nitoe ufafanuzi kidogo. Ni kwamba, Jeshi la Kujenga Taifa liliombwa kwenda kukalia eneo hilo, kwa hiyo haliwajibiki kisheria kulipa fidia. Lakini jambo hili tumelizungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeitaka Mamlaka ya Mkoa wa Mara ihakikishe kwamba taratibu za kisheria zinafuatwa ili hatimaye wahusika waweze kufidiwa. Lakini Jeshi la Kujenga Taifa liko pale kwa madhumuni ya kwenda kuleta amani ambayo kwa kipindi kirefu ilikosekana.

Mgogoro wa ardhi katika Kikosi cha Chita ulimalizika baada ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na watalaam wa ardhi kutoka Wizara ya Ardhi na Makazi pamoja na mamlaka za maeneo husika za Serikali za vijiji zilizohusika na mgogoro huo kushiriki kupima na kuainisha upya maeneo yanayopakana na kikosi.

Mheshimiwa Spika, nadhani utaona kwamba jitihada zimefanyika za kuhakikisha matatizo yanayokabili migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi kwa kiwango kikubwa yameweza kufanyiwa kazi pamoja na kwamba hatukuweza kuyamaliza yote kutokana na uhaba wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni sababu zipi za msingi zilizopelekea fedha za maendeleo kwa JKT mwaka 2013/2014 ambazo zilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 6 kutolewa kwa kiwango cha asilimia nane tu.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii tumefanya mazungumzo na Wizara ya Fedha kuwasihi watafute njia ya kuweza kutupatia fedha hizi ili hatimaye tuweze kuteleza yale ambayo yalikusudiwa. Bado tuna muda kabla ya bajeti hii kuisha, ni mategemeo yetu kwamba tutaweza kupata angalau kiwango fulani cha fedha hizo ili tuweze kukamilisha yale ambayo yalikuwa yamepangwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya JKT Kanembwa – Kigoma imetelekezwa kwa muda mrefu na hasa askari wa JKT Kanembwa ambao hawajalipwa fedha zao za mizigo na hawajalipwa fedha za likizo kwa muda mrefu toka mwaka 2007: Jibu ni kwamba madeni ya stahiki mbalimbali za wanajeshi na watumishi wa umma yakiwemo ya uhamisho na likizo ya miaka ya nyuma hadi Juni, 2013 yakijumuisha pia Kikosi cha 824KJ Kanembwa yamehakikiwa na yamewekwa katika mpango wa malipo wa Serikali.

Tatizo la makazi katika Kambi ya Kanembwa JKT linaendelea kutafutiwa ufumbuzi kadri fedha za maendeleo zitakavyopatikana na baadhi ya wanajeshi wanaishi kikosini hapo na familia zao. Aidha, JKT limeweka katika mpango wake wa maendeleo kuendelea na ukarabati na ujenzi wa makazi ya kudumu kwa wanajeshi na watumishi wa umma na familia zao waliopo katika katika makambi mbalimbali ikiwemo 824KJ Kanembwa. Kwa hiyo tunachosema ni kwamba tunajua kwamba kuna matatizo hayo, uhakiki wa madeni umeishafanyika, ni mategemeo yetu kwamba Hazina watatoa fedha hizo ili wahusika waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ni kiasi gani hadi sasa SUMA – JKT imerejesha fedha za madeni ya matrekta na Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuyaagiza tena matrekta mengine ili iweze kuboresha mpango wa kilimo kwanza. Jibu ni kwamba thamani ya matrekta na zana ambazo ziliuzwa kwa wakulima katika awamu ya kwanza ni bilioni 53.6, ambapo hadi sasa SUMA – JKT imekusanya bilioni 26.16 kama marejesho ya mkopo toka kwa wakulima ambayo ni sawa na asilimia 41. Kiasi hiki kinatarajiwa kuongezeka mara baada ya msimu wa mavuno mwaka huu. Mkataba kati ya SUMA – JKT na wakulima unataka marejesho ya mikopo yawe yamekwishafanyika ifikapo Desemba, 2017. Kwa hiyo bado muda upo na nadhani fedha hizo zitaweza kupatikana ili ziweze kuagiza matrekta mengine.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza awamu ya pili, SUMA-JKT limeomba kupata mkopo wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 92 kutoka Hazina. Aidha, SUMA – JKT imefanya mazungumzo na kampuni zinazotengeneza matrekta na zana kutoka nchi za India, China na Belarus. Kampuni hizo ni New Holand ya India, YTO, AMEC na CATIC kutoka China na *Minsk Tractor Zavod* ya Belarus. Lengo la SUMA – JKT ni kuingia ubia na kampuni ambayo itakuwa tayari kujenga kiwanda cha kuunganisha matrekta *(assembly plant)* hapa nchini. Mazungumzo na makampuni hayo yapo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu kiwanda cha Cami-SUMA: Kami-SUMA kilikuwa kiwanda cha ubia cha ushonaji kati ya kampuni ya *Cami Textiles* Tanzania Ltd. na SUMA – JKT ambacho kilianzishwa kwa lengo la kukidhi soko la ndani na pia kuuza bidhaa zake katika soko la AGOA. Ubia huu umesitishwa shughuli zake baada ya kiwanda kushindwa kujiendesha kwa faida na wabia kuamua kuondoka nchini kabla ya kukamilisha taratibu za kuvunja ubia kisheria. Kutokana na hali hiyo, SUMA – JKT kwa kumtumia mwanasheria wake inaendeleza mchakato wa kuvunja ubia huu kisheria. Hivyo mwaka wa fedha 2013/2014 hakuna faida iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda cha dawa cha Tanza-Sino nacho kilikumbwa na tatizo hilo hilo, wabia ambao walitoka China walishindwa kukiendesha kwa faida na matokeo yake ni kwamba kiwanda hicho sasa kinafanyiwa tathmini ili ubia uweze kuvunjwa rasmi. Na kwa upande huo vile vile wabia walishaondoka, kwa hiyo hatua zinazoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba taratibu za kisheria zinafuatwa ili kuvunja rasmi ubia uliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niingie katika hoja za Wabunge mbalimbali kama ifuatavyo:- Ushiriki wa JWTZ katika Umoja wa Mataifa na stahili zao: Waheshimiwa Wabunge wengi walitaka kulijua hili. Naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:- Kwanza, nizungmzie hali za wanajeshi wetu walioko katika *operation* za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa wako salama wanaendelea vizuri na kazi.

Hata hivyo kwa bahati mbaya JWTZ ilipoteza maafisa na askari wake mashujaa katika *operation* hizo. Mpaka sasa tumepoteza wanajeshi 14, kati ya wanajeshi wote 14, wanajeshi 10 wamekwishalipwa mafao yao yote na 4 bado hawajalipwa. Sababu kubwa ya kutolipwa ni za kifamilia zinazohusiana na taratibu za mirathi kutokamilika.

Kwa hiyo tunachosema ni kwamba hakuna urasimu katika kuwalipa hawa, wanalipwa kama inavyotakiwa pale ambapo taratibu za kisheria za usimamizi wa mirathi zinapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, malipo na mafao kwa wanajeshi wanoafia kwenye *operation* ni kama ifuatavyo:- Familia za wanajeshi waliofariki katika *operation* hizo walilipwa mafao yao, kwanza, familia za wanajeshi waliofariki walisafirishwa kwenda kwao, fedha za rambirambi ambazo hutolewa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, fedha hizi ni mishahara ya miezi sita ya mwanajeshi na malipo ya pensheni ambayo hugawanyika katika makundi yafuatayo:-

Kuna *death gratuity* kwa wale ambao hawajafikisha miaka 20 katika utumishi na *death pension* kwa wale ambao wametimiza miaka 20 na kuendelea katika utumishi wote wamekuwa wakipata fedha zao.

Kwa askari waliofariki wakiwa katika *operation* za Umoja wa Mataifa, wamesafirishwa kutoka eneo la *operation* hadi nyumbani na wamelipwa fidia ya dola za kimarekani 70,000/=.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kurejeshwa kwa alama za mipakani. Kama nilivyosema awali, Serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa *beacons* zote za mipakani zinarejeshwa hatua kwa hatua kulingana na bajeti ya Serikali na kwa kushirikiana na nchi tunazopakana nazo. Mpaka sasa hakuna nchi tunazopakana nazo ambayo imekwamisha zoezi hilo, nchi zote tunafanya mazungumzo kwa pamoja na tunashirikiana vizuri katika kuhakikisha kuwa suala hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Katika mpaka wa Tanzania na Uganda alama zote zilizoharibiwa zimekarabatiwa na kuongezwa alama zingine ili kufanya mpaka uonekane vizuri zaidi. Aidha, mazungumzo na Kenya yameanza na utekelezaji tayari umeishaanza na yamefikia katika hatua nzuri ya kurejesha alama zilizoharibika na kuongeza nyingine. Aidha, mazungumzo yamekuwa yakiendelea baina ya nchi ya Tanzania na Burundi, DRC na Zambia ili kupanga namna ya kuboresha mpaka wa nchi hizo kupitia Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyozungumziwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Chiligati na wengine ni kuhusu mafao, kuboresha *pension* za wanajeshi wastaafu. Mpaka sasa malipo ya *pension* kwa wanajeshi wastaafu hulipwa kwa asilimia ya mshahara wanaostaafia kwa mujibu wa viwango vilivyopo vya Serikali. Kwa sasa Serikali imebaini kuwa viwango hivyo

haviendani na hali halisi kwani viwango hivyo vinalipwa kulingana na mshahara mtu anaostaafia. Serikali imeanza mkakati wa kubadilisha na kuboresha sheria za *pension* zilizopo ili ziweze kwenda na hali halisi ya maisha. Kwa maana nyingine ni kwamba tunatambua ya kwamba wale waliostaafu zamani kwa kuwa mishahara yao ilikuwa midogo sana na *pension* zao ni ndogo sana, na hili linahitaji mabadiliko ya kisheria. Nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutalifanyia haraka iwezekanavyo ili sheria hiyo iweze kubadilishwa *pension* hizi ziweze kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu hali ya uharamia katika Bahari ya Hindi na idadi ya maharamia waliokamatwa kuanzia Januari, 2013 hadi Machi, 2014 iliyotolewa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk: Napenda nimweleze kwamba katika kipindi hiki cha miaka miwili iliyopita hali ya uharamia imedhibitiwa kwa kiasi kikubwa. Kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2013 hadi sasa hapajatokea vitendo vya uharamia katika maji ya Tanzania katika Bahari ya Hindi. Tukio la mwisho lilitokea tarehe 18 Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiteule cha Kigomasha, hatua za kukifunga zilichukuliwa kutokana na sababu za kiutawala zilizokuwepo wakati ule. Hata hivyo kwa sasa JWTZ inafanya tathmini kuona uwezekano wa kukirejesha tena Kiteule hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusu fidia kwa wanajeshi katika milipuko ya mabomu ya Gongolamboto. Madai ya fidia kwa wanajeshi kutokana na milipuko ya mabomu yamewasilishwa ofisi ya Waziri Mkuu kwa malipo. Ieleweke tu kwamba mwenye mamlaka ya kulipa fidia katika majanga yoyote yale ni Ofisi ya Waziri Mkuu na majina yalishafikishwa huko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvamizi na migogoro maeneo ya jeshi, na hili limezungumziwa na Waheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Aballah Ameir na Mheshimiwa Faustine Ndugulile. Ili kukabiliana na tatizo la uvamizi wa maeneo, Serikali inafanya mapitio ya Sheria ya Ardhi Na.4 na Na.5 kama nilivyosema ili kuliwezesha Jeshi kupata hatimiliki ya maeneo yake. Wizara imeendelea na zoezi la upimaji na ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi.

Maeneo yaliyolipwa fidia mwaka huu na yanayotegemewa kulipwa fidia yametajwa katika ibara ya 35 na 36 ya hotuba yangu. Mpaka sasa asilimia 70 ya maeneo yote ya Jeshi yameishapimwa tangu mwaka 2007 na asilimia 30 iliyobaki tunaendelea kuyafanyia kazi. Hata hivyo baadhi ya maeneo yaliyotajwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani hayana migogoro kama ilivyodhaniwa. Kwa mfano, Bulombola, Makutopora, Mlale na Makao Makuu ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya za wanajeshi kama ilivyoulizwa na Mheshimiwa Yahaya Kasim Issa; Wajiriwa wote wa Jeshi hupimwa afya zao kabla ya kuajiriwa na Jeshi. Vivyo hivyo Jeshi huwapima wanajeshi wake afya zao kabla ya kwenda kwenye *operation* mbalimbali za kijeshi. Yule anayethibitika kuwa afya yake siyo nzuri hupangiwa majukumu kulingana na afya yake huku hatua za kuimarisha au kurekebisha afya yake zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanajeshi wanaokwenda kwenye ulinzi wa amani kama ilivyoulizwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein; Wanajeshi kabla ya kwenda kwenye ulinzi wa amani huandaliwa kwa kupewa mafunzo maalum ya kioperesheni kule anakokwenda na mafunzo ya kiutawala ikiwa ni pamoja na kuelezwa stahili zao. Katika stahili hizo huelekezwa watoe maelekezo namna, wapi wanataka stahili hizo zipelekwe. Hivyo Jeshi hutekeleza kulingana na matakwa yao wenyewe.

Kuhusu malipo yanayotolewa na UN kwa ajili ya wanajeshi waliopelekwa kwenye *mission* Serikali huchukua asilimia 20 na asilimia 80 hubaki kwa askari wenyewe. Mheshimiwa Spika, sababu za kufanya hivi ni kwamba mchango huu mdogo unaokatwa asilimia 20 una lengo la

kuanza kuandaa vikosi vipya ambavyo vitaenda kuchukua nafasi za wale ambao wako kule kwa sababu huwa wanabadilishana. Pamoja na malipo hayo ambayo wanapewa wakiwa Umoja wa Mataifa, stahili nyingine zote ikiwa ni pamoja na mshahara, posho na *ration allowance* wanaendelea kupata.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana katika Jeshi la Wawananchi wa Tanzania kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein: Mpaka sasa JWTZ huchukua vijana kutoka JKT na JKU. Kwa mfano mwaka jana idadi ya vijana wote 2000 walioajiriwa na JWTZ walichukuliwa kwenye makundi hayo kutoka JKT na JKU.

Pamoja na mgawo wa nafasi za ajira unaotolewa kwa JKU, uzoefu wetu umeonyesha kwamba bado kuna vijana wengi zaidi kutoka Zanzibar wanaojiunga na Jeshi kupitia JKT. Hakuna mwanajeshi anayeajiriwa nje ya mafunzo ya JKT labda awe na taaluma maalum kama vile madaktari, wahandisi na *profession* nyingine. Waheshimiwa, kwa maana hiyo tunachojaribu kusema hapa ni kwamba utaratibu wa ajira katika Jeshi unakwenda vizuri kwa kuwachukua vijana walioko JKT kwa pande zote mbili za Muungano.

Kuhusu maonesho ya zana na vifaa katika maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano kama ilivyoulizwa na Mheshimiwa Christowaja; Hapa napenda tu niseme kwamba wachangiaji wengine walitusaidia kujibu suala hili. Hili si suala ambalo Tanzania tumeanza sisi, ni utaratibu wa kimataifa, utakwenda popote pale wakati wa maadhimisho ya siku zao za uhuru au mambo mengine wanafanya maonesho ya zana za kijeshi. Ni utaratibu wa kawaida, kwa hiyo siyo kwamba jambo hili tumelifanya sisi tukiwa ni wa kwanza kufanya hivyo, la hasha. Lakini pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Christowaja kwamba asidhani kwamba ndiyo zana zote zimeoneshwa, hapana, kuna vitu vingi ambavyo vilikuwa havijaoneshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maduka ya Jeshi *(military duty free shops)*; Kwa nini wamepewa watu wa aina fulani tu? Jibu ni kwamba upatikanaji wa uendeshaji wa maduka haya hutolewa kwa utaratibu wa njia za zabuni. Hilo la kwanza. Hivyo Jeshi hutoa vigezo vyake kwa umakini bila ya ubaguzi wowote. Mbali na watu binafsi, huduma hiyo pia hutolewa na mashirika yetu ya Mzinga na SUMA – JKT. Kwa maana nyingine ni kwamba tunajaribu kujenga uwezo ndani ya Jeshi. Mzinga na SUMA JKT wakipata uwezo wa kutosha wa kuendesha *duty free shops* hizi, hatutakuwa na sababu ya kuruhusu watu wengine waziendeshe. Kwa sasa tunafanya utaratibu huu kwa kufuata Sheria ya Manunuzi kwa kufanya tenda ya kutoa huduma katika majeshi haya.

Mheshimiwa Spika, kuhudu suala la malipo kwa Wanajeshi waliohamishwa: Swali hili limeulizwa na Mheshimiwa Sabrina Sungura. Jibu ni kwamba hatua za kuwalipa huchukuliwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Mpaka sasa waliohamishwa kufikia mwaka wa fedha uliopita wameshalipwa stahili zao, wale ambao wanadai mwaka huu madeni yao yanendelea kuhakikiwa na watalipwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo katika hili la uhamisho hakuna kigugumizi, ni suala tu la kusubiri kabla bajeti hii haijaisha tutahakikisha kwamba malipo yanafanyika.

Yapo madeni ya wanajeshi wa Jeshi la Kujenga Taifa kikiwemo Kikosi cha Kanembwa ya likizo pamoja na uhamisho hadi kufikia Juni 2013. Madeni hayo yamehakikiwa na Hazina na yanasubiri fedha ili yaweze kulipwa. Kwa hiyo kwa wale wote ambao wanadai, madeni yao yamehakikiwa na ni matumaini yetu kuwa fedha hizo zitapatikana kabla ya mwisho wa bajeti ili waweze kupewa haki yao.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja zingine ambazo ninaomba kwa uchache wake tu nizitaje. Nadhani kuna hili ambalo sikulitolea ufafanuzi kamili, ninaomba nilirudie suala la Tanza-Sino

ambacho kilikuwa ni kiwanda cha ubia cha kutengeneza dawa za binadamu kilichoanzishwa September 1997 kwa SUMA-JKT ku-*sign* mkataba wa ubia na kampuni ya Kichina iitwayo *Shanks Provincial Technical Renovation and Equipment Corporation* ambayo baadaye iliuza hisa zake kwa kampuni ya *Holly Industrial Group Ltd*. tarehe 20 Juni, 2007. Hata hivyo katika kipindi chote hicho mradi ulikuwa ukiendeshwa kwa hasara na kupelekea kusimamishwa kwa uzalishaji ilipofika Oktoba, 2010 kutokana na kutoleta tija iliyotarajiwa. Na hivi sasa mchakato wa kuvunja ubia kisheria unaendelea kwa usimamizi wa mwanasheria wa SUMA-JKT mbapo mambo muhimu yanayohitajika kutekelezwa ni haya yafuatayo:-

Kwanza, kuainisha madeni ya kiwanda ili kupanga utaratibu wa kugawana kulingana na mgawanyo wa hisa za wawekezaji. Pili, kufanya uthamini wa mali za kiwanda ili kupanga utaratibu wa kugawana au kufidia madeni. Tatu, kuandaa hati za kuvunja ubia kwa kufuata sheria husika.

Nne, taarifa ya uthamini wa mali ya kiwanda inayohitajika katika kugawana mali na madeni ili kuvunja ubia huu imekamilika katika kipindi hiki na imewasilishwa kwa wanasheria wanaoshughulikia suala hili. Kwa maana nyingine ni kwamba suala hili sasa linakaribia hatima yake ili tuweze kuondoka rasmi na ubia huo na ikiwezekana tutafute mbia bora zaidi ili kuendeleza kiwanda kile cha dawa cha Tanza-Sino.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa kiwango kikubwa nimejaribu kuzijibu hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na ni mategemeo yangu kwamba tutaendelea na utaratibu huu wa bila kujali itikadi za kisiasa kuunga mkono masuala ya Ulinzi na Usalama wa Nchi yetu. *(Makofi)*

Napenda kwa mara nyingine tena niwashukuru Wabunge wote waliochangia na wengi wenu mmezungumzia masuala ya maslahi kwa wanajeshi, jambo ambalo na sisi tunalitambua fika, na ninataka nichukue fursa hii kusema kwamba hata Serikali ina lengo la kuhakikisha kwamba maslahi ya wanajeshi wake yanaboreshwa kwa sababu kazi wanayoifanya kwa kweli ni nzuri sana. Tatizo linalotukabili mara nyingi ni uhaba wa bajeti na nimezungumza na wahusika wote akiwemo Waziri wa Fedha, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Ulinzi na Usalama imetusaidia sana kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana ili kuondoa matatizo yanayokabili hususan maslahi ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika baada ya kusema hayo ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ninaona hili Baraza jipya la Kambi ya Upinzani limekuja na mambo mapya. Ninashukuru sana. Kwa hiyo, hoja hii imeungwa mkono hatua inayofuata. *(Kicheko)*

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ndiye anaye kaimu nafasi ya Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Katibu.

FUNGU 38 – NGOME

MWENYEKITI: Msije mkaenda Ngome kuomba mshahara wa Mkuu wa Majeshi. *Vote* ya mshahara ni ngapi?

KATIBU: *Vote 57!*

MWENYEKITI: *Vote 57*. Ninaanza na Waziri Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Waziri mzoefu.
MWENYEKITI: Ngoja kwanza, hatujasoma.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru…

MWENYEKITI: Ninaomba ukae chini, hatujasoma.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Bado!

MWENYEKITI: Naomba ukae chini.

Kif. 1001 – *Defence Forces Headquarters Command* .....*Tsh.784,063,096,000/=*

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mimi niko katika hiyo programu - *Defence Forces Headquarters Command, subvote 1001*, *item 220300 - Fuel, Oils, Lubricants*. Kwa mwaka uliopita ilionekana kuna…

MWENYEKITI: Mmeipata? Mheshimiwa Waziri, umeipata?

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Bilioni 7,963,330,000. Kwa mwaka huu fedha ambazo zimetengwa ni bilioni 6,463,290,400. Na kama tunavyojua Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri anaelewa juu ya hoja au haja ya kuongezeka kwa shughuli hizi za mafuta na mambo mengine na hasa ukizingatia kuna mambo ambayo yataongezeka ambayo hakuna haja ya mimi kuyataja hapa. Ninashangaa tunaongeza mambo ambayo tunaelewa, lakini kuna upungufu wa aina hii juu ya mafuta, vilainisho na mitambo. Naomba ufafanuzi ni kwa nini tatizo hili limetokea. Naomba ufafanuzi wa kina.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna upungufu katika bajeti hii ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita lakini hii imetokana na kupunguzwa kwa viwango vya bajeti vya matumizi mengineyo kwa mwaka wa fedha huu wa 2014/2015 kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.5. Kwa maana nyingine ni kwamba bajeti ya OC ya Ngome imepungua kwa kiwango hicho, kwa hiyo ilibidi tupunguze maeneo mbalimbali kwa mujibu wa bajeti yenyewe ilivyo, kwa mujibu *ceiling* ya bajeti yenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko katika *subvote* hiyo 1001, *item* 220600 - *Clothing, Bedding, Footwear and Services.* Tunajua hizi ni kwa ajili ya nguo, *uniform*, viatu na mambo mengine. Lakini ukiiangalia *figure* yake kwa muda wa miaka mitatu, *figure* ni hiyo hiyo. Je, hakuna ongezeko lolote Mheshimiwa Waziri kwa wanajeshi ambao watahitaji labda nguo na viatu na mambo mengine au kwa wale askari wapya ambao wameingia katika Command hii? Lakini *item* hiyo inajirudia katika 229900, 230500. *Figure* kwa miaka mitatu inaonekana ni hiyo hiyo, kuna kitu gani Mheshimiwa Waziri kimetokea?

MWENYEKITI: Hili swali lako ni kwa nini *figures* zinajirudia, ama kwa sababu ya hiyo uliyotaja mwanzo ya *clothing?* Unataka kujibiwa ipi?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Nasimamia katika *clothing and bedding.*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni lilelile kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya sare na tungependa ziongezeke, lakini pale unapokuwa umepewa *ceiling* huwezi kuongeza na ndiyo maana tunarudi katika viwango hivyo hivyo.

Kwa hiyo, tunachosema hapa ni kwamba utaratibu sasa unalazimisha kwamba wawe wanapata kwa awamu ili tuweze kukidhi na fedha ambazo tunapatiwa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye hiyo *programme 10, subvote 1001* ile kasma ya 210100 - *Basic Salaries - Pensionable Posts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ukijaribu kuangalia ni kwamba *trend* inaonekana kuwa fedha zinaongezeka. Katika ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, amejaribu kudokeza juu ya mpango wa Serikali wa kuangalia wale askari waliostaafu ambao wamekuwa wanalipwa pensheni kidogo na katika majibu yake amesema kwamba Serikali imeanza kuangalia ni jinsi gani ya kuweza kuwaboreshea maslahi yao vizuri, na akasema watajitahidi kuweza kwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, tungependa labda pengine kufahamu, kama ambavyo huku inaongezeka, ni imani yangu hata wale wanaposikia wangependa kuona wanatekelezewa haraka. Je, unaweza ukatueleza pengine suala hili litachukua muda gani kuweza kuharakisha ili wale askari wasiendelee kupata shida huko mtaani walipo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Machali kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba kumekuwa kuna nyongeza ya mishahara mwaka hadi mwaka; na sisi tungepoenda kuona wale waliostaafu siku za nyuma na wao wanapata nyongeza za pensheni zao badala ya kukokotolewa kutokana na mishahara waliyostaafia.

Lakini hili ni suala la kisheria linahitaji mabadiliko ya sharia, na ninapenda nikuhakikishie kwamba mchakato umeanza wa kuweza kuileta sheria hiyo mbele ya Bunge lako tukufu ili tuweze kufanya mabadiliko, wahusika waweze kupata maslahi bora zaidi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif.1007 – *Land Forces Command……...Tshs. 8,066,929,000/=*
Kif.1008 – *Air Defence Command……...Tshs.6,207,507,000/=*
Kif.1009 – *Navy Command…….....…….....Tshs.2,709,790,000/=*

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 1010 – *Military Hospitals……...Tshs.2,495,227,000/=*

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 1010*, kifungu kidogo cha 220400 – *Medical Supplies and Services*. Mwaka huu unaoishia sasa kilitengewa Shilingi 2,106,651,000/= na mwaka unaokuja kinaombewa kiasi hicho hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu hospitali zetu hizi zinakuwa ni kimbilio wakati linapotokea tatizo kwenye hospitali nyingine na tunaona gharama zinavyozidi kukua. Imekuwaje *copy and paste,* yaani gharama za mwaka huu na za mwaka ujao zinakuwa ni hizohizo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mbatia kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema awali, pale unapopewa *ceiling* ambayo imepungua kwa bilioni 2.5, tunachoweza kufanya kwa wale ambao tunaona kuna umuhimu mkubwa kuwa-*maintain* pale walipo, kwa sababu ni lazima tupunguze baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, kifungu hiki kupata fedha hizohizo ni kwa kuona umuhimu wake ndiyo maana tume-*maintain* kwa sababu kwa ujumla bajeti imepungua kwa shilingi bilioni 2.5.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 39 – JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif. 1001- *The National Service Force…Tshs*.196,822,661,000/=

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ni cha 1001, kasma 210100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa wanacho kikosi cha ulinzi kwa maana ya the *SUMA-JKT Guard* ambacho kimethibitika kuwa kina askari waaminifu na waadilifu wanaoweza kutoa ulinzi hususan katika maeneo ya Wizara, Idara na Taasisi za Umma.

Mhweshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingi zimekuwa ziki…

MWENYEKITI: Umesema kifungu gani Mheshimiwa?

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Nimesema Kasma 210100.

MWENYEKITI: Kifungu gani unachozungumzia?

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Mishahara.

MWENYEKITI: Hakuna mshahara hapa!

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Mh!

MWENYEKITI: Mshahara ni kule kwa Waziri tu. Huku hakuna mshahara. Hapa lazima utuambie *item* gani unayoisemea.

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: *Military Supplies!*

MWENYEKITI: Naam?

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: *220500 - Military Supplies.*

MWENYEKITI: *That's Military Supplies and Service,* ehe!

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Ndiyo.
MWENYEKITI: Haya tuambie!

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Wizara za Serikali hulindwa na askari wa makampuni binafsi ambapo mimi ningeamini kuwa kama Serikali ingechukua uamuzi wa pamoja kwamba kazi hiyo ya kulinda Wizara na Idara za Serikali pamoja na Taasisi, ingepewa SUMA - JKT Guard, tungekuwa na uhakika wa kuwa na walinzi waadilifu na wenye uwezo wa kutoa ulinzi wa uhakika kwa Serikali badala ya askari ambao wengi ukweli ni kwamba makampuni binafsi wale wengi hawajapitia kwenye mafunzo!

MWENYEKITI: Hili ni swali kweli ukisoma hapo mbona haviji? *Military Supplies and Services.* Hata ukisoma kwenye…

MHE. GOODLUCK J. OLE- MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nipate ufafanuzi kwamba…

MWENYEKITI: Hapana! Unajua wewe kama unataka kuuliza swali namna hiyo uingie kwenye mshahara wa Waziri kule, hilo ni suala la kisera. Hili ni *Military Services and Supplies* haiji kabisa. Haya tunaendelea, niliona wengine, Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka ufafanuzi kuweza kuelewa katika kifungu kidogo cha 220600 - *Clothing, Bedding, Footwear and Services* ambayo imepungua kwa wastani wa shilingi bilioni moja. Nikijua wazi kuwa vijana wetu wa JKT kuna wale wa mujibu wa sheria na wale wa kujitolea, japokuwa tunajua kuwa kuna changamoto hiyo kibajeti ya *ceiling* sasa iwekeje tushuke kwa kiwango cha bilioni moja na tunajua kuwa kuna kundi kubwa la vijana wanakwenda kule na kupata sare na viatu. Ni jinsi gani zoezi hilo litaendeshwa katika kambi za JKT? Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Jafo kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba kuna upungufu wa fedha ikilinganishwa na mwaka jana, lakini kuna baadhi ya *items* hususan hapa tunachozungumzia zaidi ni sare ambazo hazinunuliwi kila mwaka, kwa maana hiyo ni kwamba unapotumia fedha nyingi mwaka huu una-*save* kwa miaka inayofuata kwa sababu siyo kitu ambacho kinabadilishwa kila mwaka, kwa hiyo ndiyo sababu ya kuwa na kasoro katika fungu hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatibu!

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nasimama Kif. *220600 - Clothing, Bedding, Footwear and Services.*

MWENYEKITI: Kanuni zetu zinasema mwenzio akiuliza hicho wewe hurudii, kimeulizwa sasa hivi huyo aliyekaa ndiye aliyezungumzia kifungu hicho.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme tu kwamba hiki nilichosimamia kilishaulizwa. Mheshimiwa umefanya haraka!

MWENYEKITI: Okay, asante. Nashukuru sana. Hapana mimi ndiye nasimamia kikao, kilichotakiwa wewe mwenyewe ungesimama na kusema kwamba umeshauliza, maana yake hatupotezi muda. Haya!

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kimeshaulizwa. Ahsante!

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.....*Tshs*.17,134,855,600/=

MWENYEKITI: Hivi nyie hamsomi kanuni?

MBUNGE FULANI: Tunasoma!

MWENYEKITI: Sasa kama mnasoma kanuni, nyie wote hamuwezekani hapa. Wapo ambao nawajua mwenyewe. Naanza na Mheshimiwa Masoud Abdallah. Nitawataja, kaeni tu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika maelezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri alieleza juu ya hali ya ulinzi na usalama mipakani, unatarajiwa sana au unategemea sana na urejeshwaji wa alama za mipakani yaani *beacons.* Amesema kwamba kuna baadhi ya maeneo wameanza kurejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikumbukwe kwamba wakati yeye akiwa Waziri katika miaka iliyopita, nami nilikuwa Waziri upande huu huu, na maandishi yake bado mimi ninayo, akaondoka akaenda Wizara ya Afya amerudi tena hapa. Naomba nimkumbushe maeneo ambayo alituahidi kipindi kile, akiwa Waziri na mimi nikiwa Waziri mwenzake. *(Kicheko)*

Becons ambazo zilizoondolewa baina ya Tarime – Tanzania na Migori – Kenya, katika vijiji vya Kirongwe, Ikoma, Panyakoo, Ruche, Kagonya na Nyamuhunda. Vyote vijiji hivyo kwa kipindi kile kwa mujobu wa maandishi yako ulisema kwamba mko katika hatua ya mwisho katika kurejesha alama za Mipaka *(beacons)*. Lakini leo katika maelezo ambayo umetueleza ni maeneo mengine ambayo *beacons* zimerejeshwa. Ulisema kwa kipindi kile kwamba una sababu za msingi maeneo haya kuyafanyia kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia Mheshimiwa Waziri kwa kipindi kile alitueleza kuna vijiji vya Kakunyo, Bugango, Rubale, Mtukula, Nyunzinza na Kashanze. Vile vile ulisema *beacons* hizi nazo zitarejeshwa.

Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri, naomba sasa unieleze na uleze wananchi...

MWENYEKITI: Sema Mheshimiwa Mwenyekiti! Tena huyu Waziri unamuonea hajawahi…

MHE. MASOUD A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri sasa ananieleze na awaeleze wananchi walio katika vijiji hivi ambao kwa kauli yake katika miaka hiyo iliyopita akiwa Waziri kipindi hicho kwamba ni hesabu zipi za msingi ambazo zilipelekea mpaka leo kuwe na kususua na kurejesha alama za *beacons* kwenye vijiji hivi? Naomba ufafanuzi wa kina nashukuru sana.

MWENYEKITI: Naomba ujibu kama Serikali, siyo kama uliwahi kuwa, hiyo haina maana yoyote. Ilikuwepo Serikali na iko Serikali. Naomba ujibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:- Kwanza ieleweke kwamba suala hili ni kweli limechukua muda mrefu. Lakini ni suala ambalo linahitaji ushirikiano wa Wizara kadhaa, ikiwemo

ya Ulinzi, Ardhi, Mambo ya Nje, Tawala za Mikoa na zote. Na haishii hapo, upande wa pili wa jirani zetu wanatakiwa wote wapatikane kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba vitu hivyo vinafanywa inavyotakiwa.

Sasa mambo ambayo yamefanyika sasa baada ya muda mrefu sana, tunafaa kuyapongeza kwa sababu angalau kazi hii imeanza kufanyika. Nilichosema wakati najibu hoja ni kwamba mpaka wetu na Uganda tatizo limemalizwa yaani Tanzania na Uganda sasa matatizo ya *beacons* hayapo tena kwa sababu kazi yote imeshafanyika Uganda.

Tumeanza upande wa Kenya; na upande wa Kenya sehemu iliyoanza kama inavyoonekana katika hotuba yangu ukurasa wa nane, upande wa Tanzania kati ya Tarime na Kurya upande wa Kenya tayari tumesharudisha *beacons.* Kwa hiyo, hatua kwa hatua tutaendelea. Hili jambo Mheshimiwa Mbunge ni zito kidogo kwa maana ya kwamba linahitaji na fedha vilevile siyo kwamba tunarudisha tu *beacons,* kuna fedha nyingi ambazo zinahitajika. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba kwa sababu tumemaliza Uganda na tumeanza Kenya na mazungumzo na DRC na wenzetu wa Zambia yanaendelea, ni matumaini yetu kwamba tutaongeza *speed* yetu ili hatimaye tatizo la mpaka tuweze kulimaliza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza ni tambue mchango wa Waziri alivyokuwa Waziri wa Ulinzi kuanzisha mchakato wa kuweka mipaka eneo la Kunduchi Mtongani, kulikuwa na mgogoro sana baina ya Jeshi na Wanachi. Lakini vilevile Mheshimiwa Nahodha akaja akalimalizia, sasa hivi kuna utulivu. Kwa hivyo, nitambue kazi uliyoianza na Mheshimiwa Nahodha akamalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili linahusu mafao ya wastaafu na kama Waziri hatanijibu vizuri kwa kweli nitatoa shilingi. Nitatoa shilingi kwa sababu hakuna watu wanaoishi maisha ya kifukara…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, eleza kwanza halafu utakapotoa shilingi sisi tutakuwa tunakuelewa. Sasa unaanza kutoa shilingi kabla haujatuambia! Sasa endelea na hoja yako halafu sema unatoa shilingi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni utangulizi.

MWENYEKITI: Aha, utangulizi hatuna muda nao.

MHE. HALIMA J. MDEE: Utangulizi muhimu.

MWENYEKITI: Haya eleza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hajatoa majibu ya kuridhisha kuhusiana na kwa nini Serikali haijaanza kuona haja ya kulifanyia utekelezaji suala la kuongeza pensheni za Wanajeshi wastaafu. Wanajeshi ambao walilitumikia hili taifa kwa uaminifu mkubwa, kwa maumivu kubwa, kwa malengo makubwa ya kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wastaafu hawa tumeliuliza si pungufu ya miaka mitano mfululizo. Majibu ambayo Waziri anatupa leo ni majibu ambayo alitupa miaka minne iliyopita. Sasa mimi ninaomba Waziri atuambie ni kwa nini mpaka leo Serikali haijaona umuhimu wa kuwalinda askari hawa ambao kimsingi ni askari wa akiba, hali ambayo inaweza ikatoa

ushawishi kwa askari hawa ambao wana uzoefu wa maswala mazima ya jeshi kuasi nchi yao kimya kimya baada ya kuona nchi yao imewatekeleza? Sasa naomba Waziri aniambie!

Wakati ananijibu aniambie ni vigezo gani ambavyo vilitumika kuanzisha ubaguzi baina ya wanajeshi wastaafu ambao walistaafu kabla ya mwaka 2007, kiwango chao cha pensheni ni tofauti kabisa na wanajeshi wastaafu ambao walistaafu baadaye. Mtu ambaye alistaafu kwa cheo cha *Sir Major* miaka ya zamani, analipwa shilingi laki 4 kwa miezi mitatu. Mtu ambaye amestaafu kwa cheo hicho hicho miaka ya karibuni analipwa shilingi laki 9 kwa miezi mitatu. Sasa mimi nilitaka Waziri wakati anajibu yote hayo pamoja na mambo mengine, kwanza aniambie kwa nini kuna huo ubaguzi? Pili, kwa nini wamechelewesha? Tatu, ni sheria gani ambazo zinaweka hivyo vikwazo anavyovisema, na hizo sheria zitaletwa nini? Asipojibu nitatoa shilingi, huo ni utangulizi usije ukasahau. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Waziri, maelezo!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba suala la maslahi ya wastaafu wa Jeshi ni suala ambalo Serikali inaona umuhimu wake, ni suala ambalo uchungu huo hana yeye tu Mheshimiwa Halima tunao wote na tungependa hali hiyo ibadilike ili Wanajeshi hawa wapate pensheni ambazo zinaendana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa akisema kwamba Serikali haijaona umuhimu wa kuanza mchakato, hilo siyo sahihi. Mchakato umeanza na mchakato huu unaanza katika ngazi ya pale Makao Makuu ya Jeshi, wamekaa, wamefanya ile kazi, wameweka viwango, wamekamilisha, wamepeleka Wizara ya Ulinzi. Wizara ya Ulinzi kuna kikao cha kutoa maamuzi kinachoitwa DFC, kimekaa kimefanya maamuzi. Hii kazi imepelekwa mbele kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa madhumuni sasa ya kuja kuandaliwa Muswada wa kuletwa Bungeni. Kwa hiyo, kusema kwamba hatujaanza siyo sahihi, kazi imeanza na ni matarajio yetu kwamba hatua zote zilizobaki zitafanya haraka ili hatimaye Muswada huo ufike hapa tuweze kurekebisha sheria kuweza kuwapatia maslahi yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenykiti, pili,…

MWENYEKITI: Ya pili mbona…, ilitakiwa hoja moja tu. Ameuliza, lakin hoja moja tu. Mheshimiwa Waziri unapenda kujibu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliweka vizuri tu hili la kwa nini watu wanatofautiana katika viwango vya pensheni wakiwa na cheo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni kwamba pensheni inakokotolewa kutokana na mshahara. Kwa hiyo, hata kama mna cheo kimoja inategemea wakati wewe unastaafu mshahara wako ulikuwa ni kiasi gani. Kwa hiyo, *Sir Major* aliyestaafu mwaka wa 1970 au hata 1980 hawezi kulingana na *Sir Major* wa sasa kwa sababu mishahara yao ni tofauti. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sababu. Kwa hiyo, lengo ni kwamba tutakapokuja na ile sheria sasa turekebishe hiyo hali ili waweze kupata pensheni ambazo zinaendana na wakati tulionao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, tusifanye ubishi isipokuwa tuwe *logical.*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi. Ninachotaka kusema hapa kama ambavyo nilisema, hata nilivyomuuliza swali akiwa Waziri wa Ulinzi alijibu hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunakihitaji hapa ni *commitment* ya Serikali ya huo Muswada unakuja lini? Ninasema hivi kwa nini! Kwa sababu kumekuwa na *excuse* kwamba hakuna fedha, lakini siyo kwamba Serikali haina fedha. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juzi amesema kwamba trilioni 1.2 zinapotea kwa mishahara hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana imetoka taarifa ya chombo cha Kimataifa cha *Global Integrity* kinasema Tanzania inapoteza trilioni 3 kila mwaka. Tunajua misamaha ya kodi kwa wafanyabiashara wakubwa trilioni 1.8 kila mwaka. Sasa suala la fedha siyo *issue*. Kwa hiyo, mimi ninachotaka, na nimetoa shilingi ili Wajumbe wenzangu wajadili hoja kwa kina, ni lini Muswada utaletwa? Na utuhakikishie kwamba huo Muswada kwa sababu Kaimu Waziri Mkuu yupo hapa, huo Muswada utaletwa lini ili tuujadili, ili…

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi.

MWENYEKITI: Wewe mwenyewe mwenye hoja umeenda nje ya hoja. Kwa sababu huyu amesema ule mkakati wa kulipia wale wastaafu ni hatua inayokwenda katika utaratibu. Hakusema habari ya fedha, alisema ni mkakato. Usinijibu, nakujibu wewe, nakueleza kusudi na wengine wajadili hoja, wasiende nje ya hoja au sivyo tutaleta hoja nyingi sana. Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya kwamba Serikali imekuwa inazunguka zunguka kufanya maamuzi ya kufanya marekebisho ya sheria, kuwezesha wastaafu kulipwa mafao yanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametoa sababu mbili au amejibu maeneo mawili. Eneo moja amesema kuna tofauti kati ya haya mafao ya wastaafu kwa sababu ya tofauti ya viwango ambavyo wanajeshi wanapokuwa wanastaafu vyeo vina tofauti na ndiyo maana vilevile wanatofautiana viwango vya malipo. Kwenye utumishi huu huu wa umma…

MWENYEKITI: Lakini hiyo siyo hoja. Hoja ya…

MHE. JOHN. J. MNYIKA: Ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri amelisema!

MWENYEKITI: Hiyo nilimwambia akipenda ajibu asipopenda asijibu. Kwa sababu hoja yake Mheshimiwa Halima ilikuwa moja kwamba kwa nini wastaafu hawapati mishara yao, na akamwambia kuna mkakati, ndiyo hoja yenyewe. Tukitanua ikawa siyo hoja itakuwa si hoja, hii ndiyo hoja. Hiyo nyingine alijibu *ex-gracia* ndiyo maana nikamwambia jibu moja tu. Hiyo ilikuwa ni *ex-gracia* tu majibu. Mheshimiwa Mnyika, unajua kanuni, jenga hoja!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niseme kwamba kwa hili la sharia, tumekuwa na kawaida katika Bunge hili hili kwa sheria ambazo zinaonekana muhimu sana, Serikali inaji-*commit* inasema kabisa kwenye mkutano fulani wa Bunge tutaleta huu Muswada. Sasa kwa sababu jambo hili tulilihoji mwaka jana, Serikali ikaahidi italeta Muswada, mwaka umepita Serikali haijaleta Muswada, tunataka safari hii Serikali iseme mpaka kikao kipi italeta Muswada, ili tuwe na uhakika wa kuibana Serikali kwamba angalau safari hii jambo hili litafanyika. Serikali isitafute visingizio vya mambo yote hayo, ya Muswada wenyewe na hata ya mafao kwa sababu inapokuja masuala ya Mawaziri Wakuu wastaafu wanalipwa viwango vya Mawaziri Wakuu wa sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali! Kengele imegonga!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilichokuwa nataka tu pengine kuuliza ndiyo ambacho kimeulizwa kwamba tunataka *commitment* ya Serikali ni lini italeta Muswada huo? Atusaidie kuweza kujua kwamba ni lini, basi.

MWENYEKITI: Serikalini!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana nieleze kwamba Bunge fulani tutaweza kuleta Muswada huu. Lakini wote tunatambua hapa taratibu za kuleta Muswada Bungeni ni kwamba baada ya Mwanasheria Mkuu kutengeneza ile Rasimu kuna *process* yake ambayo ni Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mawaziri, halafu inaweza ikapita hata Kamati ya Bunge la Sheria ndipo ije Bungeni. Kwa hivyo, ninachoweza kusema na viongozi wa Serikali wapo hapa, ni kwamba tutajitahidi kuweza kuiharakisha hii *process* ili haraka iwezekanavyo tuje na Muswada huu Bungeni. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huwa inaleta Miswada ya Hati ya Dharura kutokana na unyeti wa mambo. Labda tu Serikali tu ikiri hapa kwamba wanajeshi wastaafu kwao siyo kipaumbele na wala hakuna unyeti wala udharura kwa sababu wanaona wameisha wafukarisha kwa miaka mingi, kwa hiyo, hawana cha kuwafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Serikali ina nia ya dhati, kama Serikali ina nia ya dhati, ina uwezo kabisa hasa ukizingatia Waziri amesema lipo katika hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Angeniambia yupo katika ngazi za chini za Jeshi huku ningeelewa, iko katika hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, mimi ninachoomba shilingi yangu siirudishi, tupige kura ili wanajeshi huko wajue jinsi Serikali yao ambayo inajisifu inawapenda sana lakini linapokuja suala la maslahi yao ndiyo ya kwanza kupiga dana dana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupige kura.

MWENYEKITI: Kwanza, Waziri *clarify,* ulisema ipo *stage* gani sasa. Lazima tu-*clarify* maana sisi hatukusikia, mimi sikusikia hivyo.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba ipo katika ngazi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWENYEKITI: Naomba tufanye maamuzi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zungu!

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa inafanana sana na ya Mheshimiwa Halima Mdee, lakini si kwa kiwango alichokimalizia yeye. Isipokuwa mimi sasa nitajaribu kuibadilisha ili isiwe inafanana na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majeshi mengi na nchi nyingi duniani zimekabidhi majeshi yao vitega uchumi ili viweze kujiendesha. Najua kuna SUMA-JKT ambao sasa hivi wanafanya kazi za kiuchumi kwenye Jeshi. Lakini bado mchango wao katika kulisaidia Jeshi ni mdogo sana. Kwenye hoja zetu za Kamati ya Kodi uliyotuchagua tulikuwa na taarifa kuwa tunapoteza siyo chini ya bilioni 500 kwenye *deep sea fishing*.

Je, Waziri sasa atakuwa na mkakati gani wa ku-*engage* SUMA-JKT ili waanze kufanya *deep sea fishing* ili kuwe na dirisha sasa la Jeshi na vyombo vya Ulinzi badala ya kutegemea bajeti ya Serikali na hasa kuwasaidia hata kwenye hii pensheni yao itokane na biashara hii ambayo watafanya kusaidia Serikali wao wenyewe waweze kujiendesha. Nilikuwa naomba majibu tu, wala sina nia ya mshahara, akinijibu tu mimi nakaa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Zungu kwamba, wazo alilolitoa ni zuri, tunalipokea, tutaangalia uwezekano wa kulitekeleza, kwa sababu hoja hapa ni kuongeza mapato kwa Jeshi letu. Tunashukuru kwa ushauri. *(Makofi)*

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Jeshi letu linafanya kazi nzuri, pamoja na mengine mengi mazuri hasa wakati tunapopatwa na majanga. Mwaka 2011, mwezi Disemba, mafuriko yalipotokea Jijini Dar es Salaam walifanya kazi nzuri sana ya uokoaji lakini hawakuwa na vifaa vya kisasa. Mwaka 2013, tarehe 29 Machi, Jengo lilipoanguka katikati ya Jiji la Dar es Salaam, Wanajeshi wetu walishiriki katika uokoaji lakini hawakuwa na vifaa vya kisasa. Mwaka 2011, tarehe 11 Aprili, mafuriko yalitokea pia na maeneo mengine ya nchi ikiwepo Jiji la Dar es Salaam.

Suala la majanga kwa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia tisini yanasababishwa na vitendo viovu vya binadamu, ambayo ni *man made risk*. Sehemu kubwa ambayo, Jeshi letu linaweza likawa na kitengo chenye vifaa vya kisasa ili kuokoa maisha ya binadamu, lakini mwaka jana tarehe 29 Machi, SIKU ya Ijumaa Kuu, Jeshi letu halikuwa na vifaa vya kisasa na wakakiri hivyo, tulishiriki nao. Baadhi ya maisha ya binadamu yakapotea, zaidi ya watu 30 walikufa.

Je, Jeshi letu kwa hali tuliyonayo sasa, Waziri anasemaje kuwa na vifaa vya kisasa vya teknolojia ya kisasa ili maafa yanapotokea wasitumie tu mtulinga bali watumie vifaa vya kisasa kutokana na sayansi na teknolojia iliyopo Duniani kwa sasa?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mpango wa Maendeleo wa Jeshi, ambao moja ya maeneo ambayo tunataka tuhakikishe tunayaboresha ni Kitengo chetu cha *Engineering,* ambacho kitakuwa na kazi na jukumu la kuhakikisha maeneo kama hayo ya maafa wanatoa msaada kwa kutumia vifaa vya kisasa. Mpango huo wa Maendeleo wa Jeshi umeshaanza na kuna vifaa ambavyo wameshapokea. *Engineering Unit* ya Jeshi ya leo siyo sawa na ile ya zamani, tutaendelea kuijengea uwezo ili hatimaye kiweze kusaidia katika majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, Kitengo hiki kipo na kimeshaanza kuimarishwa na ni mategemeo yetu kwamba kitaendelea kuimarika ili kuweza kutoa huduma hiyo anayoizungumzia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Maafa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbatia, narudia jibu la swali langu nililowahi kujibu juu ya maafa hapa kwamba; tunayo Sheria

ya Maafa, ambayo kwa sasa Serikali tumeona haitusaidii. Katika marekebisho tunayoyafanya, tungependa tuwape kisheria, ukiacha utendaji wao kama Jeshi, lakini kisheria suala hilo la uokoaji. Kwa sasa unaweza kuona Zimamoto kwa sheria ndiyo watu wanaoshughulikia Zimamoto na Uokoaji, lakini mara nyingi tumekuwa tunatumia Jeshi la Wananchi. Kwa hiyo, sheria yetu tunayoifanyia marekebisho, tumeshatambua uzoefu wa Jeshi na uwezo wao wa namna ya kushiriki. Kwa sababu ndiyo watu ambao wapo mstari wa mbele katika majanga yote kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuwape uwezo wa kisheria wa kushughulikia mambo hayo ya baharini na uokoaji kama huu, ambao utawezesha Jeshi lenyewe kuwa na bajeti ya kufanya mambo hayo, siyo kama haya yanavyotokea sasa, wanajiminya kwenye bajeti zao kufanya mambo ambayo hayako ndani ya sheria wanafanya kama Wanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ya Kitengo cha *Engineering*, lakini Sheria ya Maafa tunarekebisha kutokana na uzoefu tulioupata na ushauri huo unaoutoa Mheshimiwa Mbatia.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, ninamuungana mkono Mheshimiwa Waziri, kuwapongeza sana Wanajeshi wetu, hakika Jeshi letu lina Wataalam waliobobea. Mapema mwaka huu, walitusaidia sana katika Jimbo langu kutokana na maafa yaliyotokea katika Kata za Mussa na Kisongo. Walitusaidia kurejesha miundombinu ya uchukuzi kwa kutujengea *drift* ambazo zimewezesha Wananchi wetu kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma 210100.

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri, zungumza tu.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT wana kikosi kizuri sana cha ulinzi, wanao Askari wenye ujuzi na utaalam wa kutosha, wana silaha za kutosha, wana uadilifu na ni waaminifu wa kutosha. Idara nyingi za Serikali zimekuwa zikitumia Askari wanaokodishwa kutoka Makampuni binafsi ambao kwa uzoefu wangu, walilinda ofisi yangu na walilinda nyumbani kwangu, baadhi huajiri watumishi wasio na ujuzi, hawajapitia mafunzo yoyote ya ulinzi. Matokeo yake ni kwamba, tunawaweka Mawaziri na Viongozi wengine pamoja na Wizara za Serikali katika *risk* kubwa kwa kuendelea kutumia makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa SUMA JKT wamethibitika kuwa na uwezo mkubwa na uzoefu wa kuweza kutoa ulinzi huo, kwa nini Serikali isiajiri SUMA JKT kwa ajili ya kutoa ulinzi kwenye Makao Makuu ya Wizara na Idara mbalimbali za Serikali pamoja na Makao ya Viongozi wa Serikali ili kuwa na uhakika wa kwamba Viongozi hawa watakuwa salama na Idara za Serikali zitakuwa salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa pongezi anazotoa kwa *SUMA JKT Guard,* kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Kama nilivyosema kwenye Hotuba yangu, tayari wameshaajiri vijana 1,668 na mwaka ujao wa fedha wanatarajia kuongeza vijana wengine 2,000. Nia na madhumuni ni kujenga uwezo wao wa kutoa huduma kwa Serikali kwa ujumla pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba, huko ndiko tunakoelekea, bila shaka baada ya kuajiri vijana hao 2,000 mwakani, tutakuwa na uwezo wa kutoa huduma hii kwa taasisi nyingi za Serikali bila kuziacha *private sector* ili tuendeleze shirika hili kwa sababu kazi wanayofanya imethibitika kuwa ni nzuri.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilimshauri kuhusu kuimarisha usalama katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika, mpaka ambao ni mpana sana na kwamba kulikuwa na wazo la kujenga Kambi ya Jeshi Namanyere ambapo katika ufafanuzi wake sijasikia chochote na kwenye Hotuba yake pia sijasikia. Nikataka nimshauri kwamba, kutokana na hali ya kisiasa ya majirani zetu kutotengemaa, upo umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha maeneo ya mpakani hasa yanayopakana na Ziwa Tanganyika. Vilevile kumekuwa na matishio ya uvamizi wa Wananchi katika shughuli zao za kila siku za uvuvi kwenye Ziwa Tanganyika.

Ninataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ushauri wangu ameuzingatiaje?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake umepokelewa, ni ushauri mzuri ambao sikuweza kuutolea kauli hapa kwa sababu Wakuu wa Vyombo hivi wapo, wameusikia, wataufanyia kazi ili kuona utekelezaji wake utakuwaje. Tunatambua kwamba, upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba eneo hilo linapata usalama wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna utaratibu sasa wa kuleta boti kwa ajili ya kuweka katika Ziwa hilo ili liweze kulinda usalama wa wavuvi, ambapo mara kwa mara kumetokea matukio ya kijambazi katika Ziwa hilo.

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu ni kwamba, natoa hoja yangu nikiwa natambua na kuthamini kazi ya Jeshi la Wananchi Tanzania. Hoja yangu ipo kwenye mahusiano kati ya Wanajeshi na Raia na ninazungumza hili kutokana na mawasiliano yangu na Wizara ya Ulinzi, akiwemo *CDF* na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mahusiano yasiyo mazuri kati ya Kambi ya Kaboya na Kata zinazozunguka. Suala hili nimeliwasilisha Ofisi ya Waziri, *CDF* ana *copy* na maji yalipozidi unga nikamwaleza tajiri, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Tarehe 25 Mwezi wa Saba, Mheshimiwa Rais akasema huu mgogoro uishe. Huu ni mgogoro wa Wanajeshi kuvamia Wananchi.

Mheshimiwa Waziri umezungumza Wananchi wanapovamia Jeshi, sasa nataka mimi la kwangu unieleze; tatizo la Jeshi la Kaboya kuvamia Wananchi wa Kata zilizozunguka. Ningependa kueleza mimi hili limenifika pabaya na huko watu waliko wanatuma meseji, nitatoa shilingi kama sitapata maelezo ya kuridhisha tumefikia wapi. Jeshi la Wananchi linaweka *beacon* badala ya Wizara ya Ardhi kuweka *beacon*. *Beacon* zinazozunguka Kata zangu hizo tatu zimewekwa na Wanajeshi ilhali anayepaswa kuweka *beacon* ni Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Waziri nimekuandikia kwenye mchango wangu, lakini hukusoma sijui kwa makusudi au kwa nini, lakini nazungumzia hili suala la Wanajeshi sasa kuwavamia Wananchi. Migomba inakatwa, wiki iliyopita Wanajeshi wetu, mimi ninawathamini nimeshiriki kwenye Vita ya Uganda, Wanajeshi wetu wamevamia eneo la Mayondwe na kukata migomba. Waziri uniweke sawa katika hilo na dhamira yangu ndiyo hiyo.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa anazonipa sasa hivi ni kwamba, kuna mgogoro kati ya Wanajeshi na Wananchi wanaozunguka eneo la Jeshi. Kwa kuwa sina *facts* za kwamba ni nani mwenye haki au mwenye stahili ya eneo hilo, naomba nimshauri akubali kwamba, niunde Kamati ndogo ya Wataalam, iende mara

moja katika eneo ili wakae na wahusika wote, wadau wote wakae ili tuweze kutafuta ufumbuzi wa kudumu juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, Serikali haina taarifa kwa tamko la Rais tarehe 25 Mwezi wa Saba?

MWENYEKITI: Tuelewane utaratibu, unasikitika ndiyo unafanyaje sasa, unatoa shilingi au ndiyo nini?

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mgogoro unaozungumziwa kuna nyaraka nusu *ream* ziko kwenye Ofisi za Serikali. Wananchi wameondolewa kwenye maeneo yao, wamezuiliwa kuendeleza mazao yao, wamezuiliwa kulima na hivyo wanashindwa kuendelea kwa tatizo ambalo limedumu takribani miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanye maamuzi na inieleze wale Wanajeshi ambao wameingia sehemu ya Wananchi, warudi wawaache Wananchi waendelee ili hawa watu wa-*exit*. Mimi nathamini mchango wa Jeshi na nimewaambia, mjukuu wangu hakuelewa kwamba mimi nimeshiriki kwenye Vita ya Uganda, mimi ni Kiongozi niliyeongoza Vijana 350 kwenda kupokea Majeshi yetu yanatoka Uganda, tukiimba naapa, naahidi, kwa hiyo, nalithamini Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, Wanajeshi wetu wale wako *exit* na Wananchi wa Mayondwe na Wananchi wa Izigo, wafanye kazi pamoja, wawaache akina mama walime Ishoro, wawaache watu walime ilimradi hawa watu wasaidiane katika ulinzi mpaka pale ambapo wewe utakuwa tayari na Wizara ya Ardhi kuja kuweka *beacon* zinazotakiwa. Hiyo ndiyo lugha ambayo Wananchi wangu maskini wangeweza kuielewa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kuna mambo mengine hatubishani sana.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nadhani nimejaribu kusema ni hicho ambacho anakisema Mheshimiwa Mbunge; ya kwamba, Jeshi lingependa kuishi vizuri na majirani zake na huo ndiyo msimamo wao, mara zote wanataka iwe hivyo. Hakuna sababu ya kugombana na watu ambao wanakuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge akubali, mara moja tutengeneze hii timu ambayo itakwenda pale, itakaa na pande zote kwa pamoja, tukubaliane ni jinsi gani ya kulitatua tatizo hilo. Mimi sidhani kama ni tatizo kubwa endapo mazungumzo yatafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, tupate nafasi ya kushirikisha wadau wakiwemo Wizara ya Ardhi ili wao ndiyo watuambie hizo *beacon* ziwe wapi. Kama anavyosema, Wanajeshi wameziweka sehemu isiyostahili, zitabadilishwa ili ziwekwe kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwijage?

MHE. CHARLES P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts.... .... Sh*. 277,753,800

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Policy and Planning… … … …. Sh*. 520,760,000

MWENYEKITI: Mnaongea halafu mnashtukia; haya Mheshimiwa Mkosamali!

KATIBU: Mheshimiwa Machali.

MWENYEKITI: Aah! Mheshimiwa Machali, mimi watoto hawa huwa nawachanganya kila siku.

WABUNGE FULANI: Ni hao hao kweli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali! Ni hao hao kweli. *(Kicheko)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sisi ndiyo wale wale tunafanana ni pacha wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye Kasma 210100 - *Basic Salaries - Pensionable Posts*. Kwa sababu kifungu kinahusiana na *policy and planning*, nina swali moja kwa Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia. Katika maelezo yake wakati anatoa ufafanuzi, amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba, wale Askari wa kutoka Jeshi la Wananchi la Tanzania ambao wapo kwenye Operesheni mbalimbali, wamekuwa wanalipwa asilimia 80 ya mapato ya yote ambayo wanalipwa na asilimia 20 …

MWENYEKITI: Ngoja tukuelewe, umesema kifungu gani?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, 210100 - *Basic Salaries - Pensionable Posts.*

MWENYEKITI: Ipo kwenye *Policy and Planning*?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Mbona inaonekana hai-*fit* hii unayosema.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja utanielewa kwmaba ninakupeleka wapi.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amelieleza Bunge lako kwamba, asilimia 20 ya kile ambacho Wanajeshi wetu walikuwa wanapaswa kulipwa katika asilimia 100 inaingia Serikalini. Swali langu ni moja; hawa watu ambao ni watu wa Sera pamoja na Mipango ndani ya Jeshi au ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wanaona kwamba ni halali wanalipwa mishahara kwa kutumia kasma hii? Ni halali kiasi gani kuweza kupanga mpango wa kuchukua kiasi hiki cha asilimia 20 ya mapato ambayo wanalipwa Wanajeshi? Wangestahili kuweza kulipwa kutokana na kazi yao ni ngumu. Huu ni kama unyang'anyi. *It is like,* pengine unatoka hapa kama Mbunge unaenda katika eneo fulani labda ni kwenye *workshop* au kwenye kazi, halafu kesho utuambie kwamba utatukata pesa; hili jambo halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa kutosha vinginevyo nisiporidhika nitaondoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Huondoi shilingi wala neno lako halikubaliki, umedandia dandia tu. *(Kicheko)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 - *Internal Audit*… … … … … … … Sh. 147,273,000
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*… …. Sh.110,985,600
Kif. 1006 - *Legal Service Unit*… … … … … … Sh. 82,000,000
Kif. 1007 - *Government Communication Unit*… Sh.122,262,000
Kif. 1009 - *Independent Telecomm. Network*… Sh. 86,165,800
Kif. 2001 - *Industries, Costruction and Agriculture*Sh. 375,944,200
Kif. 2002 - *Military Research and Development*… Sh. 301,599,000
Kif. 2003 - *Building Consulting Unit*… … … … Sh. 211,565,800
Kif. 2004 - *Estate MGT and Development Unit*… Sh. 339,681,200

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 38 - NGOME

Kif. 1001 – *Defense Forces Headquarters' Command* … … … … … … … … … … Sh. 12,000,000,000

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru *Subvote 1001,* niko katika *Item 6103 - Defense Schemes.* Mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni tano na mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni saba. *Defense Schemes* hizi ni fedha kwa ajili ya ujengaji au ujenzi wa maghala. Mpaka hivi tunavyozungumza, pamoja na kazi ambayo imetokea ya milipuko ya maghala mbalimbali Gongolamboto na Mbagala lakini mpaka sasa hakuna fedha mpaka sasa iliyotoka.

Shilingi bilioni tano za mwaka jana hakuna hata shilingi moja mpaka sasa iliyotolewa. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni sababu zipi za msingi zimesababisha fedha ambayo sisi Wabunge tuliidhinisha kwa ajili ya ujenzi wa maghala hadi leo hakuna hata senti tano iliyotoka na tukijua kwamba maghala na ujenzi wa maghala ni muhimu sana hasa kutokana na mambo yaliyotokea kule Gongolamboto na Mbagala? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nisahihishe tu kwamba, eneo analolizungumza la *Defense Schemes* siyo la ujenzi, hilo ni la ukarabati wa zana maalum. Eneo analolizungumzia liko chini yake hilo la *Construction,* lakini hoja yako ya bilioni tano ipo sawa. Suala hili tumelifikisha Hazina na walichoweza kutueleza ni kwamba, mwaka wa bajeti haujaisha, bado mategemeo ya kupata fedha yapo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Huwezi kuuliza mara mbili.

FUNGU 39 – JESHI LA KUJENGA TAIFA

Kif.1001 – *The National Service Force* … Sh. 7,000,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 57 - WIZARA YA ULINZI

Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … … Sh. 150,000,000

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza kuhusiana na kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja kuhusiana na migogoro ya ardhi kati Kikosi cha Majeshi pamoja na Wananchi, kuna eneo la Kijaka kule Kimbiji ambako kuna mgogoro wa ardhi kati ya Wananchi na Jeshi.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, hujatuelekeza unazungumzia kitu gani.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Katika kifungu 103.

MWENYEKITI: Kifungu kidogo?
MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Cha 6103 katika *Defense Schemes*.

MWENYEKITI: *Okay*. Uwe na hakika unachokisema ndicho. Haya, endelea Mheshimiwa Ndugulile.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Nilichotaka kukiuliza, kwa sababu katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri hakugusia Eneo la Mazoezi la Jeshi kule Kijaka Kimbiji. Eneo lile jeshi lilichukua bila kulipa fidia Wananchi. Sasa swali ambalo nataka kuuliza; je, sehemu ya fedha hizi katika fungu hili ni hizi ambazo zitatumika kulipa fidia katika Eneo la Mazoezi la Kijaka Kimbiji?

MWENYEKITI: Uliza hizi hela ni za kazi gani, halafu utaambiwa ukweli. Eti ni za kazi gani?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili halihusiki na ulipaji wa fidia. *Policy and Planning,* hizi fedha ni kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya Miradi inayoendelea. Kwa hiyo, fedha zinazohusika na masuala ya ulipaji wa fidia na kadhalika, ipo kwenye kifungu cha mwisho pale, *Estate and Development Unit*. Sasa, naomba baadaye nimpatie Mheshimiwa maelezo ni maeneo gani ambayo yametengwa katika kulipia fidia kwa mwaka huu kwa sababu sina uhakika wa hilo eneo ambalo analizungumza.

MWENYEKITI: Inatosha ulivyosema hizi sizo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1009 – *Independent Telecommunication Network* … … … … … … … … … …Sh. 10.000,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture* … … … … … … … … Sh. 95,198,092,150

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Kasma 6103 - *Defense Schemes*, imetengewa shilingi 95,198,000,000. Natambua kwamba, ndani ya kifungu hiki vilevile bilioni nene za ujenzi wa nyumba 6,064 za Wanajeshi. Sasa ukienda kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 19, inataja maeneo ambayo nyumba zitajengwa, Arusha 792, Dar es Salaam 2,088, Mikoa inaendelea kutajwa Dodoma, Kagera na kwingineko na maeneo mengine yanatajwa.

Ningependa kupata ufafanuzi kuhusu aya ya juu yake ambayo anasema, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa nyumba hizo unatekelezwa na Kampuni ya *Shanghai Construction Group General Company,* umeanza tarehe 17 Julai, 2013. Huku kwenye utangulizi tunaelezwa kwamba, moja ya kazi ya SUMA JKT ni pamoja na ujenzi wa nyumba na tunasema SUMA JKT ina *tender* chache sana za ujenzi, inakosa pesa za ujenzi.

Sasa ningependa kupata ufafanuzi; je, SUMA JKT itahusishwa nayo kwenye ujenzi huu au zote zinajengwa na kampuni ya nje na hivyo kukosesha mapato SUMA JKT? Ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Sawa, ahsante. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Mnyika kama ifuatavyo:-

Kwanza, nataka uelewe kwamba hiyo bilioni nane ni asilimia tano tu ya fedha zinazotakiwa kutolewa, yaani huo ni mchango wa upande wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo. Huo ni mradi mkubwa sana na ni mkopo kutoka Serikali ya China na kwa mujibu wa taratibu za mikopo, wao huwa wana utaratibu wa kwamba, kampuni inayotekeleza lazima iwe inatokea nchini mwao. Kwa hiyo, ndiyo maana imechaguliwa Shanghai na hii ni asilimia tano tu ya ulipaji wa fedha inayotakiwa ya upande wa Serikali. SUMA wataendelea na ujenzi kwa kupata *tender* nyingine mbalimbali na Jeshi la Wananchi mara zote wamekuwa wakitumia SUMA katika ujenzi wa maeneo yao.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - *Military Research and Development* … … … … … … … … Sh. 118,296,907,850

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naelekwa kwamba, kifungu hiki kinahusiana na masuala ya *research* katika Majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, sasa hivi kuendana na sayansi na teknolojia wanahitaji sana kufanya utafiti. Kifungu hiki ukiangalia kuanzia mwaka juzi, fedha zinazidi kupungua na mwaka huu zimepungua kwa takribani milioni sabini na kitu, naomba maelezo au ufafanuzi kutoka kwa Waziri ni kwa nini hali imekuwa hivyo wakati tunatambua kwamba sasa hivi sayansi na teknolojia ni muhimu sana na kwa maana hiyo utafiti katika Majeshi yetu ni muhimu? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, maelezo!

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Suzan kama ifuatavyo:-

Kuna baadhi ya fedha katika kifungu hiki kama utaangalia Randama, utaona Mradi wa Utafiti wa Nyumbu umeongezewa fedha. Kwa hiyo, suala la utafiti fedha zimeongezeka kutoka bilioni nne iliyokuwepo mpaka bilioni sita ambayo inaonekana hapo sasa hivi. Sababu ya kufanya kifungu hiki kipungue ni kwamba, ndani ya kifungu hiki kuna *installment* za kulipa mikopo tuliyokuwa nayo kwa mujibu wa taratibu tulizokubaliana za ulipaji mikopo. Sasa mikopo inaweza ikaanza na kiwango fulani, mwakani kinapungua, mwaka unaofuata kinapungua mpaka unapomaliza, ndiyo maana fedha hizi zimepungua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, huwezi kuuliza kwa sababu kifungu chenyewe ni kimoja tu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 - *Building Consulting Unit* … … Sh. 1,555,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – *Estate MGT and Development Unit* … … … … … … … … … … … … …Sh. 5,000.000.000

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki ambacho kinahusiana na masuala ya *Estate Management Development.*

MWENYEKITI: Namwita kwa sababu kule alikouliza mara ya kwanza tulisema siko tukamwelekeza hapa. Mheshimiwa Ndugulile!

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Nashukuru Mwenyekiti, katika hoja yangu ya awali niliongelea kwamba, kuna eneo la mazoezi kule Kijaka Kimbiji, ambapo Jeshi lilitwaa na kuipima baadhi ya maeneo ya Wananchi bila kulipa fidia na tuna vielelezo vyote vya Jeshi kukiri kwamba kweli walichukua eneo lile bila kulipa fidia. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri; je, fedha hizi katika maeneo ambayo watakwenda kulipa fidia na maeneo ya Kijaka Kimbiji nayo yamo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wameniletea vikaratasi kuuliza maeneo yao, naomba niyasome maeneo ambayo yatahusika na ulipaji wa fedha hizi. Ongezeko katika Kasma hii inatokana na kuongezeka kwa maeneo ambayo yanahitajika kupimwa na kulipwa fidia kwa ajili ya matumizi ya jeshi. Maeneo hayo ni Kakonko - Kigoma, Ilemela - Mwanza, Ihumwa - Dodoma, Kimbiji - Dar es Salaam, Kigongo - Mwanza, Msata - Bagamoyo na Rosonti - Tarime. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

T A A R I F A

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Fungu la 39 - Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Hoja hiyo sasa imeungwa mkono, wote wameafiki. Wote wanaafiki kwa sababu wanatambua umuhimu wa Jeshi letu na kwamba, hata Maonesho yale yalikuwa murua kuonesha ulimwengu unavyofanana. *(Makofi)*

Si mlikuja wenyewe kuangalia! Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwa kazi nzuri pamoja na Wataalam wako na Maafisa wote na tuwatakie kazi njema katika kipindi kijacho. Katibu, hatua inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 Wizara ya Maliasili na Utalii

SPIKA: Napenda kutambua uwepo wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Bi. Maimuna Tarishi. Yuko wapi? Halafu na wageni wengine 15, nafikiri wote wa Wizara ya Maliasili wako hapa. Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Maliasili!

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii
Kama Ilivyosomwa Bungeni

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2013/2014. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kwa kuniwezesha kuwa hapa Bungeni siku ya leo. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii yenye jukumu la kusimamia rasilimali za maliasili na malikale na kuendeleza Utalii. Pia, nampongeza Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Aidha, kwa kushirikiana na

wafanyakazi na wadau wa sekta hii, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu, kusimamia vyema uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na maendeleo ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mheshimiwa James Daudi Lembeli (Mb), kwa ushirikiano wao thabiti na Wizara yangu. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati, hususan wakati wa kupitia na kuchambua Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015, yameiwezesha Wizara kutekeleza vyema majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo wa Jimbo la Kiembe-Samaki, Zanzibar; Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa wa Jimbo la Kalenga, Iringa; na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete wa Jimbo la Chalinze, Pwani, kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge. Aidha, natoa pole kwa familia na Wananchi wa Majimbo ya Kiembe-Samaki, Kalenga na Chalinze, kwa kuondokewa na waliokuwa wawakilishi wao hapa Bungeni. Vilevile, natoa pole kwa familia na Watanzania wenzetu walioathirika kutokana na majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko, ajali za barabarani, wanyamapori wakali na waharibifu na wengine kupoteza maisha. Namwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi; *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Taarifa hiyo imezingatia utekelezaji wa ahadi na maelekezo yaliyotolewa Bungeni, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu ya pili ni Mpango na Bajeti ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 umezingatia Sera, Sheria, Mikakati ya Kitaifa, maelekezo ya Serikali na ahadi za Waziri Bungeni wakati akihitimisha Hotuba yake kuhusu Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014. Utekelezaji huo unahusu sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii, Malikale na Uratibu, Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu.

Sekta Ndogo ya Wanyamapori; Utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori: Wizara imekamilisha mapitio ya Kanuni za Usimamizi wa Wanyamapori wa Taifa na Leseni Maalum ya Uwindaji. Kanuni hizi zitaanza kutumika mwezi Juni, 2014. Rasimu ya Kanuni za Matumizi ya Silaha za Kiraia zinazotumika kwenye uwindaji wa Wanyamapori na Kanuni za Uchimbaji Madini ndani ya Mapori ya Akiba zitaanza kutumika mwaka 2014/2015. Aidha, Rasimu ya Kanuni za Uanzishaji wa Kikosi cha Ulinzi wa Wanyamapori inaendelea kupitiwa na wadau ili kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza ushiriki wa wadau katika usimamizi na kunufaika na rasilimali za wanyamapori, idadi ya Maeneo ya Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori *(WMAs)*, zilizoidhinishwa imeongezeka kutoka jumuiya 17 hadi 19. Aidha, Jumuiya za Jamii *(CBO)*, JUHIWANGUMWA - Rufiji, UMEMARUWA – Wanging'ombe na Mbarali na *WAGA* – Iringa Vijijini, zimekamilisha baadhi ya hatua za kuanzisha *WMA*.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Wanyamapori: Mwaka 2013/2014, siku za doria 54,574 zilifanyika ndani na nje ya Mapori ya Akiba. Watuhumiwa 391 walikamatwa kwa makosa mbalimbali, ambapo kesi 277 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Kati ya hizo, kesi 123 zenye washitakiwa 164 zimeisha kwa watuhumiwa kulipa faini ya jumla ya Shilingi milioni 75.6. Kesi 154 zenye watuhumiwa 227 zinaendelea katika mahakama mbalimbali. Vilevile, nyara za Serikali na bidhaa mbalimbali zilikamatwa. Aidha, kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na

Usalama, Wizara ilifanya doria maalum nchi nzima *(Operesheni Tokomeza)* ambapo watuhumiwa 2,085 walikamatwa na jumla ya kesi 839 zilifunguliwa dhidi yao katika mahakama mbalimbali hapa nchini. Maelezo kuhusu nyara za Serikali, vifaa na mali zilizokamatwa wakati wa Doria na wakati wa *Operesheni Tokomeza* yako katika aya ya 10 na 11 katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara. Tarehe 9 – 10 Mei, 2014, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na kwa kushirikiana na *The International Conservation Caucus Foundation (ICCF)* ya Marekani, iliandaa na kufanikisha Mkutano wa Kimataifa uliojulikana kama "*Stopping Wildlife Crime & Advancing Wildlife Conservation" "A call for Action"*. Katika Mkutano huo, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

(1) Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* imefikia makubaliano ya kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Kuhifadhi Wanyamapori utakaojulikana kama *Multlateral Antipoaching and Wildlife Busket Fund,* utakaosimamiwa na *UNDP* na kuchangiwa na nchi, Mashirika na Wadau Wahisani wa Maendeleo.

(2) Katika Mkutano huo, Washirika wa Maendeleo wakiwepo *UNDP*, Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Ufaransa, Uingereza, Serikali ya China, Serikali ya Japan, Benki ya Dunia, Finland na Benki ya Maendeleo ya Afrika, walitia saini makubaliano ya ushirikiano na Serikali ya Tanzania kuhusu Uhifadhi na Ulinzi wa Wanyamapori; huku utiaji sahihi huo ukishuhudiwa na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bibi Hellen Clerk, Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*.

(3) Viongozi wa Dini kwa pamoja walitoa Tamko la kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha waumini wao kote nchini, kupinga vitendo vya ujangili na biashara haramu ya nyara.

(4) Serikali iliwatunuku "*Life Time Archievement Award*" watumishi watano wa Idara ya Wanyamapori kwa niaba ya wahifadhi wastaafu nchi nzima. Watumishi hawa na wengine, wameyatoa maisha yao kwa uhifadhi wa wanyamapori. Tuzo hizi zitaendelea kutolewa kwa wahifadhi katika sekta yote ya uhifadhi nchini katika siku, miezi na miaka inayofuata.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Wananchi Dhidi ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu: Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, iliendesha siku za doria 696 katika Wilaya 19 zilizoathirika kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu, kwa lengo la kulinda Wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, watu 11, kwa bahati mbaya sana, walipoteza maisha yao na jumla ya ekari 4,345.82 za mazao ziliharibiwa na wanyamapori hao katika Wilaya za Busega, Babati, Monduli, Iringa Vijijini, Tabora, Tunduru na Ilemela. Nachukua fursa hii kutoa pole za dhati kwa wote waliofikwa na majanga hayo. Wizara imetoa kifuta machozi cha jumla ya Shilingi 9,200,000 kwa familia za waliopoteza maisha na Shilingi 98,4 milioni kama kifuta jasho kwa Wananchi walioharibiwa mazao yao mbalimbali katika zile hekta nne nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Miundombinu, Vitendea Kazi na Huduma: Mwaka 2013/2014, barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 220 zilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba ya Moyowosi-Kigosi, Mkungunero na Maswa. Vilevile, kilomita 136 za mipaka zimesafishwa. Kazi nyingine za ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na ununuzi wa vitendeakazi ni kama zilivyoainishwa katika aya ya 15 na 16 katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, leo tarehe 13 Mei, 2014, nimetia saini agizo la kuanzishwa rasmi kwa Mamlaka ya Wanyamapori Nchini Tanzania, ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009; na kwamba, Mamlaka hii sasa itatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kazi Julai, 2014. Aidha, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeamua kuwa Makao Makuu ya Mamlaka hii ya Wanyamapori *(Tanzania Wildlife Authority – TAWA)* sasa itakuwa katika Mji wa Morogoro. Mamlaka hii itachukua majukumu yote, isipokuwa yale ya kisera yatakayoendelea kutekelezwa na Idara ndogo ya Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori *(TWPF)* ulielekeza matumizi yake katika shughuli za kulinda wanyamapori; utafiti na mafunzo; kutoa elimu kwa umma; na kukarabati miundombinu katika Mapori ya Akiba, Vyuo na Taasisi za Utafiti wa Wanyamapori. Mwaka 2013/2014, Mfuko ulikadiria kukusanya Shilingi Bilioni 16.4. na Hadi Machi mwaka huu, Mfuko ulikusanya Shilingi Bilioni 10, sawa na asilimia 61 ya makadirio yake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori ilifanya sensa sita za kuidadi wanyamapori katika mifumo ya kiikolojia ya Selous - Mikumi; Ruaha - Rungwa; Pori la Akiba Lukwika - Lumesule; *West Kilimanjaro* na Pori Tengefu la Ziwa Natron; Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makao; na Ruaha Kusini. Matokeo ya sensa katika mfumo ikolojia wa Selous - Mikumi yamebaini kuwa idadi ya tembo imepungua kutoka tembo 70,406 mwaka 2006 hadi tembo 13,084 mwaka 2013. Aidha, katika mfumo wa ikolojia wa Ruaha - Rungwa, idadi ya tembo imepungua kutoka tembo 35,461 mwaka 2006 hadi tembo 20,090 mwaka 2013. Taasisi inatarajiwa kuendelea na zoezi la sensa...

SPIKA: Huyo anayeshangilia anashangilia kwa sababu tembo wamepungua ndiyo au?

WABUNGE FULANI: ..

SPIKA: Aahh, hayo maneno ya Kiswahili. Haya, Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Taasisi inatarajiwa kuendelea na zoezi la sensa ya tembo na wanyama wengine nchi nzima kwa mwaka ujao wa fedha. Taasisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpango kuhusu njia mbadala ya kupunguza madhara yatokanayo na migongano *(conflicts)* kati ya binadamu na hawa wanyama waitwao ndovu au tembo. Aidha, Taasisi imefanya utafiti kuhusu migongano baina ya binadamu na tembo na kutoa elimu ya kupunguza madhara yatokanayo na migongano hiyo katika Wilaya za Serengeti, Bunda, Kilosa, Tunduru na Namtumbo. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yameainishwa katika aya ya 19 hadi 21 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori vilidahili jumla ya wakurufunzi 1,129 katika vyuo vya Mweka wakurufunzi 540 na Pasiansi 400. Aidha, Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Maliasili kwa Jamii cha Likuyu - Sekamaganga kimetoa mafunzo ya uhifadhi kwa Wananchi 189 kutoka sehemu mbalimbali nchini. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yako katika aya ya 22 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro zimeendelea na utekelezaji wa majukumu yao chini ya Sheria zinazosimamia mashirika hayo kama ilivyoelezwa katika Kitabu cha Hotuba, aya ya 23 hadi 31.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea na taratibu za kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998. Aidha, imeanza kukusanya maoni ya wadau kupitia warsha za kikanda, ili kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, jumla ya wakurufunzi 239 walidahiliwa kujiunga na Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wakurufunzi 40; kati yao, 29 wanajigharimia wenyewe. Chuo kimeboresha miundombinu kwa kukarabati nyumba mbili za watumishi na kuweka mtandao wa mawasiliano. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wakurufunzi 32 na kati yao 25 wamelipiwa ada na Serikali. Vilevile, Chuo kimefanya ukarabati wa mabweni na kununua samani. Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wakufunzi 167 ambao wote walijigharimia.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulihakiki mipaka ya misitu kwa kufanya soroveya na kusafisha mipaka yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,341 kwenye misitu ya hifadhi 50 ili kudhibiti uvamizi na uharibifu wa hifadhi za misitu. Mipaka hiyo iliwekewa maboya *(beacons)* 264 na mabango 553 ili kubainisha mipaka na kutoa tahadhari kwa jamii. Zoezi la kuimarisha mipaka liliendeshwa sanjari na kuwaondoa wavamizi kwenye misitu 24 yenye ukubwa wa hekta 9,500. Katika zoezi hilo, mifugo 1,200 iliondolewa na nyumba 65, kambi 9 na tanuri 10 za mkaa ziliharibiwa.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mashamba ya Miti: Kazi zilizofanyika katika mashamba 16 ya miti hadi kufikia Machi, 2014 ni kama ifuatavyo; kukuza miche 14,288,673; kupanda miti kwenye maeneo yaliyovunwa yenye ukubwa wa hekta 3,905 na maeneo mapya ya hekta 3,443; kupogolea miti kwenye mashamba 11 yenye ukubwa wa hekta 4,366 na kukagua miti yenye mita za ujazo 768,000 katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uvunaji na kukusanya maduhuli, jumla ya kiasi cha Shilingi 27,275,035,840 zilikusanywa. Aidha, Wakala umeainisha maeneo ya mashamba mapya yenye ukubwa wa hekta 27,000. Maeneo hayo ni Mbizi – Sumbawanga hekta 12,000; Wino – Songea hekta 10,000; Rubare/Kajunguti – Bukoba hekta 2,500; na Kawetire - Mbeya hekta 2,500.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti uvunaji haramu na biashara ya misitu, jumla ya siku za doria 12,436 ziliendeshwa katika maeneo ya nchi kavu na baharini kote nchini. Doria hizi zilifanyika kwenye misitu ya hifadhi ya asili 17 ikijumuisha hifadhi za mazingira asilia, mikoko na hifadhi za nyuki na manzuki. Vilevile, doria zimefanyika katika misitu isiyohifadhiwa kwenye Wilaya 37 na maeneo 40 ya masoko. Katika doria hizo, vipande 100,015 vya mbao, mkaa mifuko 48,235 na magogo 8,520 yamekamatwa. Aidha, kiasi cha Shilingi 921,611,439 zilikusanywa kutokana na udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu na watuhumiwa 263 waliokiuka sheria walikamatwa. Kati ya hao, 72 walifungwa, 176 walilipa faini, watuhumiwa watatu waliachiwa huru na 12 hukumu zao bado hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, Wakala umefanya mapitio ya Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu mwaka 2007. Mapitio hayo yanalenga kuboresha usimamizi wa uvunaji na biashara ya mazao ya misitu nchini kwa kuweka utaratibu madhubuti na kuongeza uelewa katika kuzingatia Sheria na Kanuni za misitu.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kuhusu kazi zilizofanyika kudhibiti na kusimamia moto wa msituni, ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa rasilimali misitu, uongoaji wa maeneo yaliyoharibika na kuboresha miundombinu katika hifadhi za misitu, umeainishwa katika aya ya 37 – 40 katika Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji nyuki yametolewa kwa wafugaji nyuki 2,157 kutoka vikundi 330 katika vijiji 91 vya Wilaya 20 ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya nyuki. Aidha, wafanyabiashara 50 wamepatiwa mafunzo ya kuhakiki ubora wa mazao ya nyuki na taratibu za kufanya biashara za mazao ya nyuki. Jumla ya mizinga 8,339 imetengenezwa na kusambazwa kwa Wananchi waishio karibu na maeneo ya hifadhi za misitu.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ili kuendeleza ufugaji nyuki zimeainishwa katika aya ya 41 - 43 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti. Wakala wa Mbegu za Miti umeendelea na jukumu la kuzalisha na kuuza mbegu na miche bora ya miti. Hadi kufikia Machi, 2014 kilo 8,635 za mbegu za miti ziliuzwa nchini kwa Shilingi 107,461,578 na kilo 33 zenye thamani ya Shilingi 5,519,195 zimeuzwa katika nchi za Paraguay na Vietnam. Vilevile, Wakala wameuza miche 126,074 yenye thamani ya Shilingi 126,545,000. Aina ya Mbegu na miche iliyouzwa imeainishwa katika aya ya 44 na 45 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania imeboresha mazingira na miundombinu ya utafiti kwa kuweka samani, vitendea kazi na vifaa vya utafiti katika jengo jipya la Makao Makuu, Mjini Morogoro. Vilevile, Taasisi imejenga uwezo wa rasilimali watu kwa kuwawezesha watumishi 14 kujiunga na masomo katika ngazi za shahada (3), Uzamili (4) na Uzamivu (7). Majukumu mengine yako katika aya ya 46 - 50 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2013/2014, Mfuko wa Misitu Tanzania ulikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 4,561,000,000 kutoka vyanzo vyake. Hadi Machi 2014, Mfuko ulikuwa umekusanya Shilingi 2,281,231,061 sawa na asilimia 50 ya makadirio. Mfuko umepanga kutumia Shilingi 1.7 kwa ajili ya kufadhili Miradi 161 ya wadau wa misitu na ufugaji nyuki ikiwemo Miradi mipya 69. Hadi Machi 2014, jumla ya Shilingi milioni 660.8 zimetumika kama malipo ya awali na Miradi mipya 14 ipo katika hatua ya kusaini mkataba kabla ya kupewa fedha. Aidha, Mfuko umechangia kujenga uwezo kwa kufadhili wanafunzi 15 katika fani ya misitu na nyuki katika ngazi mbalimbali. Vilevile, Mfuko umewezesha Wakala wa Mbegu za Miti kupitia na kuchapisha nakala 7,500 za Mwongozo wa Upandaji Miti Nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza na kuendeleza utalii nchini, Wizara inaendelea na zoezi la kupitia Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999. Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuandaa Sera zimekamilika na kinachoendelea ni taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la kukusanya takwimu na kufanya soroveya kuhusu watalii nchini, imekadiriwa kuwa, kwa mwaka 2013 watalii 1,135,884 waliingia nchini na kuliingizia Taifa pato la Dola za Kimarekani bilioni 1.8, ikilinganishwa na watalii 1,077,058 walioingiza mapato ya Dola za Kimarekani bilioni 1.7 katika mwaka 2014. Soroveya ya shughuli za biashara ya utalii *(Tourism Establishment Survey)* imebaini kuwa, idadi ya Wakala wa Biashara za Utalii imeongezeka kutoka 1,037 mwaka 2012 hadi 1,103 mwaka 2013. Taarifa za soroveya hizi zitasaidia kujua mwenendo wa mchango wa Sekta ya Utalii kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Utangazaji Utalii wa Kimataifa kwa mwaka 2012-2017, Bodi ya Utalii imefanya mikutano katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mwanza, Iringa, Morogoro na Arusha. Mikutano hiyo imeshirikisha wadau ikiwa ni pamoja na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali vya hapa nchini. Aidha, Bodi imekutana na Mabalozi tisa kati ya 11 ambao nchi zao zimetajwa kwenye mkakati wa Utangazaji Utalii wa Kimataifa kwa lengo la kujadili masuala ya uhamasishaji utalii. Vilevile, Bodi imefanya mikutano na Balozi za Tanzania katika nchi za Uingereza, Ujerumani, Marekani na Uholanzi ili kutambulisha Mkakati huo. Aidha, Mabalozi wa Utalii, wahisani watatu katika nchi ya Marekani na mmoja nchini Australia wameteuliwa. Juhudi zinafanywa kuteua Mabalozi wengine watano katika Masoko ya Uingereza, Ujerumani, China, Canada na Brazil. Bodi imehudhuria maonesho ya Utalii kwenye nchi 11 na kushiriki ziara za utangazaji utalii, yaani *road show*. Majukumu mengine yaliyotekelezwa na Bodi yameainishwa katika aya ya 54 - 56 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2013/2014, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii kimedahili wakurufunzi 242. Kozi ya awali kwa wakurufunzi wasiokuwa na sifa za kutosha kujiunga na chuo imeanza kutolewa ambapo wakurufunzi 18 wamenufaika na utaratibu huo. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania *(TCT)* na Chama cha Wamiliki wa Hoteli *(HAT),* kimeanza kutoa mafunzo katika Programu ya *Apprenticeship* kwa wakufunzi 20.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Hosteli za Chuo za Kampasi ya Temeke umekamilika na kuongeza uwezo wa kuchukua wanafunzi kutoka 60 hadi 120. Chuo kimenunua vifaa, yaani *small operating equipment,* kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika Kampasi ya Bustani ili kuongeza ufanisi na kutoa mafunzo bora.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utaratibu wa kurekebisha Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333 na marekebisho yake ya mwaka 1979. Taratibu zinaendelea ili kupata ridhaa ya kutunga Sheria mpya ya Mambo ya Kale.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa vipindi kuhusu vielelezo vya kisayansi, kiutamaduni na kiteknolojia kuhusu chimbuko na maendeleo ya binadamu Tanzania Bara ili kukuza uelewa wa Wananchi kutembelea na kushiriki katika uhifadhi wa Malikale. Vipindi hivyo vya zamadamu na utalii wa ndani vimerushwa kupitia Vituo vya Televisheni vya *TBC1* na *Channel Ten*. Lengo la vipindi hivi ni kuelimisha Umma kuhusu umuhimu wa malikale, kuhimiza matumizi endelevu na kukuza utalii. Jumla ya vipindi 15 kuhusu Historia na Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam na 10 kuhusu vivutio vya utalii wa malikale vilivyoko katika Mji wa Kihistoria wa Bagamoyo vimetayarishwa na kutangazwa. Aidha, Wizara imefanya uhamasishaji katika shule zilizopo Mkoa wa Iringa na Wilaya ya Bagamoyo. Utaratibu uliotumika ni kupitia shule za msingi, sekondari, vyuo na kufanya mkutano na Wakala wa Utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetangaza utalii wa urithi wa utamaduni katika maadhimisho mbalimbali ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo: Wiki ya Utalii Duniani, Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba), Sherehe za Tamasha la Utalii na Kumbukizi la Vita vya Majimaji. Aidha, Wizara imeshiriki kuandaa onyesho la kudumu katika Balozi za Tanzania nchini China na Ufaransa. Onesho hili limejikita kuonesha historia ya chimbuko la mwanadamu kwa kupitia vivutio vya utalii katika Bonde la Oldupai, Laetoli na Muhula wa zana za Mawe Isimila.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa utalii kupitia urithi wa utamaduni, Wizara imempata mtaalam wa kuandaa michoro ya Jengo la Makumbusho ya Laetoli ili kuhifadhi nyayo za Zamadamu. Kutokana na mpango kazi wa mtaalamu mshauri huyo, kazi ya kuandaa michoro ya jengo hilo, itakamilika ifikapo mwezi Desemba, 2014. Aidha, umejengwa uzio na kingo za kuzuia maji ya mvua yasiharibu nyayo za Zamadamu za Engarasero. Vilevile, vipeperushi vimeandaliwa kwa ajili ya kutangaza eneo hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za malikale, utafiti wa malikale na uhifadhi wa malikale, zimeainishwa kwa kina katika aya ya 62 – 64 katika hiki Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania limesambaza vipeperushi 10,000 katika shule, taasisi na hoteli za kitalii ili kutoa elimu na kuhamasisha Wananchi kutembelea Makumbusho. Vipindi vya televisheni vya watoto vimerushwa kwa ushirikiano kati ya Shirika, *American Garden* na Kituo cha Televisheni cha *TBC1*. Aidha, programu za watoto zinaendelea kufanyika kila Ijumaa ili kuhamasisha watoto kutembelea Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho la Taifa Tanzania kwa kushirikiana na Makumbusho ya Alcala - Madrid, Hispania liliandaa Onesho la Chimbuko la Mwanadamu kwa kutumia vielelezo vilivyotokana na utafiti uliofanyika katika Bonde la Olduvai, Ngorongoro. Onesho hilo lilizinduliwa huko Alcala, Madrid katika Hispania tarehe 10 Februari, 2014 na litachukua muda wa mwaka mmoja na baadaye litarudishwa Makumbusho ya Taifa Februari, 2015. Vilevile, Shirika limekamilisha Jubilei ya miaka hamsini ya ushirikiano wa Tanzania na Sweden, *Nyerere Day* na Onesho la Baiolojia katika Makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji, Wizara imewawezesha watumishi 112 kuhudhuria mafunzo mbalimbali. Kati ya hao, watumishi 98 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 14 mafunzo ya muda mrefu. Vilevile, Wizara imeajiri watumishi 42 na inategemea kuajiri watumishi wengine 1,342 wa kada za wahifadhi wanyamapori 937, maafisa ufugaji nyuki 50, maafisa misitu 100 na wasaidizi ufugaji nyuki 80. Taratibu za kuwaajiri zinaendelea katika Mamlaka husika na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2014. Aidha, Wizara imewapandisha vyeo watumishi 432 wa kada mbalimbali na watumishi 134 wamethibitishwa kazini. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yameainishwa katika aya ya 68 na 69 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 148,971,444,489. Hadi Machi, 2014, Wizara imekusanya jumla ya shilingi 82,086,269,449 sawa na asilimia 55.1 ya makadirio. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikia lengo ni pamoja na kurudishwa kwa baadhi ya vitalu vya uwindaji kutokana na kupungua kwa wanyama na kuchelewa kuanza kwa tozo ya Maendeleo ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka 2014/2015: Sekta ndogo ya wanyamapori. Moja uhifadhi, usimamizi wa wanyamapori na ushirikishwaji wa jamii. Mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori ndani na nje ya Mapori ya Akiba kwa kuendesha siku za doria 106,000. Vilevile, miundombinu, vitendea kazi na huduma zitaboreshwa kwa watumishi katika Mapori ya Akiba na Kanda nane za Kikosi Dhidi Ujangili ili watumishi watekeleze kazi zao ipasavyo. Ufafanuzi wa kina kuhusu barabara zitakazojengwa katika Mapori ya Akiba, ushirikishwaji wa Wananchi katika ulinzi na uhifadhi, gawio la fedha zitokanazo na uwindaji wa kitalii katika Halmashauri na *WMAs* na utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na kimataifa uko katika aya 71-73 ya kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, kuanzishwa rasmi kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* kunafungua ukurasa mpya katika historia ya Uhifadhi nchini na kuwapa matumaini mapya wahifadhi wote na hasa Maaskari wa Wanyamapori. Kimsingi, uanzishwaji wa Mamlaka umezingatia haja ya kujenga uwezo, kuboresha masilahi ya watumishi na kuimarisha shughuli za uhifadhi kwenye maeneo ya mapori na maeneo yote yaliyo nje ya Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* na Mamlaka ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Chini ya Mamlaka ya Wanyamapori, tunaongeza vitendea kazi ili kuimarisha ulinzi na doria na kuhakikisha tunawashinda majangili popote walipo nchini. Tunaanzisha Kitengo Maalum cha Doria kwa kutumia helikopta kwa ajili ya kuwalinda wanyamapori, hususan Tembo na Faru kama ifuatavyo: Katika Pori la Akiba la Selous tunanunua Helikopta moja aina ya Robertson 44 inayonunuliwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Howard Buffet ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, pili katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro mwaka huu tunanunua Helikopta moja aina ya Robertson 44. Tatu katika Shirika la hifadhi za Taifa *TANAPA* mwaka huu huu tunanunua Helikopta moja aina ya Bell, ambayo itakuwa kubwa kuliko zote na

tunatarajia kufikia mwisho wa mwezi huu Marubani sita wataanza mafunzo nchini Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ulinzi wa tembo, Wizara inaanzisha Kitengo Maalum cha Mafunzo ya Intelijensia na ukomandoo wa Kikosi Maalum kitakachokuwa na uwezo wa kuteremka kwenye helikopta katikati ya pori na kuwatia nguvuni majangili. Aidha, Chuo cha Maaskari wa Wanyamapori Pasiansi, kupitia Taasisi ya Howard Buffet, kinapata miundombinu mipya ya mabweni ya wanafunzi 300 zaidi, kinapata *GPS*, vifaa vya darubini, mabasi maalum 2, malori maalum 2, magari mengine 5, mahema ya mafunzo, mtaalam mwelekezi, pamoja na kujengewa uwezo wa kumudu mahitaji maalum ya Taaluma hii ili kulingana na changamoto tulizonazo kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania itasimamia eneo lenye ukubwa wa kilometa za Mraba zaidi ya 200,000, ikiwepo Mapori yote ya Akiba 28 na Mapori Tengefu 43. Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* litaendelea kusimamia hifadhi 16 zenye jumla ya ukubwa wa kilometa za mraba 57,000 na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itaendelea kusimamia eneo lake la kilometa za mraba 8,500.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi ujao, Wizara itakuwa na jumla ya Askari wa Wanyamapori 2,532, walio chini ya Mamlaka nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori *(TWPF)* ulio chini ya Wizara, pamoja na Mfuko wa Wadau wa Maendeleo ambao unaanzishwa chini ya UNDP na ambao utajulikana kama *Multilatoral Anti poaching and Wildlife Security Busket Fund,* pamoja na rasilimali zingine, zitatumika kuijengea uwezo Mamlaka ya Wanyamapori wakati tunaianzisha. Kama nilivyosema hapo awali, mamlaka Makao yake Makuu yatakuwa katika Mji wa Morogoro. Nia na azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa hatua hizi za kuanzisha mfumo mpya wa Mamlaka utaweza kulinda rasilimali za nchi na kuhakikisha uwepo wa tembo na wanyamapori wengine katika miaka mingine mingi ijayo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania itakuwa na Bodi inayojitegemea na itakuwa na Mkurugenzi Mkuu atakayejulikana kama *Director General,* atakayeteuliwa na Mheshimiwa Rais na itakuwa na vyanzo vyake vya mapato vitakavyoainishwa katika mabadiliko ya sheria tutakayoileta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori itaendeleza utafiti wa wanyamapori, aina za nyuki, mahusiano kati ya nyuki na mimea pamoja na kuidadi wanyamapori katika maeneo mbalimbali nchini. Mafunzo kuhusu njia stahiki za ufugaji nyuki yatatolewa katika Vijiji vya Wilaya za Simanjiro, Kiteto na Hanang na kutengeneza mizinga 1,500 kwa ajili ya kuisambaza kwa Wadau wa Sekta ya Nyuki nchini. Aidha, Taasisi itaendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti wa nyuki.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya mafunzo ya uhifadhi wanyamapori vitadahili jumla ya wakurufunzi 980; Pasiansi watadahili 400 na Mweka 580. Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa Wananchi 240. Vilevile, Chuo cha Mweka kitawezesha wakufunzi watatu kupata mafunzo ya Uzamili na wawili Uzamivu. Aidha, Chuo kitajenga madarasa mawili na matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 450 kwa ajili ya kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 litaendelea kutatua migogoro ya mipaka na shoroba na kuimarisha Mifumo ya TEHAMA. Vilevile, Shirika litaboresha miundombinu ya majengo, madaraja, barabara, maliwato

ya mlimani, nyumba za wafanyakazi, huduma za maji na umemejua. Pia, Shirika litaimarisha utalii na kupanua wigo wa vivutio na huduma kwa watalii, kuajiri watumishi ikiwa ni pamoja na kuwa na Muundo wa *Paramilitary* ili kuimarisha ulinzi katika Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi hizo, Shirika litanunua vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na silaha, vifaa vya mawasiliano vya kiintelijensia na vifaa mbalimbali vya kuboresha ufuatiliaji wa karibu wa Faru kwa ajili ya kudhibiti ujangili. Vilevile, Shirika litanunua Helikopta aina ya Bell kama nilivyosema hapo awali, magari mapya 12 na mitambo mizito ya barabara miwili. Aidha, Shirika litaweka mifumo mipya 12 ya kielektroniki ya kukusanya mapato katika Hifadhi saba, kujenga na kukarabati nyumba 15 za watumishi na kuweka seti 21 za umemejua katika vituo vya maaskari. Vilevile, Kituo cha Utalii kitajengwa katika Hifadhi ya Arusha. Pia, mabanda manne ya kulala Watalii wa ndani yatajengwa katika Hifadhi za Ruaha na Saadani. Vituo vinne vya kupumzikia wageni na mabanda mawili ya wapagazi *(Porters)* yatajengwa katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Jumla ya Kilometa 26 za barabara mpya zitajengwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Shirika litatangaza vivutio vyake kupitia televisheni za ndani na nje ya nchi kama vile *CNN, CCTV* na *CNBC*.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, mwaka 2014/2015 itaendelea kununua na kusambaza chakula kwa wafugaji waishio ndani ya Hifadhi ambapo tani 4,700 za mahindi zitatolewa. Shule za msingi 21 zimetengewa Shilingi 70,000,000 kwa ajili ya kununua chakula. Vilevile, Mamlaka itanunua helikopta moja, magari 10, basi moja la utalii wa ndani, gari la kutoa huduma kwa wagonjwa, kujenga nyumba mbili za askari katika Vituo vya Lemala na Selela na kukarabati nyumba nne za maaskari katika vituo viwili.

Mamlaka pia itaimarisha doria kwa kununua na kutumia zana mbalimbali za kisasa na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi Jijini Arusha. Majukumu mengine yatakayotekelezwa yameainishwa katika aya ya 79 hadi 81 ya Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Spika, Rasimu ya Sera ya Taifa ya Misitu imekamilika na taratibu za kuidhinishwa zinaendelea. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki yataendelea kwa kukusanya maoni ya wadau. Kufuatia kukamilika kwa mapitio ya Programu ya Taifa ya Misitu ya 2001 – 2010, utayarishaji wa programu mpya utaendelea. Aidha, uchambuzi wa Sheria ya Misitu, Sura 223 na Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura 224, utafanyika ili kuainisha majukumu ya Wakala wa Huduma za Misitu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, jumla ya wakurufunzi 308 watadahiliwa katika Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki kama ifuatavyo: Chuo cha Misitu Olmotonyi 195, Chuo cha Viwanda vya Misitu 40 na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki 73. Katika kuboresha miundombinu, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitajenga maktaba na maabara.

Chuo cha Misitu Olmotonyi kitafanya ukarabati wa nyumba tisa za watumishi, ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula na kiwanda cha kupasua mbao. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitajenga nyumba moja ya waalimu na karakana ya mbao pamoja na kukarabati Jengo la Utawala na kuliwekea samani.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wakala utaanza kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano Julai, 2014 hadi Juni 2019. Mpango huu umelenga kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki na kuboresha mifumo ya usimamizi. Aidha, mpango wa kibiashara wa mwaka 2014/2015 unaosisitiza kuimarisha uwezo wa Wakala katika kutoa huduma upatikanaji wa rasilimali na mifumo ya ikolojia pamoja na kuwezesha matumizi ya rasilimali zilizoboreshwa utatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na kudhibiti uvunaji haramu wa mazao wa misitu, wakala unatarajia kuendesha siku za doria 22,000 katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati za uvunaji katika Halmashauri 55 za Wilaya zitawezeshwa kufanya vikao vya kujadili maombi ya uvunaji. Vile vile wakala utafanya mikutano 14 kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu na nyuki katika kanda za Kaskazini, Kusini, Mashariki kati na ziwa. Lengo ni la mikutano hiyo ni kuelimisha wafanyabiashara kuhusu sheria na taratibu za kufanya biashara ya mazao na misitu. Majukumu mengine yatakayotekelezwa yameainishwa katika aya ya 86 hadi 88 katika kitabu cha hotuba.

(b) Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mashamba ya miti, katika mwaka 2014/2015 jumla ya miche milioni 15 itaoteshwa na kupandwa katika mashamba ya miti yenye ukubwa wa hekta 7,300. Wakala utarudishia miti katika maeneo yenye ukubwa wa hekta 200, utaondoa magugu kwenye eneo lenye hekta thelathini tatu elfu, mia moja na hamsini, kupogoa hekta elfu moja mia nane kumi na mbili na kukarabati barabarani za misituni zenye urefu wa jumla ya kilomita 2,691. Aidha, usimamizi wa mashamba ya miti utafanyika kwa kufanya doria kwenye eneo la hekta laki mbili na kumi na nne elfu kusafisha barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 6,120 na kusafisha mipaka kilomita 862.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza changamoto ya uhaba wa malighafi ya mazao ya misitu, wakala utaanzisha mashamba mapya yenye ukubwa wa jumla ya hekta, 2,225 ya *specie* za aina mbalimbali. Vilevile eneo la msitu wa asili Kahe, Kilimanjaro hekta 50, zitapandwa misaji na shamba la nishati ya kuni lililopo Korogwe, hekta hamsini zitapandwa mikaratusi. Aidha, Wakala unatarajia kuanzisha hekta hamsini na mikaratusi na mianzi katika msitu wa hifadhi wa Ruvu. Kazi nyingine za usimamizi wa rasilimali za misitu ushirikishaji wa jamii elimu kwa umma, kuwajengea watumishi uwezo zimeanishwa katika aya ya 85 hadi 93 ya kitabu cha hotuba.

(c) Mheshimiwa Spika, kuanzisha vituo vya kuzalishia makundi na kuendeleza ufugaji wa nyuki. Katika kukabiliana na upungufu wa makundi ya nyuki unaosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi, Wakala utaanzisha vituo vitano vya kuzalisha malikia wa nyuki. Vituo hivyo ni Naflaki Shinyanga - Ukimbu – Manyoni, Ruvu – Kibaha na Ndembo – Tunduru, na shamba la miti la Sao *Hill*. Aidha, wakala utatoa mafunzo ya uzalishaji wa makundi ya nyuki kwa wawezeshaji 40, kati ya watakaopewa mafunzo ishirini ni watumishi na ishirini watatoka katika wawakilishi wa wafugaji nyuki. Wakala utatoa mizinga 1,200 na mafunzo kwa wafugaji nyuki kutoka vijiji 94 vilivyoko kando kando ya misitu. Jumla ya wafugaji wa nyuki 1,501 kutoka vikundi 115 watanufaika na mafunzo hayo.

(d) Mheshimiwa Spika, kongamano la ufugaji nyuki la Apimondia, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara ya kwanza barani Afrika, Tanzania imepata heshima ya kuandaa kongamano la ufugaji nyuki Apimondia lengo ni kuongeza msukumo wa ufugaji nyuki na kupanua wigo wa masoko ya mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, Kongamano hili litafanyika tarehe 11 hadi 13 Novemba, 2014 katika ukumbi wa Kituo cha Mikutano wa Kimataifa *AICC* mjini Arusha. Aidha, jumla ya washiriki 550

kutoka ndani na nje ya nchi wanatarajiwa kuhudhuria. Kongamano hili litaambatana na maonesho ya biashara na ziara za mafunzo.

Mheshimiwa Spika, nne, Wakala wa Mbegu za Miti, ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu za miti unakuwa endelevu, Wakala utaanzisha vyanzo vitano vya mbegu bora za miti ya misindano aina mbili, Msenefu, Mwiluti na Mpaulonia. Vilevile Wakala utatambua na kusajili vyanzo vitatu vya mbegu za miti aina ya mkenge na mgunga. Pia utaendelea kutunza vyanzo 31 za mbegu za miti aina mbalimbali. Wakala utakusanya jumla ya kilo 12,500 za mbegu ya miche ya aina mbalimbali pamoja na kuuza kilo 11,500 za mbegu za miti na miche ya miti 100,000.

Mheshimiwa Spika, tano, taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, kutokana na wakulima wengi kuvuna miti yao katika umri mdogo na hivyo kupoteza mapato, Taasisi itafanya utafiti juu ya ubora wa mbao zitokanazo na miti ya umri tofauti. Lengo ni kutoa ushauri wa kisayansi juu ya umri stahiki wa kuvuna miti bila kuathiri ubora wa mbao kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, taasisi itaanzisha mashamba darasa katika Wilaya za Mkuranga na Handeni ili kuelimisha jamii inayozunguka misitu ya hifadhi juu ya umuhimu wa kuwa na mashamba ya miti ya kuni na matumizi mengine. Aidha, taasisi inatarajia itaajiri Watafiti Wasaidizi tisa, Watafiti Waandamizi watano, Wakurugenzi wa Vituo vya Utafiti wanne na watumishi wengine 27 pamoja na kununua samani na vitendea kazi vya ofisi na maabara.

Mheshimiwa Spika, sita, Mfuko wa Misitu Tanzania, unakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5.3 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali. Mfuko utatoa ufadhili wa shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya miradi 173 ya wadau mbalimbali wa misitu na ufugaji nyuki. Kati ya miradi hiyo 97 ni miradi mipya, wadau watakaonufaika na ufadhili huo ni pamoja na watu binafsi, vikundi vya jamii na asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Utalii, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 ili iendane na mahitaji ya sasa. Wizara itaendelea kufanya utafiti wa mwenendo wa biashara nchini pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za utalii. Kazi ya kukagua Wakala wa Biashara za Utalii itafanyika katika kanda nne, ambazo ni Kaskazini, Pwani, Nyanda za Kusini na Ziwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, Bodi ya Utalii Tanzania, nachukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuanzia mwezi Julai, 2014 tunachukua hatua madhubuti za kuhuisha mtazamo wa dunia, juu ya Taifa letu na Utalii wa nchi yetu ya Tanzania.

Bodi ya Utalii kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi la Taifa *TANAPA* na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itasimamia kutangazwa kwa vituo vya utalii vilivyopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika matangazo maalum ya Luninga, yatakayoanza kurushwa katika vituo vya *CNN* na *BBC* kwa kipindi cha mwaka mzima.

Aidha, tunarajia kumwomba Mheshimiwa Raid mpango wa kuuhisha mtazamo wa dunia kuhusu utalii Tanzania *rebranding destination* Tanzania mapema mwezi Julai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi itashiriki katika maonesho na misafara mbalimbali katika nchi ambazo zimeorodheshwa na nitaomba maelezo yote haya ya kitabu yaingie katika kumbukumbu zako.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii, chuo kitadahili wakufunzi 315 katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya ndogo ya Malikale, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Malikale na kuandaa miongozo ya utafiti na uhifadhi wa mali kale katika maeneo ya kihistoria ya Kilwakivinje, Mikindani na mji wa kihistoria wa Pangani.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho la Taifa, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika litaendelea kuitangaza makumbusho ya Taifa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na televisheni, redio na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, uratibu, utawala na maendeleo ya rasilimali watu, Wizara itawezesha watumishi 846 kuhudhuria mafunzo, ya muda mfupi na muda mrefu na aidha, Wizara itapandisha cheo watumishi 552 na kuajiri wengine 1,033 kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za dhati…

SPIKA: Naomba uombe hela kengele itagonga sasa hivi, omba fedha.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha, 2014/2015 naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, jumla ya sh. 33,119,264,000/= kati ya hizo sh. 68,921,048,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 14,198,216,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida, zinajumuisha sh. 30,627,417,000/= kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na sh. 38,298,631,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Fedha za Maendeleo zinajumuisha sh. 5,000,000,000/= fedha ndani na sh. 9,198,216,000/= fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Hotuba ya Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA LAZARO SAMUEL NYALANDU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2013/14. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/15.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

2. Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwa hapa Bungeni leo. Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii yenye jukumu la kusimamia rasilimali za maliasili na malikale; na kuendeleza Utalii. Pia, nampongeza Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Aidha, kwa kushirikiana na wafanyakazi na wadau wa sekta hii, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kusimamia vema uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na maendeleo ya utalii.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mheshimiwa James Daudi Lembeli (Mb) kwa ushirikiano wao thabiti na Wizara yangu. Maoni na ushauri unaotolewa na Kamati, hususan wakati wa kupitia na kuchambua Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015, yameiwezesha Wizara kutekeleza vema majukumu yake.

4. Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo wa Jimbo la Kiembe-Samaki, Zanzibar; Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa wa Jimbo la Kalenga, Iringa; na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete wa Jimbo la Chalinze, Pwani kwa kuchaguliwa kuwa wabunge. Aidha, natoa pole kwa familia na wananchi wa majimbo ya Kiembe-Samaki, Kalenga na Chalinze kwa kuondokewa na waliokuwa wawakilishi wao Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, natoa pole kwa familia na watanzania wenzetu walioathirika kutokana na majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko, ajali za barabarani, wanyamapori wakali na waharibifu na wengine kupoteza maisha. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

5. Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Taarifa hiyo imezingatia utekelezaji wa ahadi na maelekezo yaliyotolewa bungeni, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu ya pili ni Mpango na Bajeti ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014

6. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 umezingatia sera, sheria, mikakati ya kitaifa, maelekezo ya Serikali na ahadi za Waziri Bungeni wakati akihitimisha Hotuba yake kuhusu Mpango na Bajeti kwa mwaka 2013/2014. Utekelezaji huo unahusu sekta ndogo za: Wanyamapori; Misitu na Nyuki; Utalii; Malikale; na Uratibu, Utawala na Maendeleo ya Rasilimaliwatu.

SEKTA NDOGO YA WANYAMAPORI

(i) Utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori

7. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha mapitio ya Kanuni za Usimamizi wa Wanyamapori wa Taifa na Leseni Maalum ya Uwindaji. Kanuni hizi zitaanza kutumika mwezi Juni 2014. Rasimu za Kanuni za Matumizi ya Silaha za Kiraia zinazotumika kwenye uwindaji wa Wanyamapori; na Kanuni za Uchimbaji Madini ndani ya Mapori ya Akiba zitaanza kutumika mwaka 2014/2015. Aidha, Rasimu ya Kanuni za Uanzishaji wa Kikosi cha Ulinzi wa Wanyamapori inaendelea kupitiwa na wadau ili kuiboresha.

(ii) Ushirikishaji Jamii katika Uhifadhi wa Wanyamapori

8. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza ushiriki wa wadau katika usimamizi na kunufaika na rasilimali za wanyamapori, idadi ya Maeneo ya Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori (WMAs) zilizoidhinishwa imeongezeka kutoka jumuiya 17 hadi 19. Aidha, Jumuiya za Jamii (CBO) JUHIWANGUMWA - Rufiji, UMEMARUWA – Wanging'ombe na Mbarali, na WAGA – Iringa Vijijini, zimekamilisha baadhi ya hatua za kuanzisha WMA.

(iii) Ulinzi wa Wanyamapori

9. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2013/14, siku za doria 54,574 zilifanyika ndani na nje ya Mapori ya Akiba. Watuhumiwa 391 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ambapo kesi 277 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali. Kati ya hizo, kesi 123 zenye washitakiwa 164 zimeisha kwa watuhumiwa kulipa faini ya jumla ya Shilingi 75,686,000. Kesi 154 zenye watuhumiwa 227 zinaendelea katika mahakama mbalimbali. Vilevile, nyara za Serikali na bidhaa mbalimbali zilikamatwa. Aidha, kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, Wizara ilifanya doria maalum nchi nzima (Operesheni Tokomeza) ambapo watuhumiwa 2,085 walikamatwa na jumla ya kesi 839 zilifunguliwa dhidi yao katika mahakama mbalimbali nchini. Maelezo kuhusu nyara za Serikali, vifaa na mali zilizokamatwa wakati wa Doria na Operesheni Tokomeza yako katika aya ya **10 na 11** katika kitabu cha Hotuba.

10. Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara. Tarehe 9 – 10 Mei 2014, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), na International Conservation Caucus Foundation (ICCF) iliandaa na kufanikisha mkutano wa Kimataifa "Stopping Wildlife Crime & Advancing Wildlife Conservation" "A call for Action". Katika Mkutano huo, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na UNDP imefikia makubaliano ya kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Kuhifadhi Wanyamapori (Multlateral Antipoaching and Wildlife Busket Fund) utakao simamiwa na UNDP, na kuchangiwa na nchi, Mashirika, na wadau wahisani wa maendeleo.

(b) Washirika wa Maendeleo, wakiwepo UNDP, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, China, Japan, World Bank, Finland na Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB), walitia saini makubaliano ya ushirikiano na Serikali kuhusu Uhifadhi na Ulinzi wa Wanyamapori; huku utiaji sahihi huo ukishuhudiwa na Mhe. Mizengo Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bibi Hellen Clerk, Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa – *UNDP*.

(c) Viongozi wa dini walitoa Tamko la kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha waumini wao kote nchini kupinga vitendo vya Ujangili na Biashara haramu ya nyara.

(d) Serikali iliwatunuku "Life Time Archievement Award" watumishi watano wa Idara ya Wanyamapori kwa niaba ya wahifadhi wastaafu nchi nzima. Watumishi hawa na

wengine wameyatoa maisha yao kwa uhifadhi wa wanyamapori. Tuzo hizi zitaendelea kutolewa kwa wahifadhi katika sekta yote ya uhifadhi.

(iv) Ulinzi wa Wananchi Dhidi ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu

11. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendesha siku za doria 696 katika wilaya 19 zilizoathirika kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa lengo la kulinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, watu 11 wamepoteza maisha na jumla ya ekari 4,345.82 za mazao ziliharibiwa na wanyamapori hao katika Wilaya za Busega, Babati, Monduli, Iringa Vijijini, Tabora, Tunduru na Ilemela. Nachukua fursa hii kutoa pole za dhati kwa wote waliofikwa na majanga hayo. Wizara imetoa kifuta machozi cha jumla ya Shilingi 9,200,000 kwa familia za waliopoteza maisha na Shilingi 98,412,750 kama kifuta jasho kwa wananchi walioharibiwa mazao.

(v) Kuboresha Miundombinu, Vitendea Kazi na Huduma

12. Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 220 zimekarabatiwa katika Mapori ya Akiba ya Moyowosi-Kigosi Mkungunero na Maswa. Vile vile, kilomita 136 za mipaka zimesafishwa. Kazi nyingine za ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na ununuzi wa vitendeakazi ni kama inavyoainishwa katika aya ya **15 na 16** katika kitabu cha Hotuba.

(vi) Uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania

13. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, leo tarehe 13/5/2014, nimetia saini AGIZO la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori nchini, ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Wanyamapori Na. 5, ya 2009; na kwamba Mamlaka hii sasa itatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kazi Julai, 2014. Aidha, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeamua kuwa Makao Makuu ya TAWA yatakuwa katika mji wa Morogoro. TAWA itachukua majukumu yote, isipokuwa yale ya kisera yatakayoendelea kutekelezwa na Idara ndogo ya Wanyamapori.

(vii) Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania

14. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori (TWPF) ulielekeza matumizi yake katika shughuli za kulinda wanyamapori; utafiti na mafunzo; kutoa elimu kwa umma; na kukarabati miundombinu katika mapori ya akiba, vyuo na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori. Mwaka 2013/14, Mfuko ulikadiria kukusanya Sh. Bilion 16.4. Hadi Machi 2014, makusanyo yamefikia Sh. Bil. 10, sawa na asilimia 61 ya makadirio.

(viii) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori

15. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2013/2014, Taasisi ilifanya sensa sita za kuidadi wanyamapori katika mifumo ya kiikolojia ya Selous-Mikumi; Ruaha-Rungwa; Pori la Akiba Lukwika-Lumesule; West Kilimanjaro na Pori Tengefu la Ziwa Natron; Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makao; na Ruaha Kusini. Matokeo ya sensa katika mfumo ikolojia wa Selous-Mikumi yamebaini kuwa idadi ya tembo imepungua kutoka 70,406 mwaka 2006 hadi 13,084 mwaka 2013. Aidha, katika mfumo ikolojia wa Ruaha-Rungwa, idadi ya tembo imepungua kutoka 35,461 mwaka 2006 hadi 20,090 mwaka 2013. Taasisi inatarajiwa kuendelea na zoezi la sensa ya Tembo na wanyama wengine nchi nzima kwa mwaka wa fedha ujao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

16. Mheshimiwa Spika, Taasisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpango kuhusu njia mbadala ya kupunguza madhara yatokanayo na migongano (conflicts) kati ya binadamu na tembo. Aidha, Taasisi imefanya utafiti kuhusu migongano baina ya binadamu na tembo na kutoa elimu ya kupunguza madhara yatokanayo na migongano hiyo katika Wilaya za Serengeti, Bunda, Kilosa, Tunduru na Namtumbo. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yameainishwa katika aya ya **19** hadi **21** ya kitabu cha Hotuba.

(ix) Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori

17. Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Vyuo vya taaluma ya wanyamapori vilidahili jumla ya wakurufunzi 1,129, katika vyuo vya:- Mweka wakurufunzi (540) na Pasiansi (400). Aidha, Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Maliasili kwa Jamii cha Likuyu - Sekamaganga kimetoa mafunzo ya uhifadhi kwa wananchi 189 kutoka sehemu mbalimbali nchini. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yako katika aya ya **22** katika kitabu cha Hotuba.

(x) Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro

18. Mheshimiwa Spika, Shirika la TANAPA na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro zimeendelea na utekelezaji wa majukumu yao chini ya sheria zinazosimamia mashirika hayo kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Hotuba, aya ya **23** hadi **31**.

SEKTA NDOGO YA MISITU NA NYUKI

(i) Utekelezaji wa Sera na Sheria

19. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea na taratibu za kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998. Aidha, imeanza kukusanya maoni ya wadau kupitia warsha za kikanda ili kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998.

(ii) Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, jumla ya wakurufunzi 239 walidahiliwa kujiunga na vyuo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wakurufunzi 40 na kati yao, 29 wanajigharimia. Chuo kimeboresha miundombinu kwa kukarabati nyumba mbili za watumishi na kuweka mtandao wa mawasiliano. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wakurufunzi 32 na kati yao 25 wamelipiwa ada na Serikali. Vile vile, Chuo kimefanya ukarabati wa mabweni na kununua samani. Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wakurufunzi 167 ambao wote wanajigharimia.

(iii) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

(a) Kuimarisha Mipaka ya Misitu

21. Mheshimiwa Spika, Wakala ulihakiki mipaka ya misitu kwa kufanya soroveya na kusafisha mipaka yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,341 kwenye misitu ya hifadhi 50 ili kudhibiti uvamizi na uharibifu wa hifadhi za misitu. Mipaka hiyo iliwekewa maboya (beacons) 264 na mabango 553 ili kubainisha mipaka na kutoa tahadhari kwa jamii. Zoezi la kuimarisha mipaka liliendeshwa sanjari na kuwaondoa wavamizi kwenye misitu 24 yenye ukubwa wa hekta 9,500. Katika zoezi hilo mifugo 1,200 iliondolewa na nyumba 65, kambi 9 na tanuri 10 za mkaa ziliharibiwa.

(b) Uendelezaji wa Mashamba ya Miti

22. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika katika mashamba 16 ya miti hadi kufikia Machi, 2014 ni kama ifuatavyo: kukuza miche 14,288,673; kupanda miti kwenye maeneo yaliyovunwa yenye ukubwa wa hekta 3,905 na maeneo mapya ya hekta 3,443; kupogolea miti kwenye mashamba 11 yenye ukubwa wa hekta 4,366 na kukagua miti yenye mita za ujazo 768,000 katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uvunaji na kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 27,275,035,840**. Aidha, Wakala umeainisha maeneo ya mashamba mapya yenye ukubwa wa hekta 27,000. Maeneo hayo ni Mbizi – Sumbawanga hekta 12,000; Wino – Songea hekta 10,000; Rubare/Kajunguti – Bukoba hekta 2,500; na Kawetire - Mbeya hekta 2,500.

(c) Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu

23. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti uvunaji haramu na biashara ya mazao ya misitu, jumla ya siku za doria 12,436 ziliendeshwa katika maeneo ya nchi kavu na baharini. Doria hizo zilifanyika kwenye misitu ya hifadhi ya asili 17 ikijumuisha hifadhi za mazingira asilia, mikoko na hifadhi za nyuki na manzuki. Vile vile, doria zimefanyika katika misitu isiyohifadhiwa kwenye wilaya 37 na maeneo 40 ya masoko. Katika doria hizo vipande 100,015 vya mbao, mkaa mifuko 48,235 na magogo 8,520 yamekamatwa. Aidha, kiasi cha **Shilingi 921,611,439** zilikusanywa kutokana na udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu na watuhumiwa 263 waliokiuka sheria walikamatwa. Kati ya hao, 72 walifungwa, 176 walilipa faini, watuhumiwa watatu waliachiwa huru na 12 hukumu hazijatolewa.

24. Mheshimiwa Spika, Wakala umefanya mapitio ya Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu wa mwaka 2007. Mapitio hayo yanalenga kuboresha usimamizi wa uvunaji na biashara ya mazao ya misitu nchini kwa kuweka utaratibu madhubuti na kuongeza uelewa katika kuzingatia sheria na kanuni za misitu.

25. Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kuhusu kazi zilizofanyika kudhibiti na kusimamia moto wa msituni, ushirikishwaji jamii katika usimamizi wa rasilimali misitu, uongoaji wa maeneo yaliyoharibika na kuboresha miundombinu katika hifadhi za misitu umeainishwa katika **aya ya 37 – 40** katika kitabu cha Hotuba.

(d) Kuendeleza Ufugaji Nyuki

26. Mheshimiwa Spika, mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji nyuki yametolewa kwa wafugaji nyuki 2,157 kutoka vikundi 330 katika vijiji 91 vya wilaya 20 ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya nyuki. Aidha, wafanyabiashara 50 wamepatiwa mafunzo ya kuhakiki ubora wa mazao ya nyuki na taratibu za kufanya biashara ya mazao ya nyuki. Jumla ya mizinga 8,339 imetengenezwa na kusambazwa kwa wananchi waishio karibu na hifadhi za misitu. Kazi nyingine zilizotekelezwa ili kuendeleza ufugaji nyuki zimeainishwa katika **aya ya 41 - 43** ya kitabu cha Hotuba.

(iv) Wakala wa Mbegu za Miti

27. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mbegu za Miti umeendelea na jukumu la kuzalisha na kuuza mbegu na miche bora ya miti. Hadi kufikia Machi, 2014 kilo 8,635 za mbegu za miti ziliuzwa nchini kwa **Shilingi 107,461,578** na kilo 33 zenye thamani ya **Shilingi 5,519,195** zimeuzwa katika nchi za Paraguay na Vietnam. Vile vile, Wakala umeuza miche 126,074 yenye thamani ya **Shilingi 126,545,000**. Aina ya Mbegu na miche iliyouzwa imebainishwa katika **aya ya 44** na **45** ya kitabu cha Hotuba.

(v) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

28. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania imeboresha mazingira na miundombinu ya utafiti kwa kuweka samani, vitendea kazi na vifaa vya utafiti katika jengo jipya la Makao Makuu, Morogoro. Vile vile, Taasisi imejenga uwezo wa rasilimali watu kwa kuwawezesha watumishi 14 kujiunga na masomo katika ngazi za shahada (3), Uzamili (4) na Uzamivu (7). Majukumu mengine yaliyotekelezwa na Taasisi yameainishwa katika **aya ya 46 - 50** ya kitabu cha Hotuba.

(vi) Mfuko wa Misitu Tanzania

29. Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2013/2014, Mfuko wa Misitu Tanzania ulikadiria kukusanya jumla ya **Shillingi 4,561,000,000** kutoka vyanzo vyake. Hadi Machi 2014, Mfuko umekusanya **Shilingi 2,281,231,061** sawa na asilimia 50 ya makadirio. Mfuko umepanga kutumia **Shilingi 1,776,511,831** kwa ajili ya kufadhili miradi 161 ya wadau wa misitu na ufugaji nyuki ikiwemo miradi mipya 69. Hadi Machi 2014, jumla ya **Shillingi 660,816,168** zimetumika kama malipo ya awali na miradi mipya 14 ipo katika hatua ya kusaini mkataba kabla ya kupewa fedha. Aidha, Mfuko umechangia kujenga uwezo kwa kufadhili wanafunzi 15 katika fani ya misitu na nyuki kwa ngazi mbalimbali. Vile vile, Mfuko umewezesha Wakala wa Mbegu za Miti kupitia na kuchapisha nakala 7,500 za Mwongozo wa Upandaji Miti Tanzania.

SEKTA NDOGO YA UTALII

(i) Sera ya Taifa ya Utalii

30. Mheshimiwa Spika, katika kukuza na kuendeleza utalii nchini, Wizara inaendelea na zoezi la kupitia Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999. Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuandaa sera zimekamilika na kinachoendelea ni taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

(ii) Uendelezaji Utalii

31. Mheshimiwa Spika, katika zoezi la kukusanya takwimu na kufanya soroveya kuhusu watalii nchini, imekadiriwa kuwa, kwa mwaka 2013 watalii 1,135,884 waliingia nchini na kuliingizia Taifa dola za kimarekani bilioni 1.8 ikilinganishwa na watalii 1,077,058 walioingiza mapato ya dola za kimarekani bilioni 1.7 mwaka 2012. Soroveya ya shughuli za biashara za utalii *(tourism establishment survey)* imebaini kuwa, idadi ya Wakala wa Biashara za Utalii imeongezeka kutoka 1,037 mwaka 2012 hadi 1,103 mwaka 2013. Taarifa za soroveya hizi zitasaidia kujua mwenendo wa mchango wa sekta ya utalii kwenye Pato la Taifa.

(iii) Bodi ya Utalii Tanzania

32. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Utangazaji Utalii wa Kimataifa kwa mwaka 2012-2017, Bodi ya Utalii imefanya mikutano katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mwanza, Iringa, Morogoro na Arusha. Mikutano hiyo imeshirikisha wadau ikiwa ni pamoja na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo vya hapa nchini. Aidha, Bodi imekutana na Mabalozi tisa kati ya 11 ambao nchi zao zimetajwa kwenye Mkakati wa Utangazaji Utalii wa Kimataifa kwa lengo la kujadili masuala ya uhamasishaji watalii. Vile vile, Bodi imefanya mikutano na Balozi za Tanzania katika nchi za Uingereza, Ujerumani, Marekani na Uholanzi ili kutambulisha Mkakati huo. Aidha, Mabalozi wa Utalii wa hisani watatu katika nchi ya Marekani na mmoja nchini Australia wameteuliwa. Juhudi zinafanywa kuteua mabalozi wengine watano (5) katika masoko ya Uingereza, Ujerumani, China, Canada na Brazil. Bodi imehudhuria

maonesho ya Utalii kwenye nchi 11 na kushiriki ziara za utangazaji (road show). Majukumu mengine yaliyotekelezwa na bodi yameainishwa katika aya ya 54 - 56 ya kitabu cha Hotuba.

(iv) Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii

33. Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kimedahili wakurufunzi 242. Kozi ya awali kwa wakurufunzi wasiokuwa na sifa za kutosha kujiunga na chuo imeanza kutolewa ambapo wakurufunzi 18 wamenufaika na utaratibu huo. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania (TCT) na Chama cha Wamiliki wa Hoteli (HAT) kimeanza kutoa mafunzo katika programu ya *'Apprenticeship'* kwa wakurufunzi 20.

34. Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Hosteli za Chuo Kampasi ya Temeke umekamilika na kuongeza uwezo wa kuchukua wanafunzi kutoka 60 hadi 120. Chuo kimenunua vifaa (small operating equipment) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika Kampasi ya Bustani ili kuongeza ufanisi na kutoa mafunzo bora.

SEKTA NDOGO YA MAMBO YA KALE

(i) Sera na Sheria

35. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utaratibu wa kurekebisha Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na marekebisho yake ya mwaka 1979. Taratibu zinaendelea ili kupata ridhaa ya kutunga Sheria mpya ya Mambo ya Kale.

(ii) Utangazaji na Ushirikishwaji wa Jamii

36. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa vipindi kuhusu vielelezo vya kisayansi, kiutamaduni na kiteknolojia kuhusu chimbuko na maendeleo ya binadamu Tanzania Bara ili kukuza uelewa wa wananchi kutembelea na kushiriki katika uhifadhi wa Malikale. Vipindi hivyo vya zamadamu na utalii wa ndani vimerushwa kupitia vituo vya Televisheni vya TBC1 na Channel Ten. Lengo la vipindi hivi ni kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa malikale, kuhimiza matumizi endelevu na kukuza utalii. Jumla ya vipindi 15 kuhusu Historia na Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam na 10 kuhusu vivutio vya utalii wa malikale vilivyo katika mji wa kihistoria wa Bagamoyo vimetayarishwa na kutangazwa. Aidha, Wizara imefanya uhamasishaji katika shule zilizopo Mkoa wa Iringa na Wilaya ya Bagamoyo. Utaratibu uliotumika ni kupitia shule za msingi, sekondari, vyuo na kufanya mkutano na Wakala wa Utalii.

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imetangaza utalii wa urithi wa utamaduni katika maadhimisho mbalimbali ndani na nje ya nchi yakiwemo: Wiki ya Utalii Duniani; Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba); na Sherehe za Tamasha la Utalii na Kumbukizi ya Vita vya Majimaji. Aidha, Wizara imeshiriki kuandaa onyesho la kudumu katika balozi za Tanzania nchini China na Ufaransa. Onesho hili limejikita kuonyesha historia ya chimbuko la mwanadamu kwa kupitia vivutio vya utalii katika bonde la Oldupai, Laetoli na Muhula wa zana za Mawe Isimila.

(iii) Uhifadhi wa Malikale

38. Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa utalii kupitia urithi wa utamaduni, Wizara imempata mtaalam wa kuandaa michoro ya jengo la Makumbusho ya Laetoli ili kuhifadhi nyayo za Zamadamu. Kutokana na mpangokazi wa mtaalamu mshauri huyo, kazi ya kuandaa michoro ya jengo hilo itakamilika ifikapo mwezi Desemba, 2014. Aidha, umejengwa

uzio na kingo za kuzuia maji ya mvua yasiharibu nyayo za zamadamu za Engarasero. Vile vile, vipeperushi vimeandaliwa kwa ajili ya kutangaza eneo hilo.

39. Mheshimiwa Spika, Kazi nyingine zilizofanyika kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za malikale, utafiti wa malikale na uhifadhi wa malikale zimeainishwa kwa kina katika aya ya 62 – 64 katika kitabu cha Hotuba.

(iv) Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania

40. Mheshimiwa Spika, Shirika limesambaza vipeperushi 10,000 katika shule, taasisi na hoteli za kitalii ili kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kutembelea makumbusho. Vipindi vya televisheni vya watoto vimerushwa kwa ushirikiano kati ya Shirika, *American Garden* na Kituo cha Televisheni cha TBC1. Aidha, programu za watoto zinaendelea kufanyika kila Ijumaa ili kuhamasisha watoto kutembelea Makumbusho.

41. Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho Tanzania kwa kushirikiana na Makumbusho ya Alcala - Madrid, Spain liliandaa onesho la Chimbuko la Mwanadamu kwa kutumia vielelezo vilivyotokana na utafiti uliofanyika katika bonde la Olduvai, Ngorongoro. Onesho hilo lilizindulia huko Alcala, Madrid, Spain tarehe 10 Februari, 2014 na litachukua muda wa mwaka mmoja na baadaye litarudishwa Makumbusho ya Taifa Februari, 2015. Vile vile, Shirika limekamilisha Jubilei ya miaka hamsini ya ushirikiano wa Tanzania na Sweden; *Nyerere Day;* na Onesho la baiolojia katika Makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni.

URATIBU, UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

42. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji, Wizara imewezesha watumishi 112 kuhudhuria mafunzo mbalimbali. Kati ya hao, watumishi 98 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 14 mafunzo ya muda mrefu. Vile vile, Wizara imeajiri watumishi 42 na inategemea kuajiri watumishi 1,342 wa kada za wahifadhi wanyamapori 937; maafisa ufugaji nyuki 50; maafisa misitu 100; na wasaidizi ufugaji nyuki 80. Taratibu za kuwaajiri zinaendelea katika Mamlaka husika na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2014. Aidha, Wizara imewapandisha cheo watumishi 432 wa kada mbalimbali na watumishi 134 wamethibitishwa kazini. Majukumu mengine yaliyotekelezwa yameainishwa katika aya ya 68 na 69 ya kitabu cha Hotuba.

UKUSANYAJI MADUHULI

43. Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara ilikadiria kukusanya **Shilingi 148,971,444,489**. Hadi Machi 2014, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 82,086,269,449** sawa na **asilimia 55.1** ya makadirio. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikia lengo ni pamoja na kurudishwa kwa baadhi ya vitalu vya uwindaji kutokana na kupungua kwa wanyama na kuchelewa kuanza kwa Tozo ya Maendeleo ya Utalii.

III. MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015

SEKTA NDOGO YA WANYAMAPORI

(i) Uhifadhi, Usimamizi wa Wanyamapori na Ushirikishwaji Jamii

44. Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori ndani na nje ya Mapori ya Akiba kwa kuendesha siku za doria 106,000. Vile vile, miundombinu, vitendea kazi na huduma zitaboreshwa kwa watumishi katika Mapori ya Akiba na Kanda nane za Kikosi Dhidi Ujangili ili watumishi watekeleza kazi zao

ipasavyo. Ufafanuzi wa kina kuhusu Barabara zitakazojengwa katika mapori ya akiba, ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi na uhifadhi, gawio la fedha zitokanazo na uwindaji wa kitalii katika Halmashauri na WMAs, na utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa uko katika aya **71-73** ya kitabu cha Hotuba.

(ii) Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)

45. Mheshimiwa Spika, kuanzishwa rasmi kwa TAWA kunafungua ukurasa mpya katika historia ya Uhifadhi nchini, na kuwapa matumaini mapya wahifadhi wote, na hasa maaskari wa wanyamapori. Kimsingi, uanzishwaji wa Mamlaka umezingatia haja ya kujenga uwezo, kuboresha maslahi ya watumishi na kuimarisha shughuli za uhifadhi kwenye mapori ya akiba na maeneo yote nje ya TANAPA na NCA.

46. Mheshimiwa Spika, Chini ya Mamlaka ya Wanyamapori, tunaongeza vitendea kazi ili kuimarisha ulinzi na doria, na kuhakikisha tunawashinda majangili popote nchini. Tunaanzisha Kitengo Maalum cha doria za Helikopta kwa ajili ya kuwalinda wanyamapori, hususani Tembo na Faru kama ifuatavyo:-

(a) Selous Game Reserve – Helikopta moja aina ya Robertson 44 inayonunuliwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Howard Buffet;

(b) Ngorongoro Conservation Area – Helikopta aina ya Robertson 44; na

(c) Helikopta aina ya Bell, inayonunuliwa na TANAPA. Marubani 6 kwa ajili ya Helikopta wanaanza mafunzo nchini Afrika Kusini mwishoni mwa mwezi huu.

47. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ulinzi wa Tembo, Wizara inaanzisha kitengo maalum cha mafunzo ya Inteligensia na ukomandoo wa Kikosi maalum kitakachokuwa na uwezo wa kuteremka kwenye helikopta katikati ya pori na kuwatia nguvuni majangili. Aidha, Chuo cha Maaskari wa Wanyamapori Pasiansi, kupitia Taasisi ya Howard Buffet, kinapata miundombinu mipya ya mabweni ya wananfunzi 300 zaidi, GPS, Darubini, Mabasi maalum 2, malori maalum 2, magari 5 mahema ya mafunzo, mtaalam mwelekezi, pamoja na kujengewa uwezo kumudu mahitaji maalum ya Taaluma hii kulingana na changamoto za wakati huu.

48. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania itasimamia eneo lenye ukubwa wa kilometa za Mraba 200,000, ikiwepo Mapori yote ya Akiba (28) na Mapori Tengefu (43). Shirika la Hifadhi za Taifa litaendelea kusimamia hifadhi 16 zenye jumla ya ukubwa wa kilometa za mraba 57,000 na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itaendelea kusimamia eneo lake la kilometa za mraba 8,500.

49. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi ujao, Wizara itakuwa na jumla ya Askari wa Wanyamapori **2,532**, walio chini ya Mamlaka nilizozitaja hapo juu.

50. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori (TWPF) ulio chini ya Wizara, pamoja na Mfuko wa wadau wa maendeleo ulio chini ya UNDP (Multilatoral Antipoaching and Wildlife Security Busket Fund) pamoja na rasilimali zingine zitatumika kuijengea Mamlaka ya Wanyamapori uwezo wakati tunaianzisha, Makao yake Makuu yakiwa Mjini Morogoro. Nia na Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa hatua hizi za kuanzisha mfumo mpya wa Mamlaka utaweza kulinda rasilimali za nchi, na kuhakikisha uwepo wa Tembo na Wanyamapori wengine katika miaka mingi ijayo.

51. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania itakuwa na Bodi inayojitegemea, na itakuwa na Mkurugenzi Mkuu (Director General) atakayeteuliwa na Mhe. Rais, na itakuwa na vyanzo vyake vya mapato vitakavyoainishwa katika mabadiliko ya sheria.

(iii) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori

52. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Taasisi itaendeleza utafiti wa wanyamapori, aina za nyuki, mahusiano kati ya nyuki na mimea pamoja na kuidadi wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mafunzo kuhusu njia stahiki za ufugaji nyuki yatatolewa katika vijiji vya Wilaya za Simanjiro, Kiteto na Hanang na kutengeneza mizinga 1,500 kwa ajili ya kuisambaza kwa wadau wa sekta ya ufugaji nyuki. Aidha, Taasisi itaendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti wa nyuki.

(iv) Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori

53. Mheshimiwa Spika, vyuo vya mafunzo ya uhifadhi wanyamapori vitadahili jumla ya wakurufunzi 980: Pasiansi - 400 na Mweka - 580. Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa wananchi 240. Vile vile, Chuo cha Mweka kitawezesha wakufunzi watatu kupata mafunzo ya Uzamili na wawili Uzamivu. Aidha, Chuo kitajenga madarasa mawili na matanki matatu yenye jumla ya mita za ujazo 450 kwa ajili ya kuhifadhi maji.

(v) Shirika la Hifadhi za Taifa, Tanzania

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Shirika litaendelea kutatua migogoro ya mipaka na shoroba; na kuimarisha mifumo ya TEHAMA. Vilevile, Shirika litaboresha miundombinu ya majengo, madaraja, barabara, maliwato ya mlimani, nyumba za wafanyakazi, huduma ya maji, na umemejua. Pia, Shirika litaimarisha utalii na kupanua wigo wa vivutio na huduma kwa watalii, kuajiri watumishi ikiwa ni pamoja na kuwa na muundo wa '*Paramilitary*' ili kuimarisha uhifadhi.

55. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi hizo, Shirika litanunua vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja: silaha, vifaa vya mawasiliano ya ki-intelijensia, na vifaa mbalimbali vya kuboresha ufuatiliaji wa karibu wa Faru kwa ajili ya kudhibiti ujangili. Vile vile, Shirika litanunua Helikopta, aina ya Bell, magari 12, na mitambo mizito ya barabara miwili. Aidha, Shirika litaweka mifumo mipya 12 ya ki-elektroniki ya kukusanya mapato katika Hifadhi saba, kujenga/kukarabati nyumba 15 za watumishi na kuweka seti 21 za umemejua katika vituo vya maaskari. Vile vile, Kituo cha Utalii kitajengwa katika Hifadhi ya Arusha. Pia, mabanda manne ya kulala Watalii wa ndani yatajengwa katika Hifadhi za Ruaha na Saadani. Vituo vinne vya kupumzikia wageni na mabanda mawili ya wapagazi (Porters) yatajengwa katika Hifadhi ya Kilimanjaro. Jumla ya Kilometa 26 za barabara mpya zitajengwa katika Hifadhi ya Mikumi. Aidha, Shirika litajitangaza vivutio vya utalii kupitia televisheni za ndani na za kimataifa kama vile CNN, CCTV na CNBC.

(vi) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

56. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2014/2015, Mamlaka itaendelea kununua na kusambaza chakula kwa wafugaji waishio ndani ya Hifadhi ambapo tani 4,700 za mahindi zitatolewa. Shule za msingi 21 zimetengewa **Shilingi 70,000,000** kwa ajili ya kununua chakula. Vile vile, Mamlaka itanunua helkopta moja, magari 10, basi moja la utalii wa ndani, gari la kutoa huduma kwa wagonjwa, kujenga nyumba mbili za askari katika vituo vya Lemala na Selela na kukarabati nyumba nne za maaskari katika vituo viwili. Mamlaka pia itaimarisha doria kwa kununua na kutumia zana mbalimbali za kisasa na kuendelea na ujenzi wa jengo la kitega

uchumi Jijini Arusha. Majukumu mengine yatakayotekelezwa yameainishwa katika aya ya **79 hadi 81** ya kitabu cha Hotuba.

SEKTA NDOGO YA MISITU NA NYUKI

(i) Sera na Sheria

57. Mheshimiwa Spika, rasimu ya Sera ya Taifa ya Misitu imekamilika na taratibu za kuidhinishwa zinaendelea. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki yataendelea kwa kukusanya maoni ya wadau. Kufuatia kukamilika kwa mapitio ya Programu ya Taifa ya Misitu ya 2001 - 2010 utayarishaji wa programu mpya utaendelea. Aidha, uchambuzi wa Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 utafanyika ili kuainisha majukumu ya Wakala wa Huduma za Misitu.

(ii) Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Jumla ya wakurufunzi 308 watadahiliwa kama ifuatavyo: Chuo cha Misitu Olmotonyi 195, Chuo cha Viwanda vya Misitu 40 na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki 73. Katika kuboresha miundombinu, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitajenga maktaba na maabara. Chuo cha Misitu Olmotonyi kitafanya ukarabati wa nyumba tisa za watumishi, ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula na kiwanda cha kupasua mbao. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitajenga nyumba moja ya waalimu na karakana ya mbao pamoja na kukarabati jengo la utawala na kuliwekea samani.

(iii) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

59. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2014/2015, Wakala utaanza kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano (Julai 2014 - Juni 2019). Mpango huu umelenga kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki na kuboresha mifumo ya usimamizi. Aidha, Mpango wa Kibiashara kwa mwaka 2014/2015 unaosisitiza kuimarisha uwezo wa Wakala katika kutoa huduma, upatikanaji wa rasilimali na mifumo ikolojia pamoja na kuwezesha matumizi ya rasilimali zilizoboreshwa utatekelezwa.

(a) Usimamizi wa Rasilimali za Misitu na Nyuki

60. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na kudhibiti uvunaji haramu wa mazao ya misitu, Wakala unatarajia kuendesha siku za doria 22,000 katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati za uvunaji katika Halmashauri 55 za wilaya zitawezeshwa kufanya vikao vya kujadili maombi ya uvunaji. Vile vile, Wakala utafanya mikutano 14 kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu na nyuki katika Kanda za Kaskazini, Kusini, Mashariki, Kati na Ziwa. Lengo la mikutano hiyo ni kuelimisha wafanyabiashara kuhusu sheria na taratibu za kufanya biashara ya mazao ya misitu. Majukumu mengine yatakayotekelezwa yameainishwa katika aya ya 86 hadi 88 ya kitabu cha Hotuba.

(b) Usimamizi wa Mashamba ya Miti

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, jumla ya miche 15,000,000 itaoteshwa na kupandwa katika mashamba ya miti yenye ukubwa wa hekta 7,300. Wakala

utarudishia miti katika maeneo yenye ukubwa wa hekta 200; utaondoa magugu kwenye eneo la hekta 33,150, kupogoa hekta 1,812 na kukarabati barabara za msituni zenye urefu wa jumla ya kilomita 2,691. Aidha, usimamizi wa mashamba ya miti utafanyika kwa kufanya doria kwenye eneo la hekta 214,000, kusafisha barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 6,120 na kusafisha mipaka kilomita 862.

62. Mheshimiwa Spika, Katika kupunguza changamoto ya uhaba wa malighafi ya mazao ya misitu, Wakala utaanzisha mashamba mapya yenye ukubwa wa jumla ya hekta 2,225 ya spishi za aina mbalimbali. Vile vile, eneo la msitu wa asili Kahe – Kilimanjaro hekta 50 litapandwa misaji na shamba la nishati ya kuni lililopo Korogwe hekta 50 litapandwa mikaratusi. Aidha, Wakala unatarajia kuanzisha hekta 50 za mikaratusi na mianzi katika Msitu wa Hifadhi wa Ruvu. Kazi nyingine za usimamizi wa rasilimali za misitu, ushirikishaji jamii, elimu kwa umma, kuwajengea wwatumishi uwezo zimeainishwa katika aya ya **85 hadi 93** ya kitabu cha Hotuba.

(c) Kuanzisha Vituo vya Kuzalishia Makundi na Kuendeleza Ufugaji Nyuki

63. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na upungufu wa makundi ya nyuki unaosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi, Wakala utaanzisha vituo vitano vya kuzalishia malkia wa nyuki. Vituo hivyo ni: NAFRAC – Shinyanga, Ukimbu – Manyoni, Ruvu – Kibaha, Nandembo – Tunduru na Shamba la Miti Sao Hill. Aidha, Wakala utatoa mafunzo ya uzalishaji wa makundi ya nyuki kwa wawezeshaji 40. Kati ya watakaopewa mafunzo 20 ni watumishi na 20 wanatoka kwa wawakilishi wa wafugaji nyuki. Wakala utatoa mizinga 1,200 na mafunzo kwa wafugaji nyuki kutoka vijiji 91 vilivyoko kandokando ya misitu. Jumla ya wafugaji nyuki 1,501 kutoka vikundi 115 watanufaika na mafunzo hayo.

(d) Kongamano la Ufugaji Nyuki – APIMONDIA

64. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa mara ya kwanza barani Afrika, Tanzania imepata heshima ya kuandaa Kongamano la Ufugaji Nyuki (APIMONDIA). Lengo ni kuongeza msukumo wa ufugaji nyuki na kupanua wigo wa masoko ya mazao ya nyuki. Kongamano litafanyika tarehe 11 hadi 13 Novemba, 2014 katika ukumbi wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa wa AICC, Arusha. Jumla ya washiriki 550 kutoka ndani na nje ya nchi wanatarajiwa kuhudhuria. Kongamano hilo litaambatana na maonesho ya kibiashara na ziara za mafunzo.

(iv) Wakala wa Mbegu za Miti

65. Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu bora za miti unakuwa endelevu, Wakala utaanzisha vyanzo vitano vya mbegu bora za miti ya Misindano aina mbili, Msenefu, Mwiluti na Mpaulonia. Vilevile, Wakala utatambua na kusajili vyanzo vitatu vya mbegu za miti aina ya Mkenge na Mgunga. Pia, utaendelea kutunza vyanzo 31 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali. Wakala utakusanya jumla ya kilo 12,500 za mbegu ya miti aina mbalimbali pamoja na kuuza kilo 11,500 za mbegu za miti na miche ya miti 100,000.

(v) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania

66. Mheshimiwa Spika, kutokana na wakulima wengi kuvuna miti yao katika umri mdogo na hivyo kupoteza mapato, Taasisi itafanya utafiti juu ya ubora wa mbao zitokanazo na miti ya umri tofauti. Lengo ni kutoa ushauri wa kisayansi juu ya umri stahiki wa kuvuna miti bila kuathiri ubora wa mbao kwa matumizi mbalimbali .Aidha, taasisi itaanzisha mashamba darasa

katika Wilaya za Mkuranga na Handeni ili kuelimisha jamii inayozunguka misitu ya hifadhi juu ya umuhimu wa kuwa na mashamba ya miti ya kuni na matumizi mengine. Aidha, Taasisi itaajiri watafiti wasaidizi tisa, watafiti waandamizi watano, wakurugenzi wa vituo vya utafiti wanne na watumishi wengine 27 pamoja na kununua samani na vitendea kazi vya ofisi na maabara.

(vi) Mfuko wa Misitu Tanzania

67. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Misitu Tanzania unakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 5,357,540,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato. Mfuko utatoa ufadhili wa **Shilingi 1,992,603,7000** kwa ajili ya miradi 173 ya wadau mbalimbali wa misitu na ufugaji nyuki. Kati ya miradi hiyo 97 ni mipya. Wadau watakaonufaika na ufadhili wa Mfuko ni pamoja na watu binafsi, vikundi vya jamii, asasi za kiraia, taasisi zisizo za Kiserikali na taasisi za Serikali zikiwemo Serikali za Mitaa.

SEKTA NDOGO YA UTALII

(i) Sera na Sheria

68. Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 ili iendane na mahitaji halisi katika sekta ya utalii. Maandalizi ya sera mpya yatazingatia hatua zote muhimu kwa kushirikisha wadau kupitia mikutano. Aidha, itafanya warsha kwa wadau wa utalii katika kanda nne ili kuhamasisha utekelezaji wa Kanuni za utalii.

(ii) Uendelezaji wa Utalii

69. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa mwenendo wa biashara ya utalii nchini pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za utalii. Kazi ya kukagua wakala wa biashara za utalii itafanyika katika kanda nne ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Pwani, Kanda ya Nyanda za juu Kusini na Kanda ya Ziwa. Vile vile, Wizara itaainisha vivutio vya utalii katika mikoa ya Singida na Katavi na kutoa ushauri wa kitaalamu wa kuviboresha.

(iii) Bodi ya Utalii Tanzania

70. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kuanzia mwezi wa Julai, 2014, tunachukua hatua madhubuti za kuhuisha mtazamo wa dunia juu ya Taifa letu na Utalii nchini Tanzania. Bodi ya Utalii, kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa TANAPA, na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itasimamia kutangazwa kwa vivutio vya Utalii vilivyopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika matangazo maalum ya Runinga yatakayoanza kurushwa katika vituo vya CNN na BBC kwa kipindi cha mwaka mzima. Aidha, tunatarajia kumwomba Mheshimiwa Rais azindue "Mpango wa Kuhuisha Mtazamo wa Dunia Kuhusu Utalii Tanzania". (Re-Branding Destination Tanzania mapema mwezi Julai, 2014).

71. Mheshimiwa Spika, Bodi itashiriki maonesho na misafara ya utangazaji ya utalii ya Kimataifa itakayofanyika katika nchi za Uholanzi, Hispania, Ujerumani, Uturuki, Uingereza, China, Urusi, Afrika ya Kusini, India, Brazil, Italia na Nchi za Ghuba. Aidha, Bodi itatumia mitandao ya kijamii kutangaza vivutio vya utalii. Mikakati mingine itahusisha kuandaa Tamasha la Utalii wa Utamaduni kwa kushirikiana na Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo; kuandaa safari mbili za kupanda Mlima Kilimanjaro; kutangaza utalii kupitia michezo; na kuendesha onesho jipya la Kimataifa la Utalii (Swahili International Tourism Exhibition). Vile vile, Bodi itafungua ofisi za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

uwakilishi kwa ajili ya kutangaza utalii nchini India na Ujerumani na kuendelea kuimarisha ofisi ya uwakilishi iliyoko nchini Marekani (the Bradford Group).

72. Mheshimiwa Spika, Bodi itaendelea kutangaza utalii wa ndani kupitia Maonesho sita ambayo ni Sabasaba, Nanenane, Karibu Travel Fair, Siku ya Utalii Duniani, Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar na Tamasha la Sauti za Busara.

(iv) Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii

73. Mheshimiwa Spika, Chuo kitadahili Wakurufunzi 312 kwa mwaka 2014/2015 na wakurufunzi 50 wa kozi ya awali kwa wasiokuwa na sifa za kutosha kujiunga na Chuo ngazi ya Astashahada. Aidha, Chuo kupitia mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kitaanzisha mafunzo ya wawezeshaji (Training of Trainers) kwa ajili ya wakufunzi wa vyuo vya Hoteli na Utalii. Pia, utafanyika upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na maktaba katika Kampasi ya Arusha.

SEKTA NDOGO YA MALIKALE

74. Mheshimiwa Spika Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Malikale na kuandaa miongozo ya utafiti na uhifadhi wa Malikale katika maeneo ya kihistoria ya Kilwa Kivinje, Mikindani na Mji wa Kihistoria Pangani. Aidha, Wizara itafanya ukarabati wa Boma la Pangani na jengo la zamani la Mahakama Kalenga Iringa; ujenzi wa kituo cha taarifa cha Amboni Tanga; ujenzi wa uzio katika Kituo cha Kunduchi; na kuboresha mandhari ya kituo cha Ujiji Kigoma na Kaole Bagamoyo. Wizara itaandaa orodha ya maeneo ya wapigania uhuru katika Mkoa wa Mtwara. Vile vile, itashiriki mikutano ya kitaalamu ngazi ya Kimataifa ili kunufaika na fursa zilizopo.

(i) Shirika la Makumbusho ya Taifa

75. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Shirika litaendelea kuitangaza Makumbusho kwa kutumia vipindi vya televisheni, redio, mitandao ya kijamii, vipeperushi na kupitia maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Aidha, litajenga uwezo kwa watumishi na kuboresha mazingira ya kazi kwa vituo vya Arusha, Musoma, Ruvuma na Dar es Salaam. Vile vile, Shirika litaongeza vituo vya makumbusho Chamwino, Singida na Mwanza pamoja na kufanya upanuzi katika vituo vya Butiama na Elimu viumbe Arusha. Shirika pia litaratibu Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania litakaloshirikisha jamii kutoka Mkoa wa Kagera.

URATIBU, UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

76. Mheshimiwa Spika, Wizara itawezesha watumishi 846 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, Wizara itapandisha cheo watumishi 522 na kuaajiri 1,033 (641 kada ya Wahifadhi Wanyamapori na 322 kada ya Misitu). Vilevile, watumishi watawezeshwa kupata mikopo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Benki binafsi; Watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI wataendelea kupokea huduma ya lishe. Wizara itaimarisha Chama cha Kuweka na Kukopa (MNRT SACCOS) pamoja na kuendelea kuratibu upatikanaji wa mikopo kwa watumishi wake kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Benki binafsi. Majukumu mengine yatakayotekelezwa yameainishwa katika aya ya 107 na 108 ya kitabu cha Hotuba.

IV. SHUKURANI

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

77. Mheshimiwa Spika, shukurani zangu za dhati napenda ziende kwa Mheshimiwa Mahamoud Hassan Mgimwa (Mb) Naibu Waziri, Mbunge wa Mufindi; Bibi Maimuna Kibenga Tarishi, Katibu Mkuu na Bwana Selestine Gesimba, Naibu Katibu Mkuu. Vile vile, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Mashirika, Wakala, Taasisi na Vyuo pamoja na watumishi wa Wizara ya Maliasili kwa kujitoa kwa dhati katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

78. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wote walioshiriki kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nianze kwa kuwashukuru washirika wa maendeleo ambao ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za Kiserikali na taasisi za fedha. Kwa namna ya pekee, napenda kuwataja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Marekani, Uingereza, China, Finland, Norway, Ubelgiji, Ufaransa na Ujerumani; Jumuiya ya nchi za Ulaya; Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, ICCROM, UNDP-GEF, UNESCO na UNWTO; WB*, na Mashirika ya misaada na taasisi zisizo za kiserikali za *AWF, AWHF, BTC, DANIDA, FZS, GIZ, ICOMOS, IUCN, KfW, LATF, USAID, WMF, WHC, WWF* na kipekee, Taasisi ya *HBF*.

V. HITIMISHO

79. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/2015, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya jumla ya **Shilingi 83,119,264,000.** Kati ya hizo, **Shilingi 68,921,048,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 14,198,216,000** ni kwa ajili ya Miradi Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 30,627,417,000** kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na **Shilingi 38,298,631,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 5,000,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 9,198,216,000** fedha za nje.

80. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii. Mheshimiwa Lembeli!

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maliasili na Mazingira Kama Ilivyosomwa Bungeni

MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2013/2014, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2013, Kanuni ya 69(9) nachukua nafasi kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu makadirio mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane, ya Kanuni aa Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 kifungu namba 6(8) na 7(1) kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na kuchambua bajeti ya Wizara hii kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake mnamo tarehe Mosi Mei, 2014 Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili pamoja na wataalam wa Wizara hiyo na kujadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka 2013/2014. Mafanikio na changamoto, pamoja na mpango wa maendeleo na bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Katika mwaka 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo mbalimbali ya msingi. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati, japokuwa yapo baadhi ya maeneo ambayo juhudi zaidi zinahitajika katika utekelezaji wake. Maeneo hayo ni pamoja na mgawanyo wa mapato yanatokanayo na uwindaji wa kitalii, ulenge kuziwezesha jumuiya za hifadhi za wanyamapori.

Mbili, Serikali ichukue hatua za kupunguza migogoro ya mipaka kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Tatu, operesheni maalum ziendeshwe mara kwa mara ili kukabiliana na tatizo la ujangili wa wanyamapori na hususan tembo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaihimiza Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ilikuwa na uhifadhi endelevu kwa faida ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2013/2014, mafanikio na changamoto. Mafanikio; katika mwaka wa fedha 2013/12014 Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa jumla ya sh. 75,681,745,000/= kati ya fedha hizo, sh. 64,033,579,000/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 11,648,166,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea sh. 29,853,746,222/= sawa na asilimia 46.62 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, Wizara ilipokea jumla ya sh. 29,853,746,222/= kati ya fedha hizo, sh. 7,641,948,312/= matumizi mengineyo na sh. 22,211,797,910/= kwa ajili ya mishahara. Fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida zimeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kufuatilia na kuhakiki ukusanyaji wa maduhuli katika vituo 125.

- Kukamilisha maandalizi ya rasimu ya sheria ya uanzishwaji ya Mamlaka ya Wanyamapori.

- Doria 54,574 *(mandays)* zilifanyika ndani na nje ya Mapori ya Akiba ambapo watuhumiwa walikamatwa na kuhusishwa na makosa mbalimbali ya ukiukwaji ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

- Kufanya utafiti wa mwenendo wa biashara ya utalii pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za utalii wa ndani na wa Kimataifa. Utafiti unaonesha kuwa idadi ya watalii imeongezeka kufikia 1,095,884 kulinganishwa na 1,077,058 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilipanga kutekeleza miradi kumi ya maendeleo kwa jumla ya sh. 11,648,166,000/= ambazo fedha za nje, ni sh. 10,648,166,000/= na sh. 1,000,000,000/= fedha za ndani. Mpaka kufikia Machi, 2014 sh.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

4,033,801,000/= zilipokelewa ambapo sh. 3,858,801,000/= ni fedha za nje na sh. 175,000,000/= ni fedha ndani.

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio yaliyoonekana Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa fedha hasa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, sh. 4,033,801,000/= tu ndizo zilitolewa kati ya sh. 11,648,166,000/= zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia kwa kina mikakati ya namna Serikali ilivyojipanga kukabiliana na changamoto hizi na kuona itafaa endapo itasimamiwa na kutekelezwa. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

- Kuendelea kuajiri watumishi wapya kulingana na ikama iliyopitishwa;

- Kuongeza ushuru wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya mali asili, malikale na shughuli za utalii;

- Kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha wananchi kutembelea vituo vya utalii;

- Kufanya mapitio ya sera na sheria;

- Kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli; na

- Kuongeza bajeti ya Ulinzi, Uhifadhi na Usimamizi wa Rasilimali za Maliasili na Malikale.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa matumizi ya Wizara kwa mwaka 2014/2015. Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 inaomba kuidhinishiwa sh. 83,119,264,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Jumla ya sh. 68,921,480,000/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati ya hizo sh. 38,293,631,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na sh. 30,627,417,000/= ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, bajeti inayoombwa kwa ajili ya miradi 11 ya Maendeleo ni sh. 14,198,216,000/= kati ya hizo, pesa za ndani ni sh. 5,000,000,000/= na sh. 9,198,216,000/=) ni fedha za nje. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara na taasisi zake inategemea kukusanya maduhuli ya jumla ya sh.144,608,745,710/= ikiwa ni pungufu kwa asilimia 24 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kama inavyofahamika, Sekta ya Utalii na Maliasili ni mhimili wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwani ina mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 17. Hata hivyo, mchango huo ni mdogo ukilinganisha na fursa nyingi zilizopo hasa katika Hifadhi za Taifa, Wanyamapori na Malikale. Endapo sekta hii itasimamiwa vizuri na kuendelea kupewa kipaumbele na Serikali katika kutangaza vivutio tulivyonavyo ni dhahiri kwamba uchumi wa Taifa hili utaimarika na hatimaye kuondoa kiasi kikubwa cha tatizo la umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu na busara kwa Serikali kuhakikisha inalinda na kutetea maslahi ya Taifa letu yanayotokana na biashara ya Utalii. Habari zilizozagaa nchini kwamba

Serikali inataka kufungua lango la Bologonja kuruhusu watalii kutoka hifadhi ya Masai Mara nchini Kenya kuingia ndani ya hifadhi ya Serengeti, siyo tu habari njema kwa pato la utalii kwa nchi yetu. Vivyo hivyo si habari njema kwa kazi za uhifadhi, lakini pia kwa wafanyabiashara wa sekta hiyo wa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuachana kabisa na mpango huo kama upo kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya uwindaji pia ni miongoni mwa sekta ambazo zimekuwa zikilingizia Taifa letu pesa nyingi za kigeni. Habari kwamba vitalu vya uwindaji karibu 10 vya madaraja mbalimbali vimerudishwa baada ya waliopewa kushindwa kuendesha biashara hiyo si nzuri, kwani zimesababisha mapato ya Taifa kupungua. Kwa kuwa sababu zinazotolewa za kurejeshwa kwa vitalu hivyo ni pamoja na vitalu hivyo kuvamiwa na mifugo, idadi ya wanyama kupungua, lakini pia uwezo wa waliokabidhiwa vitalu hivyo kufanya biashara hiyo. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimni ya kina kuhusu hali hiyo, lakini pia kupitia upya Sheria ya Wanyamapori kuona kama pia imechangia hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Biashara ya Utalii. Idara ya Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii *(TTB)*, Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa pamoja wameonesha juhudi za wazi za kutangaza utalii wa Tanzania. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya Watalii wanaoingia nchini imeongezeka kutoka watalii milioni moja na sabini na saba elfu hamsini na nane mwaka 2012 hadi kufikia milioni moja tisini na tano elfu mia nane themanini na nne kwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipofanya ziara katika Hifadhi za Kusini, Katavi, Kitulo na Ruaha ilibaini kwamba hifadhi hizi hajitangazwa vya kutosha, hivyo kuwa na idadi ndogo ya watalii ukilinganisha na Hifadhi za Kaskazini. Kamati ilijulishwa kwamba, kutotangazwa kwa hifadhi hizi kunachangiwa na fedha ndogo zinazotengwa kwa ajili ya utangazaji wa hifadhi hizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini ubovu wa miundombinu kuelekea katika hifadhi hizi jambo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa biashara ya utalii. Barabara nyingi hazipitiki kwa urahisi. Kwa mfano, barabara ya kutoka Mbeya kwenda Rukwa na hatimaye Katavi na ile ya Kutoka Iringa Mjini kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha zote ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubovu huo wa miundombinu, gharama za usafiri mpaka hifadhini zimekuwa ni kubwa mno kiasi cha kuwakatisha tamaa watalii kutembelea maeneo hayo. Kwa mfano, gharama ya usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupitia Pori la Akiba la Selous na kurudi humgharimu Mtalii kati ya dola za Marekani 700 na 1000.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vyema sasa Serikali ikaongeza juhudi katika kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vilivyopo ndani na nje ya hifadhi katika Mikoa ya Kusini ili kuanza kupunguza gharama ya usafiri na pia kuwezesha shughuli za kitalii kufanyika katika msimu wote wa mwaka tofauti na sasa ambapo shughuli hizo husimama wakati wa masika.

Mheshimwia Spika, sababu nyingine inayochangia idadi ndogo ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu kuwa ndogo ni uchache wa vyumba vya kulala watalii katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba uchache huu wa mahoteli katika maeneo ya hifadhi unachangiwa na baadhi ya wafanyabiashara waliopewa maeneo ya kujenga kutoyaendeleza maeneo kwa muda mrefu. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya

Ruaha, Makampuni 11 ambayo yalipewa maeneo ya kujenga kuanzia Juni, 2009, ikiwa ni miaka takribani mitano iliyopita, hayajaanza ujenzi hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inashauri kwamba, kwa kuwa mwaka 2002, Serikali ilijiwekea lengo la kufikisha watalii milioni moja ifikapo 2010 na kwa kuwa tayari lengo hilo limefikiwa, kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Serikali ijiwekee lengo jipya la idadi ya Watalii watakaoingia nchini hasa kwa kuzingatia mazingira ya sasa ambapo matangazo ya vivutio vya utalii nchini yamefika katika nchi nyingi zaidi duniani ukilinganisha na mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, utalii wa ndani. Kamati inawapongeza Watanzania kwa kuanza kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii nchini. Hata hivyo, kasi hii ya Utalii inakwamishwa na gharama kubwa za maradhi hasa katika hifadhi za Taifa. Gharama hizi zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukweli kwamba hoteli nyingi zilizoko ndani ya Hifadhi ya Taifa zinamilikiwa na makampuni ya kigeni. Kamati inashauri Wizara kutoa kipaumbele kwa Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza katika ujenzi wa maeneo ya malazo ndani ya hifadhi kwa maana ya hoteli za kitalii, mabanda *(cottages)* maeneo ya kupiga mahema kwa watu wote *(public campsite)* na kwa watu maalum *(special camp site)*.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wanyamapori. Taarifa ya Kamati ya mwaka uliopita 2012/2013 kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilizungumzia ujangili wa wanyamapori kama changamoto kubwa katika idara hii. Kamati inasikitika kuona kwamba, bado ujangili umeendelea kuwa changamoto kubwa katika mapori yote ya akiba na hakuna dalili yoyote inayoonesha kupungua kwa changamoto hii kutokana na sababu mbalimbali ikiwa pamoja na:-

- Kuchelewa kuhukumiwa na kuharibiwa kwa kesi za Ujangili;

- Upungufu wa rasilimali watu hasa Askari wa Wanyamapori;

- Upungufu na ubovu wa magari ya doria; na

- Kubwa zaidi kukosekana kwa silaha za kisasa kwa ajili ya kukabiliana na majangili ambao wengi hutumia silaha za kivita.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba pamoja na nchi yetu kibarikiwa na kuwa hazina kubwa ya Wanyamapori, bado Serikali haijaipa kipaumbele na umuhimu unaostahili. Kamati inaona kwamba, japo kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeonesha nia ya wazi ya kukabiliana na ujangili, hivyo kununua silaha kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo, Serikali hiyo hiyo kupitia Wizara ya Fedha kwa maana ya TRA ilizuia silaha hizo bandarini ikidai kodi kwa zaidi ya mwaka mmoja na hatimaye silaha hizo kutozwa kodi ya sh. 197,880,546/=.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha wakati *TRA* inashikilia silaha hizo, tembo wa nchi hii waliendelea kuteketezwa fedha ambayo *TRA* ilikuwa inadai kama kodi ni sh. 197,880,546/= ni sawa na thamani ya meno ya tembo wanaouawa kwa siku moja. Sote tunafahamu, tatizo moja linalowakabili maaskari wa wanyamapori ni upungufu wa silaha za kisasa kupambana na majangili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ka kusikitisha ni *TRA* kutoza kodi faru wanaoletwa nchini kama msaada na wahisani kwa ajili ya kurejesha nchini wanyamapori hao ambao walikaribia kutoweka. Faru hao ni pamoja na wale waliotolewa kama msaada walioko katika

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Serengeti. Kodi ambayo *TRA* imekuwa ikotoza kwa kila Faru mmoja ni sh. 600,030/=.

Mheshimiwa Spika, taasisi kama *TRA* haioni wala kutambua jitahada za mkono mwingine wa Serikali kuokoa rasilimali za Taifa hili inayoendelea kupotea siku hadi siku. Kwa lugha nyingine *TRA* kuendelea kutoza kodi faru walioletwa kama msaada na wahisani ni kushawishi wahisani wasitishe misaada yao. Kamati inashauri na kuitaka Serikali kuondoa kodi kwa faru na vifaa vingine vinavyotolewa na wahisani kwa ajili ya uhifadhi wa faru na vile vile vinavyohusika na kujenga mazingira mazuri ya faru kuishi kama magari, magreda pamoja na silaha za kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri Askari wa Wanyamapori wa kutosha. Idadi iliyopo haitoshi na wala haikidhi mahitaji na changamoto zilizopo. Kwa mfano, Pori la Akiba la Rukwa/Lukwati/Lwafi lenye ukubwa wa kilomita za mraba karibu 10,000, lina jumla ya watumishi 45 tu. Hali hii mbaya zaidi katika mapori karibu yote ya akiba ikiwa pamoja na Pori la Akiba la Selous ambalo lina ukubwa wa zaidi ya kilomita za mraba 50,000. Kamati inashauri kwamba, ili kurejesha hali ya utulivu katika mapori yote ya akiba, Serikali inatakiwa kuajiri Askari wa Wanyamapori wasiopungua 1,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yaliyojitokeza, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendesha *Operation* Tokomeza kwa lengo la kuwalinda wanyama wetu. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka tathimini ya madhara yaliyosababishwa na *Operation* Tokemeza ili awamu ya pili iweze kufanyika. Aidha, Kamati inashauri Serikali kutekeleza maadhimio yote ya Bunge kuhusu utekelezaji wa *Operation* Tokomeza na kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la kuchelewa kutolewa hukumu na wakati mwingine ushahidi wa kesi za ujangili kuharibiwa. Ni changamoto kubwa katika mapori ya akiba na hifadhi za Taifa. Kamati inatoa rai kwa vyombo vya Serikali kama vile Jeshi la Polisi na Mahakama kushirikiana na Idara ya Wanyamapori kuhakikisha watuhumiwa wa kesi za ujangili wanashtakiwa na kupewa adhabu kali kwa mujibu wa sheria. Kamati haipendi kuamini kuwa kesi hizi zinahujumiwa kutokana na Askari Polisi na Mahakimu wachache kujihusisha na vitendo vya rushwa katika kusimamia kesi hizi.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali ya kukamilisha, kuandaa maandalizi ya uanzishaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania pamoja na rasimu ya muundo wa uendeshaji wa mamlaka hiyo. Kamati inaamini kwamba kuanzishwa kwa mamlaka hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa mianya ya rushwa, ufujaji wa mapato na ufisadi uliopo katika Idara hii ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Ujangiri wa Tembo. Kwa sasa Ujangiri wa Tembo umekuwa ni janga la kitaifa. Ni ukweli usiofichika kwamba, leo hii si tu tembo wanauawa bali wanateketezwa. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na taasisi za utafiti wa wanyamapori za Serikali na mashirika ya hapa nchini. Takwimu zinashabihiana na taarifa za utafiti wa Kimataifa zinazoonesha kwamba tembo wasiopungua 30 wanauawa kila siku.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari na ni aibu kwa Taifa letu ambalo ni la pili Barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo. Kamati inachukua fursa hii kumpongeza Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake binafsi za kudhibiti ujangili wa tembo ambapo amewezesha Tanzania kupewa misaada mbalimbali ikiwa pamoja na ndege na helikopita zitakazosaidia kupambana na ujangili. Tunamwomba azidi kuisaidia sekta hii ili urithi udumu kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mambo ya Kale. Tanzania ni moja ya nchi maarufu zenye hazina kubwa ya malikale. Malikale zilizopo ni pamoja na majengo ya zamani yaliyojengwa kwa matumbawe katika miji ya Pwani, Michoro ya Kale, Mapango ya Amboni, Nyayo za Binadamu aliyeishi miaka milioni tatu nukta sita iliyopita (3.6) na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba nchi nyingi duniani hupata mapato makubwa kutokana na utalii unaotegemea vivutio vya aina. Hata hivyo, Serikali yetu bado haijafanikiwa kuliingizia Taifa letu pato la kuridhisha kutokana na Utalii wa malikale. Maeneo mengi yenye vivutio vya aina hii ya utalii ni kama yamesahauliwa kwani hayatangazwi vya kutosha na hayana usimamizi unaotakiwa na sehemu nyingine yanaharibiwa kwa ajili ya matumizi binafsi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali ilifanya juhudi za ziada za kuvitangaza vituo hivi kwani itaongeza idadi ya Watalii wa ndani na wa nje pia. Ni vyema Serikali ikatekeleza mkakati wake wa mwaka 2014/2015 wa kuendeleza vivutio vya mambo ya kale ikiwa ni pamoja na kukarabati jengo la Kalenga, boma la Pangani, kujenga Kituo cha kumbukumbu na Taarifa cha Amboni.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho la Taifa. Shirika la Makumbusho la Taifa lilianzishwa kwa Sheria namba (7) ya mwaka 1980. Shirika hili ni taasisi ya kielimu na kiutamaduni yenye jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti, kuelimisha jamii kwa kutumia maonesho na machapisho kuhusu urithi wa asili na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona taasisi hii inashindwa kutekeleza majukumu yake kwa msingi kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(i) Kutokuwepo kwa Bodi ya Shirika kuanzia mwaka 2011 ambayo inapaswa kusimamia utendaji wa shirika hili.

(ii) Upungufu wa rasilimali watu.

(iii) Uhaba wa vifaa vya kuhifadhia makusanyo na makumbusho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ulimwenguni kote hasa katika nchi zilizoendelea, Makumbusho ya Taifa ni moja kati ya vivutio vikubwa vya utalii. Ni jambo la kusikitisha kwamba Serikali yetu bado haijaona umuhimu wa kuyafanya makumbusho ya Taifa kuwa ni moja ya vivutio vya utalii hapa nchini. Kamati inashauri Wizara kupitia Idara yake ya Utalii na Bodi ya Utalii kutangaza makumbusho ya Taifa sambamba na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, Uchimbanji wa Madini katika Mapori ya Akiba. Tangu kupitishwa kwa Sheria ya Wanyamapori mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa madini, *strategic minerals* kufanyika katika mapori ya akiba tayari Serikali imeruhusu kampuni ya *Mantra* Tanzania kuanza maandalizi ya uchimbaji wa madini aina ya *uranium* katika Pori la Akiba la Selous. Pamoja na kwamba uamuzi huu una tija kwa Taifa, Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kushughulikia suala hili kwa lengo la kuepusha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza baadaye siyo tu kwa binadamu bali pia kwa rasilimali za asili iliyopo katika eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba urani itachibwa na itakwisha lakini maliasili iliyopo ndani ya Pori la Akiba la Selous kama ikitunzwa itakaa pale milele na mapato yatakayopatikana japo kwa kiwango kidogo yataendelea kunufaisha kizazi cha sasa hata watoto wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri wadau wote wanaohusika na mradi huu hususan Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira wahakikishe taratibu zote zinafuatwa kabla ya uchimbaji wa urani kuanza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mipaka limeendelea kuwa changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii, hivyo kuongeza migogoro mikubwa ndani ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa mfano, migogoro inayoendelea katika Pori Tengefu la Loliondo. Migogoro hii ya mipaka inachangiwa na wananchi ama kutokujua mipaka ya maeneo yao au kutumiwa na wanasiasa ili kuendelea kuyatumia maeneo hayo ili hali mipaka inajulikana.

Mheshimwia Spika, kutokana na muda kuwa finyu, naomba taarifa yangu yote hii iingizwe katika *hansard*.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kama ilivyoainishwa hapo awali, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya fedha za maendeleo sh. 14,198,216,000/=, kati ya fedha hizo sh. 5,000,000,000/= tu ndiyo fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zitatumika kwa ajili ya miradi 11.

Mheshimiwa Spika, masuala mengineyo. Yapo masuala mbalimbali ambayo Kamati inaona ni muhimu kuyazungumzia ili kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii. Kumekuwa na matumizi yasiyo endelevu ya maji katika mito inayoingiza maji katika Mto Ruaha Mkuu kutokana na shughuli za umwagiliaji kwenye mashamba ya mpunga katika Wilaya ya Mbarali. Hali hii imepelekea Mto Ruaha Mkuu ambao ni tegemeo kubwa kwa wanyamapori kupungua maji kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Wizara ya Maji kuona namna bora ya kuwa na usimamizi thabiti wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu akisaidiwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Maimuna Tarishi na Naibu Katibu ndugu Selestini Gesimba kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati hii wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Vilevile nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara na ushauri ulifanikisha kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69, kwa mwaka wa fedha 2014/2015. jumla ya sh. 83,119,264,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maliasili na Mazingira kama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Kanuni ya 99 (9) nachukua nafasi hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

1.2 **Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013, Kifungu namba 6(8)na 7(1) kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hii; kuisimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu yake, mnamo tarehe 01/05/2014, Kamati ilikutana na Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na wataalam wa Wizara hiyo na kujadili kwa kina Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka wa 2013/2014, mafanikio na changamoto; pamoja na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014

2.1 **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali katika maeneo mbalimbali ya msingi. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati, japokuwa yapo baadhi ya maeneo ambayo juhudi zaidi zinahitajika katika utekelezaji wake. Maeneo hayo ni pamoja na:-

- Mgawanyo wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii ulenge kuziwezesha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori;

- Serikali ichukue hatua za kupunguza Migogoro ya mipaka kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa ; na

- Operesheni maalum ziendeshwe mara kwa mara ili kukabiliana na tatizo la ujangili wa wanyamapori hususan ujangili wa tembo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

2.2 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaihimiza Serikali kuzingatia na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kuwa na uhifadhi endelevu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014- MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

3.1 MAFANIKIO

3.1.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara ya Maliasli na Utalii iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **75,681,745,000/=.** Kati ya fedha hizo shilingi **64,033,579,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **11,648,166,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2014 Wizara ilikuwa imepokea sh. **29,853,746,222/=** sawa na asilimia **46.62** ya fedha iliyoidhinishwa**.**

3.1.2 **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Machi 2014 Wizara ilipokea jumla ya sh. **29,853,746,222/=.** Kati ya fedha hizo Sh. **7,641,948,312/=** matumizi mengineyo na Sh. **22,211,797,910/=** kwa ajili ya mishahara. Fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida zimeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kufuatilia na kuhakiki ukusanyaji wa maduhuli katika vituo 125;
- Kukamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyama pori.
- Doria 54,574 (mandays) zilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba ambapo watuhumiwa walikamatwa kwa kuhusishwa na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009;
- Kesi 277 zilifunguliwa katika vituo mbalimbali vya polisi na mahakama ambapo kesi 123 zenye watuhumiwa 164 ziliisha kwa watuhumiwa kulipa faini ya Tsh. 75,686,00 na kesi 154 zenye watuhumiwa 227 zinaendelea katika mahakama mbali mbali.
- Imekamilisha mapitio ya Kanuni za wanyamapori wa Taifa, Silaha zinazofaa kwa uwindaji na Leseni maalum ya Uwindaji.
- Kufanya utafiti wa mwenendo wa biashara ya utalii nchini pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za utalii wa ndani na wa kimataifa. Utafiti unaonyesha kwa mwaka 2013 idadi ya watalii imeongezeka kufikia 1,095,884 ikilinganishwa na 1,077,058 mwaka 2012.

3.1.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara ilipanga kutekeleza Mirada 10 ya maendeleo kwa jumla ya Shilingi **11,648,166,000/=** ambazo fedha za nje ni **10,648,166,000/=** na **1,000,000,000/=** fedha za ndani. Mpaka kufikia Machi 2014 shilingi **4,033,801,000/=** zilipokelewa ambapo Sh. **3,858,801,000/=** ni fedha za nje na Sh. **175,000,000/=** ni fedha za ndani.

3.1.4 CHANGAMOTO

3.1.5 **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyoonekana, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni :-

- Uhaba wa fedha hasa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 shilingi **4,033,801,000/=** tu ndio zilitolewa kati ya Sh. **11,648,166,000/=**zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu;
- Uhaba wa watumishi na vitendea kazi kama vile magari ya kufanyia doria na silaha za kisasa hasa katika sekta za Wanyamapori, Misitu na Malikale;
- Uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na mali kale;
- Ushirikiano hafifu wa wadau katika uhifadhi wa maliasili;
- Kubomolewa kwa majengo ya kale yanayostahili kuhifadhiwa hasa mijini;
- Ubovu wa miundombinu katika maeneo yaliyohifadhiwa;
- Ujangili uliokithiri wa wanyamapori;
- Uharibifu wa misitu; na
- Mwamko mdogo wa watanzania wazawa kutembelea vituo vya utalii vya hapa nchini.

3.2.2 **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia kwa kina mikakati ya namna Serikali ilivyojipanga kukabiliana na changamoto hizo na kuona itafaa endapo itasimamiwa na kutekelezwa. Mikakati hiyo ni:-

- Kuendelea kuajiri watumishi wapya kulingana na ikama iliyopitishwa;
- Kuongeza ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii;
- Kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii;
- Kufanya mapitio ya Sera na Sheria;
- Kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji maduhuli; na
- Kuongeza bajeti ya ulinzi, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za maliasili na malikale.

4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015

4.1 **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maliasili na Utalii **Fungu 69**, inaomba kuidhinishiwa Shilingi **83,119,264,000/=** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Jumla ya shilingi **68,921,048,000/=** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo kati ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hizo shilingi **38,293,631,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **30,627,417,000/=** ni kwa ajili ya mishahara.

4.2 **Mheshimiwa Spika**, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya miradi 11 ya maendeleo ni shilingi **14,198,216,000/=** kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi **5,000,000,000/=** na **9,198,216,000/=** fedha za nje.

4.3 **Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/ 2015, Wizara na Taasisi zake inategemea kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **144,608,745,710/=** ikiwa ni pungufu kwa asilimia **24** ikilinganisha na makadirio ya makusanyo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kama inavyofahamika, Sekta ya maliasili na utalii ni mhimili wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwani ina mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia wastani wa asilimia 17.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mchango huo ni mdogo ukilinganisha na fursa nyingi zilizopo hasa katika Hifadhi za Taifa, wanyamapori na malikale**.** Endapo Sekta hii itasimamiwa vizuri na kuendelea kupewa kipaumbele na Serikali katika kutangaza vivutio tulivyonavyo, ni dhahiri kwamba uchumi wa Taifa utaimarika na hatimaye kuondoa kwa kiasi kikubwa tatizo la umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, Ni muhimu na busara kwa Serikali kuhakikisha inalinda na kutetea masilahi ya Taifa letu yanayotokana na Biashara ya Utalii. Habari zilizozagaa nchini kwamba Serikali inataka kufungua lango la Bologonja kuruhusu watalii kutoka hifadhi ya Masai Mara nchini Kenya kuingia Serengeti sio habari njema kwa pato la Utalii kwa nchi yetu. Vivyo hivyo si habari njema kwa kazi za uhifadhi lakini pia kwa wafanyabisahra wa sekta hiyo hapa nchini.
Mheshimwia Spika, Kamati inaishauri Serikali kuachana na Mpango huo kama upo kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uwindaji pia ni miongoni mwa Sekta ambazo zimekuwa zikiliingizia taifa letu, pesa nyiingi za kigeni.

Habari kwamba vitalu vya uwindaji karibu kumi, vya madaraja mbalimbali vimerudishwa baada ya waliopewa kushindwa kuendesha biashara hiyo sio nzuri kwani zimesababisha mapato ya Taifa kupungua.

Kwa kuwa sababu zinazotolewa za kurejeshwa vitalu hivyo ni pamoja na vitalu hivyo kuvamiwa na mifugo, idadi ya wanyama kupungua lakini pia uwezo wa waliokabidhiwa vitalu hivyo kufanyabiashara hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya kina kuhusu hali hiyo lakini pia kupitia upya Sheria ya wanyamapori kuona kama pia imechangia hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

5.1 BIASHARA YA UTALII

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii (TTB), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwa pamoja wameonesha juhudi za wazi za kutangaza utalii wa Tanzania. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka kwa kutoka watalii 1,077,058 mwaka 2012 hadi kufikia 1,095,884 mwaka 2013.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu ilipofanya ziara katika Hifadhi za kusini (Katavi, Kitulo na Ruaha) ilibaini kwamba hifadhi hizi hazijatangazwa vya kutosha, hivyo kuwa na idadi ndogo ya watalii ukilinganisha na Hifadhi za Kaskazini. Kamati ilijulishwa kwamba, kutotangazwa kwa hifadhi hizi kunachangiwa na fedha ndogo zinazotengwa kwa ajili ya utangazaji wa Hifadhi.

  Aidha katika ziara hiyo, Kamati ilibaini ubovu wa miundombinu kuelekea katika hifadhi, jambo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa biashara ya utalii. Barabara nyingi hazipitiki kwa urahisi, kwa mfano; barabara ya kutokea Mbeya kwenda Rukwa na hatimaye Katavi, na ile ya kutokea Iringa mjini kuelekea katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

  Kutokana na ubovu huo wa miundombinu, gharama za usafiri mpaka hifadhini zimekuwa ni kubwa mno kiasi cha kuwakatisha tamaa watalii kutembelea maeneo hayo. Kwa mfano; gharama ya usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupitia Pori la Akiba la Selous na kurudi humgharimu mtalii mmoja dola za Marekani takribani 700 -1000.

  Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vyema sasa Serikali ikaongeza juhudi katika kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege vilivyopo ndani na nje ya hifadhi hasa katika mikoa ya kusini, ili kwanza kupunguza gharama za usafiri na pia kuwezesha shughuli za kitalii kufanyika katika msimu wowote wa mwaka tofauti na sasa ambapo shughuli hizo husimama wakati wa masika;

  Aidha, TANAPA ifanye jitihada za ziada katika kutangaza vivutio vya utalii katika Hifadhi za Taifa zilizopo katika mikoa ya Kusini kwani kuna hazina za kipekee katika hifadhi hizo ikiwa ni pamoja na 'bustani ya Mungu' ya Kitulo na Tembo weusi wa Katavi.

- **Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine inayochangia idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu kuwa ndogo, ni uchache wa vyumba vya kulala watalii katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba uchache huu wa mahoteli katika maeneo ya Hifadhi unachangiwa na baadhi ya wafanyabiashara waliopewa maeneo ya kujenga, kutoyaendeleza maeneo kwa muda mrefu. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Makampuni 11 ambayo yalipewa maeneo ya kujenga kuanzia mwezi Juni, 2009 ikiwa ni miaka takribani minne iliyopita, hayajaanza ujenzi hadi sasa.

- **Mheshimiwa Spika,** Kamati vilevile inashauri kwamba, kwa kuwa Mwaka 2002 Serikali ilijiwekea lengo la kufikisha watalii milioni moja ifikapo mwaka 2010, na kwa kuwa tayari lengo hilo limefikiwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali ijiwekee lengo jipya la idadi ya watalii watakaoingia nchini hasa kwa kuzingatia mazingira ya sasa ambapo matangazo ya vivutio vya utalii nchini yamefika katika nchi nyingi zaidi duniani ukilinganisha na mwaka 2010. TTB

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

iwezeshwe kuwa na timu ya wataalam wenye weledi kaitak uwanja wa masoko na Utalii.

5.2 UTALII WA NDANI

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza watanzania kwa kuanza kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii nchini. Hata hivyo, kasi hii ya utalii inakwamishwa na gharama kubwa za malazi hasa katika Hifadhi za Taifa. Gharama hizi zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukweli kwamba hoteli nyingi katika hifadhi za Taifa zinamilikiwa na Kampuni za kigeni.

Kamati inaishauri Wizara kutoa kipaumbele kwa Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza katika ujenzi wa maeneo ya malazi ndani ya hifadhi kwa maana ya hoteli za kitalii, mabanda (cottages), maeneo ya kupiga mahema kwa watu wote (public campsites) na kwa watu maalum(Special campsites).

5.2 IDARA YA WANYAMAPORI

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya mwaka uliopita wa 2012/2013 kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilizungumzia ujangili wa wanyamapori kama changamoto kubwa katika Idara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitika kuona kwamba bado ujangili umeendelea kuwa changamoto kubwa katika mapori yote ya akiba, na hakuna dalili yoyote inayoonesha kupungua kwa changamoto hii kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kuchelewa kuhukumiwa na kuharibiwa kwa kesi za ujangili;
- Upungufu wa rasilimali watu hasa askari wa wanyamapori;
- Upungufu na ubovu wa magari ya doria; na kubwa zaidi ni
- Kukosekana kwa silaha za kisasa kwa ajili ya kukabiliana na majangili ambao wengi hutumia silaha za kisasa za kivita

Mheshimiwa Spika, Ni jambo la kusikitisha kwamba pamoja na nchi yetu kubarikiwa kwa kuwa na hazina kubwa ya wanyamapori, bado Serikali haijaipa kipaumbele na umuhimu unaostahili. Kamati inaona kwamba, japokuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeonesha nia ya wazi ya kukabiliana na ujangili, hivyo kununua silaha kwa ajili ya kufanikisha hilo, Serikali hiyo hiyo kupitia Wizara ya Fedha (TRA) ilizuia silaha hizo bandarini ikidai kodi kwa zaidi ya mwaka mmoja na hatimaye kuzitoza kodi ya Sh.197, 880,546/= silaha hizo. Jambo la kusikitisha, wakati TRA inashikilia silaha hizo, tembo wan chi hii waliendelea kuteketezwa.Fedha ambayo TRA ilikuwa inadai kama kodi Sh 197,880,546/= ni sawa na thamani ya meno ya tembo wanaouawa kwa siku moja. Sote tunafahamu tatizo moja linalowakabili maaskari wa wanyamapori ni upungufu wa silaha za kisasa kupambana na majangili.

Mheshimiwa Spika, Lingine la kusikitisha ni TRA kutoza kodi FARU wanaoletwa nchini kama msaada na Wahisani kwa ajili ya kurejesha Nchini wanyamapori hao ambao walikaribia kutoweka. FARU hao ni pamoja na walewaliotolewa kama msaada walioko katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi na Serengeti.Kodi ambayo TRA imekuwa ikitoza kwa kila FARU ni 630,000.

Mheshimiwa Spika, Taasisi kama TRA haioni wala kutambua jitihada za mkono mwingine wa Serikaliza kuokoa rasilimali hii ya Taifa inayoendelea kupotea siku hadi siku. Kwa lugha nyingine, TRA kuendelea kutoza kodi FARU waliotolewa msaada na wahisani ni kushawishi wahisani wasitishe misaada yao. Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kuondoa kodi kwa wanyama FARU na vifaa vingine vinavyotolewa na wahisani kwa ajili ya uhifadhiwa FARU na vile vinavyohusika na kujenga mazingira mazuri ya FARU kuishi kama magari, magreda pamoja na silaha za kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuajiri askari wa wanyamapori wa kutosha. Idadi iliyopo haitoshi na wala haikidhi mahitaji na changamoto zilizopo. Kwa mfano, Pori la Akiba la Rukwa/Lukwati/ Lwafi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 9568.26 lina jumla ya watumishi arobaini na tano (45) tu. Hali ni mbaya zaidi katika mapori karibu yote ya akiba ikiwa ni pamoja na Pori la AKiba la Selous ambalo lina ukubwa wa zaidi ya kilomita za mraba 50,000 likiwa na watumishi wasiozidi 250.

Kamati inashauri kwamba**,** Ili kurejesha hali ya utulivu katika mapori yote ya Akiba, Serikali inatakiwa kuajiri askari wa wanyamapori wasiopungua 1000;

Mheshimiwa Spika, Aidha, ili kuimarisha ulinzi katika mapori ya Akiba nchini ni vyema Serikali ikatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kununua magari ya doria kwani yaliyopo sasa ni machache ukilinganisha na ukubwa wa mapori.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yaliyojitokeza, Kamati Inaipongeza Serikali kwa kuendesha Operesheni Tokomeza kwa lengo la kuwalinda wanyamapori wetu.Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka tathimini ya madhara yaliyosababishwa na Operesheni Tokomeza ili awamu ya pili iweze kufanyika. Aidha Kamati inaishauri Serikali kutekeleza maazimio yote ya Bunge kuhusu utekelezaji wa Operesheni Tokomeza na kutoa taarifa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la kuchelewa kutolewa hukumu na wakati mwingine ushahidi wa kesi za ujangili kuharibiwa ni changamoto kubwa katika mapori ya akiba na Hifadhi za Taifa, Kamati inatoa rai kwa vyombo vya Serikali kama vile Jeshi la Polisi na Mahakama kushirikiana na Idara ya wanyamapori kuhakikisha watuhumiwa wa kesi za ujangili wanashtakiwa na kupewa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria. Kamati haipendi kuamini kuwa kesi hizi zinahujumiwa kutokana na askari polisi na mahakimu wachache kujihusisha na vitendo vya rushwa katika kusimamia kesi hizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu kwa Pori la Akiba la Selous kubakiza asilimia 50 ya mapato yake (retention). Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kutoa *retention* ya asilimia 100 kwa mapori yote ya akiba ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuimarisha doria katika mapori**.** Kiwango hicho cha *retention* ya asilimia 50 hakitoshi kuyaweka mapori ya akiba katika hali nzuri hasa ya ulinzi na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali ya kukamilisha kuandaa maandalizi ya uanzishwaji wa Mamlaka ya wanyamapori Tanzania pamoja na rasimu ya muundo na uendeshaji wa Mamlaka hiyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato huo ili Mamlaka hiyo ianze kufanya kazi mara moja. Kamati inaamini kwamba Kuanzishwa kwa Mamlaka hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa mianya ya rushwa, ufujaji wa mapato na ufisadi uliopo katika idara hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

5.2.1 UJANGILI WA TEMBO

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ujangili wa tembo umekuwa ni janga la kitaifa. Ni ukweli usiofichika kwamba leo hii si tu tembo wanauwawa bali wanateketezwa. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Taasisi za Utafiti wa Wanyamapori za Serikali na mashirika hapa nchini, takwimu zinazoshabihiana na za taarifa za utafiti wa kimataifa zinaonesha kwamba tembo wasiopungua 30 wanauwawa kwa siku, 850 kwa mwezi na tembo 10,000 kila mwaka (TAWIRI, 2011).

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi kubwa ya kuuwawa kwa tembo, taarifa za kitaalam kutoka TAWIRI zinathibitisha kwamba idadi ya tembo imepungua kutoka tembo 109,000 mwaka 2009 na kufikia tembo chini ya 70,000 mwaka 2012. Endapo kasi hii ya ujangili wa tembo itaendelea bila kudhibitiwa mara moja, ni wazi kuwa tembo watakuwa wametoweka nchini katika kipindi cha miaka 7 ijayo.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni ya hatari na ni aibu kwa nchi yetu ambayo ni ya pili barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo. Kamati inachukua fursa hii kumpongeza DKT Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake binafsi za kudhibiti ujangili wa Tembo ambapo amewezesha Tanzania kupewa msaada wa Ndege na Helikopta zitakazosaidia kupambana na ujangili.Tunamuomba azidi kuisaidia sekta hii ili urithi huu udumu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

5.3 IDARA YA MAMBO YA KALE

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi maarufu zenye hazina kubwa ya malikale. Malikale zilizopo ni pamoja na majengo ya zamani yaliyojengwa kwa matumbawe katika miji ya Pwani, Michoro ya kale, mapango ya Amboni, Nyayo za zamadamu aliyeishi miaka milioni 3.6 iliyopita na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba nchi nyingi duniani hupata mapato makubwa kutokana na utalii unaotegemea vivutio vya kitalii. Hata hivyo, Serikali yetu bado haijafanikiwa kuliingizia taifa letu pato la kuridhisha kutokana na utalii wa malikale.
Maeneo mengi yenye vivutio vya aina hii ya utalii ni kama yamesahauliwa kwani hayatangazwi vya kutosha, hayana usimamizi unaotakiwa na sehemu nyingine yanaharibiwa kwa ajili ya matumizi binafsi ya wananchi**.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Serikali ifanye juhudi za ziada za kuvitangaza vivutio hivi kwani itaongeza idadi ya watalii wa ndani na wa nje pia. Aidha, ni vyema Serikali ikatekeleza mkakati wake kwa mwaka 2014/2015 wa kuendeleza vivutio vya mambo ya kale ikiwa ni pamoja na kukarabati Jengo la Kalenga, Boma la Pangani na kujenga Kituo cha kumbukumbu na taarifa cha Amboni**.**

5.3.1 SHIRIKA LA MAKUMBUSHO YA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 7 ya Mwaka 1980. Shirika hili ni taasisi ya kielimu na kiutamaduni yenye jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kuelimisha jamii kwa kutumia maonesho na machapisho kuhusu urithi wa asili na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona Taasisi hii inashindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa Bodi ya Shirika kuanzia Novemba 2011 ambayo inapaswa kusimamia utendaji wa Shirika;
- Upungufu wa rasilimali watu;
- Uhaba wa vifaa vya kuhifadhia makusanyo ya makumbusho mbalimbali; na
- Bajeti/ruzuku inayotengwa kutopatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ulimwenguni kote, hasa katika nchi zilizoendelea, makumbusho ya Taifa (museums) ni moja kati ya vivutio vikubwa vya watalii. Ni jambo la kusikitisha kwamba Serikali yetu bado haijaona umuhimu wa kuyafanya makumbusho ya Taifa kuwa ni moja ya vivutio vya utalii hapa nchini. Kamati inashauri Wizara kupitia Idara yake ya Utalii na Bodi ya Utalii kuitangaza makumbusho ya Taifa sambamba na sekta nyingine za utalii;

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuteua Bodi ya Shirika la Makumbusho ambayo Kamati inaamini kuwa itaweza kushughulikia kwa ufanisi changamoto zote zinazolikabili Shirika.

5.4 UCHIMBAJI WA MADINI KATIKA MAPORI YA AKIBA

Mheshimiwa Spika, Tangu kupitishwa kwa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa madini (Strategic Minerals) kufanyika katika mapori ya akiba, tayari Serikali imeruhusu Kampuni ya Mantra Tanzania Limited kuanza maandalizi ya uchimbaji wa madini aina ya Urani katika Pori la Akiba la Selous.

Pamoja na kwamba uamuzi huu una tija kwa taifa, Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kushughulikia suala hili kwa lengo la kuepusha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza baadae sio tu kwa binadamu bali pia kwa rasilimali ya asili iliyopo katika eneo hilo la hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba urani itachimbwa na itaisha, lakini maliasili iliyopo katika Pori la Akiba la Selous kama ikitunzwa itakaa pale milele na mapato yatakayopatikana japo kwa kiwango kidogo yataendelea kunufaisha vizazi vya sasa na hata vya watoto wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri wadau wote wanaohusika na mradi huu hususan Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira wahakikishe taratibu zote zinafuatwa kabla ya uchimbaji wa Urani kuanza.

5.5 TATIZO LA MIPAKA KATI YA VIJIJI NA HIFADHI ZA TAIFA/ MAPORI YA AKIBA NA TENGEFU

Mheshimiwa Spika, Tatizo la mipaka limeendelea kuwa changamoto katika sekta ya maliasili na utalii, hivyo kuongeza migogoro kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa mfano migogoro inayoendelea katika Pori tengefu la Loliondo; wakulima/wafugaji wa kijiji cha Kikondo na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo; wahamiaji katika ghuba ya Speke; na wafugaji wa Ihefu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii ya mipaka inachangiwa na wananchi ama kwa kutojua mipaka ya maeneo yao au kutumiwa na wana siasa ili kuendelea kuyatumia maeneo hayo ilihali mipaka inajulikana wazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuchukua hatua za ziada na za haraka ili ufumbuzi wa migogoro hii upatikane na hatimaye kuendeleza mahusiano mema katika ya vijiji na Mamlaka zinazosimamia maeneo yaliyohifadhiwa.

Aidha, Kamati inaitaka Serikali kusimamia na kutekeleza kwa hali na mali wajibu wake wa kikatiba wa kusimamia, kuendeleza na kulinda maeneo yote yaliyo hifadhiwa yenye umuhimu wa kitaifa.

5.6 UHARIBIFU WA MISITU

Mheshimiwa Spika, Suala la uharibifu wa misitu limeendelea kuwa changamoto kubwa inayoikabili sekta ya misitu Tanzania. Uharibifu huu unatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na :-

- Uvamizi wa misitu hasa wafanyabiashara haramu wa kuni, mkaa, mbao na nguzo; na

- Uhaba wa rasilimali watu kuweza kusimamia hifadhi za misitu kwa ufanisi na uaminifu.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi za misitu ya Mkungunero, Kazimzumbwi na Ruvu Kusini ni mifano halisi ya misitu inayoendelea kuharibiwa kwa kasi na wavamizi hasa wafanyabiashara haramu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa misitu katika kutunza mazingira, vyanzo vya maji, na kupunguza hewa ukaa ni muhimu Serikali ikasimamia Sheria zake na kuhakikisha misitu haivamiwi na kuharibiwa ovyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wakala wa Misitu kuchukua hatua za haraka kudhibiti ujangili wa misitu kwa kushirikiana na vyombo binafsi na Asasi nyingine za Kiraia.

5.7 FEDHA KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoainishwa hapo awali, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya fedha za maendeleo **Tsh. 14,198,216,000/=** Kati ya fedha hizo, shilingii **bilioni 5** tu ndio fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zitatumika kwa ajili ya Miradi 11.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuacha kutegemea fedha za wahisani ambazo upatikanaji wake huwa mgumu. Tunaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ndani kufikia **billion 5** ikilinganishwa na **billion moja** mwaka **2013/2014**. Kiwango hiki bado ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba miradi muhimu kama ya kuziwezesha jamii kupata mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu, **MKUHUMI** na tabia nchi haitatekelezeka kama tukiendelea kutegemea fedha za nje. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo.

5.8 MASUALA MENGINEYO

Mheshimiwa Spika, yapo masuala mbalimbali ambayo Kamati inaona ni muhimu kuyazungumzia ili kuimarisha sekta ya Maliasili na Utalii. Masuala hayo ni pamoja na:-

- Kumekuwa na matumizi yasiyo endelevu ya maji katika mito inayoingiza maji katika mto ruaha mkuu kutokana na shughuli za umwagiliaji kwenye mashamba ya mpunga katika Wilaya ya Mbarali; Hali hii imepelekea mto Ruaha mkuu ambao ni tegemeo kubwa kwa wanyamapori, kupungua maji kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira na Wizara ya Maji (hususan Rufiji Water Basin) kuona namna bora ya kuwa na usimamizi thabiti wa vyanzo vya maji na rasilimali maji;

- Kumekuwa na changamoto ya kujaa kwa tope kunako hatarisha uwepo wa baadhi ya maziwa nchini ikiwa ni pamoja na Ziwa Manyara na Ziwa Katavi. Kamati inaishauri TANAPA kuweka mikakati ya kuyanusuru maziwa haya ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii kuhusu athari za matumizi ya ardhi yasiyo endelevu kama vile kilimo cha kwenye miinuko;
- Serikali ioneshe juhudi za wazi za kufungua ushoruba wa mapito ya wanyamapori wa Ngorongoro-Ziwa Manyara- Tarangire ili wanyama waendelee kupita katika njia zao za asili;
- Kwa kuwa wananchi wameendelea kufanya shughuli za kiuchumi kama vile kilimo na ujenzi wa makazi ya kudumu kwenye Ghuba ya Speke, na kwa kuwa eneo hili ni pori tengefu Kisheria kwa ajili ya mapito ya wanyamapori kwenda kunywa maji hususani wakati wa kiangazi; Serikali ione namna bora ya kuwahamasisha wananchi kuridhia kuhama kutoka katika eneo hilo na ikibidi maamuzi magumu yafanyike;

- Kwa kuwa maslahi ya *tour guides* na wabeba mizigo wanaofanya kazi katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro(KINAPA) na mlima Meru ni madogo, Kamati inashauri Serikali kupitia wizara ya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ione ulazima wa kuboresha maslahi yao kwa mujibu wa Sheria kulingana na ugumu wa kazi wanazofanya;

- Kwa kuwa Bodi ya Utalii ndio mtangazaji mkuu wa utalii ndani na nje ya nchi,ili kuiwezesha Bodi hii kumudu majukumu yake, ni vema Serikali ikatambua umuhimu wa kuifanya Bodi kuwa Mamlaka ili iweze kujikusanyia mapato yake yenyewe. Hii itasaidia taasisi hii kujiendesha bila kutegemea bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo mara nyingi imekuwa haitoshelezi;Serikali iangalie uwezekano wa kuinusuru Bodi ya Utalii kutokana na madeni makubwa yanayokaribia Tsh.Bilioni 5.

- Kwa kuwa Pori la Akiba la msitu wa Pande (Pande Forest Reserve) linaweza kuboreshwa na kuwa kivutio kingine cha utalii, Serikali ione umuhimu wa kuboresha na kuliendeleza Pori hili kuwa hifadhi ya wanyama pori.

- Kwa kuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani kuna Kiwanda cha Chumvi cha Sea Salt Company Limited, na kwa kuwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) inathibitisha uwepo wa shughuli za kiwanda hicho ndani ya hifadhi unahatarisha uhifadhi endelevu, na kwa kuwa uchimbaji wa chumvi hifadhini ni kinyume cha Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 inayoruhusu uchimbaji wa *strategic minerals* tu, Kamati inaishauri Serikali kutokuingia mkataba na kiwanda hicho mara mkataba wa sasa utakapomalizika mwaka 2017;

- Serikali ione umuhimu wa kuharakisha uteuzi wa Bodi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro,Hifadhi za Taifa, Chuo cha wanyamapori Mweka na taasisi nyingine zilizoko chini ya Wizara hii. Mamlaka ya Ngorongoro kwa mfano imekuwa ikijiendesha bila Bodi kwa karibu mwaka mmoja na nusu. Bodi ya zamani ilimaliza muda wake mwishoni mwa 2012.

- Mwisho lakini si kwa umuhimu, Ni rai ya Kamati kuwa wabunge na viongozi wa nchi katika ngazi mbalimbali watembelee vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini ikiwa ni pamoja na kupanda mlima Kilimanjaro. Kwa kufanya hivyo si tu tutakuwa tunatangaza utalii ambao utaliongezea Taifa letu mapato, bali pia kuenzi hazina aliyotupa Mwenyezi Mungu.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, (Mb) akisaidiwa na Mhe. Mahamoud Mgimwa (Mb); na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Maimuna K. Tarishi na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Selestini Gesimba, kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati hii wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014, na makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara na ushauri uliofanikisha kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue Wajumbe wa hao wa Kamati kwa majina:-

1. Mhe. James Daudi Lembeli, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe.Abdulkarim E.H. Shah, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Mb Mjumbe
4. Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi , Mb "
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb "
6. Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mb "
7. Mhe. Muhamad Amour Chomboh, Mb "
8. Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb "
9. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb "
10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb "
11. Mhe. Amina Andrew Clement, Mb "
12. Mhe. John John Mnyika, Mb "
13. Mhe. Salim Hassan Turky, Mb "

14. Mhe. Abuu Hamoud Jumaa, Mb "
15. Mhe. Kisyeri Werema Chambiri, Mb "
16. Mhe. Al-Shymaa Kwegyr, Mb "
17. Mhe. Benedict Ole Nangoro, Mb "
18. Mhe. MwanaKhamis Kassim Said, Mb "
19. Mhe. Waride Bakar Jabu, Mb "
20. Mhe. Dkt Henry Daffa Shekifu,Mb "
21. Mhe. Clara Diana Mwatuka, Mb "
22. Mhe. Haji Khatibu Kai, Mb "

Mheshimiwa Slpika, vilevile napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati Ndg Gerald Magili akisaidiwa na Ndg. Lukindo Choholo, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, **Fungu 69** kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, jumla ya shilingi bilioni **83, 119, 264,000/=.**

Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.**

James Daudi Lembeli, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA
14 Mei, 2014

SPIKA: Sasa nimwite msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa! *(Makofi)*

Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maliasili na Mazingira Kama ilivyosomwa Bungeni

MHE. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, *Frank Herbert* aliwahi kusema;

"Utawala bora, kamwe hautegemei Sheria bali sifa binafsi za wale wanaotawala. Vyombo vya Serikali mara zote vipo chini ya wale wanaowaongoza. Kwa hiyo, sifa muhimu ya Serikali ni namna ya kuteua/kuchagua viongozi"

Serikali ya Awamu ya Nne, imeshindwa kuwajenga viongozi wake katika misingi bora na ndio maana pamoja na matatizo ya kimfumo, Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea

kubadilisha viongozi na matokeo ya ufanisi wake yamekuwa ni kioja na dhihaka katika utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maazimio 16 ya Bunge. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ililileta Bungeni Taarifa yake tarehe 20 Disemba, 2013 iliyowasilishwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa James Lembeli kuhusu uchunguzi wa matatizo katika utekelezaji wa Operesheni Tokomeza Ujangili, iliyokua na maazimio kumi na sita (16). Taarifa hiyo ndiyo iliyomwondoa aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Khamis Kagasheki na Mawaziri wengine.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya maazimio ya Bunge, yaliyoongezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni pamoja na kuundwa kwa Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama. Aidha, ni takribani miezi zaidi ya mitano kupita tangu Serikali iahidi Desemba mwaka jana, kuahidi, kupitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuunda Tume maalum ya kuchunguza kilichotokea wakati wa Operesheni Tokomeza Ujangili. Katika makujukumu yake, Tume hiyo imepewa kazi zifuatazo:-

(a) Kuchunguza na kubaini Operesheni Tokomeza ilivyoendeshwa;

(b) Kuchunguza na kubaini iwapo sheria, kanuni, taratibu na hadidu za rejea zilifuatwa na watu waliotekeleza operesheni hiyo;

(c) Kuchunguza na kubaini kama kuna mtu aliyekiuka sheria, taratibu na hadidu za rejea wakati wa operesheni;

(d) Kuchunguza na kubaini kama kuna watu ambao walikiuka sheria yoyote wakati wa utekelezaji wa operesheni hiyo na kupima kama hatua zilizochukuliwa dhidi yao au mali zao zilikuwa stahiki;

(e) Kupendekeza hatua zozote zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya mtu ambaye atabainika alikiuka sheria, taratibu na hadidu za rejea pamoja na kupendekeza mambo ya kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kutekeleza operesheni nyingine siku zijazo ili kuepuka kasoro.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuundwa kwa Tume hii, lakini Serikali haikupaswa tena kuipa Tume kazi mpya katika maeneo yote bali yale yaliyohitaji ushahidi wa ziada wa kijinai. Hii ni kwa sababu makosa mengine yako wazi ambayo Serikali ilipaswa iwe imeshachukua hatua badala ya kusingizia inasubiri taarifa ya Tume. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, sasa inaitaka Serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Wizara ili maazimio ya Bunge hili yasiishie kabatini kama ilivyokuwa kwa mengine ya miaka ya nyuma na ilivyozoeleka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uwajibishwaji wa Watendaji kutokana na Maazimio ya Bunge. Aidha, katika azimio namba Saba (7), Bunge liliazimia pia kumwajibisha Mkurugenzi wa Wanyamapori Profesa Alexander Songorwa kwa kutoa taarifa zisizo sahihi kwenye vyombo vya habari na kuudanganya umma kuhusu mazingira na kifo cha Emiliana Marrow wa Babati.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza Waziri wa Maliasili na Utalii wa sasa, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ambaye akiwa katika nafasi yake ya Unaibu Waziri, kipindi hiki kifupi tu kabla ya uteuzi wake, kwa kasi ya ajabu aliandaa mikutano mingi na ziara mbalimbali

huku akiandamana na lundo la vyombo vya habari kama kumbikumbi na kutoa matamko makali dhidi ya ujangili na watumishi wasio waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akiwa katika ziara hizo, aliwahi kuikandia sana Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Ardhi na Maliasili iliyoongozwa na Mheshimiwa James Lembeli, huku akidai kuwa ilikuwa ya uwongo mtupu. Hata hivyo, baada ya kubanwa zaidi, alikana kutoa kauli za kuikosoa ripoti hiyo ya Kamati. Sababu za kwa nini akanushe maneno aliyoyasema zaidi ya mara nne, inabakia kuwa siri yake mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshiimwa Waziri Nyalandu alitoa taarifa za kuwavua nyadhifa zao Mkurugenzi Mkuu wa Wanyamapori na Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Matumizi Endelevu ya Wanyamapori. Mhehsimiwa Nyalandu anadai kuwa moja ya sababu za kuwaondoa, ni kutekeleza maazimio ya Kamati ya Lembeli kutokana na kutowajibika wakati wa Operesheni Tokomeza.

Jambo la kujiuliza, kama aliwahi kusema kuwa taarifa ya Kamati ni ya uongo mtupu, je ni lini amethibitisha kuwa kile alichodai kwamba ni uwongo, ulikuwa ukweli? *(Makofi)*

Cha ajabu, aliyeteuliwa kukaimu nafasi ya Ukurugenzi, Paul Sarakikya, aliyekuwa kiongozi wa utekelezaji wa operesheni tokomeza na aliyehusika moja kwa moja na kinachodaiwa kuwa uvunjifu wa haki za binadamu, ndiye amepewa nafasi ya kukaimu Ukurugenzi! Wote tunafahamu ukiukwaji mkubwa wa haki za binaadamu na ukatili uliofanywa katika Operesheni Tokomeza kiasi cha kusababisha Mawaziri wanne kuwajibishwa kwa kutenguliwa nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ilitumia vigezo gani kumteua Sarakikya kukaimu nafasi ya Ukurugenzi wa Wanyamapori huku ikijua alivyoshindwa kutokomeza ujangili hapa nchini na jinsi aliyoendesha operesheni tokomeza ujangili iliyokuwa imejaa dhuluma, uporaji, utesaji na udhalilishaji wa wananchi. Jambo ambalo liliishangaza zaidi Kambi Rasmi ya Upinzani ni kitendo cha Mheshimiwa Waziri Nyalandu kumteua Ndugu Sarakikya kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori huku akijua kuwa Sarakikya alifanya makosa mengi katika utendaji wake wa kazi katika Idara hiyo ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia kuwa Ndugu Sarakikya ndiye aliyeongoza kikosi cha kuzuia ujangili hata kabla ya Operesheni Tokomeza. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishika nafasi ya kwanza kati ya nchi nane duniani zilizoongoza kwa matukio ya ujangili. Aidha, ili kuonesha kwamba Serikali hii haizingatii weledi katika utendaji, alietuliwa tena kusimamia Operesheni Tokomeza!

Mheshimiwa Spika, kauli tata za Serikali juu ya kufukuzwa kazi kwa Wakurugenzi. Mara baada ya Mheshimiwa Waziri kutangaza kuwavua nyadhifa zao Wakurugenzi hao tarehe 24 Februari, 2014, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Bi Maimuna Tarishi aliwarudisha kazini Wakurugenzi hao huku Serikali nayo kwa kupitia Kurugenzi ya Habari Maelezo ikitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwa taarifa za kufukuzwa kwa Wakurugenzi hao si sahihi. *(Makofi)*

Pia, Ikulu kwa kupitia Katibu Kiongozi, Balozi Ombeni Sefue, ilitoa tamko la kuitaka Wizara kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma za kumfukuza mtumishi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, Kifungu cha IV(23)(2) inayozungumzia mamlaka ya Rais kumwondoa mtumishi aliyemteua kazini, amri ya kumfukuza mtumishi wa umma itatekelezwa iwapo:-

(a) Hati ya mashtaka imeandikwa dhidi yake;

(b) Mtumishiwa umma amepewa nafasi ya kujibu mashtaka hayo;

(c) Maombi yametolewa kwenye hati ya mashtaka kwa mujibu wa taratibu zilizo chini ya kifungu namba 34.

Swali la kumuuliza Mheshimiwa Waziri Nyalandu, je, hatua hizi zilifuatwa katika kuwasimamisha kazi Wakurugenzi hawa? *(Makofi)*

Je, maamuzi yake ya kumfukuza Profesa Songoro katika vikao vya Kamati na kumdhalilisha hata baada ya Ikulu kutoa maagizo ya Wizara kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za kufukuza watumishi kazi ni utawala bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali na Wizara kuhakikisha kuwa, uamuzi wowote uliofanywa na kuendelea kufanywa katika kutekeleza maazimio ya Bunge katika kuwawajibisha watumishi hao uzingatie sheria, taratibu na kanuni kwa kuwa Sheria na Kanuni hizo zinaeleza wazi hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

Vile vile, tunasikitishwa na mvutano baina ya Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, hali ambayo inaonesha kuwa kuna mgongano aidha wa kimaslahi na hivyo kuthibitisha kuwa Serikali ni dhaifu kwa kuwa, Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara moja wanafanya kazi bila kushirikiana na kila mmoja akionekana kumvizia mwenzake hadharani badala ya kukaa kwa pamoja kutekeleza maazimio ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, mvutano huu pia ni ishara kuwa, maazimio ya Bunge yanaendelea kupuuzwa na Serikali kwa kigezo cha kuzingatia sheria na kanuni huku zikiwaacha watumishi wenye tuhuma wakihamishwa vitengo na idara na kuendelezea urasimu uleule hata uko wanapohamishwa.

Mheshimiwa Spika, taswira ya Taifa katika Jumuiya za Kimataifa. Kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani imeendelea kutoa taarifa kwa Serikali juu ya mtandao wa Kimataifa wa ujangili ambao pia unahusisha Viongozi Waandamizi wa Serikali, Maafisa Usalama wa Taifa, Wanajeshi, Wafanyabiashara wakubwa, Polisi, Wanasiasa, Ikulu na Watumishi wa Umma. Serikali ya CCM imekua ikitoa kauli za kubeza pamoja na majibu mepesi ya tuhuma hizi huku tatizo la ujangili likiendelea kulichafua Taifa katika Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza baada ya gazeti la *Mail on Sunday* la nchini Uingereza kutoa taarifa kuwa biashara ya ujangili inahusisha watu wa karibu na Rais wakiwemo wanasiasa, maafisa wa Serikali na wafanya biashara wakubwa, Serikali ilitoa matamko mbalimbali pamoja na kulaani taarifa za gazeti hilo na hatimaye Waziri Nyalandu, alimwalika mwandishi wa gazeti hilo kujionea mwenyewe shughuli za Serikali za kupambana na ujangili ikiwemo kutembelea ghala la kuhifadhia pembe za ndovu zilizokamatwa.

Mwaliko huo ulikua ni katika kuthibitisha kuwa Serikali ya CCM haina la kuficha, lakini katika hali ya kushangaza, uchunguzi na taarifa zaidi umeonesha kuwa ndani ya miaka minane (8) Serikali ya CCM, imekuwa ikiomba kibali bila mafanikio kutoka *CITES (Convention on International Trade on Endangered Species)* cha kuuza shehena ya pembe za ndovu takribani 34,000 zenye uzito wa tani 125 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 150 sawa na shilingi bilioni 244.5

Mheshimiwa Spika, Jumuia ya Kimataifa imeshangazwa na kitendo cha Tanzania kuomba kibali cha kuuza shehena iliyokamatwa ya pembe za ndovu kwa kuwa ni biashara haramu na kitendo cha Serikali kuomba kuyauza ni sawa na kuchochea ujangili zaidi kwa kuwa hali hii itaongeza uhitaji wa pembe za ndovu kwenye soko haramu nchini China. Jambo hili ni aibu kubwa kwa Taifa kuomba kufanya biashara haramu kwa kuwa imelidhalilisha Taifa. Hii ni sawa na Serikali ikamate madawa ya kulevya, halafu iamue kuyauza ili kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuiteketeza shehena ya meno ya pembe za ndovu, kama ishara ya kupinga vitendo vya ujangili na kuwa Serikali ya vitendo siyo ya maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Waziri wa Maliasili na Utalii kumwalika nchini mwandishi aliyesemwa kuwa ametoa taarifa za uongo na kulichafua Taifa, ili ajithibitishie kuwa Tanzania ni safi katika matukio ya ujangili, Bwana Martin Fletcher, na kumtembeza katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa na nia ya kumfunga mdomo *(damage control)*. Haikusaidia bali ilivumbua uchafu mwingi na huu wote umewekwa wazi katika vyombo vya habari vya Kimataifa na kuendelea kuonesha uozo wa Serikali katika kushughulikia tatizo la ujangili nchini.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kuwa Rais ameshindwa kusimamia suala hili vizuri kwa kuwa wanaohusika na ujangili ni watu wake wa karibu ama rafiki zake. Aidha, taarifa hizo zimeendelea kubana kauli za Waziri Nyalandu za kuwa anawafahamu majangili kwa majina na kuwataka majangili hao kuacha ujangili ama atawachukulia hatua za kisheria.

Maswali yanayoulizwa, je, ni kwa nini Waziri hawataji watu wanahousika na ujangili? Pili, inakuwaje Mheshimiwa Waziri anawajua kwa majina na hata sehemu wanazokaa, lakini anashindwa kuwachukulia hatua?

Inakuaje Mheshimiwa Waziri, awabembeleze watuhumiwa wakati kuna sheria, kanuni na taratibu za kuwachukulia hatua wahalifu? Ni nini kipo nyuma ya pazia katika kuwalinda na kuwaficha watuhumiwa wa ujangili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa Maafisa Utalii katika Balozi mbalimbali. Kuna taarifa kuwa katika Balozi zetu mbalimbali na muhimu ulimwenguni kumekuwa hakuna Maafisa Utalii ambao watakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa wanaweza kuhakikisha kuwa tunapata watalii wa kutosha kwa ajili ya kuinua pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika Ubalozi wa Tanzania – Berlin ni kati ya Balozi kubwa ulimwenguni ambao hauna Afisa Utalii pamoja na ukweli kuwa Ubalozi huu unahudumia nchi nyingine za Poland, Austria, Hungary, Frankfut, Uswis, Romania, Bulgaria, Slovakia na Jamhuri ya Czech. Kwa kipindi kirefu sana Ubalozi huu umeomba kupatiwa Afisa Utalii kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, lakini mpaka leo hawajaweza kupelekewa maafisa hao kwa ajili ya kutekeleza kwa vitendo diplomasia ya uchumi ambayo ndio msingi wetu wa diplomasia ya Kimataifa.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu ni lini Serikali itawapeleka wataalamu hao katika Ubalozi huu kwa ajili ya kuimarisha sekta ya utalii kwenye nchi zote muhimu ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika Sekta ya Utalii katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, biashara haramu ya nyara zitokanazo na wanyamapori na kukithiri kwa tatizo la ujangili nchini. Kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaojishughulisha na

uwindaji na biashara ya nyara za Serikali bila kuwa na kibali au leseni toka mamlaka zilizowekwa kisheria.

Kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori kifungu cha 80(1), sehemu ya 10: "Mtu yeyote haruhusiwi kujihusisha na biashara ya nyara *(trophies)* bila kuwa na leseni ya biashara ya nyara *(trophy dealer license)*."

Pia kifungu cha 80(2) kinampa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori mamlaka ya kutoa leseni ya biashara ya nyara kwa mtu yeyote ambaye ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kupokea maombi kwenye fomu maalum na kutimiza masharti yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kulipa ada zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa sheria hiyo, bado wanyama wetu wanaendelea kuuawa kwa kasi ya ajabu. Aidha, kumekuwepo kwa taarifa zinazoonesha kuwepo kwa mtandao mpana wa wahusika wa biashara ya wanyamapori na bidhaa za wanyamapori kutoka katika nchi kadhaa kama vile, Kenya, Msumbiji, *DRC*, Namibia na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu aliyoyatoa mbele ya Waandishi wa Habari wakati akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii katika Hoteli ya *Mount* Meru – Arusha mwaka jana, ni kwamba; kwa kipindi cha miaka mitatu, iliyopita tembo 31,348 sawa na asilimia 42 walitoweka katika Hifadhi ya *Selous* na Mikumi na kwamba kuna mtandao wa kijangili wa Kimataifa *(Sophisticated International Syndicate)* unaofanya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha alitoa agizo kwa Bodi ya Wadhamini ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* itoe maelezo ya kina kuhusu kuwepo kwa watumishi wa ndani wa Mamlaka ya Hifadhi wanaosadikiwa kushirikiana na majangili hao kuendesha ujangili ambao unahatarisha hifadhi zetu na sifa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Nyalandu aliirudia kauli hiyo Mkoani Iringa, mwezi Juni, 2013 wakati wa kikao cha siku mbili cha wadau wa ulinzi wa maliasili juu ya ujangili wa tembo katika Mikoa ya Nyanda za Juu na kuahidi kwamba majina ya majangili yakiwemo ya vigogo wanaojihusisha na ujangili wa tembo yatatangazwa hadharani, lakini mpaka sasa hakuna majina yoyote yaliyotangazwa hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la ujangili limekuwa gumu kumalizwa kabisa kwa kuna taarifa zinazohusisha askari wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi katika matukio ya ujangili na biashara haramu ya nyara na taarifa hizo zimeripotiwa sana na vyombo vya habari, lakini cha kusikitisha ni kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari wa majeshi hayo (yaani Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania). Mpaka sasa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania hawajakanusha taarifa hizo, jambo linaloashiria kwamba pengine taarifa hizo ni za kweli.

Mheshimiwa Spika, taarifa za baadhi ya askari walioripotiwa na vyombo vya habari kuhusika na ujangili ni kama ifuatavyo:-

Moja, mnamo Tarehe 7 Januari, 2013, gazeti la Habari Leo lilitoa taarifa za Askari wawili kujihusisha na biashara ya meno ya tembo na kuhusishwa na mauaji ya faru katika Mbuga ya Serengeti na mpaka sasa hakuna taarifa rasmi kutoka Serikalini juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari hao.

Mbili, mnamo tarehe 20 Januari, 2013, Sajenti wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Azizi Athuman Yusufu alikamatwa Mkoani Arusha akiwa na pembe mbili za ndovu na bunduki aina ya *Riffle* yenye namba 458 huku akitumia gari ya mkufunzi wa kijeshi kutoka Zimbabwe anayefundisha nchini.

Tatu, tarehe 23 Julai, mwaka 2013, walikamatwa watu saba wanaodhaniwa kuwa ni majangili, wakiwemo askari watatu wa Magereza Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara wakiwa na gari la Magereza aina *ya Land Cruiser* lenye namba za usajili STK 4394 lililokuwa limepakia nyara za Serikali zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 55. Nyara hizo zilikuwa ni pamoja na twiga wawili, pundamilia wawili, swala, palapala majike wawili na mbuni wawili.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Sekta ya wa Wanyamapori nchini. Licha ya umuhimu wa sekta hii, Serikali imekuwa haifuatilii Makampuni ya Uwindaji yenye leseni kuona kama wanafuata Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 2009. Matokeo ya udhaifu wa Serikali katika ufuatiliaji, kumekuwa na uvunjaji mkubwa wa sheria jambo ambalo limesababisha uwindaji ufanyike kiholela.

Kwa mfano, Kampuni ya Uwindaji ya *Green Miles Safaris Limited* imekuwa ikiwakimbiza na kuwakamata watoto wa wanyamapori pindi wanapozaliwa kinyume na kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Wanyamapori ya 2009. Aidha, Sheria hiyo inapendekeza adhabu ya kifungo cha miaka mitano gerezani na au faini kati ya sh. 500,000/= hadi sh. 2,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kwamba Kampuni ya *Green Miles Safaris Limited* ilishapewa zuio la kufanya uwindaji na Mahakama kutokana na uwindaji usiozingatia sheria, lakini kampuni hiyo ilipitia mlango wa nyuma na kuomba kibali cha uwindaji kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori na Mkurugenzi akatoa kibali na hivyo wote wawili wakapuuza amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ya *Green Miles Safaris Limited* pamoja na uhalifu mwingi inaoufanya katika mbuga zetu wakati wa uwindaji imekuwa ikilindwa na Serikali na ndiyo maana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashawishika kuamini kwamba Serikali ndiyo chimbuko la tatizo la ujangili na uwindaji haramu wa wanyamapori hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninayo *CD* hapa ambayo ni kielelezo Mheshimiwa Waziri akiitaka, inaonesha jinsi ambavyo kampuni hii inakiuka sheria, wanawinda kinyume na taratibu, wanatumia *private number* za magari, wanatumia bunduki ambazo hazistahili. Naomba Waziri aone, ni ushahidi ambao nimeupata…

SPIKA: Mheshimiwa, tunafanya hivi, ukiwa na kitu hicho unasema naweka mezani, siyo unatuhutubia, unaweka mezani.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI WA KAMBO RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni msisitizo tu. Naweka Mezani *CD* hii ili aweze kuiona na Watanzania muone jinsi kampuni hiyo inavyokiuka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo mbele ya Bunge hili ni kwa nini haijaichukulia hatua Kampuni ya Uwindaji *Green Miles* kufanya uwindaji haramu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya misitu. Misitu ina nafasi muhimu ya kumeza hewa ukaa duniani wakati ikizuia uharibifu wa udongo ardhini. Ukataji miti na uondoaji misitu uliokithiri unachangia katika ongezeko la uzalishaji wa hewa ukaa Tanzania. Kupitia misitu mingi tuliyo nayo Tanzania imeendelea kutoa huduma ya kumeza hewa ukaa duniani bila kuwepo utaratibu wowote wa Kimataifa kutoa fidia yoyote.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa na misitu mingi kumekuwepo na changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya misitu, nazo ni:-

(1) Kufanya uendelezaji wa misitu kama rasilimali ya kumeza hewa ukaa na kuinufaisha jamii inayoizunguka;

(2) Kudhibiti ubora na uendelevu wa misitu;

(3) Jamii inayozunguka misitu kunufaika na biashara ya hewa ukaa duniani;

(4) Ujenzi wa uwezo wa kufanya tafiti za uendeshaji misitu nchini; na

(5) Uendelezaji wa njia borazinazowezesha jamii inayozunguka misitu kunufaika na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo zinazoikabili sekta hii ya misitu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kwa kadiri misitu ya Tanzania inavyoendelea kutoa huduma ya Kimataifa ya kumeza hewa ukaa duniani; hivyo ni lazima nchi na wananchi wetu wanufaike kwa kupata kazi na teknolojia zinazochangia maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni kwamba ni muhimu Serikali kuhakikisha inajenga uelewa kwa jamii na wadau wa misitu juu ya uwepo wa fursa za kutumia uwezo wa misitu kumeza hewa ukaa kama chanzo cha kunufaika na biashara ya hewa ukaa duniani. Kuhamasisha ongezeko la matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati ya kupikia na kuchemsha na kupunguza msongo kwenye misitu yetu kwa hitaji hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, katika kuhamasisha hilo ni muhimu kuwepo kwa misitu mfano na miradi mfano katika ngazi za Wilaya na Vijiji na wananchi waone jinsi misitu inavyoweza kuwanufaisha wananchi wanaozunguka misitu mifano hiyo. Hili linawezekana kama mipango na umakini katika utekelezaji wake utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika kilimo cha mito, ni mojawapo ya kilimo ambacho kwa muda mrefu kinaweza kuleta kwa wananchi hasa hapa nchini. Uwekezaji huu unakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa mikopo ya muda mrefu na ambayo inaweza kuwa-*accommodate* wakulima ambao hawana dhamana ya kuweka zaidi ya umiliki wa kimila wa ardhi husika, jambo ambalo halikubaliwi na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kilimo cha miti ni maarufu sana katika Mikoa ya Iringa na Njombe. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulielekeza Bunge ni utaratibu gani hadi sasa ambao wakulima wadogo hasa wa miti wanasaidiwa kupata mikopo ya muda mrefu katika kukabiliana na tatizo hilo la uwepo wa hewa ukaa na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya bajeti kwa idara na vitengo vya Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya sh. 148,000,000,000 kutoka katika idara na taasisi zilizo chini yake. Mwaka huu wa fedha Wizara inatarajia kukusanya jumla ya sh. 144,000,000,000 ambayo ni pungufu ya shilingi bilioni 4.3 kwa kulinganisha na makadirio ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, randama inaonesha kuwa Idara ya Wanyamapori kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 ilikadiriwa kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 28.6 lakini hadi mwezi Machi, 2014 ilikuwa imekusanya kiasi cha Shilingi bilioni 8.2 ambayo ni sawa na asilimia 31.13 ya malengo. Aidha kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Wanyamapori imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 15.55 kutoka kwenye vyanzo vyake vilivyo chini ya idara. Makadirio hayo ni pungufu ya Shilingi bilioni 13.3 kwa kulinganisha na mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo ni kwamba Sekta ya Maliasili na Utalii inashuka kimapato. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza sababu zilizofanya mapato yatokanayo na makusanyo ya maduhuli kwa kushuka kiasi kikubwa namna hiyo.

Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na taarifa ya uchunguzi maalum ni kwamba, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2012 idara ilikusanya shilingi 91,000,000,000. Hali halisi ni kwamba uwezekano wa kukusanya zaidi ni mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi 19.163 kwa ajili ya matumizi ya idara hiyo, ambayo ni sawa na asilimia 22 ya makusanyo yake. Hata hivyo hadi mwezi Machi, 2014 Serikali imetoa kiasi cha Shilingi 9.161 tu. Swali hapa ni kwamba idara inawezaje kujiendesha ikiwa fedha iliyotolewa ni kidogo namna hiyo. Ikumbukwe kwamba Idara hii inasimamia Taasisi, Vyuo na Wakala zipatazo sita ambazo ni *TANAPA*, Ngorongoro, *TAWIRI*, Mweka na kadhalika zinahitaji fedha za kutosha kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo kwenye Sekta ya Wanyamapori ni kwa miradi miwili tu ambao ni mradi wa *KILORWEMP* unaotekelezwa kwa ushirika kati ya Tanzania na Serikali ya Ubelgiji. Mwaka 2013/2014, zilitengwa jumla ya Shilingi bilioni 1.8, lakini hadi Machi, 2014, Sh. 310,000,000 ndizo ambazo zilitolewa na Serikali ya Ubelgiji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni ule wa kulinda Ushoroba wa Selous ambao unatekelezwa kwenye Wilaya ya Namtumbo na Tunduru kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani. Kwa mwaka wa jana hakuna fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba mambo yote yawekwe kwenye *hansard*, yarekodiwe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haitachoka kuikosoa Serikali kwa kuwa kwa muda mrefu sasa katika Wizara hii tumekuwa tunatoa mapendekezo ambayo ambayo yanabezwa. Kwa kuwa ni wajibu wetu kuisimamia ipasavyo Serikali ya CCM, tunazidi kusisitiza kuwa Sekta ya Maliasili na Utalii iendelee. Kuna haja nzima ya kubadilisha mfumo wa usimamizi, uendeshaji wa utekelezaji wa Wizara ambao utatoa fursa kwa Viongozi Waandamizi wa Wizara pamoja na watumishi kutimiza na kutekeleza majukumu yake bila mashinikizo ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ni rai yetu kuwa Serikali itaufanyia kazi upungufu wote ambao tumekuwa tukiusema kwa muda mrefu sasa na kuisimamia ipasavyo sekta hii iwe muhimili wa uchumi kwa Taifa na kuongeza mapato pamoja na kutoa nafasi za ajira kwa wananchi wa Taifa letu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa hotuba yako.

Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa bajeti ya 2014/2015 ya Wizara ya Maliasili na Mazingira kama ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA, (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII, KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, *Frank Herbert aliwahi kusema*
"Utawala bora, kamwe hautegemei Sheria bali sifa binafsi za wale wanaotawala. Vyombo vya Serikali mara zote vipo chini ya wale wanaowaongoza. Kwa hiyo sifa muhimu ya Serikali ni namna ya kuteua/kuchagua viongozi"

Serikali ya awamu ya nne, imeshindwa kuwajenga viongozi wake katika misingi bora na ndio maana pamoja na matatizo ya kimfumo, wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kubadilisha viongozi na matokeo ya ufanisi wake yamekua ni kioja na dhihaka katika utendaji.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO 16 YA BUNGE

Mheshimiwa Spika, kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilileta Bungeni taarifa yake tarehe 20 Disemba 2013 liyowasilishwa na Mwenyekiti wake, Mhe. James Lembeli kuhusu uchunguzi wa matatizo katika utekelezaji wa Operesheni Tokomeza Ujangili, iliyokua na maazimio kumi na sita (16). Taarifa hiyo ndiyo iliyomuondoa aliyekua Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Khamis Kagasheki na mawaziri wengine.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya maazimio ya Bunge, yaliyoongezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni pamoja kuundwa kwa Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama. Aidha, ni takribani miezi zaidi ya mitano kupita tangu Serikali iahidi Desemba mwaka jana, kuahidi, kupitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuunda tume maalumu ya kuchunguza kilichotokea wakati wa Operesheni Tokomeza Ujangili. Katika makujukumu yake, Tume hiyo imepewa kazi zifuatazo;

(a) Kuchunguza na kubaini Operesheni Tokomeza ilivyoendeshwa;

(b) Kuchunguza na kubaini iwapo sheria, kanuni, taratibu na hadidu za rejea zilifuatwa na watu waliotekeleza operesheni hiyo.

(c) Kuchunguza na kubaini kama kuna mtu aliyekiuka sheria, taratibu na hadidu za rejea wakati wa operesheni;

(d) Kuchunguza na kubaini kama kuna watu ambao walikiuka sheria yoyote wakati wa utekelezaji wa operesheni hiyo na kupima kama hatua zilizochukuliwa dhidi yao au mali zao zilikuwa stahiki;

(e) Kupendekeza hatua zozote zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya mtu ambaye itabainika alikiuka sheria, taratibu na hadidu za rejea pamoja na kupendekeza mambo ya kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kutekeleza operesheni nyingine siku zijazo ili kuepuka kasoro.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuundwa kwa Tume hii lakini Serikali haikupaswa tena kuipa tume kazi mpya katika maeneo yote bali yale yaliyohitaji ushahidi wa ziada wa kijinai, hii ni kwa sababu makosa mengine yako wazi ambayo Serikali ilipaswa iwe imeshachukua hatua badala ya kusingizia inasubiri taarifa ya tume. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, sasa inaitaka Serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge wakati wa Majumuisho ya Bajeti ya Wizara ili maazimio ya Bunge hili yasiishie kabatini kama ilivyokuwa kwa mengine ya miaka ya nyuma na ilivyozoeleka sasa.

2.1 Uwajibishwaji wa Watendaji Kutokana na Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, aidha katika azimio namba Saba (7), Bunge liliazimia pia kumwajibisha Mkurugenzi wa Wanyamapori Prof. Alexander Songorwa kwa kutoa taarifa zisizo sahihi kwenye vyombo vya habari na kuudanganya umma kuhusu mazingira na kifo cha Emiliana Marrow wa Babati.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza Waziri wa Maliasili na Utalii wa sasa, Mhe. Lazaro Nyalandu ambaye akiwa katika nafasi yake ya unaibu waziri, kipindi kifupi tu kabla ya uteuzi wake, kwa kasi ya ajabu aliandaa mikutano mingi na ziara mbalimbali huku akiandamana na lundo la vyombo vya habari kama kumbikumbi,na kutoa matamko makali dhidi ya ujangili na watumishi wasio waaminifu. Akiwa katika ziara hizo, aliwahi kuikandia sana Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Ardhi na Maliasili iliyoongozwa na Mhe. James Lembeli, huku akidai kuwa ilikuwa ya uwongo mtupu. Lakini baada ya kubanwa zaidi, alikana kutoa kauli za kuikosoa ripoti hiyo ya kamati. Sababu za kwanini akanushe maneno aliyoyasema zaidi ya mara nne, inabakia kuwa siri yake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, Waziri Nyalandu alitoa taarifa za kuwavua nyadhifa zao Mkurugenzi Mkuu wa Wanyamapori na Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Matumizi Endelevu ya Wanyamapori nyadhifa zao. Nyalandu anadai kuwa moja ya sababu za kuwaondoa, ni kutekeleza maazimio ya Kamati ya Lembeli kutokana na kutowajibika wakati wa Operesheni Tokomeza. Jambo la kujiuliza, kama aliwahi kusema kuwa taarifa ya kamati ni uongo mtupu, je ni lini amethibitisha kuwa kile alichodai kwamba ni uwongo, ulikuwa ukweli? Cha ajabu, aliyeteuliwa kukaimu nafasi ya ukurugenzi, Paul Sarakikya aliyekuwa kiongozi wa utekelezaji wa operesheni tokomeza na aliyehusika moja kwa moja na kinachodaiwa kuwa uvunjifu wa haki za binadamu, ndiye amepewa nafasi ya kukaimu ukurugenzi! Wote tunafahamu ukiukwaji mkubwa wa haki za binaadamu na ukatili uliofanywa katika operesheni tokomeza kiasi cha kusababisha mawaziri wanne kuwajibishwa kwa kutenguliwa nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ilitumia vigezo gani kumteua Sarakikya kukaimu nafasi ya Ukurugenzi wa Wanyamapori huku ikijua alivyoshindwa kutokomeza ujangili hapa nchini na jinsi aliyoendesha operesheni tokomeza ujangili iliyokuwa imejaa dhuluma, uporaji, utesaji na udhalilishaji dhini ya wananchi. Jambo ambalo liliishangaza zaidi Kambi Rasmi ya Upinzani ni kitendo cha Waziri Nyalandu kumteua Ndugu Sarakikya

kukaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori huku akijua kuwa Sarakikya alifanya makosa mengi katika utendaji wake wa kazi katika idara hiyo ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia kuwa Ndg. Sarakikya ndiye aliyeongoza kikosi cha kuzuia ujangili hata kabla ya operesheni tokomeza. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishika nafasi ya kwanza kati ya nchi nane duniani zilizoongoza kwa matukio ya ujangili. Aidha, ili kuonyesha kwamba Serikali hii haizingatii weledi katika utendaji, alietuliwa tena kusimamia Operesheni Tokomeza Ujangili.

2.2 Kauli Tata Za Serikali Juu ya Kufukuzwa Kazi kwa Wakurugenzi

Mheshimiwa Spika, mara baada ya waziri kutangaza kuwavua nyadhifa zao wakurugenzi hao tarehe 24 Februari 2014, Katibu Mkuu wa wizara hii Bi. Maimuna Tarishi aliwarudisha kazini wakurugenzi hao huku Serikali nayo kwa kupitia kurugenzi ya habari maelezo,ikitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuwa taarifa za kufukuzwa kwa wakurugenzi hao si sahihi. Pia, Ikulu kwa kupitia Katibu Kiongozi Balozi Ombeni Sefue, ilitoa tamko la kuitaka Wizara kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma za kumfukuza mtumishi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, Kifungu cha IV (23) (2) inayozungumzia mamlaka ya Rais kumwondoa mtumishi aliyemteua kazini, amri ya kumfukuza mtumishi wa umma itatekelezwa iwapo;

(a)hati ya mashtaka imeandikwa dhidi yake.

(b)mtumishi wa umma amepewa nafasi ya kujibu mashtaka hayo

(c)Maombi yametolewa kwenye hati ya mashtaka kwa mujibu wa taratibu zilizo chini ya kifungu namba 34.

Swali la kumuuliza Waziri Nyalandu, je, hatua hizi zilifuatwa katika kuwasimamisha kazi wakurugenzi hawa? Na je, maamuzi yake ya kumfukuza Prof. Songoro katika vikao vya kamati na kumdhalilisha hata baada ya Ikulu kutoa maagizo ya Wizara kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za kufukuza watumishi kazi ni utawala bora?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali na Wizara kuhakikisha kuwa, uamuzi wowote uliofanywa na kuendelea kufanywa katika kutekeleza maazimio ya Bunge katika kuwawajibisha watumishi hao uzingatie sheria, taratibu na kanuni kwa kuwa Sheria na Kanuni hizo zinaeleza wazi hatua zinazopaswa kuchukuliwa. Vilevile, tunasikitishwa na mvutano baina ya waziri na katibu mkuu wa wizara, hali ambayo inaonesha kuwa kuna mgongano aidha wa kimaslahi na hivyo kuthibitisha kuwa Serikali ni dhaifu kwa kuwa, Waziri na Katibu Mkuu wa wizara moja wanafanya kazi bila kushirikiana na kila mmoja akionekana kumvizia mwenzake hadharani badala ya kukaa kwa pamoja kutekeleza maazimio ya Bunge lako tukufu.

Aidha, mvutano huu pia ni ishara kuwa, maazimio ya Bunge yanaendelea kupuuzwa na Serikali kwa kigezo cha kuzingatia sheria na kanuni huku zikiwaacha watumishi wenye tuhuma wakihamishwa vitengo na idara na kuendelezea urasimu uleule hata uko wanapohamishwa.

Mheshimiwa Spika, ngoma ikivuma sana hupasuka, tena Mungu siku zote hamfichi mnafiki na debe tupu haliachi kutika (si maneno yangu, bali ya wahenga). Si mara ya kwanza, kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhoji juu ya usafi wa Lazaro Nyalandu, Waziri wa Maliasili na Utalii, na mara

kadhaa tumeonesha kwa kiasi kikubwa udhaifu wake na kutoa vielelezo mbalimbali vinavyotilia shaka utendaji wake kabla na hata baada ya kukabidhiwa wizara hii nyeti!

3.0 TASWIRA YA TAIFA KATIKA JUMUIA ZA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani imeendelea kutoa taarifa kwa Serikali juu ya mtandao wa kimataifa wa ujangili ambao pia unahusisha viongozi waandamizi wa Serikali, maafisa usalama wa taifa, wanajeshi wafanyabiashara wakubwa, polisi, wanasiasa, Ikulu na watumishi wa umma. Serikali ya CCM imekua ikitoa kauli za kubeza pamoja na majibu mepesi ya tuhuma hizi huku tatizo la ujangili likiendelea kulichafua taifa katika jumuia ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza baada ya gazeti la Mail on Sunday la nchini Uingereza kutoa taarifa kuwa biashara ya ujangili inahusisha watu wa karibu na Rais wakiwemo wanasiasa, maafisa wa Serikali na wafanya biashara wakubwa, Serikali ilitoa matamko mbalimbali pamoja na kulaani taarifa ya gazeti hilo na hatimaye Waziri Nyalandu, alimwalika mwandishi wa gazeti hilo kujionea mwenyewe shughuli za Serikali za kupambana na ujangili ikiwemo kutembembelea ghala ya kuhifadhia pembe za ndovu zilizokamatwa. Mwaliko huo ilikua ni katika kuthibitisha kuwa Serikali ya CCM haina la kuficha.

Lakini katika hali ya kushangaza, uchunguzi na taarifa zaidi umeonesha kuwa ndani ya miaka minane (8) Serikali ya CCM, imekua ikiomba kibali bila mafanikio kutoka CITES (Convention on International Trade on Endangered Species) cha kuuza shehena ya pembe za ndovu takribani 34,000 zenye uzito wa tani 125 zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 150 sawa na shilingi Bilioni 244.5 za kitanzania (kwa wastani wa sh.1630 kwa dola 1).

Mheshimiwa Spika, jumuia ya kimataifa imeshangazwa na kitendo cha Tanzania kuomba kibali cha kuuza shehena iliyokamatwa ya pembe za ndovu kwa kuwa ni biashara haramu na kitendo cha Serikali kuomba kuyauza ni sawa na kuchochea ujangili zaidi kwa kuwa hali hii itaongeza uhitaji wa pembe za ndovu kwenye soko haramu nchini China. Jambo hili ni aibu kubwa kwa taifa kuomba kufanya biashara haramu kwa kuwa imelidhalilisha taifa. Hii ni sawa na Serikali ikamate madawa ya kulevya, halafu iamue kuyauza ili kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha waziri wa maliasili na utalii kumwalika nchini mwandishi aliyesemwa kuwa ametoa taarifa za uongo na kulichafua taifa, ili ajithibitishie kuwa Tanzania ni safi katika matukio ya ujangili, Bwana Martin Fletcher, na kumtembeza katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa na nia ya kumfunga mdomo(damage control), haikusaidia bali ilivumbua uchafu mwingi na huu wote umewekwa wazi katika vyombo vya habari vya kimataifa na kuendelea kuonesha uozo wa Serikali katika kushughulikia tatizo la ujangili nchini.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kuwa Raisi ameshindwa kusimamia suala hili vizuri kwa kuwa wanaohusika na ujangili ni watu wake wa karibu ama rafiki zake. Aidha, taarifa hizo zimeendelea kubana kauli za Waziri Nyalandu za kuwa anawafahamu majangili kwa majina na kuwataka majangili hao kuacha ujangili ama watawachukulia hatua za kisheria. Maswali yanayoulizwa, je, ni kwa nini waziri hawataji watu wanahousika na ujangili? Pili, inakuaje waziri anawajua kwa majina na hata sehemu wanazokaa, lakini anashindwa kuwachukulia hatua? Inakuaje waziri, awabembeleze watuhumiwa wakati kuna sheria, kanuni na taratibu za kuwachukulia hatua wahalifu? Ni nini kipo nyuma ya pazia katika kuwalinda na kuwaficha watuhumiwa wa ujangili?

3.1 Kukosekana kwa maafisa utalii katika balozi mbalimbali

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa katika balozi zetu mbalimbali na muhimu ulimwenguni kumekuwa hakuna maafisa utalii ambao watakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa wanaweza kuhakikisha kuwa tunapata watalii wa kutosha kwa ajili ya kuinua pato la taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika ubalozi wa Tanzania –Berlin ni kati ya balozi kubwa ulimwenguni ambao hauna afisa utalii pamoja na ukweli kuwa ubalozi huu unahudumia nchi nyingine za Poland,Austria,Hungary,Frankfut,Uswis,Romania,Bulgaria ,Slovakia na Jamhuri ya Czech , kwa kipindi kirefu sana ubalozi huu umeomba kupatiwa afisa utalii kutoka wizara ya mambo ya nje lakini mpaka leo hawajaweza kupelekewa maafisa hao kwa ajili ya kutekeleza kwa vitendo diplomasia ya uchumi ambayo ndio msingi wetu wa diplomasia ya kimataifa.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu ni lini serikali itawapeleka wataalamu hao katika ubalozi huu kwa ajili ya kuimarisha sekta ya utalii kwenye nchi zote muhimu ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika sekta ya utalii katika taifa letu. [1]

4.0 BIASHARA HARAMU YA NYARA ZITOKANAZO NA WANYAMAPORI NA KUKITHIRI KWA TATIZO LA UJANGILI NCHINI

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa na watu wanaojishughulisha na uwindaji na biashara ya nyara za Serikali bila bila kuwa na kibali au leseni toka mamlaka zilizowekwa kisheria. Kwa mujibu wa sheria ya wanyapori *kifungu cha 80(1) sehemu ya 10* ***"mtu yeyote haruhusiwi kujihusisha na biashara ya nyara (trophies) bila kuwa na leseni ya biashara ya nyara (trophy dealer license).*** Na kifungu cha 80(2) kinampa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori mamlaka ya kutoa leseni ya biashara ya nyara kwa mtu yeyote ambaye ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kupokea maombi kwenye fomu maalum na kutimiza masharti yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kulipa ada zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, leseni ya biashara ya nyara inayotolewa katika Kifungu hiki haimruhusu mhusika kuwinda, kuua au kupiga picha mnyama yoyote, badala yake inamruhusu kukamata, kutengeneza bidhaa inayotokana na nyara, kununua au kuuza nyara – 80(3)"[2].

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa sheria hiyo, bado wanyama wetu wanaendelea kuuwawa kwa kasi ya ajabu. Aidha, kumekuwepo kwa taarifa zinazoonyesha kuwepo kwa mtandao mpana wa wahusika wa biashara ya wanyama pori na bidhaa za wanyamapori kutoka katika nchi kadhaa kama vile, Kenya, Msumbiji, DRC, Namibia na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Lazaro Nyalandu aliyoyatoa mbele ya Waandishi wa Habari wakati akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii katika Hoteli ya Mount Meru – Arusha mwaka jana, ni kwamba; kwa kipindi cha miaka mitatu, iliyopita tembo 31348 sawa na asilimia 42 walitoweka katika hifadhi ya Selous na Mikumi na kwamba kuna mtandao wa kijangili wa kimataifa (Sophisticated International Syndicate) unaofanya kazi hapa nchini. Aidha alitoa agizo kwa bodi ya wadhamini ya mamlaka ya hifadhi za taifa *(TANAPA)* itoe maelezo ya kina kuhusu kuwepo watumishi wa ndani ya mamlaka ya hifadhi wanaosadikiwa kushirikiana na majangili hao kuendesha ujangili ambao unahatarisha hifadhi zetu na sifa ya nchi yetu**.**

Mheshimiwa Spika, Waziri Nyalandu aliirudia kauli hiyo mkoani Iringa, mwezi Juni, 2013 wakati wa kikao cha siku mbili cha wadau wa ulinzi wa maliasili juu ya ujangili wa tembo katika mikoa ya Nyanda za juu na kuahidi kwamba majina ya majangili yakiwemo ya vigogo wanaojihusisha na ujangili wa tembo yatatangazwa hadharani, lakini mpaka sasa hakuna majina yoyote yaliyotangazwa hadharani.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Tanzania Wildlife Research Institute-TAWIRI katika mbuga ya hifadhi ya Selou na Mikumi inaonyesha kuwa idadi ya Tembo imeshuka kutoka 74,900 mwaka 2006 hadi kufikia 43,552 mwaka 2009. Hii ikiwa na maana kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu takribani asilimia 42 ambayo ni Tembo 31,348 katika hifadhi mbili tu waliuawa na majangili[3]. Hii ni hatari kubwa sana na kwa kutilia maanani kuwa Tembo mmoja anapatikana baada ya miaka miwili (yaani Tembo hubeba mimba kwa kipindi cha miaka miwili ndipo azae).

Mheshimiwa Spika, biashara haramu ya nyara zitokanzao na wanyamapori hususan tembo imechangia sana ujangili wa kutisha wa tembo kiasi kwamba idadi ya tembo imepungua mno kiasi cha kuwafanya tembo wawe miongoni mwa jamii ya viiumbe waliopo hatarini kutoweka kabisa (endangered species). Nasema hivi kwa sababu idadi ya tembo kwa uchache, waliokuwepo katika nchi za Kiafrika kwa miaka ya sabini walikuwa ni takribani milioni moja na laki mbili **(1,200,000)** lakini kwa sasa wamebakia wasiozidi laki tano[4]

Mheshimiwa Spika, hali ya ujangili nchini imefika pabaya na ina kiasharia kibaya kwa miaka michache ijayo. Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2010, jumla ya tembo 10,000 waliuwawa Tanzania, ikiwa ni sawa na wastani wa tembo 27 kwa siku. Mwaka 2012 pekee, tembo takribani 23,000 wameuwawa kwa mwaka ambayo ni sawa na tembo 63 kwa siku. Hii ni sawa na ongezeko la 57% kwa kipindi cha miaka 2. Kwa sasa Tanzania inakadiriwa kuwa na tembo kati ya 150,000 na 170,000. Kutokana na takwimu hizi, ikiwa Tembo 63 wanauwawa kwa siku, ni dhahiri kwamba kwa kipindi cha miaka 7 ijayo Tembo hawa watakuwa wameuawa wote.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na shirika la Umoja wa Mataifa la kupamba na madawa ya kulevya na uhalifu (United Nation's Office on Drugs and Crime-UNODC-), inaonyesha kuwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na nchi za Kusini Mashariki mwa Asia ni wasambazaji wakubwa wa bidhaa haramu za wanyamapori kwenye soko la China, Marekani na baadhi ya nchi katika bara la Ulaya. Bidhaa hizo za wanyamapori ni pamoja na pembe za ndovu, pembe za faru, ngozi za chui na simba na viungo mbalimbali vya wanyamapori. Kwa mujibu wa utafiti huo ni kwamba mununuzi hulipa kiasi cha dolla za kimarekani 2,500 kwa kila pembe moja ya faru.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Ujangili limekuwa gumu kumalizwa kabisa kwa kuna taarifa zinazohusisha askari wa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi katika matukio ya ujangili na biashara haramu ya nyara na taarifa hizo zimeripotiwa sana na vyombo vya habari, lakini cha kusikitisha ni kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari wa majeshi hayo (yaani jeshi la polisi na jeshi la wananchi wa Tanzania). Mpaka sasa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania hawajakanusha taarifa hizo jambo linaloashiria kwamba pengine taarifa hizo ni za kweli.

Mheshimiwa Spika, taarifa za baadhi ya askari walioripotiwa na vyombo vya habari kuhusika na ujangili ni kama ifuatavyo:

1. Mnamo Tarehe 7 January 2013, Gazeti la habari leo lilitoa taarifa za askari wawili kujihusisha na biashara ya meno ya tembo na kuhusishwa na mauaji ya faru katika mbuga ya Serengeti na mpaka sasa hakuna taarifa rasmi kutoka Serikalini juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari hao.

2. Mnamo Januari 20, 2013 Sajenti wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Azizi Athuman Yusufu alikamatwa mkoani Arusha akiwa na pembe mbili za ndovu na bunduki aina ya Riffle yenye namba 458 huku akitumia gari ya mkufunzi wa kijeshi kutoka Zimbabwe anayefundisha nchini.

3. Tarehe 23 Julai, mwaka 2013, walikamatwa watu saba wanaodhaniwa kuwa ni majangili, wakiwamo askari watatu wa Magereza Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara wakiwa na gari la Magereza aina ya Land Cruiser lenye namba za usajili STK 4394 lililokuwa limepakia nyara za Serikali zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 55. Nyara hizo zilikuwa ni pamoja na Twiga wawili, Pundamilia wawili, Swala, Palapala majike wawili na Mbuni wawili.

Mheshimiwa Spika, Biashara haramu ya pembe za ndovu imevuka mipaka ya nchi na imeanza kushamiri katika ukanda wa Afrika ya Mashariki jambo ambalo linatishia kutoweka kabisa kwa wanyama hao ambao ni kivutio kikubwa cha utalii. Taarifa katika mtandao wa habari wa "Annamiticus" (www.annamiticus.com) zinasema kwamba mwaka 2012, makontena mawili kutoka Kenya na Tanzania yalikamatwa huko HongKong yakiwa yamebeba tani 4 (Kilo 4,000) za pembe za ndovu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo, kontena lililotoka Tanzania lilikuwa limeandikwa "plastic scrap" ikimaanisha kuwa lilikuwa na vifaa ya plastiki lakini baada ya kufunguliwa kulikuwa na vipande 972 vya pembe halisi za ndovu zenye uzito wa kilogramu 1,927 pamoja na kilo moja na nusu ya unga wa pembe za ndovu zilizosagwa. Kontena lililotoka Kenya lilikuwa limeandikwa "roscoco beans" yaani maharage aina ya roscoco, lakini lilipofunguliwa kulikuwa na vipande 237 vya pembe za ndovu sawa na kilogramu 1,884.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo, wingi wa pembe hizi za ndovu zilizokamatwa, unadhihirisha kwamba tembo takriban 600 kwa uchache waliuwawa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2013 kontena lingine lilikamatwa likiwa limesheheni pembe za ndovu 113 huko China zenye thamani ya Dola za Kimarekani 400,000. Kontena hili liliandikwa kwamba limebeba vipuri (spareparts) toka Burundi. Kwa kuwa Burundi haina bandari, kuna uwezekano mkubwa kwamba kontena hilo lilipitia bandari ya Tanzania, na hivyo kuna uwezekano pia kwamba pembe hizo zinatokana na tembo waliouwawa Tanzania.

5.0 MAENDELEO YA SEKTA YA WA WANYAMAPORI NCHINI

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya wanyamapori katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu ni mkubwa sana. Takwimu[5] zinaonyesha kuwa uwindaji wa kitalii kwa miaka mitatu kati ya 2009 na 2012 uliingiza shilingi bilioni 91. Kwa sababu hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia idara yake ya Wanyamapori inatakiwa kuilinda na kuiendeleza sekta hii ili iendelee kuchangia zaidi katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha wa kuilinda na kuiendeleza sekta ya wanyamapori, Bunge lilitunga Sheria ya Uhifadhi ya 2009, ambayo inatumika pamoja na sera ya wanyamapori ya mwaka 2007 ili kuratibu na kudhibiti shughuli za uwindaji wa wanyamapori kwa namna ambayo sekta ya wanyampaori inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa Sekta ya wanyamapori ni muhumu kwa kuwa sekta inachangia ukuaji wa uchumi katika Nyanja mbalimbali. Kwa mfano wanyamapori ni kivutio kikubwa cha watalii ambao hutoa fedha nyingi za kigeni wajapo kutalii hapa nchini kwa ajili ya kutazama na kuwapiga picha wanyama hao. Aidha sekta ya wanyama pori inachangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutoa ajira kwa wananchi na pia kukuza soko la bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu wa sekta hii, Serikali imekuwa haifuatilii makampuni ya uwindaji yenye leseni kuona kama wanafuata sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya 2009.

Matokeo ya udhaifu wa Serikali katika ufuatiliaji, kumekuwa na uvunjaji mkubwa wa sheria jambo ambalo limesababisha uwindaji ufanyike kiholela. Kwa mfano, Kampuni ya Uwindaji ya Green Miles Safaris Limited imekuwa ikiwakimbiza na kuwakamata watoto wa wanyamapori pindi

wanapozaliwa kinyume na kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Wanyamapori ya 2009. Aidha Sheria hiyo inapendekeza adhabu ya kifungo cha miaka mitano gerezani na au faini kati ya shilingi 500,000/= hadi shilingi 2,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kwamba Kampuni hii ya Green Miles Safaris Limited ilishapewa zuio na Mahakama la kufanya uwindaji kutokana na uwindaji usiozingatia sheria lakini Kampuni hiyo ilipita mlango wa nyuma na kuomba kilbali cha uwindaji kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori na Mkurugenzi akatoa kibali na hivyo wote wawili wakapuuza uamuzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii ya Green Miles Safaris Limited, pamoja na uhalifu mwingi inaoufanya katika mbuga zetu wakati wa uwindaji, imekuwa ikilindwa na Serikali ndio maana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Upinzani Bungeni inashawishika kuamini kwamba Serikali ndio chimbuko la tatizo la Ujangili na uwindaji haramu wa wanyamapori hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo mbele ya bunge hili ni kwa nini haijaichukulia Kampuni ya Uwindaji Green Miles kwa kufanya uwindaji haramu hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, Tatizo kubwa la Maendeleo ya Sekta ya Wanyapori ni kwamba Serikali huwa haifuati hata mapendekezo yanayotolewa na Kamati za zinazoudwa na Serikali yenyewe. Kwa mfano, mwaka 2006, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa wakati huo Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo (Mb), aliunda Kamati ya Wataalam ambayo aliitaka ifanye uchambuzi wa kina wa shughuli za uwindaji wa kitalii nchini. Uchambuzi huo ulitakiwa uzingatie utendaji kazi katika shughuli za uwindaji wa kitalii, mafanikio yaliyofikiwa mpaka sasa na matatizo yanayoikabili tasnia hiyo. Hatimaye, Kamati ilitakiwa kumshauri Mheshimiwa Waziri namna ya kuleta mabadiliko ndani ya sekta hiyo kwa minajili ya kulinda uhifadhi, kuwawezesha wananchi kushiriki katika uwindaji wa kitalii kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuondoa umaskini na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Hadidu za rejea kamati hiyo ilizopewa ziliitaka Kamati:[6]

(i) Ipitie utaratibu wa sasa wa uombaji na ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii pamoja na chombo chake cha ugawaji kuona kama havibagui wala havisababishi malalamiko kwa wadau mbalimbali;

(ii) Ichambue kwa makini vigezo na masharti yaliyopo yanayohusu ukaguzi wa uwezo wa Kampuni za Uwindaji zinazowasilisha maombi kwa ajili ya Uwindaji wa Kitalii ili kuona kama yanafaa kwa mazingira ya sasa;

(iii) Ichambue Mikataba mbalimbali ya kampuni za uwindaji; ya zamani na inayoendelea kwa lengo la kujiridhisha kama inafaa au ina upungufu unaohitaji marekebisho ili kulinda uhifadhi na maslahi ya umma.

(iv) Iangalie Kanuni za Uwindaji wa Kitalii na zile za Utalii wa picha pamoja na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974 na kushauri namna ya kuondoa

migongano ambayo imejitokeza baada ya kuruhusu utalii wa picha kwenye maeneo ya uwindaji wa kitalii.

(v) Ichambue Sera na Sheria zinazohusiana na Wanyamapori na Utalii, na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii ili kuona kama Wananchi wanafaidika na uwindaji huo wa kitalii.

(vi) Ichambue utaratibu wa ukusanyaji mapato, kubaini njia ambazo zitaongeza maduhuli ya Serikali, na kutathmini utaratibu wa ugawaji vitalu kwa njia ya zabuni.

(vii) Mwisho, Kamati iangalie uwezekano wa Serikali kuwawezesha Wananchi kushiriki kikamilifu katika tasnia hii ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati hiyo yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

1. Kuboresha utaratibu wa ugawaji wa vitalu kwa kuipa Kamati ya Ugawaji Vitalu nguvu za kisheria na kwa kupanua uwakilishi wake.

2. Kuunda Wakala wa Serikali wa kusimamia shughuli za uwindaji wa kitalii badala ya Idara ya Wanyamapori.

3. Kuangalia upya umiliki wa vitalu ili kuwawezesha wananchi kushiriki zaidi katika uwindaji wa kitalii kwa njia ya ubia na baadaye kumilikishwa vitalu wakati wageni na wananchi watafanya kazi ya kuwindisha.

4. Serikali iwawezeshe Wawindaji Bingwa wa Kitanzania ili waweze kumiliki vitalu na kutumia ujuzi na uzoefu walionao. Serikali inaweza kuwawezesha wananchi kwa kuzungumza na mabenki ili wapunguze riba ya kukopa fedha benki na kuruhusu matumizi ya vitalu kama dhamana. Pia wawindaji bingwa waanzishe bodi yao ya kitaalam.

5. Kuthamini vitalu vya uwindaji wa kitalii na kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Serikali.

6. Kuweka ukomo wa umiliki wa kitalu wa vipindi viwili vya miaka mitano ili ili kuruhusu waombaji wapya.

7. Kuboresha taarifa za sekta ya Wanyamapori kwa kuweka taarifa zote muhimu zinazohusu shughuli za uwindaji wa kitalii kwenye Tovuti ya Idara.

8. Idara iimarishe ufuatiliaji na tathmini ya vitalu kwa kuanzisha chombo huru cha kusimamia shughuli za uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa kiwango gani mapendekezo ya Kamati hiyo yametekelezwa na ni mangapi ambayo bado kutekelezwa na ni kwanini?

6.0 UTALII NA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA

Mheshimiwa Spika, kwa eneo kubwa la ardhi lililofunikwa na wingi wa misitu pamoja na aina mbalimbali za maua na viumbe, Tanzania ni mojawapo ya vivutio vikubwa vya utalii barani

Afrika. Nchi yetu ina raslimali nyingi asilia ikiwemo pamoja na maeneo mengi ya nyika za mapori yenye aina nyingi za banoai.

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa vivutio vya utalii ni pamoja na Mbuga za wanyama , hifadhi za taifa, hifadhi zilizozuiliwa na maeneo ya kihistoria. Hata hivyo kwa sababu ya ongezeko la joto, baadhi ya hivi vivutio ikiwemo theluji katika kilele cha mlima Kilimanjaro iko katika hatari ya kupotea. Na baadhi ya wanyama katika mbunga zenye ukame mkubwa wameanza kupungua na kuathirika.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kuwa na neema ya kuwa na vivutio vingi vya utalii, bado sekta ya utalii inakabiliwa na chamgamoto kadhaa, zikiwa ni;

(i) Uendelezaji wa kazi zitakazohakikisha kuendelea kuwepo kwa vivutio mbalimbali vya utalii kwa kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Ukarabati wa miundombinu kama vile barabara, madaraja, kambi za watalii na upatikanaji wa umeme kwa ajili ya watalii wa mbugani;

(iii) Uwezo mdogo wa idara zinazohusika kusimamia, kulinda vivutio vya utalii, kama vile kuendesha na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaamini kabisa tatizo la umeme katika vivutio vya utalii vilivyopo mbugani, suluhisho ni kutumia umeme wa jua (solar energy), hili ni rahisi katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nitaonyesha hapo baadae makusanyo yanayopatikana kutoka sekta ya utalii hayana uwiano wa moja kwa moja na uwekezaji katika sekta hiii. Ndiyo sababu kubwa ya mapato ya sekta kutokuakisi vivutio tulivyonavyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika Sekta ya Utalii ni suala lenye tija kubwa katika uchumi wetu kwa kuwa sekta hiyo imekuwa ikichangia katika uchumi wa Taifa licha ya uwekezaji mdogo uliofanyika katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa katika maeneo yote ya hifadhi zetu kwa sasa kuna kuna hoteli zenye uwezo wa kutoa huduma za malazi (carrying capacity) kwa watu 6,681 ambapo kwa miaka mitano ijayo idadi hii itafikia uwezo wa kulaza watu 8,421. Hiki ni kwango kidogo sana cha huduma za malazi kiasi kwamba tunapoteza fursa ya kunufaika katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, japokuwa uwekezaji katika sekta ya utalii ni mdogo lakini sekta imeendelea kuwa nguzo muhimu katika uchumi wetu. Kwa mwaka 2011 utalii na usafiri wa kitalii ulichangia asilimia 13 kwenye pato la taifa na kuchangia takriban asilimia 25 ya fedha za kigeni. Aidha, Mpango unaeleza kuwa lengo ni kuongeza wageni kwa asilimia 40 kutoka wageni 671,886 kwa sasa hadi 940,640 ifikap June 2016. Aidha Mpango unalenga pia kuzidisha siku za mtalii kutembelea maeneo yenye vivutio vya kitalii nchini kutoka siku wastani wa siku 11 za sasa hadi wastani wa siku 18[7].

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya mpango huo ili wananchi wajue tumefanikiwa kwa kiwango gani katiaka kuboresha sekta ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya usafiri na usafirishaji ya ndani ya nchi, uwekezaji katika ujenzi wa hotel kwenye maeneo muhimu ya utalii kama vile kwenye hifadhi, mikoa

inayozunguka mlima Kilimanjaro kutasaidia sana kuvutia watalii. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuboresha miundo mbinu ya usafiri hasa wa anga ili na kujenga hoteli za viwango vya Kimataifa katika maeneo yenye vivutio vya watalii ili kuvutia mashirika ya mengi ya ndege toka nje kuja hapa.

Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Serikali kwamba ifufue shirika letu la Ndege la Taifa ili tuweze kumudu ushindani katika usafiri wa anga na hapohapo kuongeza idadi ya watalii katika nchi yetu. Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro na ule wa Julius Nyerere Dar es Salaam vikiboreshwa vinaweza kuwa ni kitovu cha mashirika mengi ya kimataifa kubadilishia wasafiri kama kuna mkakati makini.

Mheshimiwa Spika, watalii toka nje wanapenda sana kupanda ndege za nchi wanazotembelea zaidi kuliko kupanda ndege za kuunganisha. Kwa njia moja au nyingine usafiri huo unawapunguzia gharama. Mfano mzuri ni miaka ya themanini wakati Air-Tanzania ilipokuwa inafanya safari zake nchi za Ulaya, watalii wengi walikuwa wanakuja kwa ndege zetu. Hoja ni kwamba Serikali ina mkakati gani wa kufufua Shirika la Ndege la Taifa (ATC) Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Serikali kuingia ubia na makampuni binafsi kupitia mpango wa Private Public Pertnership – (PPP) ili kuboresha huduma za usafiri wa anga hapa nchini ambao unachoche watalii wengi kuja kwa kuwa kuna usafiri wa moja kwa moja.

7.0 SEKTA YA MISITU

Mheshimiwa Spika, misitu ina nafasi muhimu ya kumeza hewa ukaa duniani wakati ikizuia uharibifu wa udongo/ardhi. Ukataji miti na uondoaji misitu uliokithiri unachangia katika ongezeko la uzalishaji wa hewa ukaa Tanzania. Kupitia misitu mingi tuliyonayo Tanzania imeendelea kutoa huduma ya kumeza hewa ukaa duniani, bila ya kuwepo utaratibu wowote wa kimataifa kutoa fidia yoyote.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa na misitu mingi, kumekuwepo na changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya misitu, nazo ni:

(a) Kufanya uendelezaji wa misitu kama raslimali ya kumeza hewa ukaa na kuinufaisha jamii inayoizunguka;

(b) Kuthibiti ubora na uendelevu wa misitu;

(c) Jamii inayoizunguka misitu kunufaika na biashara ya hewa ukaa duniani;

(d) Ujenzi wa uwezo wa kufanya tafiti za uendelezaji misitu nchini; na

(e) Uendelezaji wa njia bora zinazowezesha jamii inayozunguka misitu kunufaika na raslimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, zinazoikabili sekta hii ya misitu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka kuhakikisha kwa kadri misitu ya Tanzania inavyoendelea kutoa huduma ya kimataifa ya kumeza hewa ukaa duniani, hivyo ni lazima nchi na wananchi wetu tunufaike kwa kupata kazi na teknolojia zinazochangia maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwamba, ni muhimu Serikali kuhakikisha unajengwa uelewa kwa jamii na wadau wa misitu juu ya uwepo wa fursa za kutumia uwezo wa misitu kumeza kumeza hewa ukaa kama chanzo cha kunufaika na biashara ya hewa ukaa duniani. Kuhamasisha ongezeko la matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati ya kupikia na kuchemshia na kupunguza msongo kwenye misitu yetu kwa hitaji hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa katika kuhamasisha hilo, ni muhimu kuwepo kwa misitu mfano na miradi mfano katika ngazi za wilaya na vijiji ili wananchi waone jinsi misitu inavyoweza kuwanufaisha wananchi wanaozunguka misitu mfano hiyo. Hili linawezekana kama mipango na umakini katika utekelezaji wake utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika kilimo cha miti ni mojawapo ya kilimo ambacho kwa muda mrefu kinaweza kuleta tija kubwa kwa wananchi hasa hapa nchini, uwekezaji huu unakabiliwa na chamgamoto kubwa ya kukosekana kwa mikopo ya muda mrefu na ambayo inaweza kuwa-accommodate wakulima ambao hawana dhamana ya kuweka zaidi ya umiliki wa kimira wa ardhi husika, jjambo ambalo halikubaliwi na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kilimo cha miti ni maarufu sana katika mikoa ya Iringa na Njombe, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni utaratibu gani hadi sasa ambao wakulima wadogo hasa wa miti wanasaidiwa kupata mikopo ya muda mrefu katika kukabiliana na tatizo hili la uwepo wa hewa ukaa na kuongeza kipato.

8.0 MAPITIO YA BAJETI KWA IDARA NA VITENGO VYA WIZARA

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14 wizara ilitarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 148.97 kutoka katika Idara na taasisi zilizo chini yake. Mwaka huu wa fedha wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 144.6, ambayo ni pungufu ya shilingi bilioni 4.37 kwa kulinganisha na makadirio ya mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, randama inaonyesha kuwa Idara ya wanyamapori kwa kipindi cha mwaka 2013/14 ili kadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 28.65, Lakini hadi mwezi Machi, 2014 ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 8.92 ambayo ni sawa na asilimia 31.13 ya malengo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Idara ya Wanyamapori imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 15.55 kutoka kwenye vyanzo vyake vilivyo chini ya idara. Makadirio haya ni pungufu ya shilingi bilioni 13.1 kwa kulinganisha na mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo ni kwamba Sekta ya Maliasili na Utalii inashuka kimapato. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza sababu zilizofanya mapato yatokanayo na makusanya ya maduhuli kwa shuka kwa kiasi kikubwa namna hiyo. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Takwimu zilizotolewa na taarifa ya uchunguzi maalum ni kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2012 Idara ilikusanya shilingi bilioni 91 na hali halisi ni kwamba uwezekano kukusanya zaidi ni mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 19.163 kwa ajili ya matumizi ya Idara hiyo, ambayo ni sawa na asilimia 22.7 ya makusanyo yake. Lakini hadi mwezi machi 2014, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 9.161 tu. Swali hapa ni kwamba idara itawezaje kujiendesha ikiwa fedha iliyotolewa ni kidogo namna hiyo? Ikumbukwe kwamba Idara hii inasimamia taasisi/vyuo na wakala zipatazo sita ambazo ni TANAPA, NCAA, TAWIRI,CAWM-Mweka, PWTI na CBCTC ambazo zinahitaji fedha za kutosha kuziendesha.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo kwenye sekta ya wanyamapori, ni kwa miradi miwili tu ambayo ni mradi wa KILORWEMP unaotekelezwa kwa ushirika kati ya Tanzania na Serikali ya Ubelgiji. Mwaka 2013/14 zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 1.82, lakini hadi Machi 2014 shilingi milioni 310 ambazo zilitoka Serikali ya Ubelgiji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni ule wa Kulinda ushoroba wa Selous-Niassa, ambao unatekelezwa kwenye wilaya za Namtumbo na Tunduru kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani. Kwa mwaka jana hakuna fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14 Idara ya Utalii ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 16.896 lakini hadi mwezi mach, 2014 ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 3.25 ambayo ni sawa na asilimia 19 tu ya matarajio kwa mwaka. Aidha, fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa idara na Taasisi zilizo chini yake ni shilingi bilioni 12.1, lakini hadi Machi, zilikuwa zimetolewa shilingi bilioni 3.36.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2014/15 idara hii ya Utalii inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 16.91. Aidha, kwa maendeleo Iadara hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.2. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza inakuwaje Idara inakusanya shilingi bilioni 16.91 lakini uwekezaji unakuwa wa shilingi bilioni 1.2, aidha uwekezaji huo hauna matokeo ya moja kwa moja na ukuaji wa utalii. Je ni kwa vipi katika Dunia hii ya ushindani katika sekta ya utalii inaweza kuleta tija na kuinua uchumi?

9.0 HITIMISHO

Kambi Rasmi ya Upinzani, haitochoka kuikosoa Serikali kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa katika Wizara hii tumekua tunatoa mapendekezo ambayo yanabezwa. Na kwa kuwa ni wajibu wetu kuisimamia ipasavyo Serikali ya CCM, tunazidi kusisitiza kuwa ili sekta ya maliasili na utalii iendelee kuna haja nzima ya kubadilisha mfumo wa usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa Wizara, ambao utatoa fursa kwa viongozi waandamizi wa Wizara pamoja na watumishi kutimiza na kutekeleza majukumu yake bila mashinikizo ya kisiasa.

Ni rai yetu kuwa, Serikali itayafanyia kazi mapungufu yote ambayo tumekua tukiyasema kwa muda mrefu sasa na kuisimamia ipasavyo sekta hii hili iwe mhimili wa uchumi kwa taifa kwa kuongeza mapato pamoja na kutoa nafasi za ajira kwa wananchi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

.....
Mch. Peter S. Msigwa (MB)
Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni,
Wizara ya Maliasili na Utalii.
13.5.2014

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana kwa sababu leo tumefanikiwa kuwasikiliza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali katika Wizara hii. Kwa hiyo, kesho tutakuwa na muda mzuri zaidi wa kuzungumza.

Kama mtakavyokuwa mnaona, jana Kamati ya Uongozi tulikaa kuangalia upya ratiba yetu ile ya kazi. Katika angalizo la Kamati ya Uongozi ndipo mnakuta kwamba leo ilikuwa saa hizi ifike Wizara ya Maji lakini imebidi tuipeleke siku za mbele zaidi kwa sababu bado kuna mazungumzo ambayo inabidi yaendelee kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti; kwa sababu hailingani na vile tulivyoamua kipindi cha mwaka uliopita.

Kwa hiyo, Wizara hizo na Wizara nyingine tena nazo tumezibadilisha. Kwa hiyo, wale wote wanaohusika na kuandaa hotuba zao kwa ajili ya Wizara zinazohusika wawe tayari, msisubiri dakika za mwisho kwa sababu haya mabadiliko yanaweza kufanyika. Kwa hiyo, ili

mradi ratiba imetoka, unajua kabisa Wizara yako inafanyika lini, jiandaeni Wenyeviti, Kambi ya Upinzani na Wenyeviti wanaohusika na Kamati hizo na Serikali yenyewe, kuna wakati mwingine mtatakiwa kusogea karibu kabla hujajiandaa. Usiseme mimi niliandikiwa tarehe hii, jiandae, unajua kwamba siku yako ya kusoma ni hiyo, lakini tunaweza kubadilisha kwa sababu ya mazingira ambayo yatakuwa yanahusika.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine naomba niahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.48 Usiku Bunge liliahirisha mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)